# KAZI AMBAYO HAIJAKAMILIKA

*Sheria Tisa za kuongeza kasi*



GARY KEESEE

Rafiki mpendwa katika Kristo,

Ni maombi yetu kwamba upate nyenzo hii ya mafundisho kuwa baraka na faraja kwako! Tafadhali jisikie huru kushiriki nyenzo hii na marafiki zako, familia na washiriki wa kanisa lako. Pia, unaweza kwenda kwa FLNFree.com ili kupakua nakala za ziada na kwa mafundisho zaidi bila malipo katika lugha yako.

Mungu anakupenda na ana mpango wa ajabu kwa maisha yako! Kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi kulibadili maisha yetu na kuyafanya kuwa bora, na tunaamini kwamba itakuwa vivyo hivyo kwako!

Kwa upendo katika Kristo

Gary na Drenda Keesee



Maneno ya Ziada: Kumbuka kwenda kwenye tovuti yetu ya upakuaji bila malipo FLNFree.com ili kupakua mafundisho zaidi ya bure katika lugha yako!

# KAZI AMBAYO HAIJAKAMILIKA



*Sheria Tisa za kuongeza kasi*

GARY KEESEE

*Kazi Ambayo Haijakamilika: Sheria Tisa za Kuongeza kazi*
Hakimiliki © 2023 na Gary Keesee

Isipokuwa imebainishwa vingine, Maandiko yote yametolewa kutoka kwa Tafsiri ya Biblia ya 'UNION' ya Biblia Takatifu. Hakimiliki ©1952, United Bible Societies, Tanzania. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Maandiko yaliyowekwa alama (AMP) yametolewa kutoka kwa Amplified Bible. Hakimiliki © 2015 na The Lockman Foundation, La Habra, CA 90631. Haki zote zimehifadhiwa.

Maandiko yaliyowekwa alama (EHV) yametolewa kutoka kwa Tafsiri ya 'Evangelical Heritage Version® (EHV®)' ya Biblia Takatifu. Hakimiliki © 2019 Wartburg Project, Inc. Haki zote zimehifadhiwa. Imetumika kwa ruhusa.

Maandiko yaliyowekwa alama (DLNT) yamechukuliwa kutoka kwa Agano Disciples' Literal New Testament © 2011 na Michael J. Magill. Imechapishwa na Reyma Publishing. Haki zote zimehifadhiwa.

Maandiko yaliyowekwa alama (ESV) yametolewa kutoka kwa English Standard Version® ya Biblia Takatifu. Toleo la Maandishi: 2016. Hakimiliki © 2001 na Crossway, huduma ya uchapishaji ya Good News Publishers. Haki zote zimehifadhiwa.

Maandiko yaliyowekwa alama (BSB) yametolewa kutoka kwa Berean Study Bible. Hakimiliki © 2016, 2020 na Bible Hub. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote.

Kimechapishwa nchini Kenya. Haki zote zimehifadhiwa chini ya Kanuni ya Hakimiliki ya Kimataifa. Yaliyomo na/au jalada hayaruhusiwi kunakiliwa kwa ujumla au kwa sehemu kwa njia yoyote bila idhini ya kutoka kwa Mchapishaji.

ISBN: 978-1-945930-98-0

Kimesambazwa na huduma ya Faith Life Now.

Faith Life Now
P.O. Box 779
New Albany, OH 43054
1.888.391.LIFE

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye Mtandao katika www.faithlifenow.com.

# YALIYOMO

**UTANGULIZI**........................................................................ **7**

**SURA YA 1:** UNATAKA KWENDA WAPI?................................ **11**

**SURA YA 2:** WATUMWA HAWAOTI NDOTO ........................ **25**

**SURA YA 3:** JE, UWEZO WAKO NI MKUBWA KIASI GANI?.. **47**

**SURA YA 4:** BARAKA YA IBRAHIMU....................................... **75**

**SURA YA 5:** KANUNI YA KUTAWALA...................................... **87**

**SURA YA 6:** KANUNI YA KUWA NA UWEZO.......................... **97**

**SURA YA 7:** KANUNI YA KUMILIKI......................................... **113**

**SURA YA 8:** KANUNI YA SHINIKIZO....................................... **125**

**SURA YA 9:** KANUNI YA MKAKATI.......................................... **139**

**SURA YA 10:** KANUNI YA UHARAKA...................................... **167**

**SURA YA 11:** KANUNI YA UMUHIMU...................................... **183**

**SURA YA 12:** KANUNI YA UKARIMU....................................... **199**

**SURA YA 13:** KANUNI YA MAADHIMISHO........................... **235**

**HITIMISHO**.......................................................................... **251**

**KIAMBATISHO KUHUSU IMANI**.......................................... **253**

# UTANGULIZI

"Mbona haupo pale juu?" Hivyo ndivyo nilivyosikia Bwana akiniambia nilipokuwa nimeketi kwenye kongamano la wauzaji la kila mwaka nikitazama viongozi 10 bora wa mauzo wakitambuliwa, jambo ambalo lilijumuisha kupewa hundi ya bonasi ya $100,000. Nilishtuka kidogo niliposikia hilo. Nikasema, "Bwana, unajua kwa nini siko kule juu; uliniita nianzishe na kukuchungia kanisa. Unajua nina shughuli nyingi, nina shughuli nyingi sana. Hawa jamaa jukwaani hufanya kazi hii siku kutwa. Wanakula na kupumua mwaka mzima ili kufika hapa. Mimi ni mchungaji muda wangu wote na huwa ninafanya kazi katika kampuni yangu katika muda wangu wa ziada." Kisha nikamsikia akinijibu, "Ninakutaka huko juu. Ni fursa nzuri kwako kuniwakilisha Mimi." Naam, bila shaka, ningependa kuwa huko juu; nani asingependa hilo? Kwa hiyo, nikasema, "Vema, Bwana, tayari muda wangu umejaa shughuli, kwa hiyo itabidi unionyeshe kile ninachohitaji kufanya ili hilo liwezekane, kwa sababu sasa hivi sioni kama litawezekana."

Ili kukupa historia kidogo, kufikia hapo maishani mwangu, kando na kuwa mchungaji wa kanisa kubwa la watu 3,500, nilikuwa nimefanya kazi katika tasnia ya fedha nikiuza bima, dhamana, na kusaidia watu kutoka kwa madeni kwa miaka 34. Kongamano hilo nililohudhuria lilikuwa limeandaliwa na mchuuzi mmoja kati ya wengi ambao kampuni yangu ya kifedha hutumia kuwasaidia wateja wangu na mipango yao ya kifedha. Nilikuwa nimefanya

kazi na mchuuzi huyu kwa miaka 14 na kwa kawaida nilifanya uzalishaji wa kutosha ili kuhitimu kuhudhuria hafla yao ya kila mwaka lakini kufikia wakati huo sikuwa nimewahi kufika daraja la juu.

Uzalishaji wangu wa kawaida ulikuwa takriban milioni 4 kwa mwaka, jambo ambalo liliniweka katika nafasi ya 200 ya ofisi za juu kati ya ofisi 5,000 kote nchini, kwa hiyo sikujisikia vibaya sana kuhusu utendaji wangu, hasa kwa vile nilikuwa na shughuli nyingi. Ili kuingia katika ofisi 10 bora, ingenibidi nizalishe zaidi ya milioni 10 kwa mwaka, na tayari mwezi wa Machi ulikuwa umefika. Sikujua jinsi ya kufika kiwango hicho kabla ya mwisho wa mwaka. Kumbuka, nilikuwa nikizalisha takriban milioni 4 kila mwaka kwa miaka 14!

Lakini mimi na Drenda tulikubaliana kwamba ikiwa Bwana alitaka tuwe pale jukwaani, basi lazima kungekuwa na uwezekano fulani—lakini wakati huo hatukujua kwa jinsi gani. Nilikuwa nikihubiri ibada nne kila wikendi, nilisafiri karibu siku 75 kila mwaka kufundisha katika kongamano, nilifanya vipindi vya televisheni kila siku, nilisimamia wafanyakazi 75, na kuendesha kampuni yangu ya kifedha. Drenda pia alikuwa akifanya kipindi chake cha televisheni kila siku. Ukiongeza watoto na wajukuu wetu watano, maisha yetu yalikuwa yamejaa shughuli kabisa. Mimi na Drenda tulipanda mbegu ya kifedha na tukamwomba Mungu atuonyeshe jinsi ya kufanya kile kilichoonekana kwetu kama kitu kisichowezekana.

Ili kufupisha hadithi ndefu—au niseme, ili kuanzisha hadithi ndefu—majira ya kuchipua yaliyofuata, tulikuwa kwenye jukwaa hilo tukitambuliwa katika daraja la juu, na ndio, tulipokea hundi ya bonasi ya $100,000 pamoja na safari ya kwenda Bora. Bora! Ilikuwa safari ya ajabu na ya kushangaza. Kwa kuongeza,

tulizalisha katika kiwango hiki cha juu kwa miaka sita iliyofuata mfululizo. Haya yote yalifanywa bila kutumia mpango mpya wa uuzaji, hatukuongeza wafanyikazi, hatukuwa na gharama zaidi wala kupata wateja wapya. Hatukujitangaza au kujaribu kutafuta njia ya kufanya mauzo katika miaka hiyo sita. Kwa hivyo nilitokaje katika kiwango cha uzalishaji cha milioni 4 kwa miaka 14 mfululizo hadi zaidi ya milioni 10 chini ya miezi 10 na kudumisha kiwango cha uzalishaji cha kati ya milioni 12 na 15 kwa miaka mitano iliyofuata? Tena, haikuwa matokeo ya kuhudhuria mkutano au kongamano ya mauzo.

Mabadiliko haya yalikuwa ni matokeo ya ndoto niliyokuwa nayo ambapo Bwana alinipa ufunguo ambao ulibadili maisha yangu ya kifedha. Kitabu hiki sasa kimeandikwa miaka sita baadaye kama matokeo ya ndoto ya pili niliyoota ambapo Bwana aliniambia nikiandike. Katika ndoto hiyo, niliona kichwa cha kitabu hiki na sura zake kwa uwazi kana kwamba nilikuwa nimeshika kitabu hiki mkononi mwangu.

Kama mimi, najua kwamba unataka kushinda, kuchukua eneo, na kuruhusu Mungu akutumie kama picha ya ukuu Wake. Ikiwa huo ndio moyo wako, basi kitabu hiki kitakufaa. Ni wakati wa kuharakisha mafanikio yako na kanuni hizi tisa za kuongeza kasi. Tusiache nyuma kazi yoyote ambayo haijakamilika. Nitakapoenda mbinguni, ninataka kujua kwamba nilitimiza kazi yangu, si kuokoka tu bali nilisitawi, kupitia kwa neema ya Mungu. Nataka Mungu aangaze kupitia kwa maisha yangu, na kufanya watu waone kwamba kile kisichowezekana siku zote kinawezekana!

—Gary Keesee

## SURA YA 1

# UNATAKA KWENDA WAPI?

Ulimwengu ni mahali pakubwa! Kuna maeneo mengi mazuri ya kutembelea na kuona, lakini ajabu ni kwamba watu wengi kamwe hawayatembelei. Uchunguzi wa hivi majuzi ambao nilisoma katika jarida la *Forbes* ulisema yafuatayo:

- 11% ya waliohojiwa katika utafiti hawajawahi kusafiri nje ya jimbo walikozaliwa.
- Zaidi ya nusu ya waliohojiwa (54%) wametembelea majimbo 10 au chini ya hapo.
- 13% ya waliohojiwa walisema hawajawahi kusafiri kwa ndege.
- 40% ya waliohojiwa walisema hawajawahi kuondoka nchini Marekani.
- Zaidi ya nusu ya waliohojiwa hawajawahi kumiliki pasipoti. (Kwa miaka mingi mtu hakuihitaji kabla ya kusafiri kwenda Canada, ndiyo sababu kuna idadi hii kubwa).

Nambari hizi zilivutia umakini wangu lakini taarifa ifuatayo ambayo ilipatikana kutoka kwa uchunguzi huu ndiyo iliyonistaajabisha sana: 85% ya waliohojiwa walikuwa na hamu ya kusafiri, na zaidi ya 60% tayari walikuwa na orodha ya maeneo ambayo wangependa kutembelea siku moja. Walipoulizwa kwa nini hawakusafiri wakati walikiri kwamba wangetaka kufanya hivyo, jibu lao lilikuwa rahisi: Hawakuwa na pesa walizohitaji kusafiri. Kwa hiyo, unajua kitakachotokea? Hakuna! Watakuwa watazamaji maishani.

Hivyo ndivyo nilivyolelewa.

Familia yangu haikupenda kusafiri nilipokuwa nikikua. Sikujua hata majina ya miji jirani, sembuse kujua ilikuwa wapi na jinsi ya kufika huko. Ili kukupa kielelezo cha jinsi nilivyokuwa na tatizo la kutosafiri, nitakuambia kuhusu tukio lililofanyika nilipokuwa na umri wa miaka 14.

Nililelewa mashambani katikati ya jimbo la Ohio. Babu yangu alikuwa mkulima, na wazazi wangu walikuwa wamejenga nyumba kwenye ekari chache za shamba lake, jambo ambalo nilipenda kwa sababu kulikuwa na bwawa kubwa karibu na nyumba yetu. Kulikuwa pia na kijito kilichotoka kwenye bwawa letu hadi msituni, ambako ndiko nilikojifunza kukamata na kuwinda wanyama. Nilivua na kutembea siku nyingi karibu na msitu huo! Nilipenda maisha ya mashambani. Ingawa mji wa nyumbani kwetu ulikuwa maili chache tu kutoka mpaka wa jiji la Columbus, sikuwa napenda sana kwenda katika jiji hilo kubwa.

Naam, mwaka huo, mimi na rafiki yangu tuliamua kununua baiskeli za aina ya Schwinn. Sio baiskeli za kawaida tu bali za kasi, na zenye kifaa halisi cha kupima mwendo. Kwa kuwa nilikuwa bado mdogo sana kuendesha gari, nilifikiri kwamba baiskeli ilikuwa kitu cha pekee. Nilihifadhi pesa zangu, na mimi na rafiki yangu tukanunua baiskeli hizo mpya kabisa. Tulikuwa tukiendesha baiskeli hizo juu na chini kwa barabara ya kwetu na pia kwenda shuleni ambayo ilikuwa umbali wa maili moja na nusu.

Siku moja, tuliamua kwamba tulitaka kwenda mahali fulani, safari ya kweli na baiskeli zetu mpya. Tulichukua dola kadhaa kisha tukaelekea barabarani. Takriban maili moja kutoka nyumbani kwetu, tulifika kwenye makutano ya kwanza ya barabara. Nilijua kwamba ikiwa tungeenda kushoto, barabara hiyo ingetupeleka shuleni. Pia nilijua kwamba ikiwa tungeenda upande wa kulia, tungeishia kwenye

mpaka wa kaunti, ambao ulikuwa karibu maili moja na nusu kutoka hapo. Lakini sikujua barabara ilienda wapi baada ya kupita mpaka wa kaunti yetu; sikuwa nimewahi kwenda upande huo hapo awali. Rafiki yangu hakujua ni nini kilikuwa mbele ya mpaka wa kaunti pia, kwa hivyo tuliwaza, *Twende upande wa kulia ili tujue ni kitu gani kiko mbele ya mpaka wa kaunti yetu*. Kwa hivyo ndivyo tulivyofanya: tulienda upande wa kulia, kuelekea mpaka wa kaunti na tulijiona kuwa watu wazima na wenye ujasiri wa kutembelea mahali tusipopajua.

Tuliendelea kwa muda, tukapita mpaka wa kaunti, na kuendelea. Nakumbuka tulipopita mpaka wa kaunti niliwaza, *Vyema kabisa, sasa tunaenda mahali halisi, safari ya kweli*. Tulipoenda mbele tuliona mji mdogo mbele yetu wala hatukujua ni mji gani. Tulipofika karibu na mji huo, tuliona duka ndogo la jumla, na kwa kuwa ilikuwa siku ya joto na tulikuwa na kiu, sote tuliingia kwenye maegesho na kuingia dukani kupata vinywaji tulivyopenda. Katika nyakati hizo za maisha yangu, nilipenda kinywaji kinachoitwa *Mountain Dew*. Oh, na ikiwa wewe ni msomaji mdogo kwa umri, kinywaji hicho wakati huo kiliuzwa kwa chupa, sio kopo, na kilitengenezwa na sukari halisi, si maji matamu ya mahindi kama kinavyotengenezwa leo. Kilikuwa kinywaji bora zaidi!

Tulipokuwa tukilipia vinywaji, tulimweleza keshia yote kuhusu safari yetu na baiskeli na kumuuliza jina la mji huo. Hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa amewahi kusikia jina hilo hapo awali, kisha tukamuuliza tulikuwa umbali gani kutoka kwenye makutano ya barabara ya kwetu huko New Albany. Nakumbuka jinsi nilivyojisikia mjinga aliposema ni maili tano. Maili tano? Hizo tu? Tulikuwa tumesafiri maili tano tu? Tulihisi ilikuwa angalau maili 50! Ijapokuwa tulitambua kwamba hatukuwa tumesafiri mbali, tuliamua kwamba tulikuwa tumeendesha baiskeli vya kutosha kwa siku moja, kwa hivyo tuligeuka, na kurudi nyumbani. Hiyo ilikuwa safari kubwa kwangu. Je, unaweza kufikiria kutojua hata jina la mji uliokuwa maili

chache tu kutoka nyumbani kwenu, mahali ulipolelewa? Familia yetu haikupenda kusafiri.

Ningali nakumbuka nilipokuwa na umri wa miaka 19 nikisafiri kwenda kwa Mto Ohio na rafiki yangu kuvua samaki. Baada ya kujaribu kuvua samaki kwa muda mfupi, dhoruba ilianza kuvuma, kwa hiyo tukaamua kurudi nyumbani. Nakumbuka nilimwomba rafiki yangu ikiwa angekubali tuvuke daraja kuu la Mto Ohio tulipokuwa tukirudi ili niweze kusema kwamba kwa kweli nilikuwa nimeondoka jimbo la Ohio. Hiyo ndiyo iliyokuwa mara yangu ya kwanza kuwahi kufika jimbo la Kentucky. Lo, maisha yangu yalikingwa kama nini nilipokuwa nikikua. Pakubwa yalikuwa mazuri, lakini bila kutambua, yalikuwa maisha ya kurudisha mtu nyuma pia.

Tayari unajua kuwa napenda kukaa nje. Adhabu mbaya zaidi ambayo ungenipa nilipokuwa nikikua ni kuniambia nikae nyumbani. Nilipenda kukaa nje! Nilianza kuwinda nilipokuwa darasa la sita, si kwa sababu baba yangu aliwinda bali kwa sababu babu yangu alipokufa, nilikuwa nikipekua-pekua katika chumba chake cha chini na nikapata sanduku la kadibodi lenye sehemu za bunduki kuukuu ya miaka 65. Nilimuuliza babangu ikiwa ningeweza kuimiliki, naye akakubali, hakufikiri ningeweza kuunganisha bunduki nzima kutoka kwenye sanduku hilo la kile alichofikiri kuwa ni taka. Nadhani alishtuka kidogo siku ile nilipomletea bunduki kamili, na kumwonyesha kwamba nimeitengeneza, na kumwomba ikiwa angefyatua risasi moja ili nione kweli kama ilifanya kazi. Nilishangazwa—niruhusu niseme nilishtuka—alipokubali. Nakumbuka tukio hilo ni kama lilitokea jana.

Alitafuta baadhi ya risasi za zamani ambazo alikuwa nazo. Sikujua kwa nini alikuwa nazo maana hakuwa na bunduki. Katika nyakati hizo, risasi zilitengenezwa na aina fulani ya karatasi, si kama za leo zinazotengenezwa na plastiki. Tulitoka nje tukaenda nyuma ya nyumba, naye akaweka mkebe juu ya kijiti, akarudi nyuma yadi 40

hivi, na kufyatua risasi. Aliupiga risasi mara kadhaa kisha akanialika kuupiga. Baada ya hilo, aliniambia kwa vile nilikuwa nimeiunda kikamilifu, ningeweza kuimiliki, lakini sikuruhusiwa kuitumia bila idhini yake. Nakumbuka nilifikiri babangu alikuwa jasiri sana kuweza kupiga risasi hizo. Hadi leo nina hiyo bunduki.

Bunduki hiyo ilinifungulia ulimwengu mpya. Ulikuwa msimu wa vuli, na mwanzo wa msimu wa uwindaji. Marafiki zangu kadhaa shuleni walikuwa wakizungumza kuhusu kuwinda sungura, na kwa kuwa wakati huo nilikuwa na bunduki yangu, nilitaka kujaribu. Babangu alinishangaza hata zaidi katika msimu huo. Nilizungumza naye kuhusu nia yangu ya kuwinda sungura, naye akaniruhusu nijaribu. Nilishtuka sana!

Wakati huo tulikuwa tunaishi mashambani, na hakukuwa na familia yoyote nyingine iliyokuwa ikiishi karibu nasi. Babangu aliniambia niende nyuma ya nyumba yetu kwenye shamba la babu yangu peke yangu! Alinieleza kuwa sungura walipenda kuishi kando ya safu za uzio, kwamba pia ulikuwa msimu wa kware, na akanikumbusha kwamba wao pia walikuwa huko nyuma. Alasiri hiyo, niliua sungura mmoja na kware mmoja. Niliingiwa na shauku ya kuwinda milele!

Nilijiandikisha katika jarida lolote la uwindaji ambalo ningeweza kujiandikisha. Majarida kama *Outdoor Life, Sports Afield, Field & Stream*, *Fur-Fish-Game*, na mengine machache. Nilifurahia sana kusoma hadithi zote za uwindaji zilizokuwemo. Zamani hatukuwa na duka la bidhaa za michezo au maduka makubwa karibu, lakini tulikuwa na katalogi yenye orodha ya bidhaa ya duka linaloitwa *Herter*. Ilifanana katalogi ya duka lingine la kisasa la bidhaa za michezo linaloitwa *Cabela* na nilivutiwa sana na mambo yote mazuri yaliyokuwemo. Nilikuwa ninapenda kubeba katalogi yangu kwenda shuleni na kuiangalia wakati wa kusoma kibinafsi.

Lakini cha kusikitisha katika hadithi hii ndicho hiki. Majarida haya yalitumwa nyumbani kwetu kila mwezi hadi nikamaliza shule ya upili, na kuendelea kwa miaka minne iliyofuata nilipokuwa nikimfanyia babangu kazi. Kamwe sikupata wazo hata mara moja kwamba, *nitaenda huko ili kufanya kile nilichokiona kwenye jarida hilo*. Hata mara moja! Hilo halikuingia akilini mwangu! Ingawa niliyapenda majarida hayo na kuvutiwa sana nayo, hata baada ya kununua gari langu na kuwa na pesa zangu, sikuwahi kuwa na wazo la kwenda na kuhusika na kile nilichokuwa nikisoma. Unaweza kufikiri, *Maajabu gani hayo*; na ninapotafakari sasa juu yake, nakubali, hilo kweli lilikuwa jambo la kushangaza. Kwa hivyo kwa nini sikuwa na ndoto ya kufanya mambo hayo yote niliyoyasoma, au kutembelea Milima ya Rocky? Ilikuwa rahisi kwangu kwenda huko. Kuna barabara kuu inayopitia Columbus inayoelekea huko moja kwa moja. Lakini sikuwahi hata mara moja kufikiria kuendesha gari kwenda huko. Kwa nini? Hilo ndilo swali linalopaswa kujibiwa.

**Sikujua kamwe kwamba ningeweza kufanya hivyo.**

Sijasema haingewezekana. Nimesema sikuwahi kujua kwamba "mimi" ningeweza kufanya hivyo. Ninajua mawazo yako: *Jamaa huyu ana kichaa kidogo, labda nimepoteza muda wangu kusoma kitabu hiki.* Hebu nifafanue. Akilini mwangu, sikujiona katika hadithi na picha nilizokuwa nikisoma. Kwa sababu wazazi wangu hawakupenda kusafiri na hatukuwa na pesa za kutosha nilipokuwa nikikua, nilikuwa nimejifunza kukataa kabla ya kusema ndio. Mafunzo yangu ya kusema "La" yalikuwa makamilifu kiasi kwamba sikuthubutu hata kufikiria kuwa hilo lingewezekana. Kwa maneno mengine, ilikuwa kawaida kwangu kutupilia mbali uwezekano wa kwenda hata kabla ya kupata wazo kwamba ingewezekana. Ninaelewa kabisa watu ambao mwanzoni mwa sura hii hawakufanya kile walichotamani kufanya. Hebu tena tuangalie matokeo ya uchunguzi ule wa awali.

"Asilimia 85 ya wale waliohojiwa walisema walikuwa na hamu ya kusafiri, na zaidi ya asilimia sitini tayari walikuwa na orodha ya maeneo ambayo wangependa kutembelea siku moja."

Koma hapo! Asilimia themanini na tano walitaka kusafiri, na asilimia sitini tayari walikuwa wameandika maeneo ambayo walitaka kutembelea? Basi kwa nini hawakuenda? Najua uchunguzi ulisema pesa ndio shida. Vema, lakini nasema, "La, hicho ni kisingizio tu; pesa si shida."

Ni kama ule wakati nilipotaka kununua baiskeli mpya aina ya Schwinn yenye mwendo wa kasi. Niliitaka, na nilipata njia ya kufanya kazi ya muda ili kupata pesa za kuilipia. Kila nilipoifikiria baiskeli hiyo, nilijiona nikiiendesha na jinsi ningeifurahia. Kama mimi, kupendezwa na maeneo hayo na yote mazuri yaliyokuwa katika majarida hayo, wahojiwa hao hawakujiona wakitimiza ndoto yao. Ikiwa wangejiona wakisafiri, wangetafuta njia ya kufanya hivyo.

Hebu tuseme ukweli: Nilikuwa na gari, nilikuwa na pesa; na kama pesa zingekuwa shida, ningeweza kupiga kambi katika bustani ya serikali kwa $5 kwa usiku. Cha kusikitisha ni kwamba nilikuwa na umri wa miaka 40 nilipotembelea Milima hiyo ya Rocky mara ya kwanza. Kusema nilijawa na msisimko itakuwa ni kutilia maji ukweli. Lakini ninakumbuka nilipokuwa huko niliwaza, *Kwa nini sikufanya hivi awali?*

Kitabu hiki kinaitwa *Kazi Ambayo Haijakamilika*. Ni kuhusu kwenda mahali ambapo unapaswa tayari kuwa umefika, lakini kama mimi umekuwa ukisitasita. Mafunzo yako ya kukataa yalisema huwezi kumudu jambo hilo, au hujui jinsi ya kulitekeleza, au sababu nyingine mbalimbali ulizotumia kujiambia kwamba wewe ni mtu wa kawaida na wa wastani. Lakini nataka kukukumbusha kile Bwana alichoniambia ambacho nilizungumzia katika utangulizi, "Nataka uwe mmoja wa hao kumi bora. Nataka upate hiyo hundi ya bonasi ya

$100,000. Nataka watu waone ukuu Wangu ndani yako!"

Neno langu kwako ni hili: "Mbona isiwe wewe?"

Nafikiri ni muhimu kabla hatujaingia zaidi katika kitabu hiki, na kabla sijaanza kukufundisha jinsi ya kuharakisha malengo na maendeleo katika maisha yako, kwamba utumie muda mfupi na kujiuliza swali hili:

**"Nataka kwenda wapi?"**

Kabla hujaanza kupuuza jibu lako huku ukichuja kupitia mafundisho yako mwenyewe ya kukataa kabla ya kukubali, hebu nifafanue swali. Sikuulizi utayawezaje au utayalipiaje. Ninakuuliza: "Unataka kufanya nini?" Najua kwamba kile ambacho tumezungumzia kinaweza kuonekana kama zoezi rahisi sana, lakini kinaweka msingi wa kila kitu kinachofuata na kutuleta kwa swali lingine ninalotaka kukuuliza:

**"Je, unataka kufika huko kwa kasi gani?"**

Katika miaka ya 1800, watu hawakuwa na njia nyingi za kusafiri ila kwa farasi. Ikiwa mtu alitaka kusafiri kutoka Mto Missouri hadi Sacramento, kule California, ingemchukua miezi 4 hadi 6 kufika huko. Kawaida basi ilikuwa kusafiri katika kikundi kwa mabehewa yaliyovutwa na farasi, kwa ajili ya usalama na urafiki. Mabehewa hayo yalisafiri umbali wa maili 12 hadi 15 tu kwa siku, jambo ambalo lilifanya safari hiyo kuwa ndefu na ya hatari. Kulikuwa na mito yenye dhoruba kali na milima mirefu ya kuvuka, na, bila shaka, kulikuwa na Wahindi wa kukabiliana nao. Kuanzia mwaka wa 1835 hadi 1855, watu 10,000 walikufa walipochukua safari hiyo ndefu, si kutokana na mashambulizi ya Wahindi bali kutokana na magonjwa au ajali, na ndio, karibu asilimia 4.2 ya watu walikufa kutokana na mashambulizi ya Wahindi.

Tuseme umeona brosha ya hivi punde ya mauzo ya mabehewa yenye picha zinazometameta, kisha inasema, "Watu 10,000 wamekufa

katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, na tunajivunia rekodi yetu ya kupoteza asilimia 4 pekee ya wasafiri kwa sababu ya mashambulizi ya Wahindi." Je, unafikiri ni watu wangapi wangejisajili kwa hilo? Takwimu hizo zinaweza kukufanya ufikiri kwamba hakuna mtu mwenye akili timamu angeweza kuchukua safari kama hiyo, lakini utakuwa umekosea. Mamia ya maelfu walichukua safari hiyo. Nafikiri tunaweza kukubaliana kwamba ilikuwa safari ya hatari, lakini kwa nini walijihatarisha hivyo? Jibu rahisi ni kwamba walikuwa wakitafuta maisha bora, maisha mapya ya baadaye. Kwa kweli hawakuwa tofauti na wewe, lakini walikuwa na hamu kubwa ya mabadiliko, na ndoto hiyo ilikuwa kubwa kuliko shida yoyote ambayo wangeweza kukutana nayo njiani.

Njia nyingine bora ya kusafiri ilikuwa kwa mashua, na wengine katika enzi hiyo wangesema ilikuwa bora zaidi kwa sababu ya ustarehe wake. Ninazungumzia kupitia Panama; na la, sizungumzi kuhusu Mfereji wa Panama bali Panama yenyewe. Ungeanza safari yako kwa meli na kusafiri hadi upande wa mashariki wa Marekani kisha kuelekea Amerika ya Kati hadi Panama. Kisha ungeshuka kutoka kwa meli na vitu vyako na kuvuka sehemu nyembamba ya Panama hadi Bahari ya Pasifiki, kisha ungerudi kwenye meli nyingine na kuelekea California. Safari hiyo ilichukua miezi minne.

Sasa, ikiwa hukupenda nyoka wenye sumu na wazo la kufa kutokana na malaria, au magonjwa mengine mengi ambayo yangeweza kukuua, basi ungeweza kuzunguka ncha ya Amerika Kusini. Walakini, meli nyingi ambazo zilijaribu kufanya hivyo hazikufanikiwa kwani kulikuwa na dhoruba za kutisha karibu na Cape Horn.

Ni hizo tu. Njia hizi za kusafiri ambazo nimetaja ndizo zilizotumiwa katika miaka ya 1800 hadi reli ilipojengwa na kuwezesha watu kupita mabara katika usafiri. Njia hiyo ya reli ilileta mabadiliko ya kweli. Badala ya kuchukua miezi minne kusafiri kutoka Missouri

hadi California, mtu angeweza kufika kwa juma moja! Hebu tukome na tutafakari hili—miezi minne au juma moja? Je, ungechagua ipi? Nafikiri chaguo ni dhahiri.

Bila shaka, sasa kuna barabara kuu za magari za kisasa zinazofanya muda wa kusafiri nchi nzima kuwa masaa 42 tu. Na usafiri wa kisasa wa ndege hupunguza masaa hayo hata zaidi hadi masaa manne hadi matano. Kwa hivyo unataka kwendaje? Ingawa usafiri wa anga ni wa haraka sana, ailimia 50 hadi 60 ya Wamarekani hawasafiri hata mara moja kwa mwaka. Mmarekani wastani husafiri kwa ndege mara 1 hadi 1.5 kwa mwaka.

Na, ndio, ikiwa ningetaka kusafiri Amerika nzima, ninaweza kufanya hivyo na baiskeli yangu, ambayo kawaida itanichukua takriban siku 65. Ingawa nisingeita hiyo njia ya kusafiri lakini safari kwa hiari.

Lakini hebu nitoe hoja yangu hapa: Zaidi ya nusu ya watu katika taifa hili hawasafiri kwa ndege hata mara moja kwa mwaka! Bado wako katika miaka ya 1800 huku wakisafiri kwa magari, mashua, na baiskeli. Na hiyo ni sawa ikiwa una wakati. Na inaonekana wana wakati!

Kulingana na uchunguzi wa hivi majuzi, 50% ya Wamarekani hutumia masaa matano hadi sita kwenye simu zao kila siku, bila kujumuisha matumizi ya simu yanayohusiana na kazi. Asilimia nyingine 22 hutumia kati ya masaa matatu hadi manne kwa siku kwenye simu zao.

**Swali ni je, hii ni kwa sababu wana muda au hawana maono?** Acha nizungumzie wakati hapa kwa muda mfupi tu. Takwimu hapo juu zinatuonyesha ni muda gani tunaopoteza katika maisha yetu ya kila siku. Tunafikiri tuna wakati mwingi duniani, lakini hatuna. Sote tuna ratiba fupi sana katika ulimwengu huu ya kukamilisha mambo. Sote tuna tarehe ya kuanza na ya mwisho ya maisha yetu. Kinachotokea kati ya tarehe hizo huamua ikiwa kweli tuliishi maisha yetu kwa kutanguliza

mambo yanayofaa na kutimiza kazi zetu tulizopewa na Mungu.

Hivi sasa, unaposoma ukurasa huu, unapiga hatua. Dunia inazunguka kwa maili 1,042 kwa saa, na dunia yenyewe inazunguka jua kwa maili 67,000 kwa saa. Mfumo wa sayari yetu unazunguka galaksi yetu ya Milky Way kwa mwendo wa maili 483,000 kwa saa. Lakini bado, unahisi kana kwamba hausogei hata kidogo.

Unajua, wakati haupo pasipo vitu vinavyosonga. Unaposafiri kwa futi 36,000 katika ndege ya kisasa, huhisi kwamba unasogea kwa kasi hata kidogo unapotazama mandhari ikisogea polepole chini yako. Lakini ndege inapoanza kushuka na kukaribia kutua kwa uwanja wake, huwa inaonekana kwamba mnaongeza kasi na ardhi iliyo chini yenu inasonga kwa kasi zaidi. Lakini hakuna kasi hata kidogo. Sasa unakuwa na mtazamo mpya wa kutathmini kasi yako. Na ndege yako inaposhuka juu ya kibarabara chake cha kupaa na kutua, unahisi virahisi kwamba inaenda kwa kasi sana.

Na ndivyo ilivyo katika maisha yetu. Bila malengo, bila kusudi, hakuna kitu cha kutathmini maendeleo yetu. Hebu niseme hivi:

**Bila kusudi, hakuna dharura!**

Kusudi hudhirisha mwelekeo na kuongeza shauku ya kufika mahali fulani. Kuendesha gari kwenda safari ya umbali wa maili 1,400 kinakuwa kitu kisichofaa wakati kusudi letu linahitaji suluhu la haraka, kama ndege. Kitabu hikikinahusu kuongeza kasi, lakini hakina thamani isipokuwa una marejeleo fulani ambayo yanaleta hitaji la uharaka katika maendeleo yako.

Takwimu nilizotoa kuhusu matumizi ya simu zinanionyesha kuwa watu wengi hawana dharura yoyote, hawana kusudi au shauku ya kuingia katika utele wa siku zao za usoni haraka. Kwa sababu moja au nyingine, wanaridhika kuwa

**KUSUDI HUDHIRISHA MWELEKEO NA KUONGEZA SHAUKU YA KUFIKA MAHALI FULANI.**

watazamaji katika mchezo wa mpira wa maisha, wanaketi mbele ya skrini kutazama wapenzi wawili wakionyeshana upendo lakini hawajihusishi wenyewe katika hilo au kujua furaha ya busu la kweli.

Kiashiria halisi cha afya ya shauku yako ni kujiuliza unafanya nini. Acha niseme hivi: Kile unachofanya kinaonyesha mahali unapoelekea. Ikiwa ungependa kuwa mpiga kinanda mzuri, hutapoteza masaa matano hadi sita kwa siku kwenye kifaa chako. Ninachoona ni kwamba watu wengi hawana uharaka na hukosa kunyakua fursa nyingi zinazoweza kubadilisha maisha yao. Kwa nini? Kwa sababu hawaoni fursa hizo.

Umewahi kuandaa *hamburger* (vipande viwili vya mkate vilivyo na nyama ya kusagwa ndani yake)? Nina hakika umefanya hivyo maana ni rahisi sana kuandaa. Naam, aliyeanzisha mkahawa wa chakula hiki ambaye jina lake ni McDonald alichukua dhana hiyo rahisi ya kupika *hamburger*, na kuifanya kuwa himaya. Sidhani kuna *hamburger* bora kuliko ile inayotengenezwa na mkahawa huu unaoitwa McDonald. Sasa uko katika mataifa na maeneo 120 duniani kote na wanahudumia wateja milioni 68 kila siku! Wanaendesha mikahawa 36,899 ulimwenguni kote na wameajiri zaidi ya watu 375,000.

Vipi kuhusu mkahawa mwingine wa sandwichi unaoitwa *Subway?* Karibu kila mtu anajua kutengeneza sandwichi ndogo, lakini sasa kuna mikahawa 42,431 katika nchi 108.

Kampuni ya usafiri Uber ilianzishwa mnamo 2009, miaka 13 tu iliyopita, na mnamo 2021 ilikuwa na thamani ya dola bilioni 86. *Uber* ilianzishwa na watu wawili ambao kusudi lao halikuwa ili waweze kupata njia rahisi ya kusafiri. La, walianzisha *Uber* wakiwa na mawazo ya kuleta mapinduzi katika usafiri. Ndani ya miaka 12 tu walikuwa wameingia katika nchi 80!

Je, makampuni haya yamewezaje kufaulu hivi? Kwa ufupi, hawakuanza wakiwa na lengo la kutengeneza *hamburger* tu. Kwa nini

nataja makampuni haya? Ni wazi, itabidi ukubali kwamba walifahamu vyema wakati na uharaka. Walikuwa na mpango.

Leo, vijana wengi hutafuta kazi katika mikahawa ya McDonald ili kupata pesa za muda tu. Ni hatua kuelekea mahali pengine, lakini wakiwa huko, huwa hawakomi kushangaa na kujifunza jinsi mikahawa hii ilivyofanyika kile ilicho leo. Wanapaswa kuandika maelezo juu ya jinsi wanavyoendesha biashara yao na kwa nini. Hilo linaweza kuwatumikia kwa njia bora kuliko elimu ya chuo kikuu.

Hiki ndicho kilichompata Cordia Harrington, mama wa wavulana watatu ambaye hakuwa na mume, na alikuwa akifanya kazi kama wakala wa mali huku akijaribu kutafuta eneo thabiti zaidi la kufanya kazi. Aliwaza kwamba kujiunga na kampuni ya McDonald kama mmiliki wa mkahawa mmoja kungeweza kumpa muda zaidi wa kukaa na watoto wake. Aliishia kumiliki mikahawa mitatu. Wakati huo, kampuni ya McDonald ilikuwa katika harakati za kupanga kufungua mahali pengine pa kuoka mikate, na Cordia aliwekwa kwenye kamati ya kupanga hilo. Kazi yake ilikuwa kutoa maoni yake juu ya mikate ambayo McDonald ililisha mamilioni ya watu, ladha yake na jinsi ilivyoitengenezwa. Aliandika maelezo mengi.

Ingawa alikuwa akifanya kazi ya kusaidia kampuni ya McDonald na mradi wao wa mikate, alikuwa akijiandikia maelezo kwa siri. Alihisi angeweza kujenga mahali bora pa kuoka mikate kuliko pale walikuwa wanataka kujenga. Aliwasilisha mipango yake kwa kampuni hiyo nao wakakataa. Lakini baada ya miaka minne na baada ya kumhoji mara 32, waliamua kununua mikate yao kutoka kwake. Shida ilikuwa bado hakuwa na duka la kuoka mikate na ilimbidi kukopa pesa za kulijenga, jambo ambalo alisema karibu limfilisishe kabisa. Ili kufupisha hadithi ndefu, mkate unaotumiwa leo katika mikahawa kama McDonald, Chili's, Ruby Tuesday's, KFC, na Pepperidge Farm iliokwa katika duka lake la kuoka mikate, Tennessee Bun Company.

Inajulikana kama kampuni ya kuoka mikate inayojiendesha kwa kasi zaidi ulimwenguni, na inaoka bidhaa milioni 9 kila siku na ina wateja 1,500. Ndio, umesoma vyema!

Kama unavyojua hadithi hizi huwa hazitokei tu, bali ili kufanikiwa bidii na maono vinahitajika. Nafikiri utakubali kwamba Cordia alikuwa na shauku na uharaka kuhusu ndoto yake. Hakutaka kupoteza muda. Kwa hivyo, hebu turudi kwa sababu iliyokufanya usome kitabu hiki. Turudi kwenye swali lile la kwanza kabisa.

**Unataka kwenda wapi?**

Jibu la kweli kwa swali hili linaweza kujumlishwa na neno—kutaka. "Unataka" kwenda wapi? Zamani, mafundisho yako ya kukataa kabla ya mafunzo kukubali yalikufungia katika maisha ya unusuru na ya wastani. Lakini sasa, una chaguo. Hebu tusome tena majarida yetu ya *Outdoor Life* lakini wakati huu tukiwa na ufahamu kwamba tunaweza kufanya yale yaliyo humo, tunaweza kusafiri. Jione ndani ya picha hiyo. Jiruhusu kuwa na ndoto!

## SURA YA 2

# WATUMWA HAWAOTI NDOTO!

Naamini umetafakari zaidi kuhusu nilichosema katika sura iliyopita kuhusu mahali unapotaka kwenda. Inaonekana kwamba watu hukimbia hapa na pale kisha wanasimama kwa sababu ya kuchoka, na kutambua kwamba hawajapiga hatua yoyote kwenda mbele. Kitabu hiki kinahusu kuongeza kasi, na mwanzo wa mchakato huo wote ni kuwa na mwelekeo kabla ya kuanza safari. Bila shaka, ninajua kwamba mara nyingi, hatujui tunakotaka kwenda. Tena, najua hiyo ni kwa sababu ya mafunzo yetu ya kukataa kabla ya kukubali. Hatujiruhusu kuwa na ndoto au, kama nilivyosema hapo awali, kujiona katika ile picha ya maisha yetu ya usoni.

Mimi na Drenda tulipokuwa na madeni ya kutisha nami nilikuwa nikivamiwa na mshtuko wa hofu na kutumia dawa za kupunguza huzuni, kwa kweli sikufikiria sana nilikotaka kwenda. Sikujali. Nilitaka tu kuishi kwa angalau wiki moja zaidi. Lengo langu lilikuwa kumudu kulipa kodi kwa mara nyingine, kununua mboga, na kulipia matumizi mengine kama umeme kabla haujakatwa. Huu ndio msongo wa mawazo watu wengi wanaoishi nao; wako na mshahara mmoja tu mbali na kutokuwa na makazi. Hakuna usalama katika hilo. Biblia inataja jambo hili katika kitabu cha Mithali.

> *Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.*
>
> —— Mithali 22:7

Watumwa hawaoti ndoto; ndoto yao ni kukoma, si kwendelea mbele. Watumwa hawana chaguo. Wanaambiwa cha kufanya. Nina hakika labda umesikia kilio cha utumwa wa nyakati za leo: "Lazima niende kazini." Inasemekana kwamba zaidi ya 80% ya Wamarekani hawapendi kazi zao, na 33% wanazichukia. Kwa nini? Ni kama vigingi vya mraba katika mashimo ya pande zote; havifaani. Hawafanyi kazi wanayoipenda bali ili kulipwa mshahara, huku wakiwa na mtazamo wa kuishi maisha ya unusuru. Kwa sababu hiyo, sisi ni wagonjwa kihisia.

Umewahi kusikia mtu akisema, "Ole wangu! lazima niende kuvua samaki leo?" Sidhani. Ana fursa ya kwenda kuvua samaki. Je, si ingekuwa vizuri kama ungependa kazi yako kama unavyopenda shughuli zako za burudani, ikiwa ungeweza kusema, "Jumatatu itakuja lini?" Tena, kwa watu wengi, hivi sivyo jinsi maisha yao yalivyo. Je, si ingekuwa vizuri kama ungependa kazi yako kama unavyopenda shughuli zako za burudani, ikiwa ungeweza kusema, "Jumatatu itakuja lini?" Tena, kwa watu wengi, hivi sivyo jinsi maisha yao yalivyo. Lakini hivyo ndivyo unavyopaswa kuwa maana ndivyo Mungu alivyokuumba. Alikupa talanta na uwezo wa kipekee na akakuumba kufanikiwa katika kusudi lako na yale uliyo na shauku kufanya. Kulipa bili kumechukua nafasi ya maono ya watu wengi. Utumwa sasa ndio mtindo wa maisha wa Marekani, huku madeni yakiteka nyara uhuru wetu na kutufanya tukate tamaa katika kutimiza ndoto zetu.

Ikiwa unajua hadithi yangu kutokana na kusoma vitabu vyangu vingine, basi utakumbuka niliishi hivi kwa miaka tisa—miaka tisa ya maisha ya kuzimu kifedha. Nilikuwa nikiishi kana kwamba nilikuwa yatima asiye na baba wala nyumba. Sikuwa na usalama wowote. Rundo la bili lilikuwa kubwa, na simu za kila siku za kujaribu kupata kutoka kwangu kile ambacho sikuwa nacho hazikukoma. Nilikuwa nimekopa kutoka kwa wazazi wangu, wazazi wa mke wangu, maduka ya wakopeshaji, na mtu yeyote ambaye ningeweza kukopa. Nilikuwa

na kadi 10 za mkopo ambazo nilikuwa nimetumia kupita kiwango, madeni ya ushuru, mikopo kutoka kwa kampuni za fedha, deni la gari na kodi ya nyumba ambayo sikuwa nimelipa. Hali yangu ilikuwa mbaya sana kiasi kwamba hofu ilitawala maisha yangu, na hata niliogopa kuondoka nyumbani kwangu. Nitakubali kwamba kulikuwa na mara nyingi, kabla ya kupata ufahamu mzuri niliuliza, "Mungu, uko wapi katika haya yote?"

Watu wanaposikia hadithi yetu, mara nyingi wao husema, "Vema, lilikuwa jambo jema kwamba ulikuja kwa Kristo kupitia hayo yote." Lakini wengi hawaelewi kwamba mimi na Drenda tayari tulikuwa Wakristo wakati huo wote. Nilikuwa na digrii ya theolojia ya Agano la Kale na kwenda kwa chuo cha Biblia kwa mwaka mmoja. Tulikuwa washirika wa kanisa kubwa ambapo nilisikia kuhusu ahadi za Mungu kila juma, lakini kulikuwa na hitilafu mahali fulani. Wakati huo tulikuwa tunaishi mashambani katika nyumba nzee ya mwaka wa 1853. Kila kitu chetu kilikuwa katika hali mbaya. Tuliokota zulia iliyokuwa kwenye chumba cha wavulana kando ya barabara. Tuliokota magodoro yao kutoka kwa rundo la taka la makao ya wazee. Vifaa vyetu vilikuwa na umri wa zaidi ya miaka 20, na magari yetu hayakufanya kazi vizuri.

Kila siku tulikuwa na dhiki ya kifedha na shinikizo. Nilitia bidii katika kazi yangu ya mauzo, lakini kile tu nilichofaulu kufanya ni kutunusuru mpaka wakati nilipofika mwisho. Sikuwa na chaguo lingine wala fedha zaidi kutoka kwa familia na maduka ya ukopeshaji, hatukuwa na vitu tena vya kubadilishana kwa maduka ya ukopeshaji ili kupata pesa, na hatukuwa na mahali pengine tena pa kukopa. Nilikuwa nimezungumza kwa simu na wakili ambaye alikuwa akitishia kunishtaki, na kwa mara ya kwanza, nilitambua kwamba nilikuwa nimefika mwisho. Wakati huu sikuwa na njia ya kuepuka hali hiyo.

Nilipanda orofa kwenda kwa chumba changu nikiwa na machozi, nikalala juu ya kitanda, na kumlilia Mungu anisaidie. Sikujua la kufanya.

Najua unachofikiria: *Yaani ulingoja miaka tisa kabla ya kumwomba Mungu msaada?* Bila shaka la. Lakini wakati huu, nilikuwa mtupu wala sikuwa na suluhu nyingine niliyojitengenezea. Miaka yote hiyo, nilikuwa nikiegemea mfumo wa ulimwengu kunifanikisha. Lakini sasa, hakukuwa na kitu. Nilipokuwa nimelala kitandani mwangu nikimlilia Mungu, nilifanya hivyo kutoka moyoni mwangu. Ilinipasa kusikia kutoka Kwake. Alikuwa ndiye tumaini langu pekee. Na ghafula nilisikia sauti Yake kwa urahisi. Haikuwa sauti iliyosikika, lakini ilikuwa halisi kana kwamba ilikuwa ya kusikika. Aliniambia kwamba nilikuwa katika hali hiyo ngumu kwa sababu sikuwa nimewahi kuchukua wakati wa kujifunza kuhusu utendaji wa Ufalme Wake.

Lazima nikubali kwamba sikujua alichomaanisha aliposema hivyo. Kama nilivyosema tayari, nilijifunza jinsi Ufalme Wake ulivyofanya kazi kwa miaka mitano; sivyo? Lakini neno Ufalme lilikamata usikivu wangu. Alimaanisha nini na hilo? Halikuwa neno nililotumia mara nyingi. Lakini jambo moja lilikuwa hakika: siku hiyo ningejua alichomaanisha. Niliteremka moja kwa moja hadi kwa Drenda. Tulishikana mikono na kuomba kwamba Mungu atuonyeshe alichomaanisha, na tukatubu kwa kujiingiza kwa janga hilo la kifedha. Vema, ili kufupisha hadithi ndefu, Mungu alianza kutufundisha alichomaanisha, na hilo lilibadili maisha yetu yote kabisa.

Kwa kutumia kile alichonionyesha, tuliweza kutoka kwa madeni kabisa katika miaka miwili na nusu. Alituonyesha jinsi ya kuzindua kampuni kadhaa mpya, na tukaanza kufanikiwa kwa njia ambayo sikuwahi hata kufikiria ingewezekana. Tulijenga na kulipia nyumba ya ndoto yetu kwenye zaidi ya ekari 55 za kupendeza. Tulikuwa na vifaa vipya vizuri vya chuma cha pua, sakafu za mbao ngumu, nyumba yetu ilikuwa na mapambo, na zaidi ya futi za mraba 7,000 za nafasi ya familia na ofisi yetu ya kuendesha biashara yangu. Siwezi kukuambia jinsi tulivyosisimka kuona utendaji wa Ufalme maishani mwetu. Tulianza

kulipia magari yetu pesa taslimu na chochote kingine tulichohitaji. Tuliwekwa huru. Badiliko kubwa zaidi lilikuwa kwamba tuliweza kuwa wakarimu na kuanza kusaidia katika kazi ya Ufalme wa Mungu kadri alivyokuwa akituongoza. Tuliacha kuwa na mtazamo wa kutoa mamia ya dola na badala yake kuanza kuwa na mtazamo wa kutoa mamia ya maelfu ya dola.

Hakika maisha yetu yalibadilika sana. Lakini pengine badiliko moja, ingawa halikuwa kubwa zaidi ni kwamba mimi na Drenda tulipata uwezo wa kuota tena. Sio tu ndoto ya kutochelewa kulipa malipo ya rehani ya mwezi uliokuwa ukifuata bali ndoto za kusudi la maisha yetu. Tulitaka kuwasaidia watu wajifunze yale tuliyojifunza, jinsi tulivyopata uhuru.

Ikiwa una nia ya kusikia hadithi yetu yote na kile ambacho Mungu alitufundisha kuhusu Ufalme, nimeandika mfululizo wa vitabu vitano vyenye mada hii ya "Mapinduzi Yako ya Fedha." Ningependekeza sana upate vitabu hivi vitano. Kumbuka, nilikuwa na madeni na sikuwa na tumaini kwa miaka tisa mirefu, lakini leo mimi ni milionea. Hilo halikutokea tu; sisi sio wema kiasi hicho. Unahitaji kujua jinsi hilo lilivyotokea na yote ambayo Mungu alituonyesha mimi na Drenda. Kwa hivyo, pata nakala ya vitabu vyote. Vitakufundisha jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi kupitia kwa sheria na kanuni ambazo utahitaji kujua. Pata maarifa kutoka kwa mtu ambaye amepitia jambo hili, akapata shahada, na kutamani kwamba hangelipitia. Habari njema ni kwamba sio lazima upitie jambo hili pia. Pata seti nzima katika garykeesee.com.

Sawa, imetosha kuhusu vitabu vyangu. Hebu nirudi katika sababu iliyonifanya niseme yale ambayo nimesema. Mwanzoni mwa sura hii nilitoa kauli kwamba wakati mimi na

Drenda tulikuwa na madeni mengi, kamwe sikufikiria nilikuwa nikielekea wapi. Tulipenda sana kukataa hakukuwa na nafasi ya kusema

**KAMWE HUTAWAHI KUGUNDUA WEWE NI NANI NA KILE ULICHOUMBWA KUWA HADI UTAKAPOSHUGHULIKIA SUALA LA FEDHA.**

ndio! Kwa hivyo, ninaelewa kabisa ikiwa sasa hujui unakoenda au unakopaswa kwenda, lakini najua ungependa kujua mwelekeo huo—na unahitaji kuujua. Kwa hivyo, hebu nikwambie kauli rahisi ambayo mimi na Drenda tumekuwa tukitoa kwa miaka mingi:

"Kamwe hutawahi kugundua wewe ni nani na kile ulichoumbwa kuwa hadi utakaposhughulikia suala la fedha."

Hadi utakaposhughulikia suala la pesa, kimsingi wewe ni mtumwa wa unusuru. Kama nilivyosema hapo awali, watumwa hawana ndoto kubwa. Nguvu zao zote ziko katika kuwafanyia wengine kazi. Ndoto yao ni kukoma, wala sio kwendelea mbele. Maono yanahitaji riziki; kusudi la riziki ni maono. Tafakari juu yake. Kusudi la riziki ni maono. Watumwa hawana maono. Wanafanya kile wanachoambiwa tu. Kwa hivyo, jambo bora zaidi unaloweza kufanya ili kuanza kujua mahali unapotaka kwenda ni kuanza kupanga pesa zako na kutoka kwenye deni.

Mara tulipotoka kwa madeni, ajabu, mimi na Drenda tulipata kila aina ya mawazo kuhusu kile ambacho tungeweza na kutaka kufanya. Tulizindua kanisa, tulianzisha vipindi vya kila siku kwenye televisheni, tulijenga jengo lenye thamani ya mamilioni ya dola, na kuzindua shule. Tuliandika vitabu na kuvitafsiri katika lugha nyingi ili kuwahubiria watu habari njema ya Ufalme wa Mungu ulimwenguni kote. Hatujakoma kupata dhana. Itakuwa vivyo hivyo kwako utakapoanza kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi, utaanza kuwa na ndoto, na kuacha kuwa mtazamaji maishani. Anza kujiona ukiwa ndani ya picha.

Kama nilivyosema katika utangulizi, kitabu hiki kilitokana na

ndoto niliyoota mwaka wa 2016. Katika ndoto, niliona kitabu hiki, sura, na mada yake. Mungu aliniambia niandike kitabu hiki kuhusu kanuni tisa za kuongeza kasi ambazo alinifundisha. Katika ndoto, nilielewa kwamba Mungu alitaka nikiandike ili kuwasaidia wafanyabiashara Wake kunyakua kile walichoitwa kunyakua. Sasa, usikose kunielewa vyema. Kitabu hiki ni cha kila mtu. Lakini katika ndoto, nilihisi kwamba ingawa Mungu alikuwa amewapa watu Wake wengi dhana na maono ya biashara, hawakuwa wakinyakua manufaa yote ambayo Mungu alikuwa amekusudia wawe nayo kutoka kwa biashara zao. Na alisema kwamba wafanyabiashara hawa walijua walipaswa kufaulu hata zaidi lakini walichanganyikiwa kwa sababu haikuwa hivyo. Alisema walijua kulikuwa na mambo zaidi lakini hawakuwa na uhakika jinsi ya kuyafikia, na kitabu hiki kingewasaidia kutimiza hilo! Unaweza kusema, "Naam, ulikuwa na ndoto mnamo 2016, na hii ni 2022. Kwa nini imechukua muda mrefu hivi?" Hili ni swali zuri. Niliomba kuhusu jambo hili tangu 2016, na sikupata idhini ya kukiandika kutoka kwa Roho wa Mungu. Badala yake, nilihisi nilipaswa kumaliza mfululizo wa vitabu vyangu vitano *Mapinduzi Yako ya Fedha* kwanza. Haijalishi kanuni hizi tisa za kuongeza kasi ni kuu kiasi gani, utahitaji kuuelewa Ufalme ili kufaidika nazo kikamilifu.

Dhana na funuo katika kitabu hiki zilianza katika maombi asubuhi ya Septemba 9, 2009. Nilikuwa nikifundisha jioni moja huko Alabama katika kanisa fulani kabla ya tukio hili kutokea. Ulikuwa mkutano mzuri, lakini nilikuwa na msukosuko. Mgogoro wa kifedha duniani ulitokea mnamo 2008 na bado ulikuwa ukiendelea mnamo 2009, na nilikuwa na masuala makubwa ambayo nilikuwa nikikabili. Chuo chetu, tunachokiita *The Now Center*, awali kilikuwa mradi wa dola milioni 5.2, ambao ulijumuisha mkopo kutoka kwa benki yetu na dola zetu binafsi milioni 2.5 tulizokuwa tumehifadhi. Mjenzi wetu alikuwa rafiki wa familia yangu, maana alikuwa ametujengea nyumba yetu ya

kibinafsi miaka kadhaa awali. Labda unakumbuka kwamba bei za bidhaa zilipanda sana mwaka wa 2008 na 2009. Bei ya chuma ya pua ambayo tulikuwa tukitumia katika jengo letu ilipanda kwa asilimia 300 juu ya zabuni, lami ilipanda sana kwamba ikawa nafuu kutumia saruji, mafuta yalipanda hadi $140 kwa pipa, na kadhalika.

Naam, ongezeko hilo la bei lilituweka karibu dola milioni moja juu ya bajeti. Maana tayari tulikuwa katikati ya mradi na karibu kumaliza, benki ilisema kwamba kutupa dola milioni ya ziada haikuwa shida; na walitupa mkopo kwa dola milioni za ziada.

Labda unakumbuka idadi kubwa ya madeni ya rehani ambayo hayakuwezwa kulipwa na wakopaji wakati huo na jinsi benki zilivyojikuta katika matatizo makubwa. Kwa kweli, mfumo wa benki ulikuwa karibu kusambaratika. Sikuwa nimesikia chochote kutoka kwa benki yetu wakati wa mgogoro huo, na nilifikiri kwa sababu mkopo wetu tayari ulikuwa umeanzishwa na tulikuwa tumefanya kila malipo kwa wakati ufaao hakukuwa na wasiwasi yoyote. Lakini siku ambayo nilisoma jarida la mtaa wetu na kuona kwenye ukurasa wa mbele kwamba benki yetu ilikuwa imeuzulu watu 550 na kuacha kukopesha, sikuwa na uhakika tena. Hakika, walinipigia simu wakasema kwamba hawangetupatia pesa za mkopo zilizokuwa zimesalia.

Shida ilikuwa kwamba mjenzi, rafiki yetu, tayari alikuwa ametumia dola zake milioni, akiamini kwamba tungemrejeshea kupitia kwa mkopo huo. Ninakumbuka siku alipokuja kuchukua dola zake milioni, ilitubidi tumwambie kwamba benki ilikuwa imekataa kutupatia pesa hizo na hivyo hatukuwa nazo. Alishtuka sana na kuwa na wasiwasi maana alihitaji kuwalipa wachuuzi wake wote na wafanyikazi wake pia. Lakini kama mwamini, alijua kwamba sisi sote tulihitaji kusali kuhusu jambo hilo na kumwamini Mungu ili tupate jibu. Kwa hivyo, asubuhi moja nilipokuwa Alabama, baada ya kuwa na mkutano wa jioni, nilianza kuomba kuhusu hali hiyo tena.

Pia ulikuwa msimu ambapo Mungu alikuwa amenena nami nianze kufundisha kwenye televisheni kuhusu Ufalme Wake. Kweli, sikujua chochote kuhusu huduma ya televisheni isipokuwa kwamba ilikuwa ghali sana, na sikujua jinsi ningepata $300,000 zilizohitajika kufanya hivyo juu ya kila kitu kingine nilichokuwa nikikabiliwa nacho. Mungu aliponiongoza kuanzisha huduma ya televisheni, aliweka wazi kabisa kwamba angeleta pesa za kufanya hivyo. Nilikuwa na neno Lake kuhusu mradi huo, lakini nitakubali, ilikuwa vigumu wakati mwingine kuzingatia kile alichosema nilipoona hakukuwa na ushahidi kwamba pesa zilikuwa zikija. Ilibidi nijikumbushe mara kwa mara kile alichosema ingawa siku zingine mawazo yangu yalikuwa yakipiga kelele kutafuta suluhu.

Kwa hivyo, asubuhi nilipoamka nilikuwa na mengi mawazoni mwangu. Niliomba kupata majibu na mwelekeo, nikijua niliporudi nyumbani, ingenibidi kufanya maamuzi muhimu na nilihitaji mpango wa utekelezaji. Nilipokuwa nikiomba asubuhi hiyo, ghafla, Bwana alizungumza nami na kusema, "Soma Waebrania 11:32-33." Nikawaza, *Vema, nafikiri najua Maandiko hayo*, lakini kwa utiifu, nilifungua Biblia yangu na kusoma mistari hiyo miwili.

> *Nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni na Baraka na Samsoni na Yeftha na Daudi na Samweli na za manabii; ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi.*
>
> —Waebrania 11:32-33a

Nilipokuwa nikitazama Maandiko, ghafla, macho yangu yalifunguliwa. Sura ya kumi na moja ya Waebrania ni orodha ya watu mashuhuri waliofanya matendo makuu kwa uwezo wa Mungu. Mwandishi wa Waebrania alipokaribia mwisho wa sura, alisema,

"Sina wakati wa kuendelea na kuwaambia yote kuhusu watu wengine waliokuwa na hadithi kuu. Lakini hebu nikuambie jinsi walivyofanya" (maneno yangu). Hili ndilo lililovutia umakini wangu, sentensi hii ya mwisho, mstari wa 33.

> *Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi.*

Hapa kuna kanuni fupi na rahisi sana ya jinsi ya kupokea ahadi za Mungu. Nilipoitazama, nilitambua kwamba Mungu alikuwa anajibu sala yangu. Alikuwa akinionyesha cha kufanya, jinsi ya kupata kile kilichoahidiwa. Kwa hivyo, hebu tuangalie aya hii ili tujue ni nini hasa alikuwa akiniambia.

Jambo la kwanza ambalo mwandishi wa Waebrania alitaja ni "kwa imani." Nafikiri kila mtu anayesoma kitabu hiki labda anafikiria, *Sawa, nina imani, sio shida.* Naam, nilifikiri nilijua imani ni nini pia—lakini mambo yalipozidi kuwa magumu, niligundua kwamba sikujua imani ilikuwa nini hasa, jinsi ya kupata imani, na kwa nini inahitajika kabla Mungu hajatenda jambo ulimwenguni. Imani ni muhimu kadiri gani? Naam, ilikuwa namba moja katika ile orodha ya Waebrania 11:33, kwa hivyo ukitaka kupata kile ulichoahidiwa, nafikiri ni bora uhakikishe unajua imani ni nini na jinsi ya kujua ikiwa una imani.

**...UKITAKA KUPATA KILE ULICHOAHIDIWA, NAFIKIRI NI BORA UHAKIKISHE UNAJUA IMANI NI NINI NA JINSI YA KUJUA IKIWA UNA IMANI.**

Kwa sababu hii ni mada muhimu sana, nimeweka kiambatisho maalum mwishoni mwa kitabu hiki ili uweze kuikagua. Ikiwa hujawahi kusoma kitabu changu kinachoshughulikia mada ya imani,

basi ninakushauri usome kiambatanisho na ujifunze imani ni nini, jinsi ya kuipata, jinsi ya kujua kama una imani, na ikiwa sivyo, ni kitu gani unachoweza kufanya. Sasa kabla ya kumaliza kuzungumzia jambo hili, nataka kusema kwamba ilibidi Mungu anionyeshe majibu ya maswali haya kwa sababu, kama wewe, nilifikiri tayari nilijua yote kuhusu imani. Kwa hivyo, tafadhali zingatia kusoma kiambatisho hata kama ni kujikumbusha tu.

Kifupi, imani ni moyo wetu kusadikishwa kikamilifu na kukubaliana na kile mbingu inachosema. Makubaliano hayo, ambayo yanaitwa imani, yanaipa mbingu mamlaka ya kisheria ya kutenda kupitia sisi, tulio katika imani, hapa katika ulimwengu. Kupitia kwa imani, tunaweza kutumia mamlaka ya mbinguni na kupinga ufalme wa Shetani, kuteka eneo, na kuliweka chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Nilielewa mengi kuhusu imani Mungu aliponiambia nisome Waebrania 11:32-33. Lakini ilikuwa sehemu ya katikati ya aya hizi, ambayo ilivutia sana fikira zangu, kiasi cha kumfanya Mungu atake niione.

> *Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, **walitenda haki,** walipata ahadi.*
>
> —Waebrania 11:33a

Nilipokuwa nimeketi pale asubuhi hiyo mwaka wa 2009, nikitazama Maandiko hayo, hatimaye niliona kile ambacho Mungu alikuwa akiniambia. Hebu nikupe tafsiri yangu rahisi ya kile ambacho Mungu alikuwa akinidhihirishia. Nitaieleza kupitia mlinganisho ufuatao. Hebu tuseme umenunua sehemu nzuri ya ardhi ya ekari 20. Una matumaini makubwa ya kuvuna mazao mazuri kwenye ardhi hiyo. Hata hivyo, ardhi hiyo imeachwa bila kutumiwa kwa miaka mingi na imefunikwa na magugu. Jambo la kwanza unalopaswa kufanya ni kushughulikia magugu hayo; inabidi yatolewe. Unayakata na kuyaondoa. Kwa

kuzingatia lugha ya Maandiko yetu katika Waebrania sura ya 11, hebu tukubaliane kwamba umeshinda magugu. Ndio! Huo ni ushindi mkubwa na kazi nyingi. Lakini pia unajua kwamba haujamaliza.

Unaelewa kwamba ikiwa hujapanda kitu kingine kwenye ardhi, ingawa unaimiliki, kimsingi haina thamani kwako. Kwa hivyo, kwa kutumia maneno katika Maandiko yetu, ikiwa hujapanda mbegu sahihi kwenye udongo huo, huwezi kupata ahadi ya mazao. Utakaa hapo ukingoja na kusubiri mazao ambayo hayatakuja kamwe.

Kwa hiyo, hebu niseme hivi. Mara tu unapotwaa ardhi hiyo, lazima uitumie. Ili kuitumia, lazima ufanye kazi fulani kuhusu kile unachotaka kuweka hapo. Usipofanya hivyo una shamba tu lisilo na magugu na lisilo na mazao, na hutawahi kumiliki ahadi ya mazao unayohitaji. Andika hili maana ni dhana muhimu sana.

**Hutawahi kumiliki usichokitendea kazi!**

Hebu nikupe mfano mwingine wa kile ninasema. Mungu alipowatoa watu wa Israeli kutoka Misri, alifanya hivyo kwa mkono wenye nguvu. Lakini Farao akabadili nia yake na kuwafuata, na alifikiri kwamba aliwatundika baharini. Lakini ukweli tunaopaswa kutambua ni kwamba Mungu ndiye aliyewaweka kwenye bahari. Mungu ndiye aliyewaongoza hadi mahali ambapo walikuwa na bahari mbele yao na milima upande wao wa kulia na kushoto. Mungu alijua kwamba Farao tayari alikuwa njiani kuwakamata tena alipomwambia Musa mahali alipopaswa kuwaelekeza.

Farao alipowajia na kupiga kambi huko, wana wa Israeli walitambua hali yao na wakajikuta katika mahali pagumu sana pasipo na njia ya kutoroka. Lakini Mungu alikuwa na mpango, mpango ambao ungemaliza dai la Misri juu yao milele. Na unajua jinsi hadithi ilivyoendelea: Bahari ya Shamu iligawanyika, na wakavuka juu ya nchi kavu! Lakini Farao na jeshi lake walipoanza kuvuka, ghafla bahari ilirudi juu yao, na wote wakazama. Huu ulikuwa ukombozi mkubwa.

Sio kwamba ilimbidi Farao kurudi nyuma na kutafuta njia nyingine ya kulifikia taifa la Israeli. La, waliangamizwa kabisa. Lakini haijalishi ukombozi huo ulikuwa mkubwa kiasi gani, kwa kweli hiyo ilikuwa sehemu ndogo sana ya hadithi yao yote. Ukombozi huo ulifungulia hadithi kuu zaidi, hatima yao, mahali ambapo waliumbwa kuwa na kuitwa kumiliki.

Kwa hiyo, hebu tuelewe kanuni hii muhimu sana. Walikombolewa kutoka Misri kwenda mahali fulani, mahali pa hatima yao. Farao alikuwa kizuizi kilichozuia mustakabali wao. Na ni sawa na wewe. Tatizo lako ni kikwazo kwa maisha yako ya baadaye. Ingawa ukombozi ni sehemu ya hadithi yako pia, ni mahali unapoenda na kile ulichoitwa kumiliki ndicho hadithi yako halisi! Sasa, kanisa linapenda kusherehekea ukombozi wa Mungu lakini mara nyingi hushindwa kutambua kwamba ukombozi hutuweka huru ili tuweze kufuatilia mahali petu pa umiliki.

Tunaona kwamba ukombozi mkuu wa Israeli kutoka kwa mikono ya Misri ulikuwa ni mwanzo tu, sio mwisho. Ingawa walikuwa huru kutoka katika utumwa wa Farao, bado walikuwa na safari ndefu kabla ya kumiliki na kufurahia ahadi. Miaka ilipita, kizazi kipya kikatokea, na hatimaye wakavuka nyika mpaka wakafika kwenye Mto Yordani. Upande wa pili wa mto huo kulikuwa na Nchi ya Ahadi ambayo wote walikuwa wamesikia kuhusu maisha yao yote. Hii ilikuwa ndoto yao tangu Musa alipowaongoza wazazi wao kutoka Misri. Kumbuka, kizazi kilichotoka Misri pamoja na Musa kilikufa nyikani kwa sababu ya uasi, isipokuwa Yoshua na Kalebu, waliomwamini Mungu.

Kufikia hapa katika hadithi, Musa alikuwa amekufa na Yoshua sasa alipeleka kizazi kipya katika Nchi hiyo nzuri ya Ahadi. Walipokaribia Mto Yordani, waliona kwamba ulikuwa umefurika na wakati huo lilikuwa jambo la hatari kuuvuka. Lakini tena, kama vile Mungu alivyomwambia Musa kuvuka Bahari ya Shamu ilipoonekana

kuwazuia, Mungu alimwambia Yoshua avuke mto lakini awatume makuhani kwanza. Taifa lilijipanga ili kuvuka makuhani wakiwa mbele kama Mungu alivyokuwa amewaagiza, na mara vidole vyao vya miguu vilipogusa maji, maji yaliacha kutiririka.

Kama walivyokuwa wamesikia kuhusu kuvuka Bahari Nyekundu maisha yao yote, walivuka mto mkavu. Lakini tofauti na wazazi wao, kivuko hiki cha maji hakikuwa ukombozi. Lilikuwa agizo la Mungu lililoelekezwa kwa wakati wao ujao. Ndio, mto huo ulikuwa kizuizi, kama vile Bahari Nyekundu ilivyokuwa kikwazo kwa baba zao kutoka Misri. Lakini katika hali hii, hilo lingetumika kama ushuhuda wa nguvu na uwezo wa Mungu wa kuwapeleka katika ahadi hasa waliposimama mbele ya miji yenye kuta na majitu. Daima hilo lingewakumbusha kwamba Mungu angefanya njia wakati ilionekana kuwa hakuna njia, kwamba angekuwa pamoja nao, na kwamba angetimiza ahadi Yake kwao.

Tena, hata kama kivuko hicho cha mto kilikuwa cha ajabu kiasi gani, bado hawakuwa wamefika. Walipaswa kuwa wenye haki mahali hapo kabla ya "kupokea" kile kilichoahidiwa. Hebu nieleze jambo moja zaidi. Haki ni neno la kisheria linalomaanisha kutumia kanuni. Iliwabidi wafuate maagizo ya Mungu, yaani kanuni Yake, katika hali hii kabla ya kumiliki nchi hiyo na kufurahia ahadi. Hebu niweke wazi kwamba ingawa Mungu aliwafikisha mbali kiasi hicho kwa madhihirisho ya ajabu ya nguvu Zake, bado hawakuwa wamemiliki chochote. Iliwabidi wafuate au kutumia na kutekeleza kile Mungu alichosema, jambo ambalo lilimaanisha kwamba walipaswa kuchukua na kumiliki ardhi hiyo.

Wazazi wao walifanya kosa ambalo Wakristo wengi hufanya. Waliona uweza wa Mungu; walisikia ahadi kuhusu nchi nzuri walipokuwa wakielekea. Lakini walifikiri kwamba jambo muhimu lilikuwa kuona ukombozi wao tu. Mungu angefanya mengine yote,

nao wangeingia humo tu na kunywa vinywaji vyao vya barafu, na kustarehe. La, hawakutambua kwamba walipaswa kutumia haki ili kupata kile walichoahidiwa. Walipotambua kwamba ingebidi wajihusishe na kukabiliana na miji hiyo yenye kuta na majitu, mioyo yao ilijawa na hofu.

Hiki ndicho Mungu alikuwa akijaribu kunionyesha pia. "Gary, utahitaji kuingia huko na kukabiliana na hali hii. Itabidi ushughulikie kile ninachotaka kifanyike hapo." Unaweza kuuliza, "Uliogopa?" Ndio, ilibidi nipigane na hofu. Kipindi changu cha televisheni kinaitwa *Fixing the Money Thing*, na nilikuwa na deni la rafiki yangu dola milioni moja—ambazo nilijua zilihitajiwa si tu kuwalipa wafanyakazi wake bali pia wachuuzi wote waliokuwa na familia za kutunza—na sikujua dola hizo milioni moja zingetoka wapi.

Nilipokuwa nikitembea kwenye uwanja wa ndege nikirudi nyumbani kutoka kwa mkutano huo, Mungu alizungumza nami tena. Nilimsikia akisema kwa udhahiri, "Inua fimbo yako!" Nilijua alikuwa anarejelea kile Musa alichofanya kwenye Bahari ya Shamu alipoinua fimbo yake na maji yakagawanyika. Pia nilijua kwamba ile fimbo iliwakilisha mamlaka ambayo Musa alikuwa nayo akiwa kiongozi wa taifa aliyewekwa rasmi. Nilipata ufahamu basi kwamba Mungu alikuwa ananiambia nisimame katika mamlaka yangu. Nilikuwa msimamizi wa huduma hii. Ilibidi nisimame katika mamlaka na hekima ya Mungu juu ya hali hii kama nilitaka suluhu. Nilikuwa na ahadi ya kuwa na chuo hicho kipya, lakini hadi nilipochukua mamlaka na kusimama katika haki, singepata faida ya umiliki. Ilibidi mtu ashughulikie jambo hilo hadi suluhu la machafuko haya ya kifedha lipatikane kupitia kwa msaada Mungu. Na huyo mtu alikuwa ni mimi, mkuu wa huduma!

Kuhusu dola milioni za mjenzi, Mungu alimpa Drenda mpango. Tulijua kwamba hakukuwa na benki zilizokopesha pesa katika mji

wetu wakati wa ule mgogoro wa kifedha wa dunia nzima. Hata nilienda kwa benki yangu na kuomba mkopo wa $100,000 nikitumia nyumba yangu kama dhamana, ili kutusaidia kupata pesa maana nilijua watu wengi walitegemea malipo yetu. Nyumba yangu ilikuwa imelipiwa kikamilifu na ilikuwa na thamani ya mamia ya dola zaidi ya kile nilichokuwa nikikopa. Nilikuwa na mtiririko mzuri wa pesa, lakini walinipigia simu na kukataa kunikopesha. Sikuamini, lakini ndivyo mambo yalivyokuwa wakati huo.

Mungu alimwambia Drenda kwamba tulipaswa kwenda kwa benki ya wajenzi wetu na kuwaomba walikopeshe kanisa letu dola milioni moja. Hatukuwa tumewahi kwenda kwa benki hiyo au hata kusikia habari kuihusu, lakini ndivyo tulivyofanya. Tuliwaza kwamba ikiwa hatungemlipa mjenzi wetu dola milioni moja alizohitaji, ingebidi isemwe kwamba amefilisika. Alikuwa na mkopo mkubwa wa biashara, na juu ya hayo, alikuwa na deni la maelfu la wachuuzi mbalimbali. Tuliona kwamba benki yake tayari ilikuwa kwenye ndoano kwa sehemu kubwa ya pesa hizo, na tulitaka watuhamishie deni hilo. Ikiwa wangetuidhinisha mkopo, basi tungemlipa mjenzi wetu, naye angekuwa na pesa za kulipa benki, wachuuzi wake, na wafanyakazi. Dhima basi ingehamishwa kwetu, na mjenzi wetu angekuwa huru. Lakini kumbuka, benki hii haikujua chochote kutuhusu.

Kwa hivyo, tuliandaa wasilisho kutuhusu, historia yetu, mpango wetu wa ukuaji, na sababu iliyoonyesha kwamba tungeweza kuwalipa dola hizo milioni moja. Kama nilivyosema, hatukuwa tumewahi kwenda kwa benki hiyo hapo awali na hatukuwa tumewahi kukutana na afisa wao wa mikopo. Lakini tulitoa wasilisho letu siku hiyo na tukaeleza ni kwa nini tulifikiri kwamba ingefaa wao kutupa zile dola milioni moja. Tulipomaliza, alisema, “Nina mamlaka ya kuandika hundi hadi $500,000 bila kuthibitisha mapato yenu,” kisha akatoa hundi na kuiandikia kanisa letu pale pale. Kisha akasema, “Nitawapa

$500,000 nyingine wiki ijayo baada ya kushughulikia ombi lenu." Ukweli ni kwamba: Bila kuthibitisha mapato yetu, bila kujaza fomu, alituandikia hundi ya $500,000 papo hapo. Mimi na Drenda tuliketi pale tukiwa tumepigwa na mshtuko huku akitukabidhi ile hundi. Lakini tafadhali nisikilize: Hilo lisingaliwahi kutokea kama hatungeanzisha taratibu hiyo. Pili, ilitupasa sisi wenyewe kwenda kwa benki. Kwa nini? Sisi ndio tuliokuwa na fimbo, mamlaka, na upako wa huduma kwa kuwa tulikuwa wakuu wa huduma. Haingefaa kumtuma mmoja wa wafanyakazi wetu kushughulikia jambo hilo. Nina hakika hangepewa hundi hiyo ikiwa ningefanya hivyo. Ilinibidi kuinua fimbo yangu, mamlaka yangu, nikiwa na mpango kutoka kwa Mungu wa kutekeleza hilo.

**ILINIBIDI KUINUA FIMBO YANGU, MAMLAKA YANGU, NIKIWA NA MPANGO KUTOKA KWA MUNGU WA KUTEKELEZA HILO.**

Hebu niendelee. Dola 300,000 za kuanzisha huduma ya televisheni zilikujaje? Kwa kweli, hiyo ni hadithi ndefu, lakini nitaizungumzia kwa ufupi. Mtu fulani huko Atlanta alipata nakala ya kijitabu kidogo ambacho nilikuwa nimeandika miaka kadhaa awali kuhusu jinsi ya kujitoa kwa madeni. Bado hatukuwa tumeanza huduma ya televisheni, redio au kuwa na ofisi au washirika huko Atlanta wakati huo. Mmoja wa wafanyakazi wetu wa ofisi yetu ya Ohio alikuwa akisafiri kwa ndege kutoka Atlanta na alikuwa amebeba kitabu changu ili kukisoma njiani. Alipokuwa akingoja kwenye uwanja wa ndege, mwanamume mmoja aliona kitabu hicho mikononi mwake na akauliza kukihusu. Mfanyakazi wangu, ambaye alikuwa amemaliza kukisoma, alimpa kitabu hicho.

Mtu huyo alisoma kitabu hicho na kuvutiwa sana nacho kiasi kwamba alinipigia simu na kusema alikipenda. Alipendezwa sana na kitabu hicho kiasi cha kupanga niwe kwenye matangazo ya

televisheni ya taifa kuzungumza juu yake. Watayarishaji wa kipindi hicho walitaka kutoa nyenzo zangu kwa watazamaji wao wakati kipindi kilikuwa kinaendelea na walituuliza ikiwa tungeweza kutoa bidhaa iliyohitajika, na, bila shaka, tulikubali. Ajabu ni kwamba, tuliuza bidhaa nyingi sana katika kipindi hicho kimoja na tukatumia faida kulipia theluthi moja ya gharama nzima ya kuanzisha huduma yetu ya televisheni.

Pili, mwanamume mmoja katika kanisa letu alinijia baada ya ibada ya Jumapili asubuhi na kunikabidhi $120,000 kwa ajili ya huduma yetu ya televisheni. Hakika nilishangazwa sana. Mwanamume huyu alikuja kanisani kwetu akiwa amefilisika kabisa na alikuwa karibu kufukuzwa kutoka kwa nyumba yake miaka michache tu awali. Lakini aliposikia mafundisho yangu kuhusu Ufalme, maisha yake yalianza kubadilika. Aliunda biashara kadhaa ambazo zilimfanya afanikiwe kweli.

Tena, unaweza kuona mchakato katika hadithi hii. Sikupata hundi ambayo ingelipia hitaji hilo kwa kisanduku cha barua. Ilibidi nipitie mchakato wa kuandaa maelezo ya televisheni, jambo ambalo lilifanya niweze kupata fedha hizo. Ilibidi nisafiri kwa ndege hadi mahali nilipohitaji kwenda kurekodi vipindi halisi. Nilikuwa na jukumu langu katika jambo hili.

Jambo ambalo Mungu alikuwa akitaka nione kuhusu Waebrania 11:33 asubuhi ile katika maombi lilikuwa kwamba imani inahitajika, lakini sio imani tu inayohitajika. Tuna sehemu yetu ya kutekeleza katika kupokea ahadi.

**Mungu anaweza kuleta samaki, lakini inabidi tuwavue!**

Kwa hiyo, hebu nifafanue jambo hili kidogo. Kumiliki kunamaanisha kutumia na kudumisha utawala wako wa kisheria juu ya kitu ambacho umenyakua, kitu kilicho chini ya mamlaka yako ya kisheria. Kunyakua hakumaanishi kitu ambacho umenyakua kwa njia ya migogoro au nguvu, ingawa inaweza kumaanisha hivyo.

Kwa mfano, kulipia kipande cha ardhi hunyakua ardhi hiyo na kuileta chini ya mamlaka yako ya kisheria. Lakini tena, usipofanya kile unachopenda katika ardhi hiyo, itabaki bila kitu na bila maana. Kwa hivyo, kusimamia kitu ni nini? Kulingana na kamusi, ni kitendo au mchakato wa kutekeleza au kusimamia kitu ili kupata matokeo yanayotarajiwa.

Andiko letu katika Waebrania 11 linatuambia kwamba tunahitaji kutumia haki ikiwa tunataka kufurahia ahadi za Mungu. Hii ina maana kwamba tunapaswa kutekeleza kile ambacho Mungu anataka katika hali fulani, kile ambacho Neno lake, kanuni Yake inasema. Inapohusu kipande chetu cha ardhi, itamaanisha kwamba tutekeleze kile tunachotaka kuona kikitokea katika ardhi hiyo.

**Ili kutumia kanuni hii kwa biashara au maisha yako, itamaanisha kutumia mchakato, ambao utaleta matokeo unayotarajia kutoka kwa kitu kilicho chini ya mamlaka yako ya kisheria.**

**HUWEZI KAMWE KUMILIKI KILE USICHOKIFANYIA KAZI**

Hapa ndipo watu kwa kawaida hukosea. Hawatambui kwamba wana sehemu ya kutekeleza katika kumiliki ahadi. Na kumbuka, huwezi kamwe kumiliki kile usichokifanyia kazi. Watu wengi hutegemea imani pekee huku wakitumaini kwamba Mungu atafanya kila kitu. Lakini sivyo ilivyo.

Drenda na mimi tuna nyumba nzuri yenye nafasi zaidi ya futi za mraba 7,000 kwenye zaidi ya ekari 55 ambazo tulijenga takriban miaka 25 iliyopita. Wakati huo, tulikuwa tumeanza kutoka kwa madeni na kujifunza juu ya Ufalme, kwa hiyo ilitubidi tufanye kazi nyingi sisi wenyewe. Tuliajiri mkandarasi wa kutengeneza fremu ya nyumba yetu na kuhakikisha maji hayaingii ndani, na kazi iliyobaki tungeifanya sisi wenyewe au kutumia mkandarasi wa kawaida. Na hebu niseme hatukujua chochote kuhusu kujenga nyumba, nasema chochote. Kwa

hiyo, tulinunua kitabu cha mwongozo wa jinsi ya kujenga nyumba yako mwenyewe, na tukaendelea mbele. Kweli hatukujua chochote. Hata hivyo, ndivyo tulivyofanya. Nilifanya kazi ya kuweka nyaya za umeme ndani ya nyumba, ingawa wakati huo sikujua waya wa 12:2 ni nini. Sikujua chochote kuhusu umeme. Tulikuwa na rafiki ambaye alitusaidia kuweka mabomba. Tuliweka sakafu za vigae (Drenda alifanya kazi hiyo), tulichimba mitaro, tukaweka viunzi vyote, tukapaka rangi nyumba nzima, na zaidi.

Jioni mmoja, nilikuwa nimechoka. Wakati huo, tulikuwa wachungaji, kila jioni tulienda kuuza bima ya biashara yangu, kila siku tulikaa hadi usiku wa manane kufanya kazi ya nyumbani, na kweli nilikuwa nimechoka. Siku moja, nilianza kumlalamikia Bwana kuhusu jambo hilo, naye akasema, “Vema, ulitarajiaje nyumba hii kufika hapa?” Naam, hilo ndilo nililotarajia. Lakini nyumba hii iko hapa na imelipiwa kwa sababu ya jinsi tulivyoijenga. Tuliokoa pesa nyingi sana. Zaidi ya hayo, watoto wetu wote walitusaidia, na ni mahali spesheli sana kwetu sote.

**Mungu atafanya sehemu yake, lakini lazima nasi tufanye sehemu yetu ili kufurahia ahadi Zake.**

Mungu aliniambia kusimamia kazi yetu wenyewe ni ufunguo mkuu katika kuongeza kasi! Ndio, kuna maelezo ya kuchosha, lakini lazima kazi isimamiwe ili iweze kufanyika. Mimi ni mmiliki wa nyumba, na kazi nyingi inahitajika ili kuweza kuifurahia. Ushuru, matengenezo, na ukarabati, yote lazima yafanywe ili mambo yote yawe sawasawa nyumbani.

Kwa hivyo kwa nini kusimamia kazi ni muhimu sana katika kuongeza kasi yako? Hebu nitumie mfano kueleza sababu. Umewahi kuendesha gari au labda gari ndogo lenye kifaa cha kuzuia mwendo wa kasi kwenye injini? Haijalishi ni kiasi gani utakanyaga mafuta kuongeza kasi, halitaenda haraka. Kabureta iliundwa kupima mtiririko

fulani wa mafuta kwa injini, na haijalishi ni kiasi gani unataka gari liende haraka, hakuna tofauti. **Mpaka ubadilishe kiasi cha mafuta kinachotumika, utakuwa na kizuizi.**

Na hapa ndipo watu wengi sana walipo, wanataka kwenda kwa kasi, lakini kila kitu kimefungwa na masuala ya usimamizi.

Ili kuthibitisha hoja yangu, acha nikuulize swali: "Kwa nini Farao alimweka Yusufu juu ya taifa la Misri?" Ninajua watu wengi watasema: "Ni kwa sababu Yusufu aliweza kufasiri ndoto ya Farao." Lakini wamekosea. Subiri nikuonyeshe.

> *"Ndivyo nilivyomwambia Farao, ya kwamba Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. Tazama, miaka saba ya shibe inakuja, katika nchi yote ya Misri. Kisha kutakuja miaka saba ya njaa baada yake; na shibe ile yote itasahauliwa katika nchi ya Misri, na njaa itaiharibu nchi. Wala shibe ile haitajulikana katika nchi kwa sababu ya njaa inayokuja baadaye, maana itakuwa nzito sana. Na ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi. Basi, Farao na ajitafutie mtu wa akili na hekima amweke juu ya nchi ya Misri.*
>
> *Farao na afanye hivi, tena akaweke wasimamizi juu ya nchi, na kutwaa sehemu ya tano katika nchi ya Misri, katika miaka hii saba ya kushiba. Na wakusanye chakula chote cha miaka hii myema ijayo, wakaweke akiba ya nafaka mkononi mwa Farao wakakilinde kuwa chakula katika miji. Na hicho chakula kitakuwa akiba ya nchi kwa ajili ya miaka hiyo saba ya njaa, itakayokuwa katika nchi ya Misri, nchi isiharibike kwa njaa."*
>
> ***Neno hilo*** *likawa jema machoni pa Farao, na machoni pa watumwa wake wote.*
>
> — Mwanzo 41:28-37

La, haikuwa kwa sababu Yusufu aliweza kufasiri ndoto ya Farao. Hilo lilimpa Yusufu uaminifu na nafasi ya kuzungumza na Farao, lakini ni mpango wake wa kina wa usimamizi uliovutia usikivu wa Farao na kumpa kazi hiyo. Hebu niseme ukweli hapa:

**Usimamizi uliokoa Misri! Na usimamizi wako utakuokoa pia.**

SURA YA 3

# JE, UWEZO WAKO NI MKUBWA KIASI GANI?

Siku ile katika mwaka wa 2009 ambapo Mungu alinionyesha Waebrania 11:32-33 na kunena nami jinsi usimamizi ulivyo muhimu, aliniambia pia nisome Isaya 54. Hapo alinionyesha mfano wa kuongeza kasi ambao nilihitaji kuelewa pamoja na usimamizi. Naam, hakika usimamizi ulikuwa sehemu kubwa ya kile alichokuwa akinionyesha katika Isaya 54 siku hiyo, lakini kulikuwa na maelezo zaidi ambayo alitaka nione. Wakati huo, nilitambua mambo manne ambayo lazima yafanywe ili kuongeza na kutwaa maeneo zaidi. Usimamizi ulikuwa mojawapo. Niliziita hatua hizi nne alizonionyesha kanuni nne za kuongeza kasi. Nilifundisha kuhusu kanuni hizi nne mara kadhaa kwa miaka mingi, na zimejumuishwa katika kitabu hiki kama kanuni nne kati ya tisa nilizojifunza kwa miaka kadhaa.

Mwaka wa 2015 nilikuwa nimefikisha umri wa miaka 60, na katika siku yangu ya kuzaliwa, Bwana alizungumza nami katika ndoto kuhusu miaka 10 iliyokuwa ikifuata maishani mwangu. Alinikumbusha kuhusu agizo alilonipa nikiwa Albania mwaka wa 2006 ambapo aliniita niende kwa mataifa kuwafundisha agano Lake la baraka za kifedha. Aliniambia kwamba ningefanya mengi zaidi kati ya miaka yangu ya 60 na 70 kuliko nilivyokuwa nimetimiza katika miaka yangu yote ya awali ya huduma. Lo! Nakumbuka nikiwaza kwamba hilo lilikuwa jambo la kushangaza. Bila shaka, tayari nilikuwa nimejitolea na kushughulikia mwito huo kwa uaminifu, lakini hakika hilo lilinitia moyo.

Mimi na Drenda tulimwona Mungu akifanya mambo ya ajabu sana katika maisha yetu kufikia wakati huo. Tulikuwa tumesafiri ulimwenguni kote kuhubiri na kufundisha. Tulikuwa tumeanzisha vipindi vya televisheni vya kila siku, ambavyo vilikuwa vikionyeshwa katika kila eneo ulimwenguni. Kanisa letu lilikuwa limeongezeka na kufikia maelfu, na tulikuwa tumeona maisha mengi yakibadilika. Tulikuwa tumeona watu ambao madaktari walisema walikuwa na masaa manne ya kuishi wakiponywa na kurudi katika maisha ya kawaida. Tulikuwa tumeona watu ambao walitangazwa kuwa wamekufa hospitalini wakifufuka na wako hai na wanaendelea vizuri leo. Tulikuwa tumeona uvimbe ukitoweka na kuona waliopooza wakiamka na kurudi kazini siku iliyofuata. Bila shaka, jambo la kusisimua zaidi lilikuwa kuona maelfu kwa maelfu ya watu wakigundua jinsi Ufalme wa Mungu ulivyo wa kustaajabisha, huku wakitoa mioyo yao kwa Mungu, na kisha kuona maisha yao yakibadilishwa kabisa. Ilikuwa fursa ya ajabu. Kwa hiyo, nilisisimka aliposema miaka 10 iliyofuata ingekuwa ya ajabu zaidi kuliko miaka ya awali!

Hata hivyo, mnamo Oktoba 2016, jambo lisilo la kawaida lilitokea. Bwana alinena nami tena kuhusu usimamizi na kanuni nne alizokuwa amenionyesha hapo awali.

Asubuhi moja, malaika alikuja chumbani mwangu na kusema maneno mawili tu, "Una misheni." Kwa kweli sikumwona yule malaika, lakini nilisikia sauti yake. Nilipomuuliza Roho Mtakatifu kama hiyo ilikuwa sauti Yake, alisema, "La, ni malaika wako." Sawa, lakini wakati huo, nilichanganyikiwa kidogo maana nilijua tayari nilikuwa na misheni, na nilikuwa nimeshughulika sana kuitekeleza. Kwa hiyo, nilianza kutafakari kuhusu kile malaika alikuwa amesema na kwa nini alisema hivyo. Nilijikumbusha maneno ya malaika na kujaribu kuchambua maelezo yoyote ambayo yangeweza kunipa fununu. Nikakumbuka kulikuwa na uharaka na mamlaka katika sauti

yake. Nilihisi kwamba alikuwa akisema kwamba kazi niliyoipokea kutoka kwa Mungu huko Albania ilikuwa ya maana sana na muda huo ulikuwa mfupi. Nilifafanua maneno yake kumaanisha kuwa makini na kudhamiria ili kutimiza kazi hiyo.

Baada ya siku hiyo, nilianza kuomba kuhusu jinsi ya kuongeza kasi katika kile nilichopaswa kufanya ili kuhakikisha kwamba nimetimiza misheni yangu. Ilikuwa miezi michache baada ya malaika kunijia nilipoota kuhusu kitabu hiki, kama nilivyotaja katika sura ya iliyopita. Katika ndoto hii, niliona kitabu hiki, mada yake, na vichwa vya sura zote. Katika ndoto, nilihisi Bwana akisema kwamba hizi zilikuwa kanuni tisa za kuongeza kasi nilizohitaji kujifunza na kuzimiliki ikiwa nilitaka kumaliza safari yangu nikiwa nimekamilisha kila kitu alichokuwa ameweka moyoni mwangu. Sisemi kwamba kanuni hizi tisa ndizo kanuni pekee za kuongeza kasi, lakini aliniambia kuwa hizi ndizo nilizohitaji kujua na pia kuweka katika kitabu hiki.

**Katika ndoto, Mungu aliyaita maeneo haya tisa niliyopaswa kujifunza "kanuni tisa za kuongeza kasi."**

Nilitambua kanuni nne za kwanza maana alikuwa amenifundisha hizo, na nilikuwa nimefundisha kuzihusu kwa miaka mingi. Na hakika, kanuni hizi nne, kulingana na sura za kitabu nilizoziona, ndizo nilizopaswa kujadili katika kitabu hiki. Baada ya kuota ndoto hiyo, nilianza kusoma na kuandika maelezo juu ya kanuni zingine tano ambazo alinionyesha. Katika somo hilo, niliona kwamba kweli kulikuwa na mambo mengi ambayo nilipaswa kurekebisha katika maisha yangu ya kibinafsi na katika huduma.

Baada ya ndoto hiyo ya ajabu na dhahiri, nilifurahi sana kuandika kitabu hiki. Nilihisi nilipaswa kuanza haraka iwezekanavyo, lakini nilijua kwamba bado sikuwa tayari maana kulikuwa na mengi zaidi ya kujifunza kabla ya kuanza. Sasa, miaka sita baada ya kuwa na ndoto hiyo, nimeandika kitabu hiki, na ninafurahi sana kuona ndoto hiyo

ikitimizwa. Lakini kabla sijazungumzia kanuni hizi tisa halisi za kuongeza kasi, ninahitaji kuweka msingi na kukupeleka katika Isaya 54, ambapo Mungu alifunua kanuni nne za kwanza za kuongeza kasi.

> *"Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake yeye aliyeolewa," asema Bwana.*
>
> *"Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako. Kwa maana utaenea upande wa kuume na upande wa kushoto; na wazao wako watawamiliki mataifa; wataifanya miji iliyokuwa ukiwa kukaliwa na watu."*
>
> —Isaya 54:1-3

Hapa tunaona unabii juu ya mwanamke ambaye ni tasa na hana mume lakini ana watoto wengi kuliko mwanamke aliye na mume. Ana watoto wote bila kupitia uchungu wa kuzaa. Nafikiri hilo limevutia umakini wako. Wazo lako la kwanza linapaswa kuwa, *Je! Hilo linawezekanaje?* Nafikiri tunaweza kuanza kuelewa jibu la swali hili kwa kuangalia sura ya 53. Sura ya 53 ni unabii kuhusu Yesu, kile alichokuja kufanya, na jinsi alivyolipa gharama ya dhambi kwa ajili yetu sote.

Hebu nikuonyeshe kidogo sura ya 53, na nione kama utakubaliana nayo.

> *Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa*

*juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.*

*Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote.*

—Isaya 53:4-6

Na aya ya 12 ya sura hii inasema:

*Walakini alichukua dhambi za watu wengi, na kuwaombea wakosaji.*

Nafikiri utakubali kwamba sura ya 53 bila shaka inazungumza juu ya Yesu. Kwa hiyo, tukiwa na hilo akilini, twende moja kwa moja katika sura ya 54, mstari wa 1.

*Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake yeye aliyeolewa, asema Bwana.*

Tunaweza kuuliza tena, "Mwanamke huyo angewezaje kupata mtoto bila kupitia uchungu wa kuzaa?" Sasa, una jibu. Ni wazi, sura ya 54 inazungumzia kuzaliwa upya, watoto wasiohesabika, waliozaliwa kwa Roho na sio kwa mwili. Isaya anazungumzia wewe na mimi na kanisa. Lakini haizungumzii kuzaliwa upya tu; inazungumzia agano jipya kabisa. Paulo alitufasiria Isaya 54 katika Wagalatia 4:21-31.

*Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je! Hamwisikii sheria? Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Ibrahimu alikuwa na wana wawili mmoja kwa mjakazi, na*

*mmoja kwa mwungwana. Lakini yule wa mjakazi alizaliwa kwa mwili, yule wa mwungwana kwa ahadi.*

*Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio kama maagano mawili, moja kutoka mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa, ambalo ni Hajiri. Maana Hajiri ni kama mlima Sinai ulioko Arabuni, umelingana na Yerusalemu wa sasa; kwa kuwa anatumika pamoja na watoto. Bali Yerusalemu wa juu ni mwungwana, naye ndiye mama yetu sisi.*

— Wagalatia 4:21-26

Paulo alifasiri maana ya wanawake hawa wawili hapa katika mstari wa 24 kwamba inawakilisha maagano mawili. Mwanamke mmoja yuko utumwani; hiyo inawakilisha agano la kale na kanuni. Mwanamke wa pili anawakilisha agano jipya ambalo halifungamani na sheria bali ni agano jipya linalotegemea yale ambayo Yesu alitufanyia, ambayo hupatikana kwa imani. Lakini kuna kitu unahitaji kuzingatia kwa karibu ambacho ni kikubwa sana hapa! Angalia kwa makini mstari wa 30.

*Lakini lasemaje andiko? "Mfukuze mjakazi na mwanawe, kwa maana mwana wa mjakazi* ***hatarithi*** *kabisa pamoja na mwana wa mwungwana."*

— Wagalatia 4:30

Je, umewahi kupokea urithi? Kweli, hauko peke yako. Katika mtandao Credit.com ilichunguza hifadhidata na kugundua kuwa 73% ya watu waliokufa kati ya Oktoba na Desemba 2016 walikufa wakiwa na madeni. Wastani wa bili walizoacha zilikuwa $61,554. Lakini huo sio urithi ulio nao. La, urithi ninaouzungumzia ni bora kuliko kitu chochote ambacho umewahi kusikia.

Paulo alisema una urithi, lakini ni wazi kabisa kwamba hutaweza kuupokea kwa kujaribu kuupata, kwa kujaribu kuwa mwema vya kutosha kwa Mungu kwa uwezo wako mwenyewe. Urithi huja kwa kufanywa mwana katika familia ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, ambako kunaitwa kuzaliwa mara ya pili. Unapozaliwa mara ya pili, unafanyika sehemu ya familia ya Mungu, mwana au binti. Kumbuka, sio lazima ufanye kazi ili kupata urithi; bali unapewa kama yule mwanamke ambaye alikuwa na watoto wengi bila kupitia uchungu wa kuzaa. Alipokea tu. Ninapozungumza kuhusu urithi huu wa ajabu, nataka uzingatie kauli hiyo: Alipokea tu. Alikuwa tasa, jambo ambalo lilikuwa aibu katika nyakati hizo. Lakini alikuwa na watoto wengi, bila kupitia uchungu wa kuzaa. Alipokea kwa urahisi, na hiyo inazungumza juu ya agano ulilo nalo sasa. Yote yanapatikana kwako sasa.

**KUMBUKA, SIO LAZIMA UFANYE KAZI ILI KUPATA URITHI; BALI UNAPEWA...**

**Uwezo wako umebadilishwa kiasi kikubwa!**

Sasa haijalishi wewe ni nani au una uwezo gani bali yote yanaamuliwa na Mungu, Yule anayetoa urithi. Si ni jambo la ajabu? Basi, hebu tuangalie kwa kina kuhusu urithi wako. Eti unasema hujapokea barua iliyoidhinishwa ambayo inasema kwamba una urithi? Naam, nafikiri umeipokea!

Huenda umesikia watu wakitumia neno wosia na agano la mwisho mtu anapokufa. Maana yake ni wosia ambao marehemu ameandika kueleza jinsi mali yake itakavyogawiwa warithi wake. Neno agano linamaanisha mwongozo rasmi, ulioandikwa unaotoa ugawaji wa mali ya mtu baada ya kifo, yaani wosia.

Sehemu moja ya Biblia tunayosoma inaitwa Agano Jipya, ambayo ina maana kwamba ni mwongozo rasmi ulioandikwa na Mungu kuhusu kile ambacho ametupa. Kwa hivyo ndio, umepewa barua

ya urithi wako. Lakini umeisoma? Ukipokea barua iliyoidhinishwa ambayo inasema kwamba umeorodheshwa kama mrithi na mjomba wako, je, utaifungua? Bila shaka utafanya hivyo.

Basi kwa nini watu wengi hawafungui barua ya urithi wao, Biblia? Kwa sababu, kwanza kabisa, hawajawahi kusikia kuhusu urithi huu. Pili, walichosikia ni kwamba Mungu ni msimamizi mgumu. Huwa wanamwona Mungu kama Mungu mwenye hasira ambaye ana orodha kamili ya mambo ya kufanya na kutofanya. Wanajua kwamba hawajawahi kuishi kulingana na orodha hiyo, kwa hiyo mbona wasome kile ambacho Mungu anasema? Pia wanamwona Mungu kama mkosa haki na mjeuri, kwa hiyo hawajifanyi hata kidogo kwamba wanamwamini Yeye au Neno Lake.

Kwa mfano, hivi karibuni nilisoma kichwa cha habari kuhusu binti wa umri wa miaka saba ambaye alikufa alipokuwa akifanyiwa upasuaji wa kifuko cha koo. Ingawa huu ni upasuaji wa kawaida na kwa kawaida ni salama sana, moyo wake ulisimama, na kukawa na matokeo ya kuhuzunisha sana. Nafikiri mioyo yetu sote iliumia kidogo tuliposikia kwamba hilo lilifanyika. Walakini, ingawa tukio hili lilikuwa la kusikitisha, kulikuwa na sehemu nyingine ya hadithi ambayo itaathiri familia hii maisha yao yote. Hebu ninukuu kile baba alichomwambia mwandishi wa habari (na ninakuu hapa):

> "Huwezi kuelewa kwa nini mambo haya hutokea, lakini tunajua ulikuwa ni mpango wa Mungu. Na hilo ndilo jambo pekee linaloweza kutuvusha, kwa sababu tunajua ilikuwa ni Mungu."

Acha nimnukuu mchezaji Aaron Rodgers wa timu ya Green Bay Packers, ambaye hadithi yake ilikuwa katika jarida la People mnamo Januari 22, 2020.

> "Rodgers alieleza kuwa alitilia shaka dini akiwa mtoto na tangu wakati huo amekuwa akihusiana na mambo ya "kiroho kwa njia tofauti" kadri anavyozidi kuwa mkubwa. "Watu wengi niliowajua, kanisa lilikuwa ... lazima uende." Pia alisema, "Sijui jinsi unavyoweza kumwamini Mungu anayetaka kuhukumu karibu dunia nzima kwenye moto wa jehanamu. Ni kiumbe wa aina gani mwenye upendo, nyeti, aliye kila mahali, na mwenye uwezo wote anayetaka kuhukumu uumbaji wake mzuri kwenda kwa jehanamu ya moto mwishoni mwa haya yote?"

Maoni ya kichaa! Lakini ikiwa hivi ndivyo wanavyoamini kumhusu Mungu, itabidi ukubali, ni nani anaweza kumtumaini au kutamani kumtumikia Mungu ambaye anataka kumchukua bintiye mwenye umri wa miaka saba? Hakuna mtu! Na ni nani anayetaka kumtumikia Mungu ambaye "anataka" kuhukumu karibu dunia nzima kwenda kwa moto wa mateso? Hakuna mtu! Lakini ndivyo Wakristo wengi wanavyoamini. Maisha yako yote umesikia watu wakisema: "Mungu aliruhusu hilo," "Mungu alifanya hivi," "Huo ulikuwa mpango wa Mungu," "Ulikuwa ni wakati wao wa kwenda," na kauli nyingi zaidi kama hizo. Kwa kweli, nitaweka dau kwamba labda unafikiria vivyo hivyo. Kwa hivyo nitakuwa mkweli. Ikiwa unaamini kweli kwamba Mungu yuko hivyo, kwamba anaweza kuua mtoto kwa hiari au kumpa mtu ugonjwa wa saratani, basi tunahitaji kuwa na mazungumzo mazito. Acha niseme hivi:

**KAMWE HUWEZI KUMWAMINI MTU USIYEMTUMAINI na hakika hutakuwa na hamu yoyote ya kusoma chochote kuhusu kile kinachoitwa urithi kutoka kwake!**

Hii ndiyo sababu mimi hutumia muda mwingi kuwashirikisha watu jinsi Mungu alivyo mwema. Sio kwa kuwaambia tu bali kwa kuwaonyesha pia. Sababu nimetumia muda mwingi katika sura hii

kuzungumzia urithi wako, yaani uwezo wako usio na kikomo, ni kwamba nisipokusaidia kuona uwezo ulionao kweli, utalenga chini sana tutakapoanza kuzungumzia kanuni tisa za kuongeza kasi. Ikiwa tunaweza kupata picha ya utambulisho wetu hasa na ukuu wa Mungu wetu, anayetuunga mkono, nafikiri hilo litasaidia kufafanua malengo ya maisha yetu. Msingi wa hilo, bila shaka, ni kwamba Mungu ni mwema na tunaweza kuamini ahadi Zake kwetu.

Acha nikupe mfano kwa kushiriki hadithi ambayo hivi majuzi niliisikia kutoka kwa mwanadada ambaye ni mshirika katika kanisa letu. Amy ni mama wa wavulana wawili wazuri, na furaha yake kuu maishani ni kuwa mama. Hii ilikuwa ndoto yake tangu aolewe. Lakini kwa miaka mitatu ya kwanza ya ndoa yake, hakuweza kupata mimba. Alikumbwa na kuharibika kwa mimba na kuvunjika moyo kila mara. Lakini siku moja, alisikia jambo la kushangaza. Rafiki yake alipatikana na ugonjwa wa saratani na akapewa siku nne tu za kuishi lakini aliponywa papo hapo kwa uwezo wa Mungu. Rafiki huyo alimjulisha mafundisho yangu kuhusu Ufalme wa Mungu.

Siku moja alipokuwa akizungumza na mke wa mtu fulani, mwanamke huyo alimuuliza ikiwa alikuwa akijaribu kushika mimba. Akajibu, "Ndio." Kisha mwanamke huyo akamwambia, "Ni mapenzi ya Mungu kwamba upate mtoto, na ushindi wako unakuja." Wakati huo, Amy alitokwa na machozi, kwa sababu mimba yake ilikuwa imeharibika muda usio mrefu. Maneno hayo yalimfariji, lakini hakujua ni kwa nini mwanamke huyo alisema hivyo. Daima alikuwa amefundishwa kwamba Mungu ndiye anayejua vyema zaidi, na ikiwa hakushika mimba, basi Mungu alikuwa na mpango bora zaidi. Lakini maneno ya mwanamke huyo, ambayo yalikuwa na uhakika sana katika mapenzi ya Mungu, yalimvutia sana. Alitaka kujua zaidi. Alipokuwa akisoma Neno, alipata Andiko hili:

*Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka?*

— Luka 11:11

Kwa ghafula, alitambua kwamba akimwomba Mungu ampe mtoto, angempa mtoto, si kuharibika kwa mimba au maisha ya baadaye ya kuwa tasa. Alitii Maandiko hayo, naye akapata mimba ya mvulana baada ya miezi michache. Mimba yake ilikuwa sawa; na baadaye katika ujauzito wake, alienda hospitalini kujua jinsia ya mtoto wake. Siku hiyo alipokuwa njiani kutoka hospitalini simu yake ililia. Muuguzi aliuliza kama angeweza kurudi mara moja, kwa sababu daktari alitaka kuzungumza naye maana kulikuwa na jambo ambalo lilihitaji uangalizi wa haraka. Amy alirudi hospitalini. Daktari alimwambia na kumuonyesha kwamba mtoto wake alikuwa na tundu moyoni mwake, pamoja na masuala kadhaa mazito ya kiafya. Aliambiwa kwamba alihitaji kuona mtaalamu mara moja.

Mkutano na mtaalamu ulipangwa kuwa baada ya siku tatu. Katika siku hizo tatu, yeye na mume wake waliomba na kukaa katika Neno kuhusu mtoto wao na waliazimia kutompoteza mtoto huyo. Baada ya mtaalamu huyo kutumia masaa kadhaa kupiga picha na kumchunguza, alimwambia Amy kwamba kamwe hakuwa ameona jambo hilo hapo awali, lakini shimo lililokuwepo siku tatu awali lilikuwa limetoweka, huku kukiwa na sehemu ndogo tu iliyobaki. Mtoto alikuwa na afya njema kabisa. Amy alifurahi sana! Sasa yeye ni mama wa watoto wawili, na sasa anajua kwa hakika kwamba Mungu ni mwema! Hii ni hadithi nzuri na ni moja ya maelfu ambayo nimesikia kwa miaka mingi.

Mungu ni mwema, na ikiwa ni mwema unafikiri una urithi wa aina gani?

Katika Wagalatia sura ya 4, Paulo aliandika barua kwa waumini

wa Kiyahudi ambao walikuwa wamemwani Kristo. Hata hivyo, bado walikuwa wakipambana na dhana mpya kwamba sheria haikuhitajika tena. Paulo aliwafundisha na kuwasahihisha kuhusu imani yao ya zamani, ambayo ilikuwa ya utumwa.

> *Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ni* ***bwana wa yote;*** *bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa* ***wana,*** *Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi,* ***u mrithi kwa Mungu.***
>
> — Wagalatia 4:1-7

Hapa, Paulo alitoa hoja kwamba baada ya kuokoka, wewe sasa ni mwana au binti wa Mungu na umekombolewa kutoka kwa wale anaowaita, mawakili na watunzaji wa sheria. Sheria ilikuwa aina ya haki yenye msingi wa woga ambayo hakuna mtu angeweza kupata. Kwa hiyo, dhabihu zilipaswa kutolewa mwaka baada ya mwaka, lakini dhabihu hizi hazikuwa na uwezo wa kuweka watu huru kutoka kwa dhambi zao. Sasa kupitia kwa Yesu Kristo, Biblia inasema kwamba katika Kristo, umefanywa kiumbe kipya.

> *Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.*
> — 2 Wakorintho 5:17

Roho wa Mungu sasa anaishi ndani yako, na utumwa wako wa dhambi umevunjwa. Kama mwana au binti wa Mungu, huna lawama mbele Zake, si kwa msingi wa kile unachofanya au usichofanya bali kwa msingi wa kile ulicho. Sasa unastahili kupata urithi, kama Paulo asemavyo katika Wagalatia 4:7. Lakini urithi ni nini? Mstari wa nne unasema nini?

**BWANA WA YOTE!**

Lo, huo ni urithi mzuri sana, lakini nafikiri inategemea ni mali gani tunazungumzia. Kuna baadhi ya mashamba ya watu nisingependezwa nayo hata kidogo.

Kwa hivyo, Paulo alisema umerithi mali ya nani?

> *Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, "Aba, yaani, Baba." Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi;* ***warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo****; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye*
> —Warumi 8:14-17

Paulo alisema sisi ni warithi wa Mungu! Maana yake tumerithi vyote alivyo navyo Mungu! Tafakari hilo kwa muda. Una madai ya kisheria juu ya mali yote ya Mungu kama mmoja wa wana au binti Zake. Sasa, subiri kidogo. Paulo hakomi hapo. Aliendelea kusema kwamba

sisi ni warithi pamoja na Kristo. Mrithi mwenza inazungumzia mpangilio tofauti na ule ambao watu wengi hufikiria wanapofikiria urithi. Kwa kawaida tunafikiria urithi kuwa kitu kinachogawanywa kati ya warithi. Lakini hapa neno mrithi linamaanisha **kushiriki kwa pamoja**. Hii ina maana kwamba warithi wote wanashiriki katika urithi sawa; wote ni wamiliki. Kwa mfano, mume na mke wakinunua nyumba, huenda wataisajili kuwa wapangaji kwa pamoja, kumaanisha kwamba wote wawili wanaimiliki kwa pamoja. Mmoja wao akifa, hakutakuwa na kesi ya kuthibitisha chochote. Mwenzi aliye hai ataendelea kuimiliki. Mchakato huo wa kuthibitisha huhakikisha kwamba mtu ana madai halali kisheria juu ya mali. Mali inapomilikiwa kwa pamoja, watu wote wawili ni wamiliki, kwa hivyo hakuna kinachobadilika mmoja wa wanandoa anapokufa. Hakuna mkanganyiko, hakuna kupigania nani anamiliki nini, hakuna changamoto za kisheria. Mwenzi aliyebaki huendelea kumiliki nyumba nzima.

**UNA MADAI YA KISHERIA JUU YA MALI YOTE YA MUNGU KAMA MMOJA WA WANA AU BINTI ZAKE.**

Fikiria kuhusu kile ambacho nimesema hivi punde. Wewe ni mrithi wa Mungu na mrithi pamoja na Yesu. Chochote alicho nacho Yesu, nawe unacho pia. Kwa hivyo, kumbuka, una madai ya kisheria juu ya mali yote! Kwa hiyo, acha kuomba-omba kwako, kunung'unika, kulia, na sala zako za huzuni, ukitumaini kupata usikivu wa Mungu. Koma.

**Tayari una dai la kisheria juu ya mali yote!**

Hatuombi kana kwamba sisi ni yatima! Tunaketi mezani mwa Baba, na tunaweza kusema kwa ujasiri, "Pitisha biskuti." Kwa hakika, Yesu alisema kwamba uponyaji ni mkate wa watoto katika Marko 7:27, hivyo pitisha uponyaji. Kwa kweli, kuna ahadi zaidi ya 7,000

katika Biblia, na zote ni ndiyo na amina kwako. Basi furahia yote; tayari ni yako! Nafikiri Paulo alifupisha ukweli huu vyema katika Wafilipi 4:6-7.

**Huna haja ya kuwa na wasiwasi juu ya chochote!**

> *Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*
>
> —Wafilipi 4:6-7

Usijisumbue! Kwa nini? Kwa sababu huna haja ya kuwa na wasiwasi ikiwa unaweza kupata jibu. Paulo alisema, "Lakini katika kila neno…" Una jibu. Nafikiri hiyo inajumuisha shida au hitaji lolote unaloweza kukutana nalo. Kisha alituambia jinsi ya kushughulikia mahitaji yetu au cha kufanya tunapohitaji msaada katika hali yoyote. "*Katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.*" Nafikiri watu wengi wanaelewa zaidi kuhusu maombi, kwa njia moja au nyingine. Nitazungumza zaidi kuhusu hilo baada ya muda mfupi, lakini nafikiri watu wengi wanaelewa kwamba maombi ni kuzungumza na Mungu.

Ni sehemu inayofuata ambayo nafikiri Wakristo wengi wana shida nayo, na wengi hawajui Paulo anazungumzia nini. Nazungumzia hilo neno kuomba. Neno hili hapa linamaanisha hati rasmi, iliyoandikwa kuomba haki au manufaa kutoka kwa mtu au kikundi kilicho katika mamlaka au maombi rasmi ya

***"KATIKA KILA NENO KWA KUSALI NA KUOMBA, PAMOJA NA KUSHUKURU, HAJA ZENU NA ZIJULIKANE NA MUNGU."***

kimaandishi ya kutaka mahakama kuingilia kati na kuchukua hatua kuhusu jambo fulani. Kuomba haki au manufaa? Hiyo inaonekana kwamba ni ombi mahususi sana kulingana na hadhi ya kisheria au uhusiano. Je, unaweza kufikiria kuomba mahakama kusikiliza kesi yako, na hakimu anakuuliza kwa nini uko hapo? Unajibu, "Naam, nina mahitaji fulani." "Sawa," hakimu asema, "unahitaji nini, na unafikiri kwa nini mahakama hii inapaswa kusikiliza ombi lako?" Unajibu, "Nina mahitaji fulani tu; ni hayo tu." Unacheza? Huna hadhi ya kisheria katika mahakama hiyo ikiwa huwezi kutoa uthibitisho wa haki yako ya kisheria kuwa hapo na kwa nini hasa uko hapo. Hakimu atakufukuza tu; huo utakuwa mzaha.

Lakini, bila shaka, una msimamo ufaao wa kisheria katika mahakama ya mbinguni. Kwa nini? Kwa sababu kama raia wa Ufalme huo mkuu, tayari una dai la kisheria kwake. Lakini turudi kwenye neno hilo kuomba. Tunaelewa kwamba tunahitaji kuomba, lakini ombi letu ni nini? Kwa kuzingatia ufafanuzi wa neno dua tulilotaja hapo awali, jibu lako lingekuwa lipi? Je, ombi lako rasmi na lililoandikwa lingeonekanaje? Je, utaandikaje ombi rasmi la kutaka mahakama kuingilia kati na kuchukua hatua kuhusu jambo fulani? Nafikiri utakubali litakuwa lenye undani mkubwa.

Naweza kukuambia jinsi watu wengi wanavyosali—kwa maombi yasiyoeleweka sana huku wakisema "ikiwa ni mapenzi Yako." Hawana uhakika kuhusu msimamo wao kisheria, wala kuwa na uhakika ni nini kilicho chao hasa. Ikiwa mtu haelewi mambo hayo mawili wakati anapoomba, basi kilichobakia kufanya ni kuomba-omba tu. Hebu nikusaidie: **Koma.** Huwezi kamwe kuruhusiwa kuingia mahakama bila ombi lenye undani sana, pamoja na taarifa za kisheria zilizoandikwa ili kuthibitisha kwamba ombi lako kwa mahakama ni la kisheria na la haki.

Wakristo wengi hawajui hadhi yao kisheria, hawajui jinsi ya

kuiomba mahakama ya mbinguni kwa msingi huo, wala kujua kilicho chao kihalali katika Ufalme. Wengi hukasirika ninapozungumza na kufundisha kuhusu kanuni hizi. Huwa wananiambia ni kukosa heshima kudai chochote kutoka kwa Mungu. Hatudai chochote kutoka kwa Mungu. Tunasema tu, "Pitisha biskuti." TAYARI biskuti ni zako; Mungu amekupa tayari. Yeye huchukizwa wakati hatupokei anachotupa.

Ikiwa ningekuwa na amana kubwa katika benki yangu na nikaenda humo kutoa pesa, kisha wakala wa benki akaniambia kwamba siruhusiwi kutoa pesa yangu, ningefanya nini? "Oh, samahani kwamba nilikusumbua. Ni upumbavu ulioje kwangu kuomba ombi kama hilo kutoka kwa benki yenye hadhi kama hii." Je, hivyo ndivyo ningefanya? LA HASHA! Ningedai pesa yangu; tayari ni yangu. Ninapoenda benki kutoa pesa, huwa nina taarifa ya kina. Sisemi, "Nyinyi mnajua kilicho bora zaidi. Nipe kiasi fulani cha pesa; amueni."

**Ombi linapaswa kuwa na maelezo mengi, lakini hilo haliwezekani ikiwa hujui ulicho nacho.**

Hebu nikupe mfano wa ombi mahususi. Miaka mingi iliyopita, tulipokuwa tukijifunza kuhusu utendaji wa Ufalme, nilitaka pikipiki. Wakati huo tulikuwa tungali tunaishi katika nyumba ile nzee ya mashambani, na hatukuwa na karakana. Kwa hivyo, nilitoa matoleo kama mbegu ya pikipiki mpya aina ya Honda ST 1100 ambayo niliona siku moja na nikafikiri ilionekana kama baiskeli nzuri ya kumiliki. Hata hivyo, nilipotoa mbegu yangu hiyo, niliandika kwenye hundi yangu kwamba sitaki ije hadi nitakapokuwa na karakana nzuri ya kuiweka. Kwa sababu sikutaka kuiweka nje, mahali ambapo ingeathiriwa na hali ya hewa. Mchungaji wangu wakati huo alipenda sana kuendesha pikipiki. Kila mwaka, nilimwandikia hundi ya $300 na ningeandika kwenye hundi: Pesa ya mafuta ya pikipiki yako na mbegu kwa ajili ya ST 1100 yangu. Pia nilinunulia wachungaji wengine na

marafiki pikipiki tatu zilizotumika, wakati wote huo nikisema hiyo ilikuwa mbegu yangu ya ST 1100.

Naam, baada ya kujenga nyumba yetu, tulikuwa na karakana nzuri. Siku moja, wanandoa wawili walikuja nyumbani kwangu wakiwa na ST 1300 mpya na kunipa kwa ajili ya siku yangu ya kuzaliwa. Kampuni ya Honda ilikuwa imeunda upya modeli 1100 na kuipa injini mpya yenye nguvu zaidi—Honda ST 1300. Hii ilikuwa haswa ndoto niliyokuwa nayo. Ilikuwa pikipiki ya kushangaza ambayo niliendesha kwa miaka 14. Tangu wakati huo nimeibadilisha na Harley Ultra Limited ambayo mimi hutumia kutalii. Lakini nataka ujue ombi langu lilikuwa maalum kiasi gani, na hilo ndilo hasa lililojitokeza. Na ndivyo itakavyokuwa kila wakati unapoomba.

Ninaweza kukuambia hadithi nyingi sana za jinsi Ufalme ulivyo mahususi mno na jinsi ombi lako linavyohitaji pia kuwa mahususi. Miaka michache iliyopita, kanisa letu lilikodisha magari kadhaa aina ya Escalade kwa ajili ya mkutano tuliokuwa nao. Tulizikodisha ili kusafirisha wageni wetu humo, na tulitaka gari zuri za kufanya hivyo. Hii haikuwa mara ya yetu ya kwanza kufanya hivyo. Sisi hufanya hivyo kila wakati. Lakini ilikuwa mara yangu ya kwanza kuendesha gari aina hiyo maana tulikuwa nazo kanisani kwa ajili ya mkutano wetu. Ingawa sijui ni kwa nini tuliamua kuendesha gari moja wakati wa mkutano wetu huo, tuliipeleka nyumbani kwetu ikakaa hadi asubuhi. Na unajua nini? Niliipenda. Mimi na Drenda tulipenda jinsi ilivyokuwa tulipoiendesha na mwonekano wake.

Wakati huo, tulikuwa tukiendesha gari nzuri aina ya *Honda Pilot*, lakini hii *Escalade* bila shaka ilikuwa hatua moja juu ya gari letu. Ilikuwa ya rangi ya lulu nyeupe ya platinamu na ilikuwa na muundo mfupi. Ikiwa unajua mengi kuhusu magari haya, kuna yale yenye muundo mrefu na pia mfupi. Tulipenda lile fupi zaidi maana tulihisi ilikuwa rahisi zaidi kuliendesha na kuligeuza. Nilipokuwa nikiliendesha nikiwa

na Drenda, alisema, "Wajua, napenda gari hili; nafikiri tunafaa kuwa na moja kama hili." Nilikubali. "Tunapaswa kuwa na moja kama hili, lenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe." Sote wawili tulikubali.

Ingawa hatukumwambia mtu yeyote kuhusu mazungumzo yetu, mwezi mmoja baadaye, nilipokuwa nikienda nje kuchukua jarida langu, simu yangu ya rununu ililia. Niliitambua sauti ya aliyenipigia simu kama mshirika wa kanisa langu. Alisema, "Hujambo," kisha akasema kwamba alitaka kuninunulia gari aina ya Escalade. Nilistaajabu kwa dakika moja lakini nikasema, "Vema!" Kisha akaniuliza ningependa rangi gani, nami nikamwambia kwamba tulilipenda lenye rangi ya lulu nyeupe. Akasema, "Nitakupigia simu tena nitakapolipata." Hata hivyo, hakuniuliza ikiwa nilitaka lile fupi au ndefu.

Mwezi ulipita nikadhani labda alikuwa amesahau kuhusu gari, lakini hakika, alipiga simu na kutuambia tupitie kwake, kwamba gari aina ya *Escalade* lilikuwa tayari kuchukuliwa. Tulipokutana naye, tuliona *Escalade* yenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe ikiwa imeegeshwa hapo. Ilikuwa kamilifu kwa kila njia, na bila mkwaruzo. Tulimwambia tuliipenda. Kisha akaomba msamaha, akasema alisikitika ilichukua muda mrefu, kwamba ingawa alikuwa amejaribu kutafuta muundo mrefu, aliloweza kupata ni lile fupi tu. Tulicheka na kusema, "Lile fupi ndilo tulilotaka." Tuliliendesha gari hilo hadi nyumbani na tulijihisi kama matajiri zaidi duniani kuliendesha.

Ninaweza kujaza kitabu hiki na vielezi vya jinsi Ufalme ulivyo wa pekee. Wafilipi inapozungumzia ombi, inamaanisha hilo haswa. Si kuomba-omba; ni kufanya ombi. Sio tofauti na mmoja wa watoto wangu akisema, "Baba, pitisha biskuti." Watoto wangu hawaniombi-ombi chakula wanachokula. Wanafanya kama wamiliki, na hakika ndicho walicho.

Napenda jinsi Sala ya Bwana inavyotufundisha kuomba, na nafikiri inaweka wazi mfano mwingine mzuri wa mtazamo tunaopaswa kuwa

nao katika maombi. Kwa urahisi sana, inasema, "*Utupe leo riziki yetu.*" Ni maneno ya moja kwa moja, sivyo? Yesu aliwakemea watu wa kidini kwa sababu walikuwa wakiomba na kuendelea na maombi marefu, wakitumaini tu kwamba Mungu angewafanyia jambo fulani.

> *Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba.*
>
> *Basi ninyi salini hivi:*
>
> *"Baba yetu uliye mbinguni, jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje, mapenzi Yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu.*
>
> —Mathayo 6:7-11

Najua maombi yaliendelea zaidi ya yale ambayo nimenukuu hapa, lakini nimenukuu vya kutosha ili kufafanua hoja yangu. Walidhani wangesikilizwa kwa sababu ya maneno yao mengi. Hilo linakuambia nini? Hawakujua hadhi yao kisheria mbele ya mbingu, na cha kusikitisha ni kwamba, ndivyo ilivyo leo kwa wengi pia. Yesu aliposema walidhani wangesikiwa kwa sababu ya maneno yao mengi, neno kusikiwa hapa halimaanishi kwamba Mungu hasikilizi. Yeye husikiliza kama hakimu anavyosikiliza kesi. Kisha Yeye huishughulikia kesi hiyo na haki inatendeka. Kwa sababu hawakuelewa hadhi yao kisheria katika mahakama za mbinguni, kilichobaki ni kuomba tu kwa sala ndefu, wakitumaini kwamba Mungu angewafanyia jambo fulani. Na Yesu alisema nini kuhusu hilo? **Koma!** Omba hivi.

Kumbuka, Sala ya Bwana ni kiolezo kinachotufundisha jinsi ya kuomba. Mara nyingi, watu huinukuu tu kana kwamba ni maombi

ya kawaida. La, Mungu anakuonyesha jinsi ya kuomba. Maombi huweka hadhi yako kisheria katika mstari wa kwanza: "Baba yetu." Yeye ni Babako, jambo ambalo linamaanisha kuwa una dai la kisheria na haki ya kupokea kutoka Kwake. Kisha inaendelea na kukuelekeza jinsi ya kuleta maombi yako mbele Zake. Upo hapo ili kudai kile ambacho mbingu inasema ni chako, na sasa ombi lako litaleta dai hilo la kisheria duniani kutoka milki ya mbinguni. Unapoomba, usiombe rehema, bali omba, "Nipe leo riziki yangu." Tazama kwamba hakuna kuomba-omba katika kauli hiyo. Ni rahisi na hakika: Pitisha biskuti. Unaweza kweli kutamka chochote unachohitaji. Tena, ni kiolezo cha jinsi ya kuomba, na hairejelei kitu kimoja tu. Inasema:

**Nipe leo riziki yangu.**

Ombi lako linaleta kilicho mbinguni duniani, jambo ambalo linapatana kabisa na yale ambayo Yesu alifundisha.

> *Amin, nawaambieni, yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote **mtakayoyafungua** duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*
>
> — Mathayo 18:18

Hebu nifafanue yale ambayo tumesoma. Hakuna kitu kilicho mbinguni kitakachojitokeza hapa Duniani katika maisha yako usipotoa madai yake ya kisheria! Kwa nini? Kwa sababu mbingu haina mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Miaka kadhaa iliyopita, nilikuwa na msichana fulani katika kanisa langu ambaye alikuwa na shida na roho ya woga. Siku moja nilipokuwa nikizungumza naye, nilikuwa nikijaribu kutafuta mzizi, mlango ambao Shetani alikuwa ameutumiakumtesa. Kisha akaniambia kwamba alipokuwa mdogo, alilelewa katika nyumba tajiri na alikuwa na chumba cha kulala cha kifahari. Kitanda chake kilikuwa na mito ya

kupendeza, na kitanda kilistaajabisha. "Juu ya kitanda chake kulikuwa na wanasesere wa ajabu zaidi," alisema. Lakini ingawa alikuwa na hayo yote chumbani mwake, hakuwahi kulala humo. Ilimbidi alale kwenye chumba chini ili asichafue chumba chake. Mamake alikuwa akimfukuza kutoka ndani ya nyumba asubuhi na hakumruhusu kuingia hadi jioni, na kisha tu baada ya kuvua viatu vyake na kuhakikisha kwamba hakuna majani ya nyasi kwenye nguo zake. Kwa hiyo, ingawa msichana huyo mchanga alikuwa na wazazi matajiri na alikuwa na vitu vya kupendeza, hangeweza kuvifurahia na ilimbidi kuishi kama yatima. Inasikitisha jinsi gani. Si ajabu kwamba binti huyu alikuwa na wakati mgumu sana kupokea kutoka kwa Mungu na alipambana na woga na mshuko wa moyo. Lakini, namshukuru Mungu, kupitia kwa kuzoeza akili yake mara kwa mara, alitoka katika gereza hilo la woga, na wewe pia unaweza. Ili kuwa huru kutokana na uwongo wa utamaduni wa kidini na kuelewa kikamilifu wewe ni nani na una nini, utahitaji pia kupanga upya akili yako.

**HAKUNA KITU KILICHO MBINGUNI KITAKACHOJITOKEZA HAPA DUNIANI KATIKA MAISHA YAKO USIPOTOA MADAI YAKE YA KISHERIA!**

> *Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
>
> —Warumi 12:1-2

Naomba radhi dakika moja, lakini ninahitaji kuwa mkweli hapa. Hutaweza kamwe kupokea urithi wa Mungu hadi utakapoondoa uwongo wa dini akilini mwako na kuweka ukweli kuhusu utambulisho wako katika Ufalme. Paulo alijua hili alipoliandikia kanisa la Efeso kuhusu jambo hili hili.

> *Kwa sababu hiyo mimi nami, tangu nilipopata habari za imani yenu katika Bwana Yesu, na pendo lenu kwa watakatifu wote, siachi kutoa shukrani kwa ajili yenu; nikiwakumbuka katika sala zangu, Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua Yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito Wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi Wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza Wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza Wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono Wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia.*
>
> —Waefeso 1:15-21

Paulo anasema, "*macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito Wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi Wake katika watakatifu*. Kutiwa nuru kunamaanisha kuangaziwa. Aliomba kwamba Roho Mtakatifu atusaidie kuona jinsi urithi tulio nao katika Kristo ulivyo mkubwa. Aliuita urithi mtukufu! Urithi wetu katika Kristo ni urithi wa kiroho, bila shaka, lakini pia ni urithi wa kimwili hapa ulimwenguni.

Nilifikiri nisuse tu sehemu ndogo kuhusu urithi wetu ambayo

Wakristo wengi hawaelewi—baraka ya Ibrahimu. Baadhi ya watu wanafikiri kwamba kwa sababu tuna Agano Jipya kwamba faida zote za Agano la Kale zimebatilishwa—si kweli.

> *Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba* ***baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo****, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.*
>
> —Wagalatia 3:13-14

Kwa hivyo baraka ya Ibrahimu ni nini hasa? Nafikiri unahitaji kujua kwa kuwa unayo.

Tukirudi nyuma, hapo mwanzo dunia ilipoumbwa, Mungu aliwaweka Adamu na Hawa juu ya dunia ili kuitawala kwa niaba ya Ufalme Wake. Shetani, ambaye tayari alikuwa ametupwa chini duniani, alitamani mamlaka ambayo mwanadamu alikuwa amepewa. Kisha Shetani akaweka mpango wa kuwadanganya Adamu na Hawa wamfuate. Kwa kuwadanganya kuhusu tabia ya Mungu na kuwaahidi maisha bora, Adamu na Hawa walichagua kwa hiari kumfuata Shetani na kumwacha Mungu. Kwa sababu Mungu alikuwa amewapa mamlaka kamili juu ya dunia, Mungu hangeweza kuwazuia (Waebrania 2:7-8). Matokeo? Tunapata hilo katika Mwanzo 3:17b-19.

> *Ardhi imelaaniwa <u>kwa ajili yako</u>; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

Dunia ililaaniwa, jambo ambalo linamaanisha kwamba dunia ilipoteza baraka za Mungu. Na tafadhali tazama kwamba Mungu alimlaumu Adamu kwa sababu ya jambo hili. Yeye hakuilaani dunia; bali Adamu. Hebu niseme hivi: Adamu alimfukuza Mungu kutoka kwa maisha yake! Dunia ambayo hapo awali ilikuwa ya kupendeza na ya kijani kibichi sasa ingetokeza miiba isiyohesabika. Adamu na Hawa, ambao walikuwa wakila kwa urahisi kutoka katika Bustani ya Mungu, sasa wangekuwa na maisha ya kuishi kwa taabu na kutokwa jasho lenye uchungu. Mungu alipoteza ushawishi Wake juu ya wanadamu maana Shetani alifanyika mungu wa ulimwengu huu.

> *Ambao ndani yao <u>mungu wa dunia hii</u> amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu Wake Kristo aliye sura Yake Mungu.*
>
> —2 Wakorintho 4:4

Matokeo mabaya zaidi ya uasi wa Adamu yalikuwa kwamba wanadamu wote, nasaba yake, walitengwa na Mungu na kuwekwa chini ya mamlaka ya Shetani. Katika hukumu yote ya Shetani, hakutaja jambo moja. Ilikuwa ni kwamba hukumu yake ilikuwa tayari imewekwa na hatima yake ilikuwa mahali paitwapo kuzimu. Sasa, mwanadamu, ambaye alikuwa amefanyika sehemu ya ufalme wa Shetani na kuwa chini ya mamlaka yake ya kiroho, angepelekwa huko pia. Huu haukuwa uamuzi wa Mungu. Ulikuwa wa Adamu. Kuzimu haikutayarishwa kamwe kwa ajili ya wanadamu, kama Mathayo 25:41 inavyosema.

> *…moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.*
>
> —Mathayo 25:41b

Watu wengi wanafikiri kwenda mbinguni au kuzimu kunatokana

na matendo yao, na ikiwa ni wema wa kutosha wataenda mbinguni. Lakini wacha niseme hivi kwa uwazi:

**Kwenda mbinguni au kuzimu hakuna uhusiano wowote na jinsi ulivyo mzuri au mbaya.**

Adamu alipomwasi Mungu, alichukua wanadamu wote kuzimu pamoja naye. Sitaki kuwa butu hapa, lakini inabidi. Kila mtu tayari anaenda kuzimu kwa sababu ya Adamu, na kuna njia moja tu ya kutoka. Njia pekee ya kuepuka hukumu hiyo ni kwamba jina lako liandikwe katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kilicho mbinguni. Na njia pekee ya hilo kutokea ni ikiwa unaamini Yesu ni yule ambaye alisema alikuwa na kuliitia jina Lake ili uweze kuokolewa.

> *Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.*
>
> —Matendo 2:21

Yesu aliita kitendo hiki kuzaliwa mara ya pili; na ikiwa hujaliitia jina la Yesu, ningekutia moyo ufanye hivyo sasa. Yesu alikuwa mpango wa Mungu wa uokoaji wa kurudisha uumbaji Wake katika Ufalme Wake ambako alikuwa amepanga mwanadamu kuishi. Lakini kwa sababu kila mwanamume, mwanamke, na mtoto ana uhuru wa kuchagua na ana mamlaka ya kisheria juu ya maisha yake mwenyewe, Mungu hawezi kumlazimisha yeyote apokee karama Yake ya bure ya uzima.

> *Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo Lake.*
>
> —Wakolosai 1:13

Adamu na Hawa walipoasi, Mungu alipoteza uwakilishi Wake duniani. Ilimbidi amtafute mtu mwingine ambaye angempa kiingilio ulimwenguni, ili aweze kuimarisha mpango Wake wa uokoaji. Mtu

huyo alikuwa Abramu, ambaye baadaye angeitwa Ibrahimu. Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, na Sara alikuwa amepita umri wa kupata mtoto. Lakini Mungu aliwatokea na kuwaambia kwamba hakika wangepata mwana. Ibrahimu alimwamini Mungu, na Mungu akafanya mapatano ya kisheria, kiapo, akamwapia Ibrahimu kwamba hilo lingetukia.

Agano hili kwa mara nyingine lingempa Mungu fursa ya kuwabariki wanadamu lakini kupitia kwa Ibrahimu na warithi wake tu, maana agano lilifanywa kati ya Mungu na Ibrahimu na warithi wake. Ilikuwa ni kupitia kwa agano hili na ukoo huu kwamba Yesu alikuja ulimwenguni. Kwa wengi, sura ya kwanza ya kitabu cha Mathayo ni orodha inayochosha sana ya wazawa, lakini ni rekodi ya kina sana ya nasaba ya Ibrahimu hadi kuzaliwa kwa Yesu. Sura hii haichoshi kama unavyofikiri kwa kuwa inathibitisha kwamba Yesu alikuja kupitia kwa ahadi hiyo kwa Ibrahimu. Imeandikwa ili kutoa ushahidi mbele ya mbingu na dunia, ili watu wote waone, na inathibitisha kwamba Yesu alikuja kihalali duniani. Ni muhimu hasa kwa Shetani, mungu wa ulimwengu huu ambaye angepinga uhalali wa Yesu, lakini uthibitisho upo kwa wote kuona.

Sawa, kwa kuwa sasa tunajua Ibrahimu alikuwa nani, hebu turudi kwenye mjadala wetu wa baraka ya Ibrahimu na jinsi hilo linavyotuathiri hapa katika Agano Jipya. Mungu alipofanya agano hilo na Ibrahimu, alitoa ahadi kwake. Mungu alimwambia kwamba angefanyika taifa kubwa na kwamba angebariki mataifa yote ya dunia kupitia yeye, jambo ambalo bila shaka, lilikuwa likirejelea uhakika kwamba Yesu angekuja kupitia ukoo wake. Mungu alisema kwamba angembariki Ibrahimu. Ahadi hizi ambazo Mungu alimpa zinaitwa baraka ya Ibrahimu.

Ni lazima tukumbuke kwamba Ibrahimu hakuzaliwa mara ya pili, kwa sababu Yesu alikuwa bado hajaja kulipa gharama ya dhambi, hivyo

Ibrahimu hangeweza kwenda mbele za Mungu. Lakini Ibrahimu alishikilia ahadi kwamba kupitia kwa uzao wake mwenyewe, Masihi angekuja na kulipa gharama ya wokovu. Hadi wakati huo, Mungu alimpa Ibrahimu ahadi zilizohusu ulimwengu, akitangaza jinsi ambavyo angembariki na kumpa ushawishi mkuu duniani.

Hadi wakati huo, Shetani alikuwa amemshikilia mwanadamu katika maisha ya utumwa na umaskini kutokana na dhambi ya Adamu. Lakini kupitia kwa ahadi za Ibrahimu, Mungu angeweza basi kisheria kufuta laana ya dunia ya uasi wa Adamu na kumbariki Ibrahimu. Badala ya Ibrahimu kuwekewa mipaka na kazi yake yenye uchungu na jasho, Mungu alitangaza kwamba angemfanya Ibrahimu kuwa mkuu na kumfanikisha.

Tunaposoma katika Wagalatia, ahadi hizi zingali halali kwetu leo—baraka ya Ibrahimu.

## SURA YA 4

# BARAKA YA IBRAHIMU

Kama nilivyosema katika sura iliyotangulia, kama muumini wa Agano Jipya, una urithi wa kiroho wa kuzaliwa upya lakini pia baraka ya Ibrahimu. Tena, baraka za Ibrahimu ni ahadi ambazo Mungu alimpa Ibrahimu ambazo ziliweka wazi yeye alikuwa nani, maisha yake ya baadaye, na utajiri mwingi ambao angekuwa nao siku moja. Ili kuweka msingi wa mjadala wetu, hebu turudi kwenye mstari huo katika Mwanzo 3:17-19 kuhusu uasi wa mwanadamu.

> *Ardhi imelaaniwa <u>kwa ajili yako</u>; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;* ***michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula****, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*
>
> —Mwanzo 3:17b-19

Laana ya Dunia—kwa taabu yenye uchungu na kwa jasho la nyuso zetu, tutapitia maisha. Kimsingi, uwezo wako chini ya mfumo huu utakuwa kadiri ya kazi yako mwenyewe. Bila shaka, sisi sote tulizaliwa chini ya mfumo huu wa unusuru na tumejizoeza kutathmini uwezekano wetu wa kufaulu kupitia kwa kichujio hiki—itatugharimu kazi kiasi gani? Lakini ahadi ambazo Mungu alimpa Ibrahimu katika

Mwanzo sura ya 12 zilibadili hayo yote.

> *Bwana akamwambia Abramu, "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."*
>
> —Mwanzo 12:1-3

Umeona mabadiliko? Mungu alisema,

***"Nitakufanya wewe kuwa!"***

Tafakari hilo. Mungu alisema, "Nitakufanya wewe kuwa" Ibrahimu. Hangekuwa mateka tena wa siku za usoni ambapo angepaswa kuunda au kutimiza mambo kupitia kwa taabu na jasho lake lenye uchungu. Mungu alikuwa akimwambia kwamba angemfanya. Kwa maneno mengine, Mungu alikuwa na mlango halali kupitia kwa imani ya Ibrahimu kumbariki. Mungu alikuwa amemuahidi Ibrahimu kwamba angembariki, kulifanya jina lake kuwa kuu, na kwamba angekuwa taifa kubwa. Pia Mungu alisema kwamba kupitia yeye, watu wote duniani wangebarikiwa, jambo ambalo lilikuwa likirejelea ukweli kwamba Yesu angekuja kupitia ukoo wake. Ahadi hizi ambazo Mungu alimpa Ibrahimu, kama nilivyosema, zinaitwa baraka ya Ibrahimu. Ili kuwa na uhakika kwamba Ibrahimu alifahamu jinsi ahadi hizi zilivyokuwa kuu, Mungu alimpa picha kadhaa za kile alichotaka kufanya kupitia yeye.

*Baada ya mambo hayo neno la Bwana likamjia Abramu katika njozi, likinena, "Usiogope, Abramu, Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana."*

*Abramu akasema, "Ee Bwana MUNGU, utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto, na atakayeimiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdameski?" Abramu akasema, "Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu."*

*Nalo neno la Bwana likamjia likinena, "Huyu hatakurithi, bali atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayekurithi." Akamleta nje, akasema, "**Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota**, kama ukiweza kuzihesabu." Akamwambia, "Ndivyo utakavyokuwa uzao wako."*

*Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki. Kisha akamwambia, "Mimi ni Bwana, niliyekuleta kutoka Uru wa Wakaldayo **nikupe nchi hii ili uirithi.**"*

—Mwanzo 15:1-7

Mungu alitumia picha mbili hapa kumsaidia Ibrahimu kufahamu ukubwa wa ahadi alizompa. Kwanza, alisema "hesabu nyota, ikiwa unaweza. Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Bila shaka, wakati wa mazungumzo haya, Ibrahimu hakuwa na mtoto hata kidogo. Pili, Mungu aliweka mipaka ya ardhi yote ambayo Ibrahimu angerithi, ambayo ilikuwa zaidi ya ekari milioni 35! Ardhi ambayo hangeweza kumaliza kutembea urefu na upana wake. Ili kufafanua jinsi urithi wa Ibrahimu ulivyokuwa mkubwa, hebu tuseme ulikuwa mkubwa kuliko jinsi angelivyoweza kukadiria!

Baraka hii ya Bwana iliyokuwa juu ya Ibrahimu ilikuwa na matokeo ya mara moja. Baada ya sura moja tu baada ya kupokea ahadi ya Mungu, tunaona mabadiliko makubwa.

> *Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu.*
>
> —Mwanzo 13:2

Kama ilivyo wazi, kwa kweli aliepuka mfumo wa laana ya dunia ya kazi chungu na jasho.

Sasa, hebu tuende mbele wakati Waisraeli walipokuwa wakitoka Misri kuelekea Nchi ya Ahadi. Kabla yao kuvuka kuingia katika Nchi ya Ahadi, Mungu alitaka waelewe jinsi urithi wao ungekuwa mkubwa. Aliwaambia haya kupitia Musa katika Kumbukumbu la Torati 6:10-12.

> *Tena itakuwa atakapokwisha Bwana, Mungu wako, kukuleta katika nchi aliyowaapia babu zako, Ibrahimu na Isaka na Yakobo, ya kuwa atakupa; miji mikubwa mizuri usiyoijenga wewe, na **nyumba** zimejaa vitu vyema vyote **usizojaza wewe**, na visima vimefukuliwa **usivyofukua wewe**, mashamba ya mizabibu na mizeituni **usiyoipanda wewe**, nawe utakula na kushiba; ndipo ujitunze, usije ukamsahau Bwana aliyekutoa nchi ya Misri, nyumba ya utumwa.*
>
> — Kumbukumbu la Torati 6:10-12

Nafikiri unaelewa hili; wangerithi haya yote bila kazi! Hebu tukumbuke kwamba Israeli walipotwaa ardhi hizi, ilikuwa ni hukumu juu ya watu walioishi humo maana walikuwa waovu sana.

> *Usiseme moyoni mwako, Bwana, Mungu wako, atakapokwisha kuwasukumia nje mbele yako, ukasema, "Ni kwa haki yangu alivyonitia Bwana niimiliki nchi hii;" kwani ni kwa ajili ya uovu wa mataifa haya Bwana awafukuza nje mbele yako. Si kwa haki yako, wala kwa unyofu wa moyo wako,*

> *hivi uingiavyo kuimiliki nchi yao; lakini ni kwa uovu wa mataifa haya Bwana, Mungu wako, awafukuza nje mbele yako; tena apate kuliweka imara hilo neno Bwana alilowaapia baba zako Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo. Basi jua ya kuwa Bwana, Mungu wako, hakupi nchi hii nzuri uimiliki kwa ajili ya haki yako, kwa maana u taifa lenye shingo ngumu.*
>
> —Kumbukumbu la Torati 9:4-6

Lakini hoja yangu iko katika sentensi ya kwanza ya Kumbukumbu la Torati 6:10, *"Tena itakuwa atakapokwisha Bwana, Mungu wako, kukuleta katika nchi aliyowaapia babu zako, Ibrahimu."*.

**Mungu atakuleta katika nchi.**

Sio kwamba ingewabidi wapigane ili kuingia humo huku wakiegemea nguvu zao wenyewe; Mungu angewaingiza humo Yeye mwenyewe.

**Nitakufanya wewe kuwa!**

Pengine mahali pazuri zaidi katika Biblia panapodhihirisha baraka za Ibrahimu ni katika Kumbukumbu la Torati 28. Tunaposoma jambo hili, tafadhali weka jina lako humo, kwa sababu ahadi hizi zote ni zako sasa kama zilivyokuwa zao wakati huo.

> *Itakuwa utakaposikia sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa bidii, kutunza kuyafanya maagizo Yake yote nikuagizayo leo, ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukuza juu ya mataifa yote ya duniani; na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako.*
>
> *Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani.*
>
> *Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako.*

*Litabarikiwa kapu lako, na chombo chako cha kukandia unga.*

*Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo.*

*Bwana atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako; watakutokea kwa njia moja, lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.*

*Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako.*

*Bwana atakuweka uwe taifa takatifu Kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia Zake. Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako.*

*Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa.*

*Atakufunulia Bwana hazina Yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati Wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe.*

*Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya; msipokengeuka katika maneno niwaamuruyo leo kwa lolote, kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto, kwa kuifuata miungu mingine na kuitumikia.*

—Kumbukumbu la Torati 28:1-14

Ndio, huyu ni wewe! Natumai sasa unaona ni kwa nini nilitaka

usome maandiko haya. Hakuna mawazo ya unusuru hapa hata kidogo. Chochote utakachofanya na mikono yako kitafanikiwa!

"*Bwana atakuweka uwe taifa takatifu Kwake.*" Kukuweka? Watu wengi hawajawekwa. Mti wa mwaloni ulio na umri wa miaka 100 umewekwa; hakuna anayeweza kuuhamisha! Lakini kwa watu wengi, dhana hiyo ni ya kigeni. Maisha yao yamejaa dhiki, huku wakijaribu kushinda hali ya ukosefu wa usalama inayowazingira. Hawana kitu! Wao hulipia kila kitu, na ikiwa hawajalipa, basi mmiliki wa kisheria huja na kuchukua mali zao. Kuwekwa kunamaanisha huwezi kuhamishwa, katika nyakati nzuri au mbaya.

Mungu aliwaambia Wasraeli kwamba hakuna mtu ambaye angeweza kuwahamisha kutoka kwa nchi yao wenyewe, na mkazo ni juu ya neno wenyewe. Kuwekwa kunamaanisha wewe ndiye mmiliki! Hakuna deni. Wewe ndiye mmiliki. Andiko linaendelea na kusema, "*Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako. Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri.*" Mungu alisema kwamba watakapoimarishwa, watu wataona kwamba wameitwa kwa jina la Bwana. Vipi? Mungu haonekani, kwa hiyo watu wasiomcha Mungu watamwonaje Mungu? Mstari wa 11 unatuambia, "*Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri!* Watauona utajiri wako na itawabidi wakiri kwamba Mungu amekubariki. Ikiwa hiyo haitoshi, andiko linaendelea na kusema, "*nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia.*" Utabarikiwa sana utakuwa mkopeshaji, sio mkopaji. Utakuwa kichwa na sio mkia.

**UTABARIKIWA SANA UTAKUWA MKOPESHAJI, SIO MKOPAJI.**

**Kutokuwa na Madeni! Hii ni sehemu ya urithi wako.**

Sasa, ninahitaji kukuuliza jambo. Ikiwa kile tulichosoma hivi

punde ni kweli, na ni kweli, na ikiwa nimekuthibitishia kwamba kama muumini wa Agano Jipya, una ahadi hizo hizo, je, hilo lingebadilisha chochote kuhusu maisha yako? Ikiwa ungepokea urithi wa dola bilioni moja leo kutoka kwa mjomba tajiri, je, ungebadilisha maisha yako ya siku za usoni? Nafikiri ndio.

> *"Imba, wewe uliye tasa, wewe usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele, wewe usiyekuwa na utungu; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake yeye aliyeolewa," asema Bwana.*
>
> *"Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako."*
>
> —Isaya 54:1-2

Tayari tumezungumza jinsi mwanamke anavyoweza kupata watoto wengi bila uchungu kuliko mwanamke anayepitia uchungu wa kuzaa. Sasa tunajua kwamba Isaya alikuwa akizungumzia kuzaliwa upya kiroho, kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Na tumeshagundua kwamba wanawake wawili wanawakilisha maagano mawili—agano la kale la utumwa, ambalo ni njia ya kawaida, na agano jipya na uzoefu wa kuzaliwa mara ya pili, ambayo hutubadilisha kwa nguvu za Roho. Matokeo ya agano hilo jipya yanaonyeshwa wazi katika kielelezo ambacho Isaya alitumia. Mwanamke mmoja anapata mimba na kujifungua mtoto kwa njia ya kawaida ya ujauzito wa miezi tisa. Lakini agano lingine halizuiliwi na mwili, linatungwa kwa ahadi, na huzaliwa kwa uwezo wa Roho. Sisi tumepewa njia hii isiyo na vizuizi, sio njia yenye mipaka. Hatuzuiliwi tena na uzoefu wetu au uwezo wetu. Kumbuka, Mungu ndiye aliyemuumba Ibrahimu. Hakuwa na uwezo wa kupata watoto, lakini Mungu alimwezesha kufanya hivyo.

Kumbuka hadithi yangu. Nilijaribu kwa miaka tisa kufanikisha biashara yangu, lakini sikufaulu. Pamoja na Mungu nilifaulu na sasa mimi ni milionea. Nilifikiri kwa sababu ya ratiba yangu isingewezekana kuwa katika kampuni 10 bora kote nchini kupitia kwa mmoja wa wachuuzi wetu. Nilikuwa nimezalisha takriban milioni 4 kwa muda wa miaka 14 mfululizo na sikufikiri ingewezekana kuwa moja ya kampuni 10 bora. Lakini niliweza kuingia katika kiwango hicho, na nimekuwa nikipokea hundi ya bonasi ya $100,000 ambayo kampuni 10 bora hupata, na imekuwa hivyo kwa miaka mingi mfululizo.

Binti yangu Amy alikuwa na uvimbe wa kilo 13 kwenye fumbatio lake, na ilionekana kwamba hakukuwa na njia ya kuepuka upasuaji, lakini alifanya hivyo. Usiku mmoja akiwa amelala, uvimbe ulitoweka. Alipoteza pauni 13; inchi 9 kiunoni; na mgongo wake, ambao ulikuwa na fundo na kupinda, uliumbwa upya kabisa.

Binti-mkwe wangu aliambiwa alikuwa na miezi minne ya kuishi maana alikuwa na uvimbe mkubwa kwenye sehemu ya makalio yake, lakini hakufa. Uvimbe huo ulitoweka usiku mmoja akiwa amelala pia.

Ninaweza kuendelea na kuendelea, lakini nafikiri umeelewa. Siku zako za usoni hazina kizuizi tena. Mungu anasema atakufanya uwe. Kwa sababu ya mabadiliko haya makubwa, Isaya alisema unahitaji kujiandaa kwa ajili ya ongezeko. Kumbuka, Ibrahimu aliambiwa kwamba urithi wake ulikuwa mwingi kiasi cha kutohesabika. Mungu ametangaza jambo hilo hilo kwako.

> *Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.*
>
> —Waefeso 3:20

**Mungu anaweza kufanya zaidi ya kile unachofikiri!!!**

Baada ya Isaya kutangaza kwamba agano hili jipya lingesababisha ongezeko lisilo la kawaida katika mstari wa 1 wa Isaya 54, alisema kile tunachohitaji kufanya ili kujiandaa kwa mavuno haya katika mistari minne inayofuata. Katika Alitaja mambo manne ya msingi tunayohitaji kufanya ili kupokea ongezeko hilo. Hizi ndizo kanuni nne za kwanza za kuongeza kasi!

Hebu nikupe mfano mwingine wa jambo hili. Mwaka wa 2021, kwa sababu ya ugonjwa wa Covid, uzalishaji wetu ulipunguka kidogo. Nilikuwa nimepanda mbegu na kumwomba Mungu kwamba 2021 uwe mwaka bora zaidi kuliko miaka yangu yote katika biashara. Ulikuwa msimu wa vuli wa 2021, na mambo hayakuwa yakisonga mbele kabisa ingawa hatukurudi nyuma, yalikuwa sawa tu. Lakini, sikuwa nimepanda mbegu ili mambo yawe sawa. Nilikuwa nimepanda mbegu ili kuwa na mwaka bora zaidi.

Mwanzoni mwa Novemba, nilikuwa na ndoto. Niliota kwamba mkoba wangu ulikuwa wazi, na ulikuwa umejaa pesa. Bwana alinena nami katika ndoto hiyo na kusema, "Bado ninaweza kufanya jambo kubwa kabla mwaka haujaisha." Ajabu, hilo lilinitia moyo kweli.

Baada ya majuma machache, kijana mmoja alinipigia simu na kusema kwamba alitaka kuzungumza nami juu ya uwekezaji wetu ambao alikuwa amesikia kuuhusu sana. Alikuwa amesikia kwamba katika zaidi ya miaka 20, hatukuwa tumewahi kupoteza pesa za mteja yeyote kutokana na mabadiliko ya soko. Alipoona jinsi mambo yalivyokuwa magumu nchini Marekani, alitamani kujua sababu. Kwa hiyo, nilikutana naye, nikamweleza mkakati wetu wa uwekezaji, na akaupenda. Naam, ili kufupisha hadithi ndefu, aliwekeza kiasi kikubwa cha pesa. Kwa sababu ya kuwa naye kama mteja, pamoja na wateja wachache zaidi wa dakika za mwisho, nilikuwa na mwaka bora zaidi kuliko yote katika biashara.

Ninachoweza kusema ni kwamba sheria za Ufalme na upako

wa kufanikiwa zilileta pesa hizo. Lakini hebu niseme kwamba pesa hazikujitokeza tu. Mimi ndiye niliyepanda mbegu ili kupokea pesa hizo, na ikawa kama nilivyoomba. Ajabu!

SURA YA 5

# KANUNI YA KUTAWALA

Kama nilivyosema katika sura ya 4, kutokana na agano hili jipya, mambo mengi hubadilika. Hebu niseme tena: Kila kitu kitabadilika! Baada ya Isaya kutabiri kuhusu agano hili jipya na kuzaliwa kwetu katika Ufalme wa Mungu, aliendelea kusema jinsi jambo hili linavyoweza kubadili jinsi tunavyoishi. Kuzaliwa mara ya pili hutupatia ufikiaji wa mali yote ya Mungu kama washiriki wa nyumba ya Mungu mwenyewe. Kama Ibrahimu, tunaepuka mfumo wa laana ya dunia na kubadilisha falme. Kama nilivyosema awali, mstari wa 2 una kanuni nne za kwanza za kuongeza kasi. Kanuni hizi nne ndizo kanuni Mungu alizonionyesha tulipokuwa katika hali mbaya ya kifedha tulipokuwa tukijenga *The Now Center.* Ni dhana zenye nguvu sana ambazo zitakusaidia kuharakisha biashara yako au chochote unachohitaji kuona kikisonga mbele haraka. Hebu tuanze na kanuni ya kwanza ya kuongeza kasi—**kanuni ya kutawala**.

> *Panua mahali pa hema yako, na wayatandaze mapazia ya maskani yako; usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako.*
>
> —Isaya 54:2

**Panua mahali pa hema yako.**

Hili ndilo agizo la kwanza ambalo Mungu alitoa: Panua mahali pa

hema yako, si hema yenyewe bali mahali pa hema. Hema inawakilisha maisha yako, na mahali panarejelea maono kuhusu maisha yako. Badala ya kuishi na mtazamo wa robo ekari, Isaya alisema kwamba utahitaji nafasi nyingi zaidi, ili kuweza kupokea yote yaliyo katika urithi wako. Kanuni hii inasema panua mahali unapoishi, ongeza eneo lako, utawala wako. Kumbuka, Mungu anaweza tu kubariki kile kilicho chini ya mamlaka yako ya kisheria.

**Chaguo litakuwa ni lako!**

Kumbukumbu la Torati 28:8 inasema:

> *Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako.*

Baraka ni yako, lakini tena, ikiwa kitu hakiko chini ya mamlaka yako, basi Mungu hana mamlaka ya kisheria juu yake. Kwa hivyo hapa kuna swali: Je! unataka mimea 3 ya nyanya iliyobarikiwa au 50,000? Ikiwa ungejua kwamba chochote utakachoweka chini ya upako huo kitafanikiwa, ungeweka kiasi gani hapo? Unaweza kujaribiwa kurudi katika mtazamo wa zamani na swali hilo. Mafunzo yetu ya kukataa kabla ya kukubali yanaweza kutaka kurudi kwetu hapa. Lakini hauko peke yako katika uamuzi huu. Biblia inasema kwamba unaweza kumwomba Mungu akusaidie.

> *Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na **hekima**, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.*
>
> —Yakobo 1:5

Lakini watu wengi huwa hawafikii kiwango hiki kwa vile mafunzo

yao ya kukataa hufunga mlango kabla hawajafikiria kwamba Mungu anajaribu kuwaletea kitu. Ninajua. Nimefanya hivyo pia mara nyingi, na imenigharimu maelfu ya dola.

Kwa mfano, nilipitia jambo kama hili takriban mwaka mmoja au zaidi uliopita ambalo lilionyesha wazi mtazamo huu mbaya. Ninahitaji kuwa macho sana maana jambo hili hujitokeza virahisi. Hata sasa baada ya miaka yote hii, nisipokuwa mwangalifu, mtazamo huu unaweza kuongoza uamuzi wangu.

Siku moja, nilitafakari 2 Wakorintho 9:10-11 bila kukoma. Nilijua Bwana alitaka kunifundisha jambo fulani, kwa hivyo nilitafakari Maandiko haya huku nikimruhusu Roho Mtakatifu anene nami kuyahusu. Sehemu ya Maandiko iliyokuwa akilini mwangu ilikuwa, "*Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula.*"

> *Na **<u>Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa</u>** mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*
>
> —2 Wakorintho 9:10-11

Nilipoendelea kuwaza juu ya Maandiko haya, ilionekana kwamba Roho Mtakatifu alianza kuangazia, "na mkate uwe chakula," sehemu hiyo ilinirukia tu. Nilitambua kwamba watu wengi hukabiliwa na hofu wanapotaka kutoa kwa sababu hawaelewi maneno haya. Watu wengi hufikiri kwamba wanapotoa, wanaacha kitu fulani, na kwamba hilo litawagharimu. Lakini kile Mungu alikuwa akinikumbusha ni kwamba sio tu kwamba Yeye hutoa mbegu ya kupanda, na pia mkate kwa ajili ya chakula, yaani mahitaji ya kibinafsi. Bila shaka, tayari nilijua hilo, lakini nilihisi kwamba alitaka kuhakikisha kuwa

ninawaambia watu hivyo, ili waelewe kwamba Yeye hutupa sisi yote mawili na hawahitaji kuogopa kutoa.

**YEYE HUTOA MBEGU YA KUPANDA, NA PIA MKATE KWA AJILI YA CHAKULA, YAANI MAHITAJI YA KIBINAFSI.**

Usiku mmoja, wiki kadhaa baada ya kupanda mbegu ya dola 15,000, nilikuwa karibu kuzima taa na kuelekea kitandani wakati, ghafla, nilikuwa na wazo la kuangalia hisa chache ninazomiliki ili kuona jinsi zilivyokuwa zinaendelea katika soko la hisa. Nilipofungua akaunti yangu, niliona kwamba zilikuwa zimeongezeka kidogo. Nilipotaka kuweka simu yangu chini, macho yangu yalivutiwa na hisa fulani ambayo sikuimiliki. Nilikuwa nimeiona mara moja hapo awali, na kuwa na wazo la kuinunua. Nilipochunguza utendakazi wake wa siku za nyuma, niliona haikuwa na ongezeko lolote kwa miezi 12, kwa hivyo niliamua kutoinunua. Lakini kwa sababu moja au nyingine, usiku huo, hisa hii ilinivutia. Ajabu ni kwamba nilihisi nilipaswa kununua kiasi fulani cha hisa hiyo, jambo ambalo halikuwa kawaida kwangu. Kwa hivyo, nilinunua hisa ya thamani ya $1,500 na kuweka simu yangu chini.

Drenda na mimi tulizungumza kwa muda mfupi, kisha nikamwambia kwamba nilikuwa nimenunua hisa hiyo, na nikafungua simu kumuonyesha. Nilipoifungua nilishtuka. Ilikuwa imepanda zaidi ya asilimia 100 kwa saa moja tu! Tulikaa macho na kuongea huku tukitazama thamani yake ikiendelea kupanda taratibu.

Kwa muda wa masaa tatu yaliyofuata, hisa ilipanda hadi thamani ya zaidi ya $17,000, kisha ikatulia. Nilimwambia Drenda, “Hizo ni dola zetu 15,000!”

Niliuza hisa hiyo haraka na kupata faida hiyo. Asubuhi iliyofuata thamani ya hisa hiyo ilipungua na haijaongezeka tena kwa kiwango

hicho kwa miezi kadhaa tangu wakati huo. Lilikuwa jambo la ajabu sana kuona. Ninajua kwamba ni Roho Mtakatifu aliyeniangazia hisa hiyo, na nilimwambia Drenda ni Mungu aliyekuwa anarudisha mbegu yetu. Mungu humpa mpanzi mbegu, naye hutoa mkate kwa ajili ya chakula! Unajua, sijali jinsi anavyofanya, lakini Yeye hutimiza neno Lake kila wakati. Lakini lilikuwa jambo la kushangaza kweli.

Baada ya kuuza hisa hiyo na kurejesha pesa kwenye akaunti yangu, niliwaza, *Jamani, kama ningejua ingepanda hivyo, ningenunua zaidi ya $1,500*. Daima mtu unapotazama nyuma ndipo unapoona kwa udhahiri kabisa. Ndio, ningenunua hisa ya $10,000, au akili yako inaweza kuyumbayumba na kuwaza, *Je, kama ningenunua hisa ya $100,000? Fikiria kiasi cha pesa ambacho ningepata kutokana na uwekezaji huo*. Lakini sikununua hisa ya $100,000, $10,000 au hata $5,000; bali ya $1,500. Faida yangu ilizuiliwa. Nilinunua hisa ya $1,500, na ingawa nina hakika ningependa faida zaidi, hilo halingefanyika kwa sababu nilinunua hisa ya $1,500 pekee. Kwa hiyo, ni nini kilitokea? Ndio nilipata nusu yake. Nilihisi kununua hisa hiyo, lakini sikumuuliza Bwana kiasi cha kununua. Niliruhusu mtazamo wangu wa kawaida katika ubongo wangu kufanya uamuzi huo bila mimi kufikiria juu yake. Ndio, nilivuna mbegu yangu ya kwanza ya $15,000 tena, lakini sikupata nusu ya pili ya ahadi hiyo.

> *Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula,* ***atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu.***
>
> —2 Wakorintho 9:10

Sikupata ongezeko na mavuno yaliyozidishwa ambayo nilipaswa kuwa nayo. Mungu alikuwa na mengi zaidi aliyokuwa ameniandalia usiku ule, sio tu kurudisha mbegu yangu, ingawa hilo lilikuwa

jambo zuri. Lakini sikumuuliza Mungu kiasi cha kuwekeza na hivyo nikakosa ongezeko ambalo lingekuwa langu kama ningeuliza. Kwa nini sikumuuliza Mungu? Nilikuwa na shughuli nyingi na sikuifikiria hisa hiyo sana hadi thamani yake ilipopanda kama mshale. Ni rahisi kuruhusu mtazamo wa zamani kutuelekeza, lakini tunaweza kubadili mtazamo wetu wa kimsingi na kukoma na kuzingatia ili tusiwe na fikra za kuamua haraka. Omba hekima kutoka kwa Mungu katika hali kama hii, na utaona matokeo makubwa.

Bwana alinenana nami siku moja: "Usifanye mipango midogo!"

**KUNA MENGI ZAIDI!**

Watu wengi sana hukosa fursa nyingi sana ambazo Mungu huweka mbele yao. Wanapanda mimea mitatu ya nyanya, na inapozaa vyema, wanasema, "Jamani ningepanda zaidi." Na kama nilivyokuonyesha, ni rahisi kufanya hivyo.

Hebu tuangalie baadhi ya mistari kuhusu Ibrahimu katika kitabu cha Mwanzo.

> *Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, "Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi; maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele. Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi; hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, uzao wako nao utahesabika. Ondoka, ukatembee katika nchi hii katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo."*
>
> —Mwanzo 13:14-17

Tazama Mungu alisema *"Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo... nitakupa wewe na uzao wako hata milele."* Kisha katika

mstari wa 17, alisema, *"Ondoka, ukatembee katika nchi hii katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe."*

Kuna hatua tatu muhimu ambazo Bwana alimwonyesha Ibrahimu. Kwanza, tazama! Ndio, kutoka kwa upande wako unaweza kusema, "Vema, sina mali mengi." Hakusema utazame kile ulichonacho bali uanze kutoka mahali ulipo. Yote unayoyaona, atakupa. Mara nyingi hapa ndipo tunapokosea. Tunahitaji kuzingatia kumruhusu Mungu kunyoosha mtazamo wetu ili tuweze kuona mbali zaidi. Kuona kutoka mahali tulipo kunagharimu kupata picha fulani mawazoni; vinginevyo, tutaona pale tulipo tu.

**TUNAHITAJI KUZINGATIA KUMRUHUSU MUNGU KUNYOOSHA MTAZAMO WETU ILI TUWEZE KUONA MBALI ZAIDI.**

Kwa hivyo, kanuni ya kwanza tunayohitaji kujua vyema ni kanuni ya kutawala. Hii ndiyo ya kwanza kati ya kanuni tisa za kuongeza kasi. Kamwe huwezi kuinuka juu zaidi ya kile unachoweza kuona. Basi hebu tukome na kujibu swali lifuatalo: Je, unaona nini? Kamwe huwezi kufuatilia usichokiona!

Mungu alikuwa akimwambia Ibrahimu, "Tazama, nami nitakupa hayo yote." Tazama kwamba alisema "nitakupa yote hayo," si "nimekupa hayo yote." Yote yalikuwa yake kuchukua, lakini Ibrahimu alikuwa na sehemu yake ya kutimiza kwanza. Ikiwa Ibrahimu hangetimiza sehemu yake, Mungu hangefanya chochote maana hakuwa na mamlaka juu ya nchi hiyo. Angeweza tu kumpa ardhi aliyoikanyaga na miguu yake. Kwa nini? Kwa sababu Ibrahimu alikuwa amebarikiwa, ametiwa mafuta, na kuwa na mamlaka ulimwenguni kuleta nchi hiyo chini ya mamlaka ya mbinguni.

Na sehemu ya mwisho kuhusu jambo hili ni kwamba kamwe huwezi kumiliki kile usichokifanyia kazi. Usipokimiliki, kama

nilivyoeleza awali katika kitabu hiki, huwezi kamwe kukifanyia kazi ili kuleta manufaa katika maisha yako. Hebu tujikumbushe.

1. Je, unaona nini?
2. Unachokiona, lazima ukishughulikie.
3. Kamwe hawezi kushughulikia usichokiona.
4. Kamwe huwezi kumiliki kile usichokishughulikia.

Wakati ujao utakapokwenda kuangalia nyumba, jiulize swali moja: Ilifikaje hapo? Najua unaweza kusema hilo ni swali la kipumbavu. Lakini kweli ilifikaje hapo? Ilibidi mtu aione kabla haijajengwa. Kutokana na picha hiyo, ramani ilichorwa; kisha kutoka kwa mchoro huo makadirio ya pesa na wakati uliohitajika uliwekwa pamoja ili kuunda mpango wa gharama ya kuijenga nyumba. Hoja ninayotoa ni kwamba ilibidi mtu aione kabla ya kuijenga. Mtu alichora alichokiona kisha akajenga alichochora. Na nyumba hiyo ilipokamilika, ilifanana picha ya ramani.

Hebu niseme hivi tena:

Ilibidi mtu aione kabla haijajengwa.

Ilibidi mtu achore alichokiona (mpango).

Ilibidi mtu ajenge kile alichochora (kutekeleza mpango).

**LAKINI YOTE HUANZA NA "JE, UNAONA NINI?" KANUNI YA KUTAWALA!**

Lakini yote huanza na "Je, unaona nini?" Kanuni ya kutawala!

Nitakuuliza tena, kuhusu maisha yako, "Je, unaona nini?"

Tulia muda mfupi na uandike

maelezo machache. Kisha chunguza picha hiyo na ujiulize, "Je, hili ndilo ninalohitaji kweli?" Kumbuka, wewe ndiye mchoraji wa picha ya maisha yako. Mfano wangu wa $1,500 ungeweza kuwa $150,000 virahisi kama ningejua bei ingepanda. Kuna Yule anayejua kama bei itapanda, naye anakualika umuulize wakati wowote unapohitaji.

Ninapenda kusoma Warumi 12:2 mara kwa mara:

> *Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*

Kimsingi, Maandiko haya yanatuambia tubadili mawazo yetu na tusifuate mtindo wa maisha tuliokuwa nao zamani. Dada zangu wawili walipokuwa wadogo, mamangu alikuwa akinunua miundo tofauti ya mishono na kuwashonea nguo. Sasa ikiwa angeshona nguo na baada ya kumaliza akaichukia kisha akarudi tena na kutumia muundo ule ule angepata vazi lile lile alilochukia kila wakati, haijalishi alilishona mara ngapi. Ili kupata matokeo tofauti, ilimbidi abadilishe muundo aliotumia, na hii ni kweli kwetu pia.

Unaweza kusema, "Naam, Gary, kwa kweli sina muundo maishani mwangu." Na ninasema, "Ndio, unao; huwa unaufikiria siku nzima." Na ukisema haufikirii chochote siku nzima, basi hiyo ndiyo shida yako.

Kanuni ya kutawala hudhihirisha maono yako. Ni mahali unapoishi lakini sio jinsi unavyoishi. Ni maono yako, utawala wako, maisha yako ya baadaye ambayo unakumbatia na kujitayarishia—na hili linaibua hoja kuu. Unaweza kujua unapoelekea kila wakati kupitia kwa matayarisho yako. Ikiwa mtu anataka kuwa mpiga kinanda mzuri, atataka kufanya mazoezi. Ikiwa anataka kufanikiwa katika biashara yake, atakuwa mwanafunzi wa biashara hiyo. Kwa hivyo, niambie: Je, unafanya mazoezi gani katika wakati wako wa mapumziko? Sijaribu

kukufanya ujisikie vibaya, lakini unahitaji kukoma na kukabiliana na ukweli. Hivi ndivyo jambo hili linavyofanya kazi.

Swali langu la mwisho ni: "Unakokotwa kwenda wapi maishani?" Unasema, "Gary, sikokotwi kwenda mahali popote na mtu yeyote." Samahani kwa kutofautiana nawe, lakini unakokotwa kwenda mahali fulani. Ndivyo Biblia inavyosema.

> *Mtu ajaribiwapo, asiseme, "Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala Yeye mwenyewe hamjaribu mtu. Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.*
>
> —Yakobo 1:13-15

Yakobo alituonya tusiruhusu tamaa mbaya ituvute kwenye majaribu na dhambi. Lakini tamaa yoyote inaweza kuvuta mtu kuelekea utimizo wake, iwe ni mzuri au mbaya. Yakobo alisema mtu hujaribiwa wakati tamaa iko. Unaweza kuwa na tamaa nzuri au mbaya; zote zitakuvuta kuelekea utimizo wake. Mara tu tamaa inapokuwepo nawe unakubali kushawishiwa, mpango wa utimilifu huanzishwa. Yakobo alisema mara tu mpango unapotekelezwa, tendo la utimilifu hufuata, kisha utoshelevu halisi wa tamaa. Kwa hivyo kumbuka, kile unachoweka moyoni mwako, kile unachoruhusu kukushawishi, kitakuvuta kuelekea utimizo wake. Dhana hii inafanya kazi kwa manufaa yako au dhidi yako, kulingana na aina ya tamaa unayoitafakari. Je, unaona nini?

**Kanuni ya kutawala:**

> *Panua mahali pa hema yako.*
>
> —Isaya 54:2a

## SURA YA 6

# KANUNI YA KUWA NA UWEZO

*Panua mahali pa hema yako [Kanuni ya Kutawala], na wayatandaze mapazia ya maskani yako [Kanuni ya Kuwa na Uwezo], usiwakataze; ongeza urefu wa kamba zako; vikaze vigingi vya hema yako.*

—Isaya 54:2

Sasa, tunaendelea na kanuni ya uwezo. Baada ya kupanua utawala wetu, mambo lazima yabadilike. Kile ninachomaanisha ni kwamba ikiwa utatwaa maeneo zaidi, kiwango cha kusimamia maeneo hayo mapya kitaamuliwa na uwezo wako. Kanuni ya kutawala inahusu "mahali" unapoishi. Kanuni ya uwezo inazungumzia "jinsi" unavyoishi kila siku: tabia zako, utaratibu wako, na jinsi unavyotumia wakati wako. Hapa, Mungu anasema kwamba unahitaji kupanua nafasi kwa ajili ya ongezeko ambalo anataka kukuletea. Hema yako ya sasa, jinsi unavyowekeza wakati na uwezo wako wa sasa, kuko katika kiwango cha chini sana hakuwezi kushughulikia ongezeko la uwajibikaji unaokuja na maeneo makubwa zaidi, kwa hivyo lazima jambo libadilike.

Tandaza mapazia ya maskani yako, **wala usijizuie**. Ninapenda sehemu hii. Hata baada ya kufikiria kwamba umebadilisha mambo ili kuweza kushughulikia mengi zaidi, Mungu anasema bado fikra zako si kubwa vya kutosha. Usijizuie; andaa nafasi kwa ajili ya ukuaji mwingi, sana!

Kwa hiyo, hebu tuchimbue kanuni hii. Kanuni ya kuwa na uwezo inasema kwamba unapofikia uwezo wako, umekamilika. Hakuna nafasi zaidi ya ukuaji. Hema inawakilisha jinsi unavyoishi na taratibu unazotumia kusimamia siku na majukumu yako.

Utafiti niliousoma unasema kwamba wafanyakazi 8 kati ya 10 wamezidiwa. Hiyo ni kweli; siku za watu wengi tayari zimejawa na shughuli. Kwa sababu hii, wameacha kuota, jambo ambalo linaturudisha katika kanuni ya kwanza, kanuni ya kutawala. Watu ambao wamefikia uwezo wao huacha kuota. Tayari wamejawa na shughuli, kwa hivyo hawafurahii maoni mapya. Kwa nini? Kwa sababu hawana uwezo wa kufanya kile ambacho tayari wanapaswa kufanya kila siku.

Kwa hiyo, hebu nikuulize, "Je, umezidiwa? Je, unaamka na hofu? Umechoka kabisa?" Ikiwa ndivyo, basi umekwama kabisa. Kuna njia moja tu ya kujikwamua na kuanza kuota tena, na hiyo inamaanisha lazima ubadilishe michakato yako.

**Njia pekee ya kuongeza uwezo wako ni kubadilisha michakato yako.**

Hebu nikupe mfano wa kile ninachosema. Tuseme una shamba la futi 100 kwa 100 ambapo umepanda ngano kwa ajili ya kuota mkate wa kula nyumbani. Labda utavuna sehemu ndogo ya shamba ukitumia mundu na kupura ngano kwa njia ya zamani, kwa mkono.

Lakini tuseme unataka kuongeza mavuno yako, na ukaamua kupanda ekari 5 za ngano. Wakati wa mavuno, unapoanza kushambulia shamba hilo la ngano, utafanya kazi kwa bidii kwa masaa kadhaa, na ukitazama juu, hofu itakuingia kwa vile utaona umevuna sehemu ndogo tu ya ekari unazohitaji kuvuna. Nafikiri utaweza kukamilisha kazi yako, ukipewa muda wa kutosha na ikiwa mahitaji mengine yote maishani mwako yamesitishwa.

Lakini tuendelee na kusema ungetaka kuuza ngano yako, kwa hivyo ukaamua kupanda ekari 10,000 za ngano. Sasa utafanya nini? Vema,

kwanza kabisa, pengine hutakaribisha wazo hilo, kwa sababu utachuja uwezekano huo kupitia kwa mtazamo wa "Haiwezekani kuvuna ngano nyingi hivyo kwa kutumia mundu wangu!"

Hapa, tunaona kwamba kanuni ya kutawala sasa imesitishwa na kanuni ya pili, ile ya kuwa na uwezo. Tena, kanuni inasema kwamba unapofikia uwezo wako, unazuiliwa. Umefika mwisho wa uwezo wako, huwezi kufanya zaidi ya hapo. Je, jibu ni lipi kwa uwezo wako uliozuiliwa? Badilisha michakato yako. Itabidi ubadilishe jinsi unavyoishi katika hema yako, yaani jinsi unavyoishi maisha yako ya kila siku, ili kuweza kushughulikia ongezeko hilo. Katika huu mfano wa ekari 10,000, bila shaka utalazimika kununua mashine mmoja au mbili za kuvuna. Zaidi ya hayo, itabidi uwe na wafanyikazi, kuwa na idara ya Watumishi, faida za afya, idara ya malipo, pamoja na matrekta na vifaa zaidi. Bila shaka utaratibu wako wa kila siku utabadilika.

Nikupe mfano mwingine. Tuseme huwa unatumia takriban masaa manne kwa wiki kukata nyasi ukitumia mashine ya mkono. Unataka mauzo yako ya nyasi yaongezeke katika kampuni yako, na unajua ikiwa ungekuwa na wakati, ungeweza kufanya biashara zaidi. Lakini sasa huna wakati. Suluhu ni nini? Una suluhu kadhaa. Unaweza kununua mashine au hata bora zaidi, kununua nyasi iliyokatwa tayari na kutumia muda wako kutengeneza pesa. Kielelezo hiki rahisi kinaweza kutumika katika eneo lolote la maisha yako. Tena, lazima ubadilishe michakato yako ili kupata uwezo zaidi.

Najua sote tunapenda neno mabadiliko. Huo ni mzaha—watu wengi hawalipendi—lakini ikiwa unataka kuongeza eneo lako, ni lazima upende mabadiliko. Kuna neno katika kifungu cha Isaya 54 ambalo labda umelipitia kifupi, lakini lina ukweli mwingi.

<u>**Tandaza**</u> mapazia ya maskani yako.

Jitihada nyingi inahitajika katika kunyoosha upana wa mapazia ya hema. Kila kitu ndani ya hema kinapaswa kupangwa upya, na hilo

linatumika maishani na vile vile katika hema. Hebu tutumie mfano rahisi. Chukua puto mpya na uijaze hewa. Kawaida ni vigumu sana kuijaza mara ya kwanza. Baada ya kuijaza, sasa acha hewa itoke ndani yake. Utagundua kwamba puto sio saizi sawa na ilivyokuwa wakati ilikuwa mpya. Ni kubwa zaidi; na ukitaka kuijaza tena, utaona kwamba itakuwa rahisi zaidi kufanya hivyo. Kwa hiyo, ni nini kilifanyikia puto? Umeipanua na kuifanya iwe na muundo mpya. Puto sasa itakaa katika hali hiyo mpya iliyonyooshwa. Katika mtazamo wa kanuni ya kuwa na uwezo, umeongeza kwa ufanisi uwezo wa puto, lakini ili kufanya hivyo, umepaswa kuinyoosha.

Unahitaji kunyooshwa ili kupata uwezo mpya. Mara ya kwanza itakuwa vigumu, lakini baada ya muda, itakuwa kawaida yako mpya. Hebu nikupe mfano kutoka kwa maisha yangu. Kama unavyojua, mimi na Drenda tuna vipindi viwili vya televisheni kila siku. Hili lilikuwa jambo ambalo hakuna hata mmoja wetu alijiona akifanya, na ilikuwa vigumu kwetu hata kuanza kufanya huduma ya televisheni. Hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa na uzoefu wa kufanya huduma ya televisheni, hatukujua chochote kuihusu, wala kuwa na mamia ya maelfu ya dola zilizohitajika kuanzisha huduma hiyo.

**UNAHITAJI KUNYOOSHWA ILI KUPATA UWEZO MPYA. MARA YA KWANZA ITAKUWA VIGUMU, LAKINI BAADA YA MUDA, ITAKUWA KAWAIDA YAKO MPYA.**

Lakini siku moja, tulihisi tulikuwa tumesikia kutoka kwa Bwana kuanza kuhudumu katika televisheni. Tulianza mchakato wa kutafuta jinsi ya kufanya hivyo; na kusema kweli, kadiri tulivyojifunza, ndivyo tulivyogundua kwamba hatukujua chochote. Mungu alikuwa mwaminifu kutuletea watu ambao walijua kuhusu huduma ya televisheni; na kwa imani, mnamo mwaka wa 2007 tulizindua vipindi

vyetu kwenye mitandao miwili katika mtaa mmoja huko Ohio. Tuliajiri kampuni moja kuja mara moja kwa mwezi na kurekodi vipindi vinne au vitano, maana vilikuwa vikionyeshwa mara moja kwa wiki. Wakati huo gharama ya kuvipeperusha ilikuwa dola 9,000 kwa mwezi, ambazo zilionekana kuwa pesa nyingi sana. Mwaka uliofuata, tulianza kutumia mitandao zaidi, na bili yetu ya kila mwezi ilipanda hadi $50,000 kwa mwezi. Sasa itabidi nikiri kwamba wakati huo, nilikuwa karibu kuzidiwa; lakini tena Mungu alikuwa mwaminifu, na vipindi vyetu vilianza kuonyeshwa kwa mitandao kadhaa ya kitaifa. Kwa hivyo, ndio, nilikuwa nimenyooshwa kupita eneo langu la faraja. Lakini nilianza kuzoea kuandaa vipindi vyetu vya televisheni kila juma, na pesa za kuvilipia zilikuwa zikiingia. Lakini siku moja, yote yalibadilika. Ilikuwa katika mkutano wa kawaida wa maombi ya Jumatano jioni, na binti yangu Amy alikuwa akiongoza maombi. Ghafla, alinyamaza, akanitazama, kisha akasema yafuatayo.

**"Mavuno ni makubwa mno kwako. Ninakunyoosha. Ni kupitia kwa Roho Wangu tu utakapoweza kuelewa kile ambacho kiko karibu kutokea. Je, utasonga mbele nikuongoze katika mambo magumu kupita ufahamu wako, mambo yasiyowezekana?"**

Hii haikuwa mara yangu ya kwanza kupitia hilo. Nilijua kwamba Mungu angenipa fursa iliyopita mahali nilipokuwa, na alikuwa akinitayarisha kabla haijaja. Je, ningesema ndio? Je, nilikuwa tayari kunyooshwa? Nilijua uchungu wa kujinyoosha maana nilishajaribiwa mara nyingi, lakini pia nilielewa thawabu ya kunyooshwa. Kwa hiyo usiku ule, nilisema, "Ninakubali Bwana, ninasema ndio kwa chochote kile."

Takriban mwezi mmoja baada ya mkutano huo wa maombi, tulipokea simu kutoka kwa Mtandao wa televisheni wa Daystar ambapo tulikuwa na kipindi kimoja siku moja kila wiki. Daystar ni mtandao mkubwa wa televisheni wa Kikristo unaotazamwa katika kila eneo

ulimwenguni, na walitupatia nafasi ya kipindi kimoja kila siku. Nilijua kwamba kwa kawaida hawakuwa na nafasi ya kila siku, na pia nilijua kwamba ikiwa ningekataa, labda hawangenipa nafasi nyingine. Lakini pia nilijua kwamba kuwa na kipindi kila siku kungehitaji mabadiliko makubwa katika jinsi tulivyofanya huduma ya televisheni, si kwa wafanyakazi na vifaa tu bali pia katika fedha zilizohitajika kuilipia.

Wakati huo, tulikuwa tukiendana na gharama na utengenezaji wa matangazo ya kila wiki, na sikuona nafasi yoyote katika fedha zetu kuchukua zaidi. Bado tulikuwa tukitumia kampuni iliyokuja na kurekodi na kuhariri kipindi chetu cha televisheni cha kila wiki. Ingebidi nitengeneze timu yetu ya waandalizi na wahariri, na kununua kamera na vifaa vingine vilivyohitajika kila siku, ambavyo hatukuwa navyo. Hakika kulikuwa na jambo moja ambalo nilikubaliana na Bwana kuhusu unabii niliopokea usiku ule wa Jumatano. Aliniuliza kama ningemruhusu aniongoze katika jambo lisilowezekana. Kweli, ilibidi nikubali kwamba jambo hili halingewezekana kabisa. Ili kufupisha hadithi ndefu, Mungu alileta watu na fedha za kutosha kuanzia, lakini lilikuwa jambo gumu; na nitakubali, nilinyooshwa!

Hebu nikusaidie kuelewa kilichofuata. Nilikuwa nikilipa bili ya kipindi kimoja kila wiki. Sasa nilitakiwa kulipia kipindi kimoja kila siku kwa siku tano kila juma. Hilo lilikuwa ongezeko la ghafla la gharama hadi mara tano ya kiasi tulichokuwa tukilipa kila wiki, malipo ambayo tayari tulikuwa na changamoto kumudu. Hata hivyo, mtandao wa Daystar ulielewa hilo na walituambia kwamba pengine tungekuwa nyuma katika kulipa bili zetu za muda wa maongezi maana ingechukua muda kwa watazamaji wetu wapya kutufahamu na kuanza kuunga mkono vipindi vyetu. Tulitia saini mkataba wa kuhudumu kila siku, na bila shaka, katika mwezi wetu wa kwanza hatukuweza kulipa kampuni yetu ya vyombo vya habari iliyosimamia mkataba wetu na Daystar. Lakini sote tulitarajia hili, kwa hivyo hatukuwa na tatizo kubwa.

Lakini baada ya miezi mitano, bado tulikuwa nyuma zaidi katika kulipa bili zetu za muda wa maongezi. Kisha nikapokea barua pepe iliyosema kwamba tulikuwa nyuma $500,000 kwenye bili zetu, na mawakili walikuwa wanashangaa tutafanya nini kuhusu hilo. Je, umewahi kulipua puto unapoijaza hewa kwa sababu ya kuweka shinikizo kubwa ndani yake? Kweli, nilihisi kana kwamba nilikuwa karibu kulipuka. Sikujua jinsi ningelivyoweza kulipa bili hiyo, na hata vibaya zaidi jina la kipindi chetu cha televisheni *Fixing The Money Thing* lilihusishwa. Nilipambana na hilo sana. Hata nilimwambia Drenda labda tupunguze muda wa maongezi katika televisheni maana hatungeweza kuendelea hivyo. Lakini kile tu alichosema ni, "Mungu alisema nini?"

Tulihudhuria mkutano mdogo wa maombi, na bila kumwambia mtu yeyote kuhusu tatizo letu, wanaume kadhaa waliokuwa hapo walihisi kuniombea. Walipokuwa wakiomba, ghafla nilihisi uzito wote wa hali yetu ukiondolewa, na papo hapo nilijua kwamba kila kitu kingekuwa sawa. Baada ya siku chache, niliota ndoto ambapo niliona rundo kubwa la hundi. Niliweza kuona kiasi cha fedha na majina ya watu wengi kwenye hundi hizo. Nilipoamka nilijua Mungu angenipa pesa. Cha kushangaza ni kwamba wikendi hiyo, tulikuwa na matoleo kanisani ya $500,000 zaidi ya kiasi chetu cha kawaida, ambazo tulitumia kulipia bili zetu zote.

Gharama yetu ya vyombo vya televisheni sasa ni mamia ya maelfu ya dola kila mwezi, lakini huwa ninalala kama mtoto mchanga. Kwa nini? Kwa sababu nimeingia katika ukawaida mpya, uwezo mpya. Ndio, mabadiliko yalihitajika sana—na nyakati zingine hayakuwa ya kufurahisha; ninaweza kukuambia hivyo—lakini hakika thawabu ilikuwa ya kufaa. Kwa hivyo hebu nikupe ushauri.

**Usiruhusu kutoweza kwako kudhibiti maono yako!**

**Ruhusu maono yako yaamue mabadiliko unayohitaji kufanya katika uwezo wako!**

Hapa kuna jambo muhimu litakalokusaidia kujua hatua unayohitaji kuchukua na michakato inayohitaji kubadilishwa. Jibu swali lifuatalo.

**Ni kitu gani kinachokukatisha tamaa kuhusu maisha yako?**

Jibu lako litabainisha ni wapi unatatizika au maeneo usiyo na ujuzi wa kuyatekeleza ambayo ingefaa zaidi kuyakabidhi kwa mtu mwingine.

Tuseme unatumia kama masaa matatu kwa wiki kukata nyasi yako. Je, huo ni utumizi bora wa wakati wako? Kama nilivyokwisha sema, unaweza kubadilisha taratibu zako kwa kununua mashine ya kukata haraka au, hata bora zaidi, kumlipa kijana aliye karibu nawe akukatie. **Jali mambo yako mwenyewe**. Kaa huru ili uweze kuota jinsi ya kuchukua maeneo makubwa zaidi.

Swali la pili unalohitaji kujibu ni hili.

**Je, mchakato wako sasa hivi unalingana na matarajio yako?**

Kwa mfano, ikiwa nina mashine kubwa ya kufulia na ina uwezo wa kuosha nguo zangu zote, lakini bado nguo zangu hazijafuliwa, basi nina tatizo katika usimamizi wa wakati. Hili ni suala kuhusu mchakato ambalo ni jambo tofauti na tutalizungumzia katika sura inayofuata. Lakini ikiwa ninafua nguo zangu juu ya jiwe katika kijito na ningali na milundo ya nguo chafu nyumbani, basi lazima nitambue kuwa mchakato wangu haulingani na matarajio yangu au hitaji langu, kwa hivyo itabidi ninunue mashine ya kufulia au nilipe mtu anifulie.

**TUNAFANYA KAZI NYINGI SANA NA KWA BIDII NYINGI HATUNA WAKATI WA KUKETI NA KUOTA NA KUSIMAMIA MICHAKATO TUNAYOTUMIA KILA SIKU.**

Wengi wetu, bila kujua, tunaishi maisha ya malengo ambayo hayajatimizwa. Sio kwa sababu hatufanyi kazi kwa bidii vya kutosha.

La, tunafanya kazi nyingi sana na kwa bidii nyingi hatuna wakati wa kuketi na kuota na kusimamia michakato tunayotumia kila siku, ndani ya hema.

Kwa mfano, nilisoma makala ambayo ilisema watu wengi hupoteza masaa mengi kwa siku kutazama televisheni, kujivinjari mtandaoni, au kuzungumza kwenye simu zao. Nina hakika umesikia mtu akisema maneno haya mwishoni mwa siku, "Wakati ulienda wapi? Inawezekanaje kwamba ni wakati wa kwenda kulala?" Kweli, hili ni swali zuri linalohitaji kujibiwa. Katika sura inayofuata, tutalijibu, maana unahitaji kujua wakati ulikwenda wapi. Lakini kwa sasa, fahamu tu kwamba ikiwa huna uwezo, badala ya kujaribu kujua muda ulikwenda wapi, unapaswa kuzingatia jinsi ya kuongeza kasi ili kukamilisha kazi yako.

Jambo rahisi unaloweza kufanya ili kuongeza uwezo wako ni kutengeneza orodha ya mambo ya kufanya. Lakini watu wengi walio na orodha ya mambo ya kufanya hushindwa kutimiza yaliyoorodheshwa. Kwa nini? Kwa sababu michakato yao haina uwezo wa kushughulikia masuala yaliyopo. Pili, huwa wanaanza na vitu rahisi na hawafikii vitu vigumu vilivyo muhimu. Kwa hivyo, jambo muhimu ni hili: Shughulikia vitu vigumu zaidi usivyovipenda lakini vya dharura mwanzoni mwa kila siku, na utastaajabishwa na kiasi cha kazi utakayoweza kufanya na jinsi hukumu ya kutoimaliza itakavyokuondokea.

Taratibu husababisha mipango kukamilika; na usipoikamilisha, basi hicho ni kiashirio kwamba taratibu zinahitaji kubadilishwa. Jambo moja ninalohitaji kukuonya ni kwamba usihairishe mambo. Usivumilie kutokuwa na uwezo hata kidogo. Daima waza kuhusu yaliyo mbele na mwombe Roho Mtakatifu msaada na mwongozo. Uwezo kwa kawaida hauzuiliwi ghafla bila onyo, ingawa hilo linaweza kutokea, kama ilivyokuwa katika hadithi yangu. Kawaida mtu huona jambo kwa mbali likija. Tatizo huja tusipoangalia mbele na kuona kwamba linakuja kisha

tunapata hatuko tayari, na kila kitu kinakuwa cha dharura.

Nakumbuka wakati kanisa letu lilikuwa dogo sana lakini lilikuwa linakua. Nilikuwa na shughuli nyingi sana za kujenga kanisa na biashara yangu. Wakati huo, nilikuwa na mtunza hesabu wa wakati wa ziada aliyesimamia matumizi ya fedha kanisani, na jinsi nilivyoweza kuona ni kwamba hatungeweza kuendelea hivyo kwa muda mrefu. Katika hali ya kukata tamaa usiku mmoja, mimi na Drenda tulishikana mikono na kusali kwamba Mungu atuelekeze kwa mtu ambaye angeweza kutusaidia. Ilikuwa yapata saa nne usiku huohuo tulipigiwa simu. Ilikuwa mke wa mmoja wa viongozi wetu kanisani. Hivi ndivyo alivyosema. “Nilikuwa nikiomba, na nilihisi Bwana akiniambia nikupigie simu na kukuuliza ikiwa unahitaji msaada wowote wa kifedha. Nina uzoefu mwingi katika nyanja ya kifedha, na ningependa kutoa msaada.” Lo, tulifarijika. Tulitambua kwamba mwanamke huyu alikuwa mwaminifu na mwenye ujuzi mwingi katika maisha yake ya kila siku, hata kazini, lakini hatukujua alikuwa na uzoefu mwingi katika utunzaji wa fedha. Tulimpa kazi ya kutunza hesabu zetu na alifanya kazi nzuri sana.

Cha kusikitisha ni kwamba mimi na Drenda tulikuwa tumekaa majuma mengi katika wasiwasi na mafadhaiko tukijaribu kutafuta wenyewe jinsi ya kushughulikia tatizo letu la uwekaji hesabu badala ya kumwomba Mungu msaada kwa bidii. Nakumbuka wakati mwanamke huyu alipotupigia simu, alisema kwamba alijua wakati ulikuwa umekwisha lakini alihisi Bwana alimwambia atupigie simu saa hiyo. Mungu anajua yote kuhusu kazi ambazo amekupangia, na atakusaidia kukuza uwezo wako kabla ya kazi hizo kutokea.

Pia nataka kuzungumza kwa muda kuhusu kuwa na uwezo unaofaa katika shughuli unayoifanya. Naamini hili ni muhimu na linaambatana na neno katika Isaya aliposema panua nafasi wala msijizuie. Nafikiri watu wengi hulenga chini sana wanapoanzisha biashara au kazi mpya.

Nakumbuka nilipokuwa nimeketi karibu na kijana fulani kwenye

ndege, na tukaanzisha mazungumzo. Nilimuuliza kuhusu kazi yake, akaniambia alikuwa na duka la kuoka mikate. Nilifikiri kwamba labda alikuwa na duka ndogo la kuoka mikate kama zile za mjini kwetu zinazoshughulikia harusi na kuuza biskuti, kwa hivyo nikamuuliza kuhusu duka lake. Aliniambia ni duka la mtaani tu la kuoka mikate huko Boston, na alikuwa amelifungua miaka miwili awali. Niliuliza jinsi biashara ilikuwa ikiendelea, na jibu lake lilinishtua. Alisema walifanya biashara ya zaidi ya milioni 20 mwaka wa awali. "Subiri," nikasema, "nilifikiri ulisema ulifungua duka hili la mikate miaka miwili iliyopita." Akasema ndio. Kisha nikamuuliza aliwezaje kufanya biashara ya kiasi hicho cha fedha katika mwaka wake wa pili. Aliniambia kwamba kampuni yake haikulenga keki za sherehe ya kuzaliwa na biskuti kama biashara yao kuu. Badala yake, walilenga kampuni kubwa kuanzia siku ya kwanza. Niligundua kwamba mtu huyu hakuanzisha duka la kuoka mikate ili kulipa bili zake; alilianza ili kuwa tajiri! Mawazo yake yalinivutia sana na yalikuwa tofauti sana na ya watu wengi.

Hadithi yake ni mfano kamili wa kanuni ya kwanza, yaani kanuni ya kutawala, na kanuni ya kuwa na uwezo zikifanya kazi pamoja. Alipoazimia kuzindua biashara yake, alihakikisha alikuwa na uwezo wa hali ya juu kabla ya kuanza. Aliingia akitarajia kuwa na kampuni kubwa na alitaka kila kitu katika kampuni hiyo kiwe hivyo. Watu wengi hufanya polepole wakitumia michakato ya kizamani na kuendelea kuzidiwa na kushindwa na washindani. Kwa hivyo kila wakati hakikisha kwamba uwezo wako unapita mahali unapofikiria kuwa.

Michakato yako lazima iwe rahisi kurudiwa tena na tena. Huduma yetu ina wafanyakazi zaidi ya 100, ukiongeza wale walio katika kampuni yangu ya kifedha. Mwanzoni, mara nyingi nilikuwa nikipitia jambo ambalo halikunifurahisha sana ambapo wakati wowote mfanyikazi alipoacha kazi tulikuwa tukipoteza michakato yetu yote, kwa sababu hakukuwa na mtu mwingine aliyejua jinsi ya kufanya kazi

ambayo mtu huyo alikuwa akifanya. Hakuna mtu ambaye alifikiria kuiandika michakato hiyo ili mtu yeyote aliyekuwa akifanya kazi hiyo angeendelea na michakato yetu bila tatizo. Najua, ni kosa la kipumbavu, lakini makampuni mengi madogo na mashirika yako katika hali hii hii. Wengi wasio na mawasiliano wazi katika kampuni zao huwa hawafaulu katika miradi muhimu, jambo linalofanya uwezo kuzuiliwa na kukua kukoma, au, hata vibaya zaidi, kushindwa kabisa. Kwa hivyo hebu niseme hivi tena:

**Taratibu zako lazima ziwe rahisi kurudiwa tena na tena!**

Duka la *Subway* hutengeneza sandwichi nzuri bila shaka, lakini ni sandwichi tu—ambayo nadhani sote tungesema tunaweza kuitengeneza ikiwa tu tutaoka mkate wetu wenyewe jinsi wanavyooka mikate yao. Wameweza kudumisha maduka yao katika maeneo takriban 42,000 kote ulimwenguni, kulingana na mtandao wa statista.com. Duka lingine la chakula linaloitwa McDonald's lina maduka 39,000 ulimwenguni kote, kulingana na mtandao huo huo. Au vipi kuhusu kampuni ya usafirishaji Uber, ambayo iliingia katika zaidi ya miji 10,000 duniani kote katika miaka 12 pekee, kulingana na mtandao wa mappr.com? Je, mambo haya yalitokea yenyewe tu? La, mtu yeyote anaweza kutengeneza hamburger. Vijana wawili walioanzisha Uber hawakuwa wakitafuta njia bora ya kujipatia kazi tu. La, walikuwa na mtazamo wa kutawala ulimwengu akilini walipozindua kampuni hiyo. Lakini kwa ukuaji kama huu ilibidi kampuni hizi ziwe na michakato mizuri iliyoainishwa vyema. Na nina hakika walibadilisha michakato hiyo wakati fulani.

Nimekuwa nikifanya kazi ya mauzo maisha yangu yote. Ingawa mimi ni mchungaji wa kanisa kubwa na pia nimekuwa nikifanya huduma ya televisheni kila siku, ningali ninamiliki kampuni yangu ya huduma za kifedha. Nilipoanzisha biashara hiyo, mapato yangu yote yalitoka kwa mauzo yangu ya kibinafsi. Nilifahamu kwamba ikiwa Jumamosi ingefika kabla sijapata wateja, ningepoteza nusu ya tija ya

wiki iliyofuata. Umekisia vyema, ilibidi nitumie siku nzima Jumamosi kupiga simu ili kuandaa miadi kadhaa.

Nimefundisha mamia ya wauzaji katika kampuni yangu. Wengi wao walitarajia kuwa na wiki nzuri ya mauzo, lakini ni wachache tu waliofanikiwa. Kwa nini? Walitegemea matumaini badala ya kuwa na mpango. Wengi wao hawakuwa wakipenda kupiga simu, na hilo liliwafanya kukawia na kutotimiza kazi ya wiki nzima. Hawakuwa na mpango mzuri kuhusu ni nani wangempigia simu Jumatatu asubuhi. Walitumaini tu kwamba wangefaulu walipopigia watu simu Jumatatu asubuhi. Pia hawakufanya mazoezi ya uwiano wa biashara, ili kutambua ni simu ngapi zinazohitajika kupigwa ili kupata mteja mmoja. Kwa hiyo, watu wawili mfululizo waliposema hawakutimiza mauzo yaliyohitajika wiki nzima, sababu waliyonipa ni kwamba hawakuwa na karama ya kufanya mauzo, kisha wakajiuzulu. Lakini ikiwa wangeelewa kwamba kuzungumza na watu 10 kulimaanisha wangetarajia kulipwa wastani wa $3,000 hadi $5,000, wangeendelea kupiga simu zao, wakijua kwamba walikuwa karibu kufaulu.

Mimi na Drenda tulikutana shuleni huko Oklahoma na tulianzia biashara yetu ya huduma za kifedha huko. Ilikuwa kazi ngumu kujifunza kuhusu mauzo maana sikuwa mtu wa watu, ilinibidi nijilazimishe kufanya kazi hiyo. Lakini baada ya muda, nilifurahia kupiga simu, kuwa mjuzi wa bidhaa yangu, na kufanya kazi na wateja. Lakini siku moja nilipokuwa nikifanya mazoezi ya mwili ya kukimbia, Bwana aliniambia kwamba nilipaswa kurejea Ohio. Kwa hivyo mimi na Drenda tulirudi Ohio, lakini tena halikuwa jambo rahisi.

Ilibidi nianzishe biashara yangu kutoka chini kwa hivyo nilianza kupiga simu kutafuta wateja wapya. Niligundua kwamba ikiwa ningepiga simu 90 kwa siku, ningezungumza na watu takriban 25. Nilipata kwamba wakati mwingine baadhi yao hawakuwa nyumbani labda walikuwa kazini, kwa hivyo ningeacha ujumbe, ambao baadhi

yao wangejibu. Kati ya watu 25 ambao niliweza kuzungumza nao, takriban 6 hadi 7 tu ndio waliopendezwa na bidhaa yetu na kupanga miadi nami. Kati ya miadi hiyo 7, ningefanya mauzo 3; na kutoka kwa mauzo hayo 3, kwa kawaida ningepata takriban $2,000 hadi $5,000 kwa wiki. Mara tu nilipoanza kupata wateja ambao walielekezwa kwangu na wateja wengine, niliacha mfumo wangu wa kupiga simu na kuanza kutegemea njia hiyo mpya. Kuanzia hapo, nilianza kuajiri washirika hadi nikawa na wauzaji 300, na ofisi yetu ikawa ofisi nambari 1 kati ya ofisi 5,000 kote nchini.

Sababu ya kukusimulia hadithi hii ni kusisitiza kwamba lazima uwe na taratibu za kusimamia siku yako. Muda ni wa thamani! Leo, baada ya zaidi ya miaka 30, kampuni yangu ingali inafanya biashara, isipokuwa leo mambo yamebadilika. Michakato yetu imebadilika. Leo, tuna programu ambayo inafuatilia kila kitu. Mteja anapopiga simu ofisini mwetu, ninaweza kupata rekodi ya kila simu aliyotupigia pamoja na kile tulichozungumzia kwa kompyuta. Huwa tunaweka kwa faili kila fomu na nyenzo za mauzo zilizotumiwa wakati mteja alipigiwa simu na nakala za kila mkataba aliotia saini, utendaji wa bidhaa hizi baada ya muda fulani, mabadiliko yoyote ambayo tumefanya na mambo mengine mengi yanayotusaidia kutathimini biashara yetu. Leo, washirika wangu wanaweza kufanyia kazi kwa nyumba zao na pia kupata kila kitu wanachohitaji. Wateja wetu wanaweza kwenda mtandaoni na kusasisha mipango yao, kututumia ujumbe, au kufanya mabadiliko kwa data zao wenyewe. Dunia inabadilika, na lazima tubadilike pia.

Leo, sipigi simu za wateja katika biashara yangu. Sina wakati wa kufanya hivyo. Ilinibidi kukabidhi hilo kwa watu wengine wa ajabu wanaonifanyia kazi hiyo. Kwa nini? Kwa sababu nina mambo mengine mengi ya kufanya. Kando na mkutano wangu wa mwaka wa bodi, mimi huingia ofisini karibu mara moja kila baada ya miezi

mitatu; na pamoja na kuangalia ripoti za kila mwezi, nina uwezo wa kufikia kila kitu ninachohitaji ili kuendeleza mambo. Ilibidi niendelee kubadilisha michakato yangu ili kuniwezesha kuchukua eneo zaidi. Ingawa siku hizi huwa sikutani na wateja moja kwa moja, kampuni yangu bado inazalisha mamia ya maelfu ya faida halisi kwa mwaka. Je, ningali ninapenda kufanya kazi na wateja? Ndio! Je, bado napenda maono ya kampuni yangu? Ndio! Lakini ikiwa nitatimiza malengo yangu, siwezi kufanya kila kitu. Lazima nizingatie kile ninachopaswa kufanya.

Kumbuka kwamba kanuni ya kuwa na uwezo huchochea moto wako, au kusababisha moto wako kuwa moshi wa moto uliozimika. Ikiwa umechanganyikiwa au kuzidiwa, tayari umechelewa sana kubadilisha taratibu zako.

**KUMBUKA KWAMBA KANUNI YA KUWA NA UWEZO HUCHOCHEA MOTO WAKO, AU KUSABABISHA MOTO WAKO KUWA MOSHI WA MOTO ULIOZIMIKA.**

Uwezo wako ukifika mwisho, huwezi zaidi ya hapo. Kwa hivyo usiruhusu hilo kutokea. Unaweza kuuliza, “Nitajuaje kama taratibu zangu sasa ni nzuri au si nzuri?” Naam, ikiwa umefika mwisho, basi zinaweza kuwa taratibu nzuri, lakini umezizidi. Kaa mbele ya upeo wa uwezo wako kwa kutathmini tija yako kila mara, na hili linatupeleka kwenye kanuni ya tatu ya kuongeza kasi.

## SURA YA 7

# KANUNI YA KUMILIKI

> *Panua mahali pa hema yako* [Kanuni ya Kutawala], *na wayatandaze mapazia ya maskani yako* [Kanuni ya Kuwa na Uwezo], *usiwakataze* [Kuwa na Mawazo Makubwa Zaidi]*; ongeza urefu wa kamba zako* [Kanuni ya Kumiliki]*; vikaze vigingi vya hema yako.*
>
> —Isaya 54:2

Turudi katika Andiko letu la kimsingi la kanuni nne za kwanza za kuongeza kasi. Kanuni ya tatu inatoka kwa maneno, "ongeza urefu wa kamba zako." Ukipanua hema, sehemu kubwa ya turubai itaipa upepo nguvu zaidi ya kuisukuma hema na kuiangusha chini. Kamba na vigingi, vinavyoshikilia hema chini, lazima virefushwe ili kupata nguvu zaidi ya kustahimili mvutano wa turubai kwa sababu ya shinikizo kubwa linalotoka kwa sehemu kubwa ya turubai. Lakini hebu tuangalie kamba. Huwa zinaunganishwa kwenye hema, ambalo tumesema ni jinsi unavyoishi maisha yako ya kila siku, na vigingi, ambavyo hupigiliwa na nyundo ardhini. Ardhi ambapo vigingi hupigiliwa nyundo inahusu kanuni ya kwanza, mahali pa hema yako, maono yako na kutawala. Vigingi hupigiliwa chini ili kushikilia kamba zinazoshikilia hema yako, nazo ni taratibu zako za kila siku, zinazoongozwa na maono yako—ardhi. Zinafanyaje hivyo? Kupitia kwa usimamizi! Ningeita kanuni hii ya tatu kanuni ya usimamizi.

Lakini nilichagua kuiita kanuni ya kumiliki kwa sababu hutawahi kumiliki kile usichokisimamia.

**Hutawahi kumiliki usichokisimamia!** Kamba ni kweli, mapato kutoka kwa uwekezaji, maelezo unayohitaji ili kufanya maamuzi mazuri. Usimamizi hudhihirisha ukweli ili wote wauone. Kwa kuwa kamba hutia nanga kwenye maono yako, zinachochea taratibu zako katika hema, jinsi unavyoishi na kuwajibikia maono yako. Hivi ndivyo unavyoweza kutathmini kama taratibu zako zinaweza kukufikisha mahali uendapo.

Unaposafiri kwa treni za umeme za chini ya ardhi kule Uingereza, utaona alama zenye maneno yafuatayo "Mind the Gap" ("Zingatia Pengo") katika mahali pa kuingilia treni hizo. Ikiwa hutazingatia pengo hilo, unaweza kujeruhiwa au hata vibaya zaidi kwa kuanguka kwenye pengo kati ya treni na mahali pa kushukia. Hatari hiyo hiyo ipo hapa pia. Biashara yako yote au maisha ya nyumbani yanaweza kuingia katika fujo kubwa ikiwa hujui pengo—maelezo ya undani. Usipozingatia pengo, utajikuta umepotea njia huku ukifikiria kwamba mambo yako sawa.

Mimi ni rubani, na nilijifunza haraka sana kwamba sitaki kupotea kutoka kwa mwelekeo wa dira ninaofuata. Ninapokaribia uwanja wa ndege ninaojua, sihitaji kutazama dira. Nayajua mandhari yaliyo chini yangu. Lakini ninapoanza safari ndefu, sina mahali pa kurejelea kujua ikiwa ninaelekea kwenye njia sahihi au la bila mwelekeo wa dira. Kwa hivyo watu wengi wanatumai kwamba wanaelekea katika mwelekeo sahihi lakini wanaelekea njia mbaya.

Katika biashara yangu ya kifedha, huwa tunamwomba mteja aandae bajeti tunapokutana mara ya kwanza. Bila shaka, ikiwa tutamsaidia mteja kutoka kwa madeni au akituomba tulinde uwekezaji wake, ni lazima tufahamu hali yake ya kifedha. Swali moja tunalouliza katika dodoso hilo la awali ni kwamba ni kiasi gani cha pesa ambacho

angesema ni za ziada kila mwezi. Kwa maneno mengine, natafuta pesa ambazo tunaweza kutumia kumsaidia kufikia malengo yake ya kutoka kwa madeni. Tayari najua kabla sijauliza kwamba kwa kawaida mtu huwa hajui. Siku hizi watu wengi hawana bajeti kwa sababu ya kutumia kadi za mikopo ya kisasa. Maadamu wana idhini yoyote ya kutumia kadi zao, wanaendelea kuzitumia. Lakini kwa kweli, hii ni moja ya shida ninayojaribu kufichulia wateja wangu, ambayo hawaijui, na ni muhimu waijue.

Nashangaa kila wakati watu wanaponiambia kwamba wana $500 za ziada au zaidi kwa mwezi, lakini wanapofanya bajeti, wanapata wana upungufu wa $700 kila mwezi. Nilikuwa na mteja mmoja ambaye alisema alikuwa na $1,000 za ziada kila mwezi lakini nilishtuka kugundua kwamba alikuwa na upungufu wa $1,700 kila mwezi, na ndiyo maana alikuwa ametumia kadi zake za mkopo kupita kiwango sahihi. Hmm, nashangaa jinsi hilo lilivyofanyika. Usipokuwa na maelezo ya undani, huwezi kujua ikiwa utaweza kukamilisha kile unachopaswa kukamilisha.

Usimamizi zaidi unahitajika ili kushughulikia maelezo yote ya undani ya taratibu zako za nyumba iliyopanuliwa. Kama nilivyosema hapo awali, ikiwa unajaribu kuvuna ekari 10,000 za ngano ukitumia mundu, watu watacheka ujinga wako. Utahitaji mashine nyingi za uvunaji ili kuvuna kiasi hicho cha ngano. Kwa kweli, kama nilivyosema, kutawala kwako kunapoongezeka, hitaji la taratibu zako kubadilishwa hufanyika muhimu zaidi na zaidi. Kuacha kuwa mkulima anayepanda ngano kama shughuli ya ziada na kuwa mkulima anayepanda ngano ya biashara kubwa kunahitaji mabadiliko makubwa. Utahitaji idara ya malipo, idara ya wafanyikazi inayoshughulikia sheria ya uhusiano nao, manufaa ya mfanyakazi kama vile bima ya afya, ratiba za matengenezo ya mashine zote unazohitaji, na mengi zaidi.

**Kwa hivyo tena, ikiwa huwezi kusimamia jambo, kamwe**

**hautaweza kulimiliki.**

Hiki ndicho Bwana alikuwa akijaribu kuniambia katika Waebrania 11:33-34 iliyotajwa mwanzoni mwa kitabu hiki. Watu wanamwamini Mungu kuwapa biashara kubwa na mapato, lakini hawana uwezo wa kushughulikia kile wanachosema wanataka.

Ninamjua mchungaji mmoja wa kanisa fulani ambaye anaelewa jambo hili vizuri sana. Anapowahoji watu wanaotaka kufanya kazi katika huduma yake, huwa anawaomba wampeleke kwenye gari lao. Anajua kwamba ikiwa gari lina uchafu mwingi, basi huduma yake itaonekana kama gari hilo baada ya muda mfupi. Anajua ikiwa mtu hawezi kusimamia kile alicho nacho tayari, basi hana uwezo wa kusimamia mengi zaidi. Sasa, tuseme kwamba mchungaji amesimama kwenye gari hilo chafu pamoja na mfanyakazi ambaye sasa ameaibika, maana viazi vya kukaangwa vimemwagwa chini kwenye zulia ya gari na takataka imetapakaa kwenye gari. Unafikiri mchungaji atasikia nini? "Samahani, sijapata wakati wa kusafisha gari langu hivi majuzi." Lakini je, hicho ni kisingizio kweli? La, samahani, umejaribu. Kuna waosha magari, na kuna wafanyabiashara wanaoenda kwa nyumba za watu kuwaoshea na kuwasafishia magari yao.

Ni wazi mtu huyu ana shida kimaono. Lakini nitaweka dau kwamba gari hilo lilipokuwa jipya, alipenda jinsi lilivyokuwa nadhifu na safi, na aliazimia kuliweka hivyo. Lakini mambo hutokea maishani. Taratibu zake za kila siku hazikuweza kuambatana na maono yake. Basi ni nini kilitokea? Alipuuza maono yake na kukubali tu kuendesha gari chafu. Katika hali hii, mara tatizo lilipoonekana, taratibu mpya ilipaswa kuwekwa na kusimamiwa ili kuhakikisha kwamba jambo hili haliendelei. Kwa mfano, orodha rahisi ya mambo ya kufanya inayomkumbusha mwenye gari kuipeleka kwenye sehemu ya kuosha magari kila Jumatano anaporejea nyumbani kutoka kazini ingefanya kazi. Au kuajiri mtu wa kumsafishia gari. Jambo la msingi

ni kwamba mtu huyu alipuuza maono yake ili kuambatana na vizuizi vya uwezo aliokuwa nao.

Usimamizi una jukumu muhimu sana. Unaonyesha ni taratibu gani zinazohitaji kubadilishwa, kama nilivyosema hapo awali, lakini pia utaonyesha ni wapi unahitaji kujiondoa kwenye taratibu hizo. Ninamaanisha kwamba mambo yanavyozidi kuwa magumu, utahitaji kuajiri wasaidizi wa kitaalamu. Najua mtazamo ya yule mtu mwenye gari chafu ambaye alikuja kutafuta kazi. Aliwaza, *Siku moja, nitashughulikia hili*.

Lakini nimeona kwamba watu wanaofanya mambo makubwa kila mara huwa wanauliza, "Nimpe nani kazi hii?" Nafikiri sote huwa tunakabiliwa na mtazamo wa "Ninahitaji kufanya hivi na vile." Hii inatokana na fikra zetu ndogo kuhusu maisha. Hebu niseme hivi: Huwezi kumudu kufanya kazi hizo zote ndogo. Muda wako una thamani zaidi ya hapo.

Ndio, wakati mmoja, niliandaa na kuwasilisha ushuru wangu mwenyewe. Hakika sikuwa na ujuzi wa kushughulikia ushuru, na kawaida niliogopa kufanya hivyo. Hatimaye, nilikuwa na shughuli nyingi sana, na jinsi ushuru wangu ulivyozidi kuongezeka, nilikosa maarifa ya kufanya ipasavyo. Niligundua kwamba nilipaswa kuajiri mtu wa kushughulikia hilo muda mrefu uliopita, na kuchelewa kwangu kulikuwa kukiniumiza, sio kunisaidia. Sawa na ushuru wa mishahara; ni fujo gani ya kusimamia hilo binafsi. Nilifikiri ninaokoa pesa, lakini baada ya muda mrefu baada ya kupata adhabu chache, sikuwa naokoa pesa hata kidogo. Sasa, kwa dola mia moja kwa mwezi, kuna kampuni inayoniandalia ushuru na kuwasilisha fomu zangu zote za malipo yanayohitajika. Hilo halikupaswa kuwa tatizo!

Kusimamia wakati wangu ni sehemu kubwa ya maisha yangu. Kwa sababu ya kuwa na kazi nyingi, singeweza kuendelea peke yangu. Sasa nina wasaidizi wawili wa kibinafsi wanaoendesha

kalenda yangu na kushughulikia kila aina ya kazi. Mtu anaponiuliza kama ningeweza kukutana naye, mimi humwambia azungumze na wasaidizi wangu. Sijui lolote; wao ndio wanaoendesha kalenda yangu. Usimamizi hunionyesha mahali ninapohitaji kufanya mabadiliko ili niweze kuzingatia picha kubwa—maono. Kwa hivyo, hebu nitoe kauli ambayo unahitaji kukumbuka.

**Uwezo daima huzuiliwa na ukosefu wa wajumbe na usimamizi.**

Kauli hii ni muhimu sana unahitaji kukoma na kuisoma tena. Bora zaidi, iandike mahali ambapo unaweza kuiona mara kwa mara. Kwa hivyo, hapa kuna swali: Ni kazi gani unaweza kukabidhi kwa mtu mwingine? Wewe ni shingo nyembamba ya faneli kubwa, kwa hivyo koma kuwa kizuizi kwa kujaribu kufanya kila kitu peke yako.

**WEWE NI SHINGO NYEMBAMBA YA FANELI KUBWA, KWA HIVYO KOMA KUWA KIZUIZI KWA KUJARIBU KUFANYA KILA KITU PEKE YAKO.**

Kama kiongozi, iwe wa kampuni kubwa au ya maisha yako binafsi, lazima usimamie mabadiliko katika taratibu zako ili kuhakikisha unafanya kazi kwa kiwango cha uwezo kitakachotimiza malengo yako. Usimamizi hudhihirisha ukweli utakaoendesha mabadiliko hayo. Usimamizi hutoa maelezo ya undani ambayo ni ya thamani kwako kama kiongozi—kama vile mapato ya uwekezaji wako kulingana na taratibu ulizo nazo, wafanyakazi, uuzaji, na maeneo mengine mbalimbali ya maisha yako. Yote yanaonyesha kile kinachohitaji kubadilishwa. Mizani ya bafuni ni kifaa kinachosema ukweli wazi wazi na husaidia mtu kufanya mabadiliko katika lishe yake na tabia zake za mazoezi ya kimwili. Unahitaji kununua nini? Unahitaji kuuza nini? Usimamizi una majibu yote.

Miaka kadhaa iliyopita, tulikuwa na dhoruba kubwa ya theluji

huko Ohio ambayo ilikata umeme kwa zaidi ya wiki moja. Vituo vya mafuta vilikuwa vimefungwa, simu za rununu hazikufanya kazi; na wakati huo, hatukuwa na kuni ya mahali petu pa kuota moto. Lakini tulikuwa na chumba kimoja ambacho kilikuwa na mahali pa gesi pa moto, na ndipo tulipokaa. Watoto wangu walihisi huu ulikuwa mmoja wa wakati mzuri sana maishani mwao sote tulicheza michezo katika chumba hicho juma nzima. Lakini kwangu, lilikuwa janga ambalo lingeepukwa. Ekari zangu za msitu zimejaa miti iliyoangushwa ambayo ingekatwa na kuandaliwa kabla ya majira ya baridi kufika.

Baada ya tukio hilo, nilifanya mambo kadhaa. Kwanza, nilinunua na kuweka kwa shamba langu tanki la petroli la galoni 250 ambalo mimi huhakikisha limejaa mafuta wakati wote. Mafuta ninayotumia kukata nyasi wakati wa kiangazi hutoka kwa tanki hilo, lakini pia hutumika kama chelezo wakati wa dharura. Pia niliongeza jenereta ya umeme na gesi ambayo ni kubwa vya kutosha kuendesha kila kitu ndani ya nyumba nzima. Na, bila shaka, mimi huhakikisha tanki la gesi limejaa wakati wote. Pia ninahifadhi kuni nyingi zilizokatwa kwenye ghala langu, na wakati wote huwa nina angalau gari moja la kazi nzito ninalotumia katika nyakati za baridi. Huwa tunahifadhi bidhaa za matumizi ya mwezi mmoja kwenye orofa yetu ya chini na huwa tuna pesa taslimu mkononi pia kwa matumizi ya dharura. Mambo haya yote yalikuwepo kabla ya juma lile refu ambalo tulifungiwa ndani ya nyumba na hali ya hewa, lakini sikuyafanyia kazi. Hii ndiyo sababu mpango wa usimamizi utakusaidia kuona mambo kabla ya kuyafikia. Utaonyesha maeneo ya udhaifu ambayo yanaweza kuharibu mipango yako na malengo yako.

Kwa hivyo, turudi kwenye ile orodha ya mambo ya kufanya niliyotaja hapo awali. Ninafurahi kwamba ulifanya baadhi ya mambo kwenye orodha hiyo, lakini jiulize swali hili muhimu sana: “Kwa nini sikukamilisha mambo yote niliyoorodhesha?” Ikiwa wewe ni

kama mimi, kuna nyakati ambapo kitu kilikaa kwenye orodha yangu ya mambo ya kufanya kwa miezi kadhaa. Hilo halikuwa sawa hata kidogo. Lilimaanisha nini kunihusu? Kwamba uwezo wangu ulikuwa umefika upeo, na hata kama ningekuwa na mawazo makuu kwa njia gani, haingejalisha hata kidogo. Maana hata kama ningekuwa na bidii kiasi gani ya kuweka mawazo hayo kwenye orodha yangu ya mambo ya kufanya, singeyafanya. Orodha ingeendelea kuwa ndefu zaidi na zaidi. Ilibidi nibadilishe taratibu zangu!!!! Unajua una au ulikuwa na shida kama hii. Kusimamia, na orodha, vilinionyesha kwamba nilikuwa nikijidanganya, na mabadiliko yalitakiwa ikiwa nilikuwa makini kuhusu maono yangu.

Sasa, unapoangalia orodha yako, je, kuna mambo ambayo ungekabidhi wengine wayatekeleze? Kuna vile unaweza kubadilisha taratibu zako ili usilazimike kushughulikia suala hilo hilo tena? Je, haingekuwa vyema kuondoka ofisini kwako mwisho wa siku na kujua kwamba umekamilisha orodha nzima? Hilo linawezekana. Hebu fikiria jinsi inavyoweza kuathiri mafanikio yako ikiwa ungebadili mawazo yako kutoka kwa *lazima nikumbuke kufanya hili* hadi *ninaelekea wapi?* Hilo linaweza kuwa jambo KUU sana!

Kumbuka, kadiri maono yanavyokuwa makubwa, ndivyo unavyohitaji mabadiliko makubwa zaidi katika taratibu zako na usimamizi bora. Je, kanuni ya kumiliki ina umuhimu gani?

> *Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme,* ***walitenda*** *haki, walipata ahadi.*
>
> — Waebrania 11:33a

Inaweza tu kuwa tofauti kati ya wewe kutamani kuwa hapo na kuwa hapo hakika. Hapa kuna ukweli ambao najua utasaidia wengine, na labda wewe.

**Watu wengine wanapenda kazi ya kusimamia!**

Najua ninapozungumzia usimamizi, akili za watu wengi huwa na changamoto—sio zote, bila shaka, lakini nyingi. Najua kwa sababu sipendi usimamizi wenye taarifa ya kina; maana hilo hunimaliza nguvu. Lakini amini usiamini, watu wengine hupenda sana usimamizi! Waliumbwa kuupenda!

> *Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na* ***maongozi****, na aina za lugha.*
>
> — 1 Wakorintho 12:28

Mungu aliumba baadhi ya watu ambao wanapenda undani. Mimi si mmoja wao, kama nilivyosema awali. Ninapenda kiasi fulani cha usimamizi wala si mambo ya ukaguzi wa kina.

Binti yangu anamiliki kampuni ya uuzaji, na yuko katika hatua ya kufika mwisho kabisa. Alisema hawezi kuchukua wateja wengine hadi apate usaidizi. Alinionyesha kwamba wafanyakazi wake wote 20 wanaripoti moja kwa moja kwake. Anajua hivyo si vizuri na ni lazima abadilishe muundo wake na taratibu zake. Kwa nini? Kando na ukweli kwamba amefika mwisho, inampasa adhibiti kila idara, jambo ambalo linapunguza ubunifu wake. Alisema talanta yake ni ubunifu ni hilo ndilo linalofanya kampuni yake kwenda mbele. Dalili moja anayokabiliwa nayo ni msongo wa kihisia wa kuzidiwa. Anasema yeye hurudi nyumbani akiwa amechoka kihisia, na bidii yake imedidimia. Naam, nilimwambia uchovu wa kihisia ni moja ya dalili inayoonyesha kwamba uwezo wake umefika mwisho.

Baada ya kufanya utafiti katika kampuni zingine kubwa za uuzaji, aliamua kupigia moja simu ili kuwauliza maswali fulani kuhusu jinsi

wanavyofanya mambo. Hakuwa na uhakika kama wangempa ushauri wowote kwani wangeweza kumtazama kama mshindani. Alisema lilikuwa jambo gumu, lakini alikuwa amekata tamaa. Aliniambia alipiga simu, na, cha kushangaza, mwanamke ambaye alikuwa akizungumza naye alifurahi sana kujibu maswali yake. Binti yangu aligundua kwamba mwanamke aliyekuwa akizungumza naye alikuwa amebuni muundo wote wa kampuni yake na alikuwa ameandika maelezo yote ya kazi pia.

Binti yangu alifurahi sana kusikia kila kitu alichosema mwanamke huyo. Baada ya muda, binti yangu aliwaza, *Je, mwanamke huyu atakuwa tayari kunisaidia kubuni muundo wa wafanyakazi wangu na muundo ufaao wa msimamizi ikiwa nitamlipa anisaidie?* Hilo kweli lilikuwa jambo gumu, lakini alimuuliza. Na cha kushangaza, mwanamke huyo alisema, "Ningependa kufanya hivyo; ninapenda suala la usimamizi sana." Juu ya hayo yote, alisema hangemlipisha. Alisema alikuwa amefikiria kufanyia wateja kadhaa kile ambacho binti yangu alikuwa akiuliza, na alihisi hilo lingekuwa jaribio nzuri kwa wazo lake. Binti yangu alijawa na msisimko. Kwa hiyo jipe moyo; kuna msaada kwa ajili yako.

**Watu wengine wanapenda unachochukia!**

Usipoteze muda kufanya kile unachochukia. Lipa mtu mwingine au ajiri mtu aliye na uwezo huo na kupenda kazi hiyo. Kadiri unavyokaa hapo kwa muda mrefu ukifanya kile unachochukia, ndivyo kitakavyozidi kuiba furaha na msisimko wako juu ya safari yako na ikiwezekana kitakushawishi kukiacha kabisa.

**KUMBUKA, KAMWE HUWEZI KUMILIKI USICHOKISIMAMIA.**

Kwa kumalizia kuhusu kanuni hii muhimu sana ya kuongeza kasi, kumbuka, kamwe huwezi kumiliki usichokisimamia. Kanuni

ya kumiliki hutoa taarifa na maelezo yanayohitajika ili kutathmini taratibu zako kuhusiana na kufikia malengo yako.

Kumbuka Kuzingatia Pengo!

## SURA YA 8

# KANUNI YA SHINIKIZO

*Panua mahali pa hema yako* [Kanuni ya Kutawala]*, na wayatandaze mapazia ya maskani yako* [Kanuni ya Kuwa na Uwezo]*, usiwakataze* [Kuwa na Mawazo Makubwa Zaidi]*; ongeza urefu wa kamba zako* [Kanuni ya Kumiliki]*; vikaze vigingi vya hema yako.*

—Isaya 54:2

Kanuni ya shinikizo kwa kweli sio ngumu kuelewa unapoelewa madhumuni ya vigingi vya hema. Vigingi hushikilia vitu. Rahisi kabisa. Katika hali hii, Mungu anatuambia tuweke vigingi vyetu katika maono, mahali pa hema yetu, ili visiondolewe na ongezeko la shinikizo ambalo kusimamia hema kubwa husababisha. Kumbuka, ni katika hema ambapo taratibu za maisha ya kila siku hufanyika. Maono yetu yaliyopanuliwa sasa yanahitaji mabadiliko katika jinsi tunavyoishi, maana tuna michakato mipya na migumu zaidi. Mradi tu vigingi vimeshikilia, hema itaendelea kusimama na michakato katika hema itaendelea kubadilika kama inavyohitajika ili kukamilisha maono ambayo yanawakilishwa na msingi ambapo vigingi vimepigiliwa, yaani kanuni ya kutawala.

Kwa hivyo, hebu nifafanue maana halisi ya matumizi yake. Tayari tumegundua kwamba kamba huwakilisha usimamizi unaoshikilia michakato yetu ya kila siku kwa maono yetu, yaani msingi. Hivyo

kwa nini Mungu anatuambia tukaze vigingi vyetu? Kwa sababu tunapopanua hema yetu, ambapo maono yetu makubwa yatadai mabadiliko au taratibu mpya, kutakuwa na uzito zaidi au shinikizo la kuacha maono yetu au kuathiri maono yetu kutokana na matatizo yanayoletwa na mabadiliko. Mabadiliko yana usumbufu kila wakati. Tunahitaji kuwa na subira wakati meli inayumba huku na kule. Tukiwa wenye subira na tusibanduke, meli itatufikisha katika bandari ambayo tumeweka kwenye dira. Wakati mwingine mabadiliko hufanya mambo kuwa magumu sana, lakini mabadiliko yanafaa. Kwa maneno rahisi, kukaza vigingi vyako kunamaanisha hivi.

**Usiruhusu shinikizo likufanye upuuze maono yako. Usibanduke!**

Una ahadi za Mungu, na Neno Lake halitashindwa. Kwa hiyo, shikilia maono hayo. Ongezeko linakuja. Nimezungumza na watu wengi sana ambao wana majuto. Wameniambia kwamba wangefanya jambo fulani walipokuwa wadogo, au wangeanzisha biashara fulani, wangechukua safari fulani, au wangejenga nyumba. Orodha inaendelea na kuendelea. Bila shaka, unapotazama nyuma daima utaona kwa udhahiri zaidi, lakini kutazama mbele ukiwa na ahadi kutoka kwa Mungu ni bora kuliko kuangalia nyuma na kuona kwa udhahiri.

Kwa kusema hivyo, ni lazima ukumbuke kwamba ahadi daima inazungumzia mwisho, si mwanzo. Mungu daima huzungumza katika wakati uliokamilika, kumaanisha Yeye daima huzungumza juu ya hitimisho au ushindi katika mwelekeo au kazi. Mungu alipomwambia Ibrahimu kwamba angemfanya kuwa taifa kubwa, wakati huo, Ibrahimu hakuwa na mtoto. Lakini Mungu alikuwa anazungumza juu ya mwisho na si wakati huo.

**NI LAZIMA UKUMBUKE KWAMBA AHADI DAIMA INAZUNGUMZIA MWISHO, SI MWANZO.**

Nakumbuka niliota ndoto wakati mmoja ambapo Mungu alinionyesha kuwa biashara yangu ingezalisha pesa nyingi sana. Pesa nyingi kuliko nilivyowahi kufikiria nilipoota ndoto hiyo, na hiyo ilikuwa miaka mingi iliyopita. Nilipomuuliza Bwana jinsi hilo lingetokea, Alisema, "Itakubidi ubadilishe kampuni yako mara mbili ili kufikia kiwango hicho." Nilichanganyikiwa. Nikasema, "Sielewi. Kwa nini nibadilishe biashara yangu mara mbili na sio mara moja tu?" Alinijibu na kusema, "Kwa sababu huwezi kuona mabadiliko yanayohitaji kufanywa hadi baada ya kuibadilisha mara ya kwanza." Alichokuwa akisema ni kwamba sikuwa na uwezo wa kuona zaidi ya pale nilipokuwa. Naye alikuwa sahihi. Nilibadilisha jina la kampuni, hata nikabadilisha jina lake wakati wa mabadiliko ya kwanza, na kampuni iliboresha; lakini bado kulikuwa na masuala na taratibu nyingi ambazo hazikuwa dhahiri baada mabadiliko hayo na urekebishaji upya.

Usinielewe vibaya. Tulikabiliana na hitilafu nyingi katika mabadiliko hayo ya kwanza, lakini kadiri tulivyoendelea kukua zaidi, masuala zaidi yalijitokeza. Michakato yetu haikuwa inafua dafu. Kwa hivyo tuliweka orodha ya maeneo ya udhaifu ambayo tuliona tulipokuwa tukikua na kuanza kupanga mabadiliko na marekebisho yetu ya pili. Moja ya maeneo ambayo tulikuwa tukishughulikia ni mifumo yetu ya kompyuta. Wakati huo, kila mshirika alifanya kazi akitumia kompyuta yake ndogo na kisha akahitajika kupakia faili kwetu mara moja kwa mwezi ili ofisi yetu kuu iweze kuzihifadhi. Tulijua kwamba ikiwa tungefanyika kampuni yenye nguvu nchini kote, tungelazimika kwenda kwenye programu inayotegemea wavuti ambayo inaweza kupatikana kutoka popote na ingehifadhi kiotomatiki faili zetu zote zilizohitajika, na hivyo kutoa jukumu hilo muhimu kutoka kwa mikono ya washirika wetu.

Pia tulihitaji kutoa njia ya kuzungumza na wateja wetu na kuwapa

hali bora ya utumiaji mtandaoni walipokuwa wakifuatilia akaunti zao. Tuligundua kwamba siku za kutuma barua zilikuwa zimekwisha; na kwa sababu ya mabadiliko ya kanuni na miongozo ya kodi kila mara, tulihitaji kuwa na njia ya kuwasiliana na wateja wetu kuhusu haya yote. Pia tulijua siku za kujaza kabati na faili zilikuwa zimekwisha na kila kitu kilihitajika kuwasilishwa kwa njia ya kidijitali. Tulihitaji njia bora ya kuhifadhi kwa usalama fomu za taarifa za kibinafsi za wateja wetu na mikataba iliyosainiwa, na pia kufuatilia na kuweka kwenye faili kila simu ya mteja na mabadiliko au maagizo yoyote ambayo yangefanyika baada ya kuzungumza nao kwa simu. Hayo yote yalikuwa yakiandikwa kwa makaratasi wakati huo, lakini tulijua hatungekuwa kampuni tuliyotaka kuwa bila kubadili hilo.

Kwa hivyo, tulibadilisha kampuni nzima kwa mara ya pili. Hii ilifanyika kama miaka saba baada ya mabadiliko yale ya kwanza. Kumbuka, kampuni yetu ina umri wa miaka 35, na mengi yamebadilika katika wakati huo. Tulianza kutumia programu inayoitwa Salesforce, ambayo ilitupa uwezo wa kufanya mambo haya yote kiotomatiki. Matokeo ya mabadiliko hayo ya pili yalifungulia uwezo wetu uliozuiliwa na kutuwezesha kusonga mbele na kunyakua maeneo ambayo maono yetu yalidai. Tulianza kuona mafanikio zaidi kuliko tulivyotarajia awali wakati Mungu aliponiambia neno hilo kwa mara ya kwanza. Lakini ilibidi nitekeleze mchakato huo.

Ahadi daima huzungumzia mwisho wa jambo. Ikiwa huelewi mwisho, ahadi, na maono, unaweza kukata tamaa na kuacha kitu. Lakini mradi tu umeweka vigingi ardhini na kukataa kupuuza maono kwa sababu ya shinikizo, utapata njia yako. Mungu atakuonyesha.

Nilipoitwa kuhubiri, nilikuwa na umri wa miaka 19. Ilikuwa siku yangu ya kuzaliwa, na nilialikwa kula chakula cha jioni kwenye nyumba ya rafiki yangu. Rafiki yangu ndiye tu aliyekuwa Mkristo pale pamoja na mimi. Tulipoketi kula chakula, waliniomba nisali,

wakijua kwamba mimi ni Mkristo. Nilipoanza kuomba, ghafla, upako wa Mungu ulinijia na nikazidiwa. Nilishtuka na kupigwa na butwaa. Nilipokuwa nimeketi pale, upako uliendelea kuongezeka kwa nguvu hadi, hatimaye, nikaomba kuondoka kwa muda mfupi. Nilitoka nje kupitia kwa mlango wa nyuma hadi kwenye ua, na uwepo wa Mungu ulizidi kuwa na nguvu zaidi.

Ghafla, nikaona picha mawazoni mwangu ambapo nilikuwa nimesimama na Biblia mkononi mwangu nikihubiria kikundi cha watu. Nilikiona kile chumba, na niliona kwamba kulikuwa na giza nje kwani mapazia kwenye madirisha yalikuwa wazi, na niliona kuwa ilikuwa usiku. Niliona watu wote wamekaa kwenye viti vya kukunjana, na nikaona idadi ya watu waliokuwa pale, wapatao 20 hadi 30. Kisha nikasikia maneno haya, si kwa sauti bali ndani ya roho yangu, "Ninakuita lihubiri Neno Langu." Niliisikia kauli hiyo mara tatu, kisha upako ukaondoka. Niliporudi ndani ya nyumba na kuketi, kila jicho lilikuwa likinitazama. Waliuliza kilichotokea, nami nikasema, "Nafikiri nimeitwa kuhubiri." Hiyo ilikuwa picha dhahiri sana niliyoipata kuhusu maisha yangu ya baadaye.

Wengine wanaweza kusema, "Vema, je, ulianza kuhubiri baada ya hapo?" La sikuanza. Mungu alinielekeza kwenda chuo kikuu. Ukweli ni kwamba sikufaulu katika shule ya upili. Kulikuwa na mvulana mmoja tu ambaye alihitimu katika darasa langu. Mungu alijua kwamba, ingawa aliniita, bado sikuwa tayari. Tuseme ukweli. Ikiwa huwezi kuandika, na ikiwa huwezi kuwasiliana, hauko tayari. Kwa hiyo, nilikwenda chuo kikuu, na kwa bidii nyingi, nilimaliza kwa wastani wa alama za 2.9. Kwangu, hilo lilikuwa jambo la kushangaza. Wakati huo, chuo kilikuwa jambo gumu zaidi maishani mwangu, na nilifurahi kumaliza masomo.

Baada ya chuo kikuu, ajabu ni kwamba nilihisi Mungu akiniita kufanya kazi ya fedha, hasa kuuza bima ya maisha na dhamana. Kwa

nini Mungu alifanya hivyo? Nilikuwa na aibu, aibu sana. Nilipokuwa nikikua nilikuwa mwenye haya sana hivi kwamba niliepuka watu kama ingewezekana. Nilipoanza kazi ya mauzo, nilikufa vifo milioni. Ilibidi nijilazimishe kupiga simu na kuzungumza na watu. Lakini niliboreka zaidi, na hatimaye, ofisi yangu ilikuwa nambari moja kati ya ofisi 5,000 kote nchini.

Hapo ndipo Mungu aliposema, "Sasa, acha kampuni na uzindue kanisa, ambalo utakuwa mchungaji wake." Sikuwa tayari Mungu aliponiita. Ilibidi nipitie mchakato wa maandalizi. Usiku rasmi wa kwanza wa kanisa letu jipya, nikiwa nimesimama pale nikifundisha, niliona picha ileile niliyoonyeshwa usiku ule nilioitwa. Watu walikuwa wameketi katika viti vya kukunja, giza lilikuwa katika madirisha, chumba kilikuwa kile kile. Huo ulikuwa uthibitisho wa ajabu kwamba nilikuwa pale ambapo Mungu alitaka niwe. Hii ilikuwa miaka 21 baada ya kuwa na maono hayo.

Mungu hutupa ahadi au picha ya kushikilia, ili kutufanya tutembee kwenye njia sahihi. Kwa hiyo, kumbuka, Mungu daima hunena katika wakati uliokamilika. Kwa hivyo usiache maono yako. Yatie nanga, nayo yatazungumza nawe katika njia ya maisha. Kisha utapata ukweli wa picha iliyokupeleka huko.

Pia nataka ukumbuke ukweli huu unapokimbia mbio zako.

**Kuna mstari wa kumaliza!**

Kuna lengo na thawabu kwa kazi ngumu ya mabadiliko unayoianza. Ninapongeza hamu yako ya kuona ongezeko na kasi katika maisha yako. Lakini elewa kutakuwa na masuala. Mabadiliko si rahisi.

**KUNA LENGO NA THAWABU KWA KAZI NGUMU YA MABADILIKO UNAYOIANZA.**

Nimependa kuendesha Nimependa kuendesha baiskeli maisha yangu yote, na nimekuwa na kadhaa. Miaka saba iliyopita, nilitaka kufanya kitu

tunachoita safari ya karne moja. Safari ya karne moja ni kuendesha baiskeli kwa maili 100 kwa siku moja. Nitakubali lilikuwa ni lengo gumu sana. Sikuwa nimewahi kuendesha umbali huo hapo awali, lakini kwa kuwa nilikuwa nikifikisha umri wa miaka 60, nilijua kwamba nilipaswa kufanya hivyo au singefanya hivyo kamwe. Kama nilivyokuambia hapo awali katika kitabu hiki, niliishi mashambani ambapo nilikuwa sehemu nzuri ya kuendesha baiskeli. Mimi na Drenda tulikuwa na baiskeli ya zamani aina ya Raleigh iliyojengewa watu wawili, ambayo tuliendesha pamoja mara kwa mara.

Kwa hivyo, nilianza kuzungumza na Drenda juu ya kufanya safari ya karne, pamoja, tukitumia baiskeli mpya yenye muundo huo maana ile yetu ya zamani ilikuwa nzito sana kwa safari hiyo ndefu. Cha kushangaza, alipenda wazo hilo. Sikuwa na uhakika kwamba angetaka kukaa kwenye kiti cha baiskeli kwa muda mrefu hivyo. Lakini Drenda amekuwa mtu anayependa mambo ya kusisimua kila wakati, kwa hivyo tuliamua kutafuta safari ya karne iliyofadhiliwa ambayo tungependa. Usafiri unaofadhiliwa ni safari iliyopangwa ambayo ina vituo vya kusimama vya maji na chakula vilivyowekwa kando ya barabara. Zaidi ya hayo, kuna usaidizi kwa matatizo ya kiufundi ambayo unaweza kupata pamoja na usaidizi wa matibabu ikiwa yatahitajika.

Siku moja tulipokuwa ndani ya ndege katika safari ya kibiashara, Drenda aliona safari ya karne iliyokuwa imetangazwa kwenye gazeti la shirika hilo la ndege kwamba ndiyo safari nzuri zaidi ya baiskeli kote ulimwenguni. Safari ilizunguka Ziwa la Tahoe, na kugeukia eneo la Truckee, California, kisha kurudi katika Ziwa la Tahoe ili kumaliza maili 100 zilizohitajika. Sote wawili tuliona picha zilizokuwa katika jarida hilo, tukawaza kwamba ingekuwa safari bora zaidi maishani mwetu, na tukajiandikisha.

Tulifahamu ili kufika huko na kumaliza safari, tungehitaji kwanza kununua baiskeli bora zaidi ya watu wawili. Kama nilivyosema, baiskeli

yetu ya zamani haingefaa maana ilikuwa nzito. Baada ya kutazama hapa na pale, tulinunua baiskeli nzuri nyeusi aina ya Cannondale juma moja kabla ya kuondoka.

Safari ilikuwa ikianzia California, na bila shaka tulikuwa tumepanga kuendesha gari letu kubwa kwenda huko kutoka Ohio maana tungeweza kuweka baiskeli yetu kwenye sehemu ya nyuma ya gari letu. Tulitafuta hoteli huko California na tukahifadhi chumba, tukawasha gari letu, na kuelekea huko. Hatimaye tulipowasili katika eneo la Ziwa la Tahoe baada ya juma moja la kuendesha gari, tulishangaa. Hatukuwa tumetambua kwamba Ziwa la Tahoe lilikuwa limezungukwa kabisa na milima mikubwa. Picha zilikuwa za kupendeza, na nilipaswa kukubali hilo, lakini sasa nilipotazama miinuko hiyo, nilikuwa na wasiwasi kidogo kuhusu uwezo wetu wa kukamilisha safari hiyo ya baiskeli. Lakini hata hivyo, tuliazimia kutokata tamaa.

Mke wangu aliposimama kwenye mstari ili kutuandikisha, mwanamume aliyekuwa mbele yake alimuuliza ikiwa alikuwa akiendesha njia fupi ya maili 75 au njia ya maili 100. Drenda alisema njia ya maili 100 na kwamba tulikuwa tunaendesha baiskeli ya watu wawili. Kisha akamuuliza alikuwa amefanya mazoezi kiasi gani, naye akamjibu alikuwa ameendesha baiskeli kwenda nyumbani mara chache. Alimkazia macho kwa kutoamini na kumwambia kwamba hatungefanikiwa kamwe. Alisema kwamba alikuwa mwendesha baiskeli mwenye bidii, na alikuwa amechagua maili 75 tu. Karibu na wakati huo, karani aliyekuwa akitusajili alimwuliza Drenda kama tulikuwa tunafanya safari ya maili 75 au ya maili 100. Drenda alimtazama kwa haraka yule mwanamume aliyekuwa karibu naye na kusema, "Tunafanya safari ya maili 100."

Tulianza safari karibu 6:30 asubuhi na kwa kweli hatukupata shida kwa maili 50 za kwanza isipokuwa marekebisho machache ya

baiskeli. Tulikuwa tumeendesha baiskeli yetu mpya mara moja tu kabla ya kujisajili kufanya safari hiyo. Najua, najua, tulikuwa wajinga kabisa. Kulikuwa na maelezo mengine madogo ambayo hatukujumuisha katika mipango yetu, nayo ni kwamba sehemu kubwa ya safari yetu ilihitaji tupande kati ya futi 7,000 na 8,500 kwenda juu. Hatukuwa tumehesabu kwamba hewa ya oksijeni ni kidogo katika miinuko kama hiyo. Tulipokuwa tumesafiri maili 50, nilikuwa nimeanza kuhisi vingine, na nilijua nilikuwa shidani. Lakini baada ya kupumzika kidogo na kula chakula, nilihisi vyema, na tukaanza safari tena. Sehemu ngumu zaidi ya safari bado ilikuwa mbele yetu—mwinuko wa maili 11 kabla ya mstari wa kumalizia.

Ilikuwa katika maili 86 na nusu ya safari ya kupanda mwinuko huo wa maili 11 ambapo singeweza kwendelea mbele zaidi. Vipini vya baiskeli yangu vilikuwa vimekuwa vyeupe kwa sababu ya chumvi kutokana na kutokwa na jasho kwenye jua kali, na misuli yangu ilikuwa imeacha kufanya kazi. Niliketi pale kando ya barabara nikiwa karibu kukata tamaa wakati mwanamke mmoja alikuja kwangu na kusema, "Inaonekana unahitaji chumvi." Aliweza kuona kwamba nilikuwa nimepauka na vipini vilikuwa vimefunikwa na chumvi. Alienda kwenye gari lake na kuleta chupa lenye maji yaliyochanganywa na chumvi nyingi na siki. Alisema alipenda kubeba kinywaji hicho wakati wowote alipokuwa katika safari ndefu kama hiyo. Alinipa chupa hiyo na kuniambia ninywe, nikafanya hivyo. Ndani ya dakika chache, niliweza kuhisi nguvu ikirudi ndani ya mwili wangu; nami nikainuka na kuanza kupanda mlima ule tena.

Tulipofika kwenye kilele cha mlima, yote yalikuwa rahisi hadi kwenye mstari wa kumalizia. Nilipotazama mbele yangu na kuona mstari wa kumalizia, hakuna kitu kilichoonekana bora kwangu wakati huo kuliko mstari huo! Nilijua nikifika pale, kungekuwa na chakula, kuoga na maji moto, na kuridhika kwa kufanya jambo

ambalo lilionekana kutowezekana. Katika safari hiyo yenye takriban watu 300, baiskeli yetu ilikuwa moja kati ya mbili tu zilizoendeshwa na watu wawili. Niligundua baadaye kutoka kwa wale niliozungumza nao kwamba kuendesha baiskeli ya watu wawili katika safari hiyo ilikuwa ngumu zaidi kuliko baiskeli ya mtu mmoja. Tulipovuka mstari wa kumalizia, sidhani kama maneno yangeweza kueleza hisia zetu za shukrani na unafuu kwamba tulikuwa tumemaliza.

Safari yako itafanana na hii safari yetu ya baiskeli. Kila kitu kinaonekana kuwa kizuri unapoanza safari yako, lakini kila mara kuna masuala ambayo lazima yatatuliwe. Kwa upande wetu, tungefanya safari yetu kuwa rahisi zaidi ikiwa tungefanya matayarisho yaliyofaa awali na kutafiti eneo hilo na barabara kabla ya kwenda.

Lakini sababu iliyonifanya nikuambie kisa hiki ni kukutia moyo kuzingatia mwisho—thawabu, wakati Mungu anapozungumza nawe kuhusu maisha yako ya baadaye. Kumbuka, Yeye anazungumza kuhusu mstari wa kumalizia, si mwanzo. Jinsi itakavyokuwa vizuri ukifika huko. Kwa hiyo, wakati njia inapokuwa ngumu kidogo na unajaribiwa kuvuta vigingi vyako na kuacha maono yako, lazima uwe na picha dhahiri ya mstari huo wa mwisho katika akili yako. Hiyo ndiyo sababu iliyokufanya uianze safari, na ndicho unachohitaji kuhakikisha kwamba umeshikilia. Kwa kuwa Biblia inasema uvikaze vigingi vyako, unahitaji kujua jinsi ya kufanya hivyo.

Hebu tuangalie Habakuki 2:2.

> *Bwana akanijibu, akasema, "iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji."*

Jambo la kwanza unapaswa kufanya ni kuandika maono. Huu sio mchezo wa hiari, na ni muhimu sana kwamba unaweza kuamua ikiwa utafaulu au kushindwa.

Shinikizo lina uwezo wa kufanya kile kilichoonekana kuwa wazi wakati ulianza ghafla kutokuwa dhahiri. Watu wengi huanza kuangalia nyuma wakati wa shinikizo, wakati mambo ni magumu, na inaonekana hakuna uhakika wa mafanikio. Huu ndio wakati ambao unahitaji kutazama maono, mwisho, na ujiulize, "Nataka kurudi kwa kitu gani?"

Nina rafiki ambaye aliachishwa kazi na alikuwa akitafuta majibu kuhusu maisha yake, kisha akapata nyenzo zetu. Alisema alisikiliza mafundisho yangu kila siku kwa masaa mengi, na fikra zake zilianza kubadilishwa. Aliamua kuanzisha kampuni yake ya lori badala ya kutafuta kazi mpya ya ofisi. Hapo mwanzo, ilikuwa yeye tu na lori, lakini alikuwa na mafanikio kidogo na aliweza kulipa bili zake. Lakini alipoendelea kusikiliza, maono yake yaliendelea kukua. Alianza kununua lori moja hadi nyingine mpaka sasa ana lori 18 barabarani kila wakati. Mtiririko wake wa pesa ulitoka $4,000 kwa mwezi hadi zaidi ya $100,000 kwa wiki katika miaka mitano. Aliniambia ilikuwa kazi ngumu na kulikuwa na mengi ya kujifunza kuhusu tasnia ya lori. Ilimbidi ajifunze kanuni zote za shirikisho na kisha jinsi ya kusimamia kundi la malori. Alisema kuna nyakati alishindwa kukabiliana na matatizo kwani kampuni hiyo ilikuwa ikikua kwa kasi. Lakini basi angejiuliza, *Vema, nataka kurudi kwa kitu gani? Kisha ningeendelea kusonga mbele*. Ilimbidi kukoma na kutazama mbele na pia kutambua kwamba hakukuwa na kitu chochote alikotoka.

**...UNAHITAJI KUTAZAMA MAONO, MWISHO, NA UJIULIZE, "NATAKA KURUDI KWA KITU GANI?"**

Vigingi hivyo ambavyo Isaya alizungumzia kukaza ni ahadi na maono yaliyo mbele yako. Hakuna kitu nyuma yako kinacholingana na siku zijazo ambazo Mungu ameweka mbele yako.

Hapa kuna hatua za kukaza vigingi vyako.

1. Andika maono yako, na hakikisha umeorodhesha kwa nini umekubali maono hayo. Maisha yatakuwaje ukiyatimiza? Ni malipo gani yanakungoja huko?

2. Fanya maono kuwa wazi, yaani kuwa na mpango. Unahitaji kufanya nini ili kunyakua maono?

3. Kimbia nayo, maana yake chukua hatua. Mara baada ya kuandaa mpango wako na kumaliza uchunguzi wote, endelea mbele.

4. Ninaongeza hii: Kuwa mwangalifu ni nani unashiriki naye maono yako na watu walio karibu nawe.

> *Kisha mkutano wa wafuasi waliokuwa kati yao, wakashikwa na tamaa; wana wa Israeli nao wakalia tena, wakasema, "N'nani atakayetupa nyama tule? Twakumbuka samaki tuliokula huko Misri bure; na yale matango, na matikiti, na mboga, na vitunguu, na vitunguu saumu; lakini sasa roho zetu zimekauka; hapana kitu chochote; hatuna kitu cha kutumaini isipokuwa hii mana tu!"*
>
> —Hesabu 11:4-6

Kulingana na kamusi inayoitwa Century Dictionary, neno rabble (mbwembwe) linamaanisha umati wenye ghasia na maneno machafu na kelele; mkusanyiko uliochanganyikiwa, usio na utaratibu; kundi la watu wasiojua.

Watu hawa walitaka kurudi Misri ambako walikula samaki

bila gharama yoyote?! Walikuwa vipofu au wajinga? Hakukuwa na chochote huko walikotoka ila utumwa! Amka! Najua ni jambo la kichaa, na sielewi, lakini inaonekana watu wangependelea kurudi nyuma katika hali ya uharibifu badala ya kulipa gharama ya mabadiliko na uhuru.

Nakumbuka mwakilishi mmoja wa mauzo ambaye alikuwa karibu kupoteza nyumba yake. Katika kutaka kumsaidia, nilimpa orodha kubwa ya wateja ambao walihitaji kuboresha bidhaa yao kwa kuchukua bidhaa yetu mpya kwa bei ya chini. Yaani ilikuwa kazi rahisi kama nini? Unampigia simu mteja na kumwambia kwamba ungependa kupunguza kiwango chake cha bima. Kumbuka, tayari walikuwa wateja wetu; yalikuwa mazungumzo rahisi ambayo nina hakika wateja wangefurahia. Lakini unajua nini? Asingefanya hivyo. Alisema kuwa hapendi kupiga simu. Unafanya mchezo? Alikuwa mmoja wa wawakilishi wangu wa mauzo. Tayari alijua jinsi ya kufanya hivyo na angeweza kufanya hilo akiwa usingizini. Kwa hivyo, hakufanya chochote na nyumba yake iliuzwa na sherifu.

Cha kuhuzunisha, si yeye tu. Nimeona jambo hili tena na tena na wauzaji. Ni jambo la kuchekesha. Mtu atafanya kazi kwa masaa manane kwa siku, lakini unapompa nafasi ya kupata malipo mara tano ya mapato yake, pamoja na kuwa huru, hatafanya kazi ya masaa mawili kwa siku. Je, utumwa ni mzuri hivyo? Bila shaka la. Unahitaji kukumbuka hilo wakati una shinikizo.

Na chagua marafiki zako kwa busara; ndege wa aina moja huruka pamoja. Unahitaji kuwa karibu na watu ambao wanaenda mbele na wanakuhimiza kufanya vivyo hivyo. Kaa mbali na watu ambao ni hasi na wenye mtazamo mbaya kuhusu maisha.

Fanya uamuzi thabiti wa kutogeuka kulia au kushoto mara tu unapomsikia Mungu na anza kuelekea unakoenda. Shikilia kwa uthabiti kile ambacho Mungu alisema. Nimekuwa na nyakati ambapo

nilifikiri ningenyauka kutokana na shinikizo. Nilikuambia katika sura iliyopita kuhusu kuanzisha huduma ya televisheni ya kila siku na jinsi nilivyolazimika kupambana na yale ambayo Mungu alisema wakati sikuwa na majibu. Ilinibidi kushikilia kwa uthabiti ahadi Yake na kutotikisika.

> *Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.*
>
> — 2 Timotheo 1:7

Unaweza! Sukuma vigingi hivyo ndani ya ardhi kabisa. Ongezeko linakuja. Wewe si mtumwa. Unasimama kama mwana au binti katika nyumba ya Mungu, na umerithi ufikiaji wa mali yote. Yote yanapatikana kwako!

**Kumbuka, vigingi vikiteleza, hema yote itaanguka!**

## SURA YA 9

# KANUNI YA MKAKATI

Kanuni ya mkakati ni kanuni yetu ya tano ya kuongeza kasi. Na unaweza kukisia jinsi kanuni hii ilivyo muhimu—MUHIMU SANA! Ufafanuzi wa neno mkakati, kulingana na mtandao wa freedictionary.com, ni mpango wa muda mrefu wa mafanikio, au mpango. Nilitaja katika sura iliyotangulia hitaji la kuwa na ramani kabla ya kutarajia kuona nyumba ikijengwa. Kanuni hii ni kweli katika kila eneo la maisha. Ikiwa ungeomba mkopo wa biashara, jambo la kwanza ambalo benki ingependa kuona ni mpango wako wa biashara. Watatathmini mpango wako ili kuona ikiwa una maana, ikiwa wanafikiri utafanya kazi. Watu wengi wana ndoto ya kwenda mahali fulani maishani lakini hawana mpango wa kufika huko. Huwa ninazungumza na watu kila wakati, nikiwauliza wanachotaka kufanya, na wao hunipa maono ya hali ya juu. Kisha ninawauliza watayalipiaje, nao hawajui; hawana mpango. Jibu ni nini? Andika hili:

**Mara tu unapokuwa na mpango, una kila kitu!**

Hebu nikupe mifano michache ya kile ninachomaanisha. Je, nikikuambia kuwa naweza kutatua masuala yako yote ya kifedha kwa ushauri wangu? Kwamba kile ninachotaka kukuambia kitakuweka huru kifedha, kwa hivyo tafadhali weka karatasi na kalamu yako tayari kuandika haya? Sawa, jibu ndilo hili hapa: Pata mapato halisi ya $10,000,000 mwaka huu. Bila shaka, kuna baadhi ya watu ambao hilo haliwezi kutatua matatizo yao yote, lakini kwa Waamerika wengi, litafua dafu.

Ninapotumia mfano huu katika makongamano yangu, kila mtu huanza kucheka kana kwamba ni mzaha fulani. Lakini sifanyi mzaha. Ikiwa wangepata kiasi hicho cha pesa kwa mwaka, hilo linaweza kubadilisha maisha yao. Ninapozungumzia haya katika makongamano yangu, watu huendelea kuchekacheka, lakini kwa nini? Wanacheka kwa sababu hawawezi kujiona wakipata pesa kama hizo, na kwao, inaonekana kuwa ni ujinga kuzingatia hilo. Tatizo ni kwamba hawawezi kujiona kwenye picha hiyo.

Lakini vipi ikiwa ningekuambia kuwa ninamiliki kampuni ya kuuza vitu nje ya nchi, na ninahitaji msaada fulani? Kampuni yangu inatengeneza bidhaa za kipekee, na ninahitaji kusafirisha bidhaa 5,000 mara moja. Kwa hivyo, ninakupa mkataba wa kunisaidia kupanga bidhaa hizo kwa visanduku na kuvisafirisha. Ninajitolea kukulipa $500 kwa kila kisanduku unachopakia na kukifunga ili kisafirishwe. Tuseme unaweza kupakia visanduku 100 kwa siku, nitakuwa ninakulipa $50,000 kwa siku. Na ili kufanya mlinganisho wangu kuwa dhahiri zaidi, tuseme nikupe mkataba wa miaka mitatu kwa kiwango sawa. Sasa, baada ya kusaini mkataba wangu, nikikuambia uwe na mapato ya jumla ya $10,000,000, utafikiri ni rahisi kwa sababu unajua kwamba itakuchukua siku 200 tu kupata hizo $10,000,000. Hakutakuwa na dharau wakati huo.

Hivyo kuna tofauti gani kati ya watu waliocheka pendekezo hilo na wale nilioajiri kunifungia na kunisafirishia bidhaa hizo? Tofauti ni mpango. Mara tu unapokuwa na mpango, una kila kitu. Kwa nini ninasema hivyo? Kwa sababu ingawa bado hujalipwa $10,000,000, maana umekuwa kazini kwa siku chache, utajua tayari una $10,000,000 kwa mkataba ikiwa utafuata mpango tu. Ndiyo maana nilisema, "Ukishakuwa na mpango, una kila kitu."

Wakati mimi na Drenda tulikuwa na madeni ya kutisha, sikujua njia ya kutoka katika msukosuko wa kifedha tuliokuwa nao. Tulikuwa

na madeni ya ushuru, mikopo kutoka kwa maduka ya kubadilisha vitu na pesa, kadi za mkopo 10 zilizotumiwa kupita kiwango na kughairiwa, na mikopo 3 ya kampuni za fedha kwa riba ya 28%. Tulidaiwa na daktari wetu wa meno, wasafishaji kavu, wazazi wetu, na marafiki zetu. Tulidaiwa kila mahali. Kiasili, hatukuwa na tumaini. Biashara yangu ya mauzo ya kifedha haikuwa ikiendelea vyema, na sikuwa na majibu kwa matatizo yangu ya kifedha. Kadiri tulivyojifunza zaidi na zaidi kuhusu Ufalme, tulijua kwamba Mungu angetuonyesha njia ya kutoka.

Kisha usiku mmoja, Mungu alinipa ndoto na kunionyesha katika ndoto hiyo kwamba nilipaswa kuacha kampuni niliyokuwa nayo kwa miaka tisa na kuanzisha kampuni yangu. Sasa pata hili: Kampuni yangu ingekuwa ya kusaidia watu kutoka kwenye madeni! Najua. Jambo la kichaa, sivyo? Kama ningejua jinsi ya kutoka kwa madeni, ningefanya hivyo zamani. Lakini hivyo ndivyo hasa alivyosema nifanye. Nilikuwa na mshtuko kidogo, kwa kweli, na sikujua jinsi ya kuanzisha kampuni yangu mwenyewe. Lakini kampuni inayosaidia watu kutoka kwa madeni? Halo, bado nilihitaji mtu wa kuniambia jinsi ya kufanya hivyo!

Nilipoanza kuomba kuhusu jambo hilo, Roho Mtakatifu alibadilisha maisha yangu kabisa kuhusu jinsi ya kutoka kwa madeni. Ilitokea nilipokuwa ninazungumza na moja wa wateja wangu wa biashara yangu ya bima. Lo, nilisahau kukuambia kwamba nilikuwa katika tasnia ya huduma za kifedha nikiuza bima na dhamana huku fujo hizi zote za kifedha zilipokuwa zikitokea. Najua, ni kama fundi bomba aliye na bomba linalovuja ambaye anashughulikia shida ya kila mtu lakini anapuuza yake mwenyewe. Ingawa sikuwa nikifaulu katika kazi yangu ya huduma za kifedha, uzoefu nilioupata katika ufahamu wangu wa jumla kuhusu eneo hilo kwa miaka tisa ulikuwa muhimu sana kwa kile ambacho Mungu alitaka kunionyesha.

Nikiwa nimekaa na mteja wangu na mke wake kwenye meza yao ya jikoni, tulipitia uwasilishaji wa kawaida, ambapo nilitathmini picha ya mahali walipokuwa kifedha kwa kuuliza maswali mbalimbali na kujaza kile tulichoita fomu ya taarifa. Taarifa hiyo ilitumiwa kimsingi kubaini ni kiasi gani cha bima ya maisha walipaswa kuwa nayo na kuchunguza njia mbadala za uwekezaji. Tulipokuwa tukipitia orodha yao ya madeni, wote wawili walikasirika, na mke akaanza kulia walipoeleza jinsi wote wawili walivyohisi kutokuwa na tumaini. Wote wawili walikuwa na kazi lakini walikuwa wakipungukiwa kila mwezi.

Sasa, baada ya kuishi hivyo kwa miaka tisa na Mungu kuanza kunifundisha na Drenda kuhusu Ufalme, unaweza kuwazia jinsi nilivyohisi kwa ajili yao. Kama mimi na Drenda, walikuwa Wakristo lakini bila ujuzi wowote kuhusu utendaji wa Ufalme. Wakati huo, sikuweza kueleza mengi kuhusu Ufalme isipokuwa baadhi ya mambo ya awali ambayo Mungu alikuwa ametuonyesha. Nilishiriki nao, na, bila shaka, nilishiriki baadhi ya hadithi za ajabu ambazo tulikuwa tumeona zikitukia katika hali yetu wenyewe. Bila shaka, ningeweza kusema kwamba bima ya maisha haikuwa shida yao kuu. Nilitumia muda fulani kueleza yale ambayo Mungu alikuwa ananifundisha kuhusu Ufalme, lakini nilitamani kitu ambacho ningeweza kufanya ili kutoa majibu halisi ya kifedha kuhusu hali yao.

Nikiwa ofisini mwangu usiku huo, nilipokuwa nikimaliza siku yangu na kuchambua rundo langu la kawaida la mafaili na jumbe ambazo nilihitaji kujibu, ghafla nilipata mawazo: Je, nikiangalia nyuma ya suala lao la bima ya maisha na kuchunguza kwa muda mrefu picha yao yote ya kifedha? *Je, kuna chochote ningeweza kufanya? Je, ningeanza kutafuta pesa?* Nilichomaanisha ni kwamba, je, kuna njia za bei nafuu zaidi ambazo ningeweza kupata za kufanya mambo ambayo tayari walikuwa wakifanya? Lengo langu lingekuwa rahisi, kutafuta njia za bei nafuu zaidi za kufanya mambo ambayo tayari walikuwa wakifanya

na kisha kutumia pesa zozote nilizopata kwa mtiririko wao wa pesa kulipa madeni. Lilionekana kama pendekezo rahisi, lakini kwa kweli sikujua mengi kuhusu nyanja zingine za kifedha nje ya bima ya maisha na dhamana. Na ninahitaji kukuambia kuwa hii ilikuwa kabla ya siku za mtandao. Utafiti ambao ningehitaji kufanya ungefanywa kwa njia za kizamani—kwa simu na kurasa za saraka ya simu.

Nilifanya kazi hiyo wiki nzima maana nilikuwa nimepanga kukutana na mteja huyu tena wiki iliyofuata. Nilishangazwa na kiasi cha pesa ambacho ningeweza kuokoa kwa mwezi maana nilichukua wakati wa kuchimba kila eneo la kifedha. Kufikia wakati nilipomaliza, kiasi hicho kiliongezwa hadi mamia ya dola kwa mwezi. Kwa kikokotoo changu cha fedha, nilijumlisha madeni yao yote kisha nikatumia pesa zilizookolewa kwenye malipo yao ya kawaida ya kila mwezi. Nilipobofya kitufe cha kikokotoo, nilishangazwa na jibu lililokuwa kwenye skrini—miaka 6.2. Mteja wangu angehitaji miaka 6.2 kulipa madeni yake yote, ikiwa ni pamoja na rehani ya nyumba yake, bila kubadilisha mapato yake. Ndio, unasoma ukweli, bila kubadilisha mapato yake ya kila mwezi. Nilishtuka na kufikiri kwamba nilikuwa nimekosea, kwa hivyo nilifanya hesabu tena na tena hadi nikahakikishiwa kwamba nilikuwa na jibu sahihi. Je, hili lingewezekana? Kwa nini kila mtu hakujua kuhusu jambo hilo?

Haraka nilichukua faili za wateja wengine niliokuwa nao na kuzichanganua haraka na kupata matokeo sawa. Kila mmoja wao angeweza kutoka kwa madeni katika miaka 5 hadi 7, pamoja na rehani yao, bila kubadilisha mapato yao ya kila mwezi. Kulikuwa kumekucha ofisini wakati huo nilipomaliza mahesabu yangu, lakini nilipokuwa nikielekea nyumbani, nilikuwa nimejawa na msisimko. Ikiwa nilichopata kilikuwa kweli, na hesabu zangu zote zilionyesha hivyo, basi hili lilikuwa jambo kubwa, kubwa sana.

Nilikuwa na hamu ya kujua jinsi mteja wangu angeitikia habari kama hii. Kwa ajili ya mkutano wangu uliofuata, niliamua kuandika taarifa

yote kwa ukurasa mmoja. Lengo langu lilikuwa kuwapa matumaini tu; hakukuwa na sababu nyingine. Nilijua kwamba uwezekano wa mauzo ya bima ya maisha haukuwezekana. Lakini pia nilijua wangetaka kusikia kile nilichokuwa nimegundua. Wiki iliyofuata, nilipitia tena mahesabu yangu na nilikuwa na uhakika nilikuwa sahihi.

Nilipogonga kengele ya mlango wao, nilihisi woga. Nikiwa nimekaa kwenye meza yao ya jikoni, niliwaeleza nilichokifanya wiki nzima na hesabu zao. Nilizipitia taratibu zile hesabu nilizoziandika huku nikiwaeleza jinsi nilivyookoa pesa pamoja na jina na nambari ya simu ya kampuni yoyote ambayo ingehitajika kutekeleza kile nilichowaonyesha. Ninaweza kusema kwamba walichangamka wakati pesa zilizookolewa zilipoendelea kuongezeka. Lakini nilipofikia hitimisho la kutoka kwa madeni kabisa katika miaka 6.2, pamoja na rehani ya nyumba yao, bila kubadili mapato yao, wote wawili walianza kulia, wakati huu kwa furaha. Waliketi machozi yakiwatoka huku wakiendelea kusema jinsi walivyoshtushwa na matokeo hayo. Waliruka na kunikumbatia, tukawa na wakati mzuri wa sherehe usiku huo.

Tuseme ukweli. Je, shirika la ushuru litakuambia jinsi ya kulipa kodi kidogo? Je, mwenye benki atakuambia jinsi ya kuepuka kulipa riba? La, mfumo wote umeundwa kuchukua pesa zako, sio kuzilinda. Nilijua kwamba nilichokuwa nimegundua kilihitaji kufundishwa kwa kila familia huku Amerika! Usiku huo ulibadili maisha yangu sana, na nilitaka kufanya vivyo hivyo kwa kila mteja niliyekutana naye. Kwa hiyo, nikiwa na habari hiyo na kwa uthibitisho wa ndoto ambayo Mungu alinipa, niliacha kazi yangu katika kampuni ya bima ya maisha, na mimi na Drenda tukaanzisha kampuni yetu tukifanya kile nilichokuwa nimemfanyia mteja huyo.

Katika miaka hiyo ya awali, tuliita kampuni yetu "Faith-Full Family Finances." Jina la kampuni lilisema kwa udhahiri kazi tuliyoifanya—ikiwa ungeelewa Ufalme na imani, fedha zako zingekuwa kamili.

Ninakubali halikuwa jina zuri sana la kampuni, jaribu kulisema mara 10 mfululizo, lakini lilifanya kazi. Baadaye tulibadilisha jina kuwa Forward Financial Group, ambalo liko hadi leo, na bado kampuni inaendelea kuimarika.

Kwa kweli, fedha zetu binafsi hazikuwa kamilifu. Bado tulikuwa na madeni mengi ya kulipa, lakini tulijua tumepata mwelekeo wa kufuata. Tulipozindua kampuni yetu mpya, tulikuwa na mchanganyiko wa msisimko na wasiwasi kidogo. Tulikuwa na mengi ya kujifunza kuhusu kuanzisha na kuendesha kampuni, lakini kikwazo kikubwa tulichokabiliana nacho ni jinsi ya kupata pesa za kufanya hivyo. Changamoto yetu ilikuwa tulihisi haingewezekana, na hatukutaka kuwatoza watu pesa ili kuwasaidia waondoke kwenye madeni. Hiki kilikuwa kikwazo kikubwa, na tulitumia muda mwingi sana kusali kuhusu jambo hilo na kutafuta suluhu. Bila kuingia kwa undani, Bwana alituonyesha mkakati mzuri wa kuanzisha kampuni na kupata pesa bila kumtoza mteja ada.

Kisha, ilitubidi kutafuta njia ya kuharakisha mahesabu marefu ya mikono niliyokuwa nikifanya na taarifa za wateja wangu. Nilijua kwamba ningelazimika kuandaa programu ya kompyuta ili kufanya kile tulichokuwa tukifanya, lakini sikujua chochote kuhusu kompyuta au jinsi ya kupata mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Tena, Mungu alifanya jambo la ajabu. Nilipokea simu ya mbali kutoka kwa mtu wa nyumbani kwetu ambaye alikuwa amesikia habari zetu. Alitaka kuona kile tulichokuwa tukifanya. Alipendezwa na kampuni yetu, na tulipokuwa tukizungumza, niligundua kwamba alikuwa mtaalamu wa programu za kompyuta kama kazi ya ziada. Nilizungumza naye kuhusu uhitaji wetu, naye alisema kwa shauku sana kwamba alitaka kutusaidia katika yale tuliyokuwa tukifanya. Nilimwambia kwamba tulikuwa tunaanzisha kampuni yetu na sikuwa na pesa za kulipia kazi yake, ingawa alikuwa ametupunguzia malipo pakubwa. Bado alitaka kufanya

kazi hiyo na akasema ningeweza kumlipa kila wakati pesa zilipoingia. Na hivyo ndivyo tulivyofanya.

Bila shaka watu walipenda kampuni yetu. Ilikuwa bila malipo, na watu walipenda kutafuta pesa na kutoka kwa madeni. Biashara ilinawiri haraka, na tuliweza kutoka kwa madeni katika miaka miwili na nusu. Hivi karibuni, tulikuwa na zaidi ya wawakilishi 300 wa mauzo walioshiriki mpango wetu kote nchini. Kampuni yetu ilikua na imetuwezesha kutoa mamia ya maelfu ya dola ili kusaidia Injili na watu kwa miaka mingi.

"Mpango wa madeni," kama tunavyouita, bado unatolewa bila malipo leo, baada ya zaidi ya miaka 30. Kampuni ilikua katika utume wake kadiri miaka ilivyopita. Tuliendelea kuzingatia uwekezaji wa kustaafu baada ya janga la kifedha ya mwaka wa 2001 na kisha, bila shaka, janga la 2008, ambapo mamilioni ya watu walipoteza 50% hadi 80% ya akiba zao za kustaafu. Tulitafiti suluhu salama za uwekezaji na tukazindua kipengele hicho cha biashara yetu mnamo 2001.

Ninajivunia kusema kwamba kati ya zaidi ya dola milioni mia moja za wateja wetu tunazosimamia sasa, hatujapoteza hata senti moja za uwekezaji wao katika kipindi cha miaka 21 iliyopita ya majanga ya kifedha katika nchi yetu na ya ulimwengu wote. Na kama ilivyo katika mpango wetu wa madeni, hakuna ada, hakuna ada ya usimamizi au ada ya wakala inayohusika mwanzoni au kila mwaka kwa wateja wetu wa uwekezaji. Ikiwa umechoka kucheza kamari na pesa zako za kustaafu, unaweza kufikia Forward Financial Group kwa nambari 1-(800)-815-0818 au kuwasiliana nasi katika mtandao wetu Forwardfinancialgroup.com kwa maelezo zaidi.

Lakini hoja ninayotoa ni kwamba Mungu alitupa mpango. Nilijua usiku ule ambapo yule mteja aliruka kutoka kwenye kiti chake huku akitokwa na machozi na kuzunguka meza na kunikumbatia kwamba amepata jibu lake, mpango wake. Bila shaka, tulikuwa na baadhi ya

mambo ya kushughulikia na kuunda ili kuweza kuchuma mapato na kuzalisha mpango wetu kwa ufanisi wa wateja wetu. Na kisha, bila shaka, tulihitaji kuajiri na kuwafundisha wengine kufanya jambo hilo hilo, pamoja na wafanyakazi wa ofisi yetu. Lakini sijawahi kuwa na msisimko zaidi, kuliko ule niliokuwa nao usiku wa kwanza na mteja huyo hata baada ya miaka hii yote. Kwa nini? Naam, bila shaka nilifurahi kwa ajili yao, lakini nilijua—nasema nilijua—huu ulikuwa mpango mzuri. Huu ulikuwa mpango wangu, njia ya familia yangu na mimi kuondoka kwa madeni.

**Mara nilipopata mpango huo, nilijua kwamba vita vimekwisha. Kilichobaki ni kuutekeleza tu!**

Inashangaza, sivyo, kwamba wazo moja rahisi kutoka kwa Roho Mtakatifu lilibadilisha maisha yetu milele?! Ndio, tulipaswa kuutekeleza, lakini Mungu alituonyesha mahali pa kupitia. Je, ulijisikiaje, Gary, kuwa huru kutokana na madeni? Amani! Pumziko! Tafakari jambo hili. Tulitoka katika hali mbaya ya kifedha mpaka tukatoka kwa madeni kabisa, tulilipia magari yetu pesa taslimu, nyumba yetu, na kila kitu kingine tulichohitaji. Kwa miaka tisa mirefu, nilikuwa chini ya shinikizo kubwa kila dakika ya kila siku. Sikuwa na raha. Haijalishi ilikuwa siku gani ya juma au hata likizo. Sikuwa na amani. Masuala yangu ya kifedha yalinifuata kila mahali nilipoenda. Nilivumilia aibu na fedheha mara kwa mara kutokana na hali yetu ya kifedha. Hofu ilikuwa rafiki yangu wa mara kwa mara, mashambulizi ya hofu na dawa za kupunguza huzuni vilikuwa vitu kawaida maishani mwangu katika kilele cha kukata tamaa kwangu. Lakini sasa nilikuwa huru!

Sawa, Gary, nimeelewa, na nimefurahi kwa ajili yako. Lakini nitapataje mpango wangu, mkakati wa maisha yangu? Naam, nimefurahi umeuliza. Nitazungumzia hilo. Tutaanza katika Luka sura ya tano.

*Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, Yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.*

*Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, "Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."*

*Simoni akajibu akamwambia, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu."*

*Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama.*

*Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana." Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni.*

*Yesu akamwambia Simoni, "Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu. Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao, wakaacha vyote wakamfuata.*

— Luka 5:1-11

Hiki ndicho ninachotaka uone katika hadithi hii. Kwanza kabisa, walikuwa wavuvi kitaaluma, lakini walikuwa wamevua usiku kucha na hawakupata chochote. Lakini Yesu alikuja na kuazima mashua yao ili kuhubiri kutoka humo kisha akamwambia Petro, "*Tweka*

*mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.*" Petro na washirika wake wawili, Yakobo na John, walishangazwa na kiasi cha samaki walichovua siku hiyo. Kilikuwa kikubwa sana hivi kwamba kingezamisha mashua zao zote mbili.

Kwa hiyo, hebu tujibu swali: Walipataje samaki hao? Tayari walikuwa wamejaribu usiku kucha na hawakupata chochote, lakini ghafla, wakapata matokeo makubwa zaidi ya kazi yao yote. Hili lilitokeaje? Jibu ni hili hapa. Yesu alimwambia Petro mahali pa kuvua samaki! Alisema, "*Tweka mpaka kilindini.*" Yesu akikuonyesha mahali pa kuvua samaki, unaweza kuvua samaki pia. Mtu yeyote angeweza kuvua samaki!

**Yesu akikuambia mahali pa kuvua samaki, unaweza kupata samaki!**

Sikiliza, siku za kuamini mipango na mikakati yako mwenyewe zimekwisha. Nilijaribu hilo kwa miaka tisa mirefu na migumu. Lakini unahitaji wazo moja tu kutoka kwa Mungu, mkakati mmoja tu na mpango kutoka kwa Mungu, ili kubadilisha maisha yako milele. Nitazame, sikuwa na matumaini mpaka Mungu aliponipa wazo hilo moja la kuanzisha biashara ambayo imeniletea mamilioni. Mimi si mzuri kiasi hicho. Na nina hakika kwamba ikiwa Petro angesimama hapa kukuambia kuhusu samaki wengi aliokuwa nao siku hiyo, angesema kwamba hakuwa mzuri kiasi hicho pia. Kwa hiyo, ninapozungumzia sheria ya mkakati, sisemi wewe unapaswa kujua la kufanya peke yako, la. Ninazungumzia kusikia mikakati isiyo ya kawaida kupitia kwa Roho Mtakatifu. Kumbuka Mungu alimwambia Ibrahimu nini? "Nitakufanya wewe kuwa."

**LAKINI UNAHITAJI WAZO MOJA TU KUTOKA KWA MUNGU, MKAKATI MMOJA TU NA MPANGO KUTOKA KWA MUNGU, ILI KUBADILISHA MAISHA YAKO MILELE.**

Kwa hiyo tunasikiaje mikakati

hiyo ya Roho Mtakatifu? Jinsi Petro alivyofanya kwenye mashua ile.

Vema, Gary, Yesu hayupo hapa, lakini hakika ingependeza kama angekuwa hapa. Angeniambia cha kufanya. Ninakubali Yeye hayupo hapa ana kwa ana, lakini yuko hapa. Amemtuma Roho Mtakatifu kunena kwa niaba Yake na kukusaidia.

> *Lakini huyo Msaidizi (Mfariji, Wakili, Mwombezi—Mshauri, Mtia Nguvu, Tegemeo), Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina Langu [katika nafasi yangu, kuniwakilisha na kutenda kwa niaba Yangu], atawafundisha yote. Naye atawasaidia kukumbuka yote niliyowaambia.*
>
> — Yohana 14:26 (Tafsiri ya *'Amplified'*)

Ndio, Yesu angali Mshauri na msaada wako kwa njia ya Roho Mtakatifu. Atasema nawe na kukuonyesha njia ya kufuata.

Lakini ikiwa utaishi maisha yaliyojaa mikakati ya Roho Mtakatifu na ushindi unaoongozwa na Roho Mtakatifu, unahitaji kuzaliwa mara ya pili kwanza na kisha, pili, kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Ikiwa hili ni jambo geni kwako, ni sawa. Nitakueleza kila kitu kuhusu hilo. Lakini hebu nishughulikie hoja la Roho Mtakatifu moja kwa moja: Yesu alisema ni muhimu sana kubatizwa kwa Roho Mtakatifu hivi kwamba hupaswi kuondoka nyumbani bila Yeye! Sikusema hivyo; Yesu ndiye aliyesema katika Matendo 1:4-5.

> *Wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika <u>Roho Mtakatifu</u> baada ya siku hizi chache.*
>
> — Matendo 1:4b-5

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu."*

— Matendo 1:8a

Tazama Yesu alisema, "Usiondoke nyumbani bila Yeye—hili ni jambo muhimu!" Kimsingi, alikuwa akisema, "Unahitaji nguvu hizi ili kufanya kazi ya Mungu ya kuwa shahidi wa Ufalme." Lakini leo, kuna makundi ya Wakristo ambao bado hawajasikia au kupata Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Makundi ya Wakristo waliolelewa kanisani bado hawajasikia kuhusu hitaji la Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Au walilelewa kanisani na kuambiwa kwamba Ubatizo wa Roho Mtakatifu si wa leo, kwamba miujiza imepita.

Nililelewa katika kanisa kama hilo na sikuwa nimewahi kusikia juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huwa ninapokea barua pepe nyingi kutoka kwa watu ulimwenguni kote ambao bado hawajasikia ukweli huu wenye nguvu pia. Barua pepe nyingi ninazopokea zinahoji uhalali wa karama hii katika nyakati zetu, ndiyo maana nimechukua muda kuandika ukweli kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ndio ufunguo wa uwezo wako wa kusikia mikakati ya kipekee, isiyo ya kawaida kutoka kwa Roho Mtakatifu.

Naamini kwamba Biblia iko wazi sana kuhusu suala hili, na ninataka kuiacha Biblia ijinenee yenyewe. Itajibu maswali yako yote. Lakini kwanza, nataka kukupa usuli fulani juu ya jinsi nilivyogundua ukweli kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Nilipokuwa mdogo, nilikuwa na njaa ya Mungu (ningali na njaa ingawa sasa nina umri mkubwa), na nilikuwa mshiriki katika kanisa la kimadhehebu. Tulipitia taratibu za kawaida za kidini kila Jumapili asubuhi. Labda ulilelewa hivyo pia. Nakumbuka nyimbo kadhaa zilizoimbwa na wakati wa kimya wa kutafakari. Kila mara tulinukuu

Sala ya Bwana, kasisi angehubiri, tungemalizia na wimbo, kisha baraka. Kila ibada ilifuata taratibu hiyo hiyo.

Watu huko walikuwa wa ajabu, na, ndio, walimpenda Mungu kikweli. Lakini sikuwahi kuona ukweli wa Injili. Sikuona maisha ya watu yakibadilika sana au watu wakiponywa kwa uwezo wa Mungu. Nafikiri ninaweza kusema kwamba sikuona maonyesho mengi ya Ufalme wa Mungu.

Kwa hivyo nilikuwa pale na njaa ya Mungu, katika umri wa miaka 18, nikiwa nasimamia duka la pizza la babangu. Usiku mmoja, kijana mmoja alikuja kwenye duka letu la pizza na kunialika kwenye mkutano wa uamsho. Ulikuwa unafanywa katika kanisa dogo la Kimethodisti, na mnenaji mgeni alikuwa mwinjilisti ambaye alizungumza kuhusu jinsi Yesu anavyofanya mambo yale yale leo kama aliyoyafanya katika Biblia.

Sasa hilo lilivutia umakini wangu, kwa sababu nilitaka hilo ndilo nililotaka kuona. Marafiki zangu kadhaa walikuwa washirika wa kanisa hili, kwa hivyo niliamua kutembelea mkutano huo wa uamsho. Ingawa sikusikia kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu usiku huo, niliguswa sana na uwepo wa Mungu katika ibada hiyo. Marafiki zangu waliokuwa washirika pale walinitia moyo nirudi Jumapili, jambo ambalo nilifanya. Nilipenda sana kanisa hilo na nililifanya kanisa langu jipya la nyumbani.

Wiki chache baada ya uamsho, nilikutana na kundi la wanawake waliokuwa washirika wa kanisa hilo na waliofanya mafundisho kuhusu Biblia kila juma. Walikuwa wakizungumzia mambo kama Ubatizo wa Roho Mtakatifu, karama za Roho, na mambo mengine mbalimbali ambayo sikuwa nimewahi kusikia kuyahusu hapo awali. Nilikuwa na hamu sana ya kusikia kuhusu nguvu hizo hivi kwamba niliwauliza ikiwa ningeweza kuhudhuria mafunzo yao ya Biblia ya wanawake. Mafunzo yao ya Biblia kawaida yalifanyika asubuhi, na

kwa sababu nilikuwa nikifanya kazi usiku katika duka la babangu, niliamua kuhudhuria.

Nilipofika huko, niligundua kwamba hakika mimi ndiye niliyekuwa mvulana pekee pale na kijana mwenye umri wa miaka 18 pia, lakini sikujali kuhusu hilo. Nilihudhuria mafunzo ya Biblia kwa sababu nilikuwa na njaa ya Mungu. Niliuliza maswali mengi *sana*.

Walinivumilia sana na kunipitisha katika Maandiko na kunionyesha katika Biblia yangu kwamba Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa wa leo na kwamba nguvu za Mungu zinapatikana leo kama ilivyokuwa katika nyakati za Yesu. Jambo zuri zaidi walilosema ni kwamba nguvu hizo zipo kwa ajili ya waumini wote—yeyote anayeuliza.

Baada ya kuhudhuria mafundisho kwa majuma kadhaa, waliniambia kwamba huduma ya kitaifa iitwayo *Women's Aglow* ilikuwa ikifanya mkutano katika jiji zima. *Women's Aglow* lilikuwa wakati huo na bado ni shirika linalofundisha mengi kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wanawake hao walikuwa wakipanga kuhudhuria mkutano huo, na wakanialika niende nao. Katika nyakati hizo, watu kutoka madhehebu yote walikusanyika ili kusikia na kufurahia ubatizo huu ambao, hadi kufikia wakati huo, ulikuwa unazungumziwa hasa katika makanisa ya Kipentekoste pekee. Hizo ndizo siku ambazo watu wengi huziita Ufufuo wa Kikarismatiki, ambapo mafundisho haya ya Roho Mtakatifu yalivuka mipaka yote ya madhehebu.

Nilipohudhuria mkutano wa *Women's Aglow*, niliona kwamba mamia ya wanawake walikuwa wamekusanyika. Tena, nilikuwa kati ya wanaume wachache waliohudhuria, lakini uwepo wa Mungu katika chumba hicho ulikuwa mkuu kiasi cha kushikika. Siku hiyo, mnenaji alimwomba yeyote aliyetaka kupokea kipawa hiki cha Roho Mtakatifu aje mbele kwa maombi mwishoni mwa mkutano. Kwa hiyo nilikwenda mbele ili wanawake wasali pamoja nami. Walipokuwa

wakiomba, nilijikuta nikifadhaika huku uwepo wa Mungu ukizidi kuongezeka. Nilipojisalimisha kwa uwepo Wake, nilishangaa kujisikia nikianza kuomba katika Roho Mtakatifu, na kusema maneno ambayo sikuelewa. Niliomba kwa lugha kwa muda mrefu sana usiku huo, nikiwa nimezidiwa.

Nilitaka kumwambia kila mtu niliyekutana naye kuhusu kile kilichonipata! Lakini niliposhiriki na marafiki zangu kanisani yale niliyojionea, hawakusisimka sana. Walisema kwamba ndimi ni za shetani, au kwamba ni kitu kisicho cha leo. Walinionya nijiepushe na Wakristo hao wainjilisti wanaoonyesha ari ya kidini kwa msisimko mkali!

Katika nyakati hizo, makanisa hayakuwa wazi kwa karama za Roho, na mafundisho yaliyoenea yalikuwa kwamba miujiza ilikuwa imepita pamoja na mitume. Lakini sasa nilielewa kwamba nguvu za Mungu hazikuwa zimepita hata kidogo!

Kabla ya mkutano huo wa *Women's Aglow* kufanyika, nilikuwa nimewekwa kusimamia vijana katika kanisa hilo dogo la Kimethodisti. Kwa kweli sikuhitajika kufanya mengi isipokuwa tu kuwa na mkutano wa vijana kila Jumapili usiku katika chumba kilichokuwa chini ya kanisa. Kwa kawaida tulicheza michezo, tulipata viburudisho, kisha kuwa na mafundisho mafupi ya Biblia. Nilikuwa kijana tu, lakini waliona kwamba nilikuwa na bidii kwa ajili ya mambo ya Mungu na nilikuwa tayari kusaidia katika hilo.

Kwa kawaida kulikuwa na vijana wapatao 15 katika kikundi, na baada ya yale niliyoyaona katika mkutano wa *Women's Aglow,* nilitaka kuwaambia kuhusu Ubatizo huu wa Roho Mtakatifu niliokuwa nimepokea. Niligundua kwamba, kama mimi, wengi wao hawakuwa wamesikia kuhusu jambo hili, na nilijua kwamba hawangesikia kulihusu wakati wa ibada ya Jumapili asubuhi katika kanisa hilo.

Kabla sijakuambia kilichofuata, nafikiri ninafaa kukupa sasisho

la haraka kuhusu mtazamo wangu wa wakati huo. Sikupata kibali cha mchungaji kuzungumza na vijana kuhusu hili. (Sasa ninaona kwamba ningefanya hivyo.) Pia sikuwa nimemwambia kuhusu kile nilichokuwa nimepokea.

Sikuwa ninajaribu kuasi kanisa langu na mchungaji wangu, wala kujaribu kufanya mambo kichinichini. Nilikuwa na msisimko mwingi tu. Wakati huo, kwa kweli sikuelewa utata juu ya mada hii, na hakika sikufikiri mchungaji hangetaka hilo.

Jumapili usiku baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, nilipanga kuwaeleza vijana juu ya kile nilichopokea, na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko yaliyozungumzia jambo hilo katika kitabu cha Matendo. Tulikuwa tumeketi sakafuni kwa mviringo katika kile chumba chetu chini ya kanisa niliposhiriki nao na kuwaonyesha baadhi ya Maandiko kuthibitisha tukio hilo.

Jioni hii hasa, kasisi alikuja kwa mkutano wetu na alikuwa ameketi upande wangu wa kushoto nilipokuwa nikishiriki. Sikufikiria chochote kuhusu kuwepo kwake pale. Hata hivyo, nilifikiri yeye kama mchungaji wangu, tayari alijua kila kitu ambacho ningeshiriki.

Kwa hiyo, nilishiriki nao kuhusu mkutano niliokuwa nimehudhuria na mambo niliyoyaona. Sikuzungumzia kwa kina kuhusu kunena kwa lugha. Badala yake, nilielekeza mawazo yangu kwenye Matendo 1:8 ambapo inasema kwamba tutapokea *nguvu* wakati Roho Mtakatifu atakapokuja juu yetu kuwa shahidi wa Mungu. Mwishoni mwa mkutano, sikujua jinsi ya kumalizia somo langu, kwa hiyo niliwaomba vijana wainue mikono yao ikiwa walitaka kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Sikujua la kufanya wakati huo. Namaanisha, sikuwa nimewahi kuona mtu yeyote akimhudumia mtu kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu isipokuwa kile nilichokuwa nimeona katika mkutano wa *Women's Aglow.* Nafikiri huenda nilijua Maandiko mawili au matatu

tu yaliyorejelea jambo hilo wakati huo.

Kwa hiyo, nilisema, "Kama ungependa kupokea karama hii ya bure ya Roho Mtakatifu, inua mkono wako, na tuinamishe vichwa vyetu tuombe." Hayo ndiyo tu niliyoyasema. Sikuwagusa wala kuwafundisha jinsi ya kupokea Roho Mtakatifu. Tuliinamisha vichwa vyetu na tukaomba. Bila shaka, tulifunga macho yetu kuomba kama Wakristo wote "wema" wa madhehebu walivyofundishwa.

Nilipokuwa nimeketi pale baada ya kusema "Amina," nilianza kusikia mtafaruku fulani miongoni mwa vijana. Nilifungua macho yangu na kuona kwamba baadhi yao walikuwa wakilia, wengine walikuwa wakitetemeka, na vijana saba walikuwa wameanza kunena kwa lugha. Walipoanza kunena kwa lugha, niliona mwanga usio wa kawaida kwenye nyuso zao. Walikuwa wameng'aa kama taa! Nilishtuka!

Mchungaji wangu, ambaye alikuwa hajasema lolote hadi wakati huo, alinigusa begani haraka na kuniuliza ikiwa angeweza kuzungumza nami mara moja. Tuliingia kwenye chumba kilichofuata, kisha akanitazama machoni na kusema, "Haya ni mambo ya kishetani. Huwezi kuendelea kuwa kiongozi wa vijana hapa. Hatutakuwa na mambo haya hapa."

Nikawaza, *Unawezaje kusema ni ya kishetani? Waangalie vijana hawa! Wanang'aa!* Upako juu yao ulikuwa dhahiri kabisa. Kwa kweli, sikujua neno upako lilikuwa na maana gani wakati huo. Nilijua tu kwamba walikuwa wanang'aa, na sikuwa nimewagusa au kuwaambia cha kufanya. Nilikatishwa tamaa na kuchanganyikiwa sana mchungaji wangu aliponikaripia hivyo, wala sikujua la kufanya.

Jumapili iliyofuata, nilirudi kanisani, lakini badala ya kuketi karibu na madhabahu kama kawaida, niliketi nyuma. Nilijua nilikuwa mahali pabaya machoni pa mchungaji wangu kwa sababu ya ule mkutano wa vijana, na niliwaza ni bora nitulie kwa muda mfupi huku nikiwaza cha kufanya.

Wakati wa ibada, kulikuwa na ule muda wa kawaida wa kukaa kimya ili kutafakari. Huu ulikuwa wakati wa heshima na utulivu sana wa maombi katika kanisa langu. Kichwa cha kila mtu kiliinamishwa, na hapakuwa na sauti yoyote kanisani. Ungesikia hata pini ilipoanguka. Ulikuwa wakati huu ambapo nilihisi mtu akigonga bega langu. Nilikuwa nimeketi mwishoni mwa kiti, na kumbe kulikuwa na mtu ambaye alikuwa amesimama kwenye njia na kunigonga begani mwangu.

Mwanzoni, nilishtuka na kufikiria kwamba ni nani alikuwa amesimama na kutembea wakati wa utulivu sana wa maombi. Nilipotazama juu, nilishangaa kuona mmoja wa wale vijana waliokuwa katika mkutano wetu wa vijana wiki moja awali. Nilifahamu pia kwamba alikuwa mmoja wa wale saba waliokuwa wamepokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu usiku ule. Alinitazama na kusema, "Twende!" Nikawaza, *Twende? Twende wapi?*

Ajabu ni kwamba, alikuwa na mng'ao ule ule aliokuwa nao usiku ule alipopokea Roho Mtakatifu, na nilijua Mungu alikuwa akifanya jambo fulani. Lakini sikuwa na uhakika huu ulikuwa wakati au mahali pa kufanya chochote kwa kuwa tayari nilikuwa shidani na mchungaji. Pia nilijua kwamba hatungeweza kufanya chochote tulichotaka katika ibada ya Jumapili asubuhi.

Hapo ndipo alisema, "Ninaenda kumwombea mamangu." Sasa, nilianza kuelewa alichokuwa akimaanisha. Nilimfahamu mamake. Alikuwa mwanamke mdogo, mwembamba na alikuwa mgonjwa kwa muda mrefu sana. Mifupa mitano ya uti wa mgongo wake ilikuwa na shida na tumaini pekee la daktari lilikuwa kuiunganisha mifupa hiyo pamoja. Upasuaji huu ulikuwa mgumu sana, na rafiki yangu alikuwa mtoto wake wa pekee. Bila shaka alikuwa na wasiwasi nyingi kuhusu mamake.

Baada ya kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu, alihisi hakika

kwamba Yesu angemponya mamake. Kwa hiyo aliposema, "Twende," nilifikiri angeenda kwa mamake na kumwekelea mikono na kumwombea kwa utulivu. Lakini hakufanya hivyo. Alimwendea mamake, akamnyanyua pale pale kwenye kiti na kumpeleka mbele ya kanisa.

Alimketisha chini na kuanza kumuombea kwa sauti ya juu kama awezavyo kwa ndimi. Sasa kumbuka, haya yote yalifanyika wakati wa kukaa "kimya" na kutafakari, ambao sasa haukuwa kimya tena. Nilishtuka! Kisha akanigeukia na kusema, "Sasa wewe toa maelezo ya kile kinachoendelea hapa."

Sasa nilipata ufahamu wa sababu alitaka niende pamoja naye. Aliwaza kwamba kwa sababu mimi ndiye niliyemwambia kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, basi ingefaa niwaambie washirika maana yake baada yao kumsikia akiomwombea mamake kwa ndimi.

Kwa hiyo nilisimama mbele ya mkusanyiko wa washirika nikiwa mnenaji wake, naye alikuwa akimwombea mamake kwa ndimi. Kwa kweli sikujua la kusema, hasa kwa vile mchungaji wetu alikuwa ameketi pale akinikazia macho. Niliwaambia washirika kwamba mamake alikuwa mgonjwa na kwamba alikuwa akimwombea kwa ndimi, kama Biblia inavyosema. Lakini wajua nini? Aliponywa papo hapo kanisani asubuhi hiyo!

Hiyo ilikuwa imani ya mwana ambaye kwa kweli hakujali kile mtu mwingine alichofikiria kuhusu maombi yake. Alikuwa na hakika kwamba Roho Mtakatifu alikuwa hai na angeweza kumponya mamake.

Ingawa aliponywa papo hapo, kanisa halikupokea hilo. Wengi wao walinijia baadaye na kusema, "Naam, hatukujali kwamba alimwombea mamake, lakini ndimi hizo, hatuwezani na mambo hayo ya ndimi." Ninaweza kukuhakikishia kwamba shetani anachukia jambo la kunena katika ndimi, lakini ninatumai nitakusaidia

kuelewa kwa nini anachukia ndimi kabla ya mwisho wa kitabu hiki.

Labda ulilelewa katika kanisa ambapo ndimi na karama za Roho hazikutumiwa. Au labda ulipokuwa ukikua ulifundishwa kwamba ndimi sio za leo au zilikwisha zamani. Maswali haya si magumu kujibu. Biblia iko wazi sana kuhusu jambo hili. Kwa hiyo hebu tuliangalie Neno vyema ili tupate ukweli juu ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hebu turejee kwenye mistari tuliyosoma mwanzoni mwa sura hii.

*"Msitoke Yerusalemu, bali ngojeni ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari Zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache."*

— Matendo 1:4b-5

Kuna mambo kadhaa muhimu tunayoweza kuona katika aya hii:

1. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na kubatizwa kwa maji.

2. Yesu alisema ni muhimu sana. Kwa kweli, Aliweka wazi kwamba hakika huwezi kufanya chochote bila hilo.

Kumbuka, Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi waende kuhubiri Injili kwa kila taifa, lakini hawangeweza kuonyesha au kuthibitisha Ufalme wa mbinguni bila ubatizo huu. Kwa hiyo akasema, "Subirini mpaka mpate uweza huu."

*"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi Wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

— Matendo 1:8

Nguvu! Neno la Kigiriki la nguvu hapa ni dunamis na ndipo tunapata neno letu la baruti. Kwa hiyo tunaona kwamba nguvu za Mungu zinakuja juu yetu kufanya kazi zake. Mapema katika huduma ya Yesu, Alikuwa ametaja kwamba nguvu, au upako Aliokuwa akitenda chini yake, ulitoka kwa Baba Yake.

> *"Hayo maneno niwaambiayo Mimi siyasemi kwa shauri Langu; lakini Baba akaaye ndani Yangu huzifanya kazi Zake."*
>
> — Yohana 14:10b

> *Amin, amin, nawaambia, "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe.*
>
> — Yohana 5:19b

Wajua, Yesu Mwenyewe alihitaji kutiwa nguvu na Roho wa Mungu. Neno *upako* linamaanisha "kutumika kwa." Yesu alipokea upako huo kwenye Mto Yordani kutoka kwa Baba Yake wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake katika umbo la njiwa.

Ni baada tu ya Yesu kupokea upako huo ndipo alipoweza kufanya kazi za Ufalme. Ikiwa Yesu aliuhitaji, sisi pia tunauhitaji! Nguvu hiyo itashuhudia (au kuwa shahidi) kwa kuonyesha kwamba Mungu yuko halisi kwa wale wasiomjua.

Biblia pia inasema kwamba mtapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu ATAKAPOKUJA JUU YENU, sio atakapokuja ndani yenu kama wakati mlipozaliwa mara ya pili.

Wengi huchanganyikiwa tunapozungumza kuhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakifikiri kwamba tayari wamempokea Roho Mtakatifu walipomkubali Kristo. Na ukweli ni kwamba *walimpokea* Roho Mtakatifu walipompokea Kristo. Roho Mtakatifu alihuisha roho zao kwa Mungu na kuzifanya ziwe kitu kimoja na Mungu.

Tunahuishwa kwa Mungu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yetu tunapozaliwa mara ya pili. Lakini tazama kwamba Maandiko haya yanasema wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yako. Hili ni jambo muhimu ambalo tutalishughulikia baadaye katika kitabu hiki: kuzaliwa mara ya pili na kutiwa mafuta au kubatizwa na Roho Mtakatifu ni matukio mawili tofauti. Tunaweza kupata ufahamu mzuri zaidi kuhusu hili katika Yohana 20:21-22.

> *Basi Yesu akawaambia tena, "Amani iwe kwenu; kama Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawapeleka ninyi." Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, "Pokeeni Roho Mtakatifu."*
>
> — Yohana 20:21-22

Hapa tunamwona Yesu baada ya kufufuka akiwasalimia wanafunzi Wake na kuwapulizia na kusema wampokee Roho Mtakatifu. Huu ndio wakati walipozaliwa mara ya pili na roho zao kuhuishwa kwa Mungu. Hata hivyo Yesu aliwaambia wangojee Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao ungekuja juu yao siku nyingine baadaye.

Ikiwa walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu kikamilifu Yesu alipowapulizia, kwa nini aliwaambia wangoje Yerusalemu hadi wampokee Roho Mtakatifu ambaye aliahidiwa kuja juu yao? Tena, haya ni matukio mawili tofauti na kazi mbili tofauti, bali Roho yule yule. Pia, kama nilivyosema, nataka kutaja kwamba Yesu alipaswa kubatizwa na Roho Mtakatifu ili aingie na kuwa na ufanisi katika huduma Yake. Kabla ya Yesu kubatizwa na Roho Mtakatifu, hakuna mahali tunaona akifanya muujiza hata mmoja. Je, Yesu alizidisha mkate mezani alipokuwa akikua? Je! Alifanya miujiza alipokuwa mtoto mchanga? Je, alizidisha chakula Chake alipokuwa mtoto kilipoisha kwa sababu bado alikuwa na njaa? La! Hakufanya hivyo.

Kwa nini hakufanya hivyo? Jibu rahisi na la ukweli ni: *Hangeweza*.

Haikuwa mpaka *baada* ya kupokea Roho Mtakatifu katika Mto Yordani ambapo alianza kufanya miujiza. Wajua, Yesu alikuja kama mwanadamu. Hakuja kama Mwana wa Mungu katika nguvu na utukufu Wake. Alikuwa na vizuizi kama mwanadamu yeyote yule. Hakuwa na uwezo wa kuponya au kufanya miujiza yoyote, kama ilivyo kwako na mimi.

Lakini, tofauti na sisi, roho ya Yesu ilikuwa hai kwa Mungu alipozaliwa kama mtoto. Roho Yake ilikuwa hai daima kwa Mungu; Yeye hakuhitaji kuzaliwa mara ya pili kama sisi. Hata hivyo, ingawa roho Yake ilikuwa hai kwa Mungu kama Mwana, bado alihitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu kabla ya kuanza huduma Yake, kama ilivyo kwetu sisi.

> *Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu Yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, "Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa naye."*
>
> — Mathayo 3:16-17

Kumbuka, tunamuona Yesu kama Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, lakini hakuhudumu na cheo hicho. Miujiza ilianza baada ya Roho Mtakatifu kuja juu Yake katika Mto Yordani.

Huduma yako (kwa sababu kila mwamini ameitwa kufanya kazi ya Yesu) haiwezi kuanza hadi ubatizwe na Roho Mtakatifu—unahitaji nguvu za Roho Mtakatifu ili kufanya mambo. Na unahitaji uwezo wa kuomba katika Roho ili kujua jinsi ya kuyafanya.

Bila shaka, unaweza kuwaambia wengine jinsi ulivyozaliwa mara ya pili kama Biblia inavyosema. Wakristo wengi ambao hawajabatizwa

na Roho Mtakatifu wana ujuzi wa kushiriki Habari Njema ya Injili, lakini hawana uwezo wa kudhihirisha Ufalme jinsi Yesu alivyofanya. Hii inasababisha udhaifu mwingi katika mahubiri.

Yesu alipowakabili Mafarisayo kuhusu kutokuamini kwao, alirejelea miujiza aliyokuwa akifanya. Alisema,

> *"Mnisadiki ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani Yangu;la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe."*
>
> — Yohana 14:11

Kimsingi Yesu alikuwa akisema kwamba udhihirisho huu wa Ufalme ulikomesha mabishano yote; tosha. Sasa, bila shaka, kila muumini ana haki kamili za kisheria kudai kila kitu ambacho Yesu alilipia, ikiwa ni pamoja na uponyaji. Kila muumini anaweza kupokea kila ahadi ya Mungu kwa imani (kukubaliana na mbingu), na hahitaji Ubatizo wa Roho Mtakatifu ili kupokea kutoka kwa Mungu.

Lakini ili nguvu hiyo itiririke kutoka kwako kwenda kwa wengine, na ili wewe uweze kutumia karama za Roho na kufurahia faida ya kufahamu siri za mbinguni kwa njia ya kuomba kwa ndimi, lazima uwe na nguvu ya upako huo!

Unaweza kuuliza, "Kwa nini niombe kwa lugha?" Ibilisi anawachukia waumini wanaojua kuomba katika Roho (kwa ndimi), na ninataka kuwa na uhakika kwamba unaelewa kwa nini.

Paulo aliposema kwamba alifurahi kwamba aliomba kwa lugha zaidi ya mtu mwingine yeyote, lazima kuwe na sababu iliyomfanya ahisi hivyo. Paulo alitoa maoni katika 1 Wakorintho 14 ambayo tunahitaji kusoma.

> *Yeye anenaye kwa lugha* ***hujijenga*** *nafsi yake, bali ahutubuye* ***hulijenga*** *kanisa.*
>
> — 1 Wakorintho 14:4

Tutazame jambo hili kwa kina zaidi kidogo. Je, ina maana gani kujengwa? Neno jenga linamaanisha "kufundisha au kufaidika, hasa kiadili au kiroho; kuinua."

Itakupasa kukubali kwamba kuna nyakati nyingi ambapo unahitaji kufundishwa ili kujua njia ya kufuata, kuelewa hali fulani, au kufanya uamuzi unaofaa. Huu ndio msaada unaoweza kupata kupitia kwa kuomba kwa lugha: kujijenga au kuleta mafundisho maishani mwako. Paulo anaweka wazi jambo hili.

> *Kwa maana yeye anenaye kwa lugha hasemi na watu, bali husema na Mungu; kwa maana hakuna asikiaye, bali yeye husema siri katika roho yake.*
>
> — 1 Wakorintho 14:2 (Tafsiri ya '*DLNT*')

Tena, Paulo anazungumza juu ya roho zetu kuwa na uwezo wa kusema mambo ambayo hatujawahi kuona, kusikia, au kuwa na ujuzi kuyahusu, au kama vile Paulo ayaitavyo "siri." Pia tazama katika mstari huu kwamba Paulo alisema tunaomba siri <u>katika roho zetu</u> wenyewe, si Roho wa Mungu. Je, jambo tusilolijua huingiaje katika roho zetu? Hiyo ni rahisi! Kwa Roho wa Mungu, ambaye sasa ni kitu kimoja na roho zetu.

> *Kwa maana ni nani katika wanadamu ayajuaye mawazo ya mtu isipokuwa roho yake iliyo ndani yake? Vivyo hivyo mawazo ya Mungu hakuna ajuaye ila Roho wa Mungu.*
>
> — 1 Wakorintho 2:11

Roho zetu zinapopata mawazo ya Mungu, akili zetu pia hupokea mawazo haya. Akili zetu zinapotafakari mawazo ya Mungu, tunaita hilo "ufunuo," "kutiwa nuru," au, kama Paulo asemavyo, "kujengwa." Sasa unajua kwa nini Paulo alisema alifurahi kwamba aliomba kwa lugha zaidi ya mtu yeyote mwingine; alipata faida ya kujua mapenzi ya Mungu katika kila hali.

Hili ndilo Paulo alilorejelea katika 1 Wakorintho 2:15-16:

*Lakini mtu wa rohoni huyatambua yote, wala yeye hatambuliwi na mtu. Maana, "Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe?" Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.*

Hatuzuiliwi na hukumu ya kibinadamu, lakini tunaweza kufanya maamuzi kuhusu mambo yote kupitia kwa msaada wa Mungu. Hii ni habari njema ajabu! Tunao uwezo, kwa kuomba katika Roho (ndimi), kupokea siri, mambo ambayo hatukujua; na kwa ujuzi huo, tunaweza kufanya maamuzi sahihi kuhusu mambo yote!

**UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU NI SILAHA YA SIRI YA MUNGU!**

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni silaha ya siri ya Mungu! Anaweza kushusha mapenzi Yake duniani bila shetani kujua ni nini kinaendelea. Hakika kuomba katika Roho kumeorodheshwa kama sehemu ya silaha zetu za kiroho katika Waefeso 6:18a:

*Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho.*

Kuomba katika Roho hutupatia fursa ya kupata mikakati ambayo itatuwezesha kumweka adui kando, au kupiga hatua kwenda mbele kwa kutumia mbinu za kipekee na zisizo za kawaida. Paulo

alisema kwamba Roho wa Mungu atatufunulia yale mambo ambayo tumepewa bure.

Faida inayodokezwa ni kwamba tutaweza kufanya maamuzi yanayofaa maishani kwa kutumia akili ya Kristo. Nafikiri inakupasa ukubali kwamba hili ni jambo zuri sana!

(Baadhi ya sura hii imechukuliwa kutoka kwa kitabu changu *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa na Mkakati.* Kwa habari zaidi kuhusu kusikia kutoka kwa Roho Mtakatifu, tafadhali fikiria kupata nakala hiyo.)

SURA YA 10

# KANUNI YA UHARAKA

Ninapoketi hapa nyumbani kwangu, huwa ninatazama nje dirishani kuelekea kwa miti yangu ambayo iko nyuma ya nyumba yangu. Ninaishi katika kipande kizuri cha shamba hapa Ohio ambacho kina vilima vyenye miti mirefu mizuri. Nina zaidi ya ekari 55, ambazo takriban ekari 20 zina miti, takriban ekari 10 hadi 12 ni kinamasi, na ekari zingine ni shamba la nyasi.

Kitu pekee kilichokosekana ni bwawa. Ndiyo, kinamasi huwa na maji ndani yake na hunipa fursa ya kuwinda bata wengi katika msimu wa vuli, lakini, kwa kweli, hakina kina cha kutosha kuwezesha samaki kustahimili joto la kiangazi. Mwaka jana, niliamua kuweka bwawa zuri nyuma ya nyumba yetu. Sasa ninapoketi kwenye sitaha yangu ya nyuma, huwa ninatazama kinamasi, misitu, na bwawa zuri pia. Nimefurahishwa na hilo. Sababu halisi ya kuweka bwawa pale ni kwa sababu napenda kuvua samaki. Nililelewa karibu na bwawa, na siwezi kuhesabu jioni zote mimi na marafiki zangu tuliketi kando ya bwawa hilo na kuvua samaki aina ya kambare.

Nilipojenga The Now Center, makao makuu ya huduma yetu, niliweka bwawa nyuma ya mlango wangu wa nyuma wa ofisi, na nguzo yangu ya uvuvi iko pale pale ikiningoja. Nimejaza bwawa hilo na samaki wakubwa wa kila aina, hivyo ninaweza kutoka nje ya mlango wa ofisi yangu, na kutembea kama futi 40, na kupata mlo wangu wa jioni. Nilitaka kuwa na kitu kama hicho nyumbani kwangu.

Kwa hivyo, nilijaza bwawa langu jipya na samaki aina tofauti. Lo, ni usanidi mzuri ulioje.

Ninazungumzia uvuvi kwa sababu hili litatumika kuonyesha kanuni ya uharaka ambayo ni muhimu sana katika kazi yako.

Wiki iliyopita, nilifundisha katika makanisa kadhaa huko Florida. Rafiki yangu mmoja ana nyumba huko kwenye ufuo wa Gulf Coast, na alinialika nikae nyumbani kwake kwa siku kadhaa. Naam, singekataa mwaliko huo, haswa ikiwa ningevua samaki kidogo nikiwa huko. Hivyo Mimi na Drenda tulikaa huko kwa siku kadhaa. Asubuhi ya kwanza, nilitoka kwenda ufukweni, na katika muda wa saa moja hivi, nilikuwa nimekamata samaki weupe sita, kambare wawili, samaki mmoja aina ya *ladyfish*, na papa wawili. Tulikula papa na samaki mweupe katika chakula cha mchana.

Lakini hapa kuna somo. Wakati ninapovua, ninavua. Huwa nasimama pale na nguzo yangu mkononi nikingojea iguzwe kidogo. Kila wakati mimi huwa macho. Huwa niko tayari kuvuta nguzo hiyo mara moja. Kwa sababu hiyo, huwa sikosi kunasa samaki wengi. Karibu miezi miwili iliyopita nilikuwa nimesimama kando ya bwawa nikiwa na fimbo wala sikuwa nimeishikilia. Si ungelijua hilo? Samaki alikamata kamba hiyo, na nguzo ikaruka moja kwa moja angani na kuanguka baharini. Sikuwa macho na nilimkosa yule samaki pamoja na nguzo yangu!

Kwa hivyo hii ndiyo kanuni ya uharaka: **Je! unataka kuvua samaki au kukata chambo?** Labda umesikia usemi huu hapo awali. Unahusu watu wawili, mmoja ambaye anajishughulisha na kukata chambo, na msisitizo mkubwa uko katika neno kujishughulisha, na mwingine ambaye anazingatia uvuvi. Ninapovua samaki, huwa niko macho, tayari kuchukua hatua dakika yoyote. Lakini nimewahi kwenda kuvua samaki na watu wasiozingatia kamba zao. Samaki wakigonga kamba zao, inanibidi nipige kelele, “Wewe, kamba yako imeumwa!” Kisha

wanaposhikilia nguzo zao, samaki wametoweka. Au lazima niseme, “Wewe, inaonekana unahitaji chambo kwenye ndoano hiyo” au “Hebu nikusaidie kutoa kamba yako kwenye mti huo.” Nafikiri sote tumekutana na watu kama hawa.

Najua inaonekana kama ninazungumza kuhusu uvuvi, lakini sivyo. Ninazungumza juu ya wafanyikazi wako, watu unaoshirikiana nao, na labda hata wewe. Ninazungumza juu ya kupoteza fursa. Ukweli wa mambo ni huu. Watu waliokengeushwa hawajui kwamba walipoteza fursa! Ikiwa uliniajiri kama mshauri, na tayari umefanya hivyo kwa kusoma kitabu hiki, ninaweza kukuhakikishia kwamba unapoteza fursa; na kwa kutotumia kanuni hii, unapoteza pesa nyingi sana.

Mke wangu alimpigia simu muuzaji wa magari aina ya Honda katika mtaa wetu hivi majuzi kwa sababu tulihitaji kazi ya ukarabati ifanywe kwenye gari letu. Walisema ingekuwa wiki tatu hadi nne kabla yao kuikarabati. Kwa hiyo, mke wangu akasema, “Huo ni muda mrefu sana. Mume wangu pia anataka kununua gari lingine akija hapo. Je, kuna uwezekano wowote wa kuikarabati hii kabla ya muda mrefu kuisha? Tunahitaji tu kubadilisha betri na kuweka magurudumu mapya. “La. Samahani, haiwezekani.” Hiyo ni kauli kali kwamba haiwezekani. Haiwezekani? Ingechukua labda saa moja tu kufanya hivyo, au hata chini ya saa. Kisha Drenda akamwambia meneja kwenye simu, “Sawa, hivyo si vyema kwa sababu utakosa mauzo. Nafikiri tutaipeleka kwenye duka lingine la Honda, lakini asante kwa wakati wako. Kisha meneja akasema, “Sawa, samahani.” Hebu nifafanue taarifa ya mke wangu kwa msimamizi huyo. “Najua tulinunua gari kutoka kwenu, lakini labda hatutarudi kwenye duka lenu tena.”

Sasa, hebu tuseme kuwa idara yao ya wakarabati imejaa kazi. Wanafanya kazi kabla ya masaa na baada ya masaa kukarabati magari ya watu wengi. Je, ungeitikiaje simu hiyo? Ningeuliza kila mtu pale,

labda hata kutoa bonasi ndogo ya malipo kwa fundi yeyote ambaye alikuwa tayari kubaki na kushughulikia hitaji hilo. Yeyote aliye na akili angetambua sio tu kwamba alikuwa akikataa kazi bali pia mteja aliyekuwa amemwamini, ambaye sasa angeenda kwa washindani, na labda hangerudi tena.

Nilipotafakari kile nilichoona wakati nilikuwa nikinunua gari langu kutoka kwa muuzaji huyo hapo awali, nilikumbuka jinsi hawakuwa makini. Hakuna aliyenisaidia; ilibidi nitafute mtu mwingine wa kunisaidia. Hawakunieleza jinsi gari hilo lilivyopaswa kutumiwa. Baada ya takriban miezi sita, nilipokea kifurushi kwenye barua chenye mwongozo wa jinsi ya kutumia gari langu, pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono iliyosema, "Tulipata mwogozo huo karibu na idara ya wakarabati, na tulipouchunguza tulitambua ni wa gari lako."

Kulingana na uzoefu wetu kumhusu msimamizi huyu, kuna mambo kadhaa ambayo ninaweza kukuambia. Kwanza, yeye sio mmiliki! Na pili, pengine anazingatia zaidi timu yake ya mchezo kuliko kazi yake. Lakini hili si jambo jipya katika utamaduni wetu; huu ndio utamaduni wetu.

Sawa, sasa ninahitaji kunena moja kwa moja zaidi hapa, na ninataka kurejelea mfano aliotumia Yesu katika Luka 16. Najua, ni mrefu kidogo, lakini unahitaji kuchukua wakati wa kutafakari kile Yesu alikuwa akisema hapa.

> *Tena, aliwaambia wanafunzi Wake, "Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyekuwa na wakili wake; huyu alishitakiwa kwake kuwa anatapanya mali zake. Akamwita, akamwambia, 'Ni habari gani hii ninayosikia juu yako? Toa hesabu ya uwakili wako, kwa kuwa huwezi kuwa wakili tena.'*
>
> *Yule wakili akasema moyoni mwake, 'Nifanyeje? Maana,*

*bwana wangu ananiondolea uwakili. Kulima, siwezi; kuomba, naona haya. Najua nitakalotenda, ili nitakapotolewa katika uwakili, wanikaribishe nyumbani mwao.'*

*Akawaita wadeni wa bwana wake, kila mmoja; akamwambia wa kwanza, 'Wawiwani na bwana wangu?'*

*Akasema, 'Vipimo mia vya mafuta.'*

*Akamwambia, 'Twaa hati yako, keti upesi, andika hamsini.'*

*Kisha akamwambia mwingine, 'Na wewe wawiwani?' Akasema, 'Makanda mia ya ngano.'*

*Akamwambia, 'Twaa hati yako, andika themanini.'*

*Yule bwana akamsifu wakili dhalimu kwa vile alivyotenda kwa busara; kwa kuwa wana wa ulimwengu huu katika kizazi chao wenyewe huwa na busara kuliko wana wa nuru. Nami nawaambia, Jifanyieni rafiki kwa mali ya udhalimu, ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao ya milele.*

*Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia; na aliye dhalimu katika lililo dogo, huwa dhalimu katika lililo kubwa pia. Basi, kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?*

*Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali."*

—Luka 16:1-13

Lo, Lo, Lo! Mfano huu kweli umepiga shabaha. Msimamizi huyu hakujali kuhusu mmiliki wa duka la magari. (Samahani, ninatumia tukio hili kama mfano katika hadithi yetu.) Alichojali ni kuondoka

saa kumi na moja jioni au labda kwa sababu zingine. Lakini ikiwa angekuwa mmiliki wa biashara hiyo, angekuwa na picha wazi ya malipo yote aliyopaswa kulipa ili kuendesha duka hilo, na kuelewa kwamba alikuwa mtu wa mwisho kulipwa ikiwa kulikuwa na pesa zilizobaki baada ya kufanya malipo yote, basi ninaweza kukuhakikishia kwamba kamwe hangeweza kusema, "haiwezekani."

Katika mfano wa Yesu alisema meneja huyo ambaye hakuwa mwaminifu alikuwa na uwezo wa kufikiri kama mmiliki wa nyumba, lakini alichofikiria ni yeye mwenyewe. Alikuwa mfanyakazi asiye mwaminifu! La, wacha nitumie maneno mengine: Alikuwa mtu asiye mwaminifu. Alikuwa mwajiriwa.

**Na kama hamkuwa waaminifu katika mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?**

Ni yule mtu anayezungumza kwa simu yake wakati wote wakati wa kuvua samaki kisha anashangaa jinsi alivyokosa kukamata samaki.

Inashangaza sana kwangu kutazama jinsi jambo hili limetokea katika biashara yangu kwa miaka mingi. Kuna wakati ambapo nimeajiri watu wa kuandaa michoro na wauzaji ambao hawana haraka. Inanibidi niendelee kuwakumbusha kutuma hili au kuhakikisha wameweka tukio hili au lile kwenye tovuti. Wakati mwingine ninapata tukio lililotokea miezi kadhaa iliyopita bado liko kwenye tovuti. Lakini baadaye ninagundua kwamba wana biashara yao ya "kando," na kila kitu katika tovuti yao kiko kamili na viungo vyote vinafanya kazi. Au ninaajiri mfanyakazi ambaye haonekani kuwa mwepesi katika kufanya chochote, kisha ninashtuka kumtazama akitimiza majukumu yake ya kibinafsi kwa uharaka mkubwa.

Kusema kweli, ukosefu huu wa uharaka na ukosefu wa umiliki umekuwa janga katika nchi hii. Nina hakika unaweza kuuona kwenye migahawa ya karibu ya vyakula vya haraka katika mji wako. Tulikuwa na duka la chakula la McDonald's katika mji wetu ambapo mfanyikazi

wao angeweka viti juu ya meza na kuzima mataa ya sehemu ya kulia chakula saa moja kabla ya kufunga. Mataa yalikuwa yakiwaka katika sehemu ya mbele ya kuhifadhia pesa, lakini yalizimwa katika sehemu ya kukaa. Kila mtu alidhani wamefunga walipokuja na kuona viti juu ya meza na taa zimezimwa.

Siku moja, niliingia ndani wakati taa zilikuwa zimezimwa na viti vilikuwa juu ya meza, na nikasema, "Samahani. Najua mnafunga, lakini nahitaji tu kupata chai ili niende." Nilishtuka wakati mtunza fedha aliposema, "Oh, hamna shida, hujachelewa. Hatufungi hadi baada ya saa nzima kwanzia sasa." Niliuliza, "Je, chumba chenu cha kulia chakula kiko wazi?" "Ndio, ondoa kiti kutoka kwa meza yoyote." Kwa hiyo, niliuliza ikiwa chumba cha kulia kilikuwa wazi hadi wakati wa kufunga, na akasema ndio. "Kwa hiyo," nikasema, "unaweza kuniambia kwa nini viti vyenu huwa juu ya meza na mataa ya chumba chenu cha kulia huwa yamezimwa kila usiku saa moja kabla ya kufunga?" "Unaweza kuja wakati wowote. Meneja anapenda kuondoka wakati wa kufunga, kwa hivyo anataka sakafu zipanguzwe na viti viwekwe tayari kabla ya kufunga." "Inashangaza. Kwa hiyo, meneja wenu anataka kujiandaa kufunga ilhali hamjafunga badala ya kujiandaa kukaa wazi wakati duka liko wazi." Inaonekana kwangu meneja huyo ni mwajiriwa!

**Uko wazi au la?**

Hapa kuna maneno ya kutegemewa yenye msingi wa yale ambayo Yesu alifundisha. Kamwe usimweke mwajiriwa kusimamia mambo yako—KAMWE. Nafikiri jambo zuri kuhusu utelezi huu wa kitamaduni katika hali ya wastani ni kwamba usipochelewa kazini, unajidhihirisha kama jua katika ulimwengu wa giza. Kila mwajiri ninayemjua hutatizika kupata

**HAKUNA VYEO VIDOGO AU VISIVYO NA MAANA MAISHANI.**

wasaidizi wanaofikiri kama wamiliki. Kuitii kanuni hii ya kuongeza kasi hakutakuletea pesa nyingi tu bali pia kunaweza kukufanya usonge mbele kwa ghafula juu ya wenzako, moja kwa moja hadi kileleni, kama vile Yusufu alivyofanya alipotolewa gerezani na kusimama mbele ya Farao. Alifanywa mkuu wa pili katika Misri nzima. Hakuna vyeo vidogo au visivyo na maana maishani. Mungu anajua moyo wako na nidhamu yako ya kufanya kazi kwa uadilifu na uharaka. Atahakikisha kwamba watu watajua kukuhusu.

Katika utangulizi, nilikusimulia hadithi yangu ya jinsi nilivyogundua kanuni hii ya uharaka kama moja ya kanuni tisa ambazo nilihitaji kufahamu vyema. Kama nilivyosema kwenye utangulizi, mbali na kuchunga kanisa kubwa na kufanya huduma ya televisheni kila siku, pia nina kampuni ya kifedha inayosaidia watu kutoka kwa madeni na kusaidia watu wasiotaka kuhatarisha pesa zao za kustaafu kwa kuwapa suluhu salama za uwekezaji mahali wasipohitaji kuwa na wasiwasi juu ya kupoteza amana ya kwanza ya pesa kwa sababu ya mabadiliko ya soko.

Ili kujikumbusha kidogo, nilikuwa nimefanya kazi na muuzaji fulani kwa miaka michache. Kila mwaka huwa wana mkutano wa wawakilishi wao wa mauzo wanaohitimu kiwango fulani. Kila mwaka nilihitimu kupata safari kwa kufanya biashara ya takriban $4,000,000. Katika mkutano huo, pia walitambua wawakilishi 10 bora katika kampuni na kuwazawadia bonasi ya $100,000 na manufaa mengine mazuri yaliongezwa. Kwa miaka 14, nilizalisha takriban kiasi sawa cha biashara nao, karibu $4,000,000. Mwaka mmoja, mimi na Drenda tulifika kwenye kusanyiko tena na uzalishaji wetu wa wastani wa karibu $4,000,000. Sasa, usinielewe vibaya. Siku zote mikusanyiko yenyewe ilikuwa mizuri sana, nami nilifurahi kustahili kuwa mmoja wa wale 80 au zaidi waliokuwa hapo kati ya mamia ambao hawakuwepo.

Mwaka huo nilipokuwa nimeketi pale nikitazama wawakilishi 10

bora wakitambuliwa na kupata bonasi, ghafla, Bwana alizungumza nami na kusema, “Ninakutaka huko juu!” Nilishangazwa na alichokisema kwa muda mfupi. “Bwana, unajua kwa nini siko kule juu. Niko na shughuli nyingi za uchungaji na huduma ya televisheni kila siku. Hawa watu walio huko juu hufanya kazi hii tu siku hadi siku. Sina muda wa kufanya hivyo; tayari nimechoka.” Kisha nikamsikia akisema, “Ninakutaka wewe huko juu uwe shahidi kwa ajili Yangu.” Ilikuwa tayari majira ya kuchipua, na ili kufuzu kuwa mmoja wa wale 10 bora, ingebidi nizalishe zaidi ya $10,000,000 katika biashara.

Baada ya kujadili hili na Drenda, tulipanda mbegu kwa ajili ya uzalishaji wa $10,000,000 na kutangaza kwamba hilo limekamilika. Lakini hatukujua ni kwa jinsi gani tungeongeza mauzo yetu hadi zaidi ya $10,000,000 katika muda uliobaki mwakani maana tulikuwa tumezoea kuzalisha $4,000,000 kwa miaka 14 ya awali. Naam, ingetupasa kuamini upako na kwamba Mungu angetupa mpango.

Baada ya siku chache niliota ndoto rahisi sana. Katika ndoto, Mungu aliniambia kile nilichohitaji kufanya ili kuwa mmoja wa wale 10 bora. Ajabu ni kwamba, yalikuwa maneno mawili tu, lakini nilijua alichomaanisha nilipoyasikia. Maneno hayo yalikuwa, “Nyakua Fursa!”

**Nyakua Fursa!**

Nilipoomba kuhusu hiyo ndoto, nilielewa kile ambacho Bwana alikuwa akinionyesha. Kama unavyojua, nina shughuli nyingi, shughuli nyingi sana, lakini Bwana alinionyesha kwamba kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingi na wafanyikazi wangu pia walikuwa na shughuli nyingi, wakati mwingine hatukuwa wepesi wa kujibu simu tulizopigiwa kuhusu habari au huduma tunayoitoa kama ilivyohitajika. Hakuna aliyekuwa mvivu; kila mtu alikuwa na shughuli nyingi na wateja wengine.

Ninakatisha sura hii ili kukupa kichemsha bongo. Kulingana na kile ambacho nimesema hivi punde na kutoka kwa yale ambayo tayari

umejifunza katika kitabu hiki, utambuzi wako ni nini? Uko sahihi. Tulikuwa na ugonjwa wa kutisha unaoitwa kufika upeo wa uwezo. Na unasema unaweza kuwa hatari usiposhughulikiwa haraka? Na, daktari, dawa yako ni ipi? Unasemaje? Ninapaswa kufuata taratibu mbili kabla ya kulala nikitumia taarifa kutoka kwa usimamizi? Ninajifurahisha hapa kidogo, lakini hili si suala la kuchezewa. Ni kweli, na ndio, linaweza kuwa hatari kwa maono yako.

Ilibidi taratibu zetu zibadilike ikiwa tungebadili uzalishaji wetu kutoka $4,000,000 hadi zaidi ya $10,000,000 katika chini ya mwaka mmoja. Kwa hivyo niliita wafanyikazi wangu katika mkutano na kuwaambia kwamba nilitaka mteja yeyote au mtu yeyote ambaye alitupigia simu na kulikuwa na uwezekano angekuwa mteja ajibiwe chini ya saa moja, kwa lazima. Mimi pia nilifanya vivyo hivyo. Suala moja ambalo wakati mwingine lilifanya ufuatiliaji wa haraka sana kuwa mgumu ni kwamba tuna sheria inayosema lazima tukutane na wateja wetu ana kwa ana ikiwa wanawekeza zaidi ya $50,000. Hakuna mtu ambaye angetaka kuwekeza pesa zake bila kujibiwa maswali yake yote na mtu halisi, mtu yule yule atakayekuwa kocha wake wa pesa. Ndio, mikutano ya ana kwa ana ni nzuri, lakini tumepewa leseni katika kila jimbo, na wateja wetu wako kila mahali. Lakini sheria yetu ingali ipo. Ni lazima uwe na mkutano wa ana kwa ana na mteja yeyote ambaye anafikiria kuwekeza zaidi ya $50,000 isipokuwa mteja hayuko wazi kufanya hivyo na afadhali atumie simu au *Zoom* (Hili ni jukwaa la mtandao la mawasiliano linalowezesha watumiaji kuunganishwa na video, sauti, simu na gumzo). Lakini tulikuwa tayari kukutana na wateja wetu ana kwa ana popote nchini. Nilitambua kwamba Mungu alikuwa akisema tulihitaji kunyakua kila fursa, na haingekuwa rahisi kufanya hivyo.

Nakumbuka likizo ambayo familia yetu ilisafiri kutoka Jiji la New York hadi Roma mwaka huo, na kulingana na kanuni yangu, nilipiga

simu na kuweka miadi katikati ya Bahari ya Atlantiki. Kulikuwa na mara nyingi ambapo nilikuwa nimechoka na kufika mwisho tayari lakini mtu kutoka Pwani ya Magharibi angenipigia simu. Ili kutochelewa kwa miadi yangu ilibidi nisafiri kwenda huko kwa ndege kutoka Ohio saa tatu ya jioni nilipokuwa na miadi ya saa tatu unusu jioni. Kisha, nikiwa na macho mekundu ningeondoka pale kwa ndege usiku wa manane saa zao, na saa tisa ya usiku saa za kwetu, na kufika kwangu karibu saa moja asubuhi. Kisha ningekunywa kifungua kinywa, na kwenda kazini. Ilibidi nijifunze kulala nikiwa ndani ya ndege. Usiku mwingi, sikutaka kwenda. Tayari nilikuwa nimechoka, lakini maneno "nyakua fursa" yangenirudia akilini mwangu, na ningeondoka.

Mwishoni mwa mwaka, tulifanikiwa. Tulikuwa katika kikundi cha wale 10 bora, na tulipanda jukwa na kupokea hundi ya bonasi ya $100,000. Lakini hapa kuna ukweli wa kuvutia. Tulifikia lengo la $10,000,000 na mteja mmoja. Mteja mmoja! Ikiwa ningekataa kufuatilia mteja hata mmoja katika mwaka huo, hatungehitimu hilo. Kwa kunyakua fursa hiyo, kila eneo lingine la biashara yetu lilipanda pia.

Mwaka uliofuata, mchuuzi huyo alipandisha kiwango cha chini kinachohitajika cha uzalishaji hadi $12,000,000 ili kufuzu kupata bonasi na kuwa katika kile kikundi cha watu 10 bora. Kwa hiyo, mimi na Drenda tulipanda mbegu zetu na kumwamini Mungu kuzalisha dola hizo 12,000,000; na tulifanikiwa, tena na mteja mmoja. Mwaka uliofuata ilikuwa vivyo hivyo na kila mwaka baada ya hapo kwa miaka sita iliyofuata.

Nakumbuka tulipozalisha $12,000,000 mwaka wa kwanza. Safari tuliyozawadishwa ilikuwa kule Budapest. Ni jiji tukufu kama nini! Lakini katika safari hiyo, watu walianza kuniuliza, "Uliwezaje kufanya kile ulichofanya? Je, ulitumia kiasi gani cha pesa kufanya matangazo? Ningejibu, "Hakuna. Hatukufanya matangazo; yote yalikuwa ni

mapendekezo kupitia maneno ya mdomo." Na hawakuweza kuamini hilo. Bila shaka, kila wakati niliwaambia kuhusu hadithi yangu na jinsi Ufalme wa Mungu ulivyobadili maisha yangu. Mara nyingi kuwa kwenye jukwaa hilo kulinipa fursa ya kushiriki Injili.

Katika utangulizi, nilikuacha na swali: "Tulitokaje katika kiwango cha kuzalisha $4,000,000 hadi kiwango cha zaidi ya $10,000,000 na mchuuzi huyo mmoja?" Kwa kweli, mabadiliko tuliyofanya yalitusaidia kufanya mengi zaidi hata na wachuuzi wengine pia, na hilo lilizidisha uzalishaji wa uwekezaji wetu takriban $20,000,000 kwa jumla kwa mwaka.

Kuwa na nia na kuwa wa haraka katika kila hali kulibadilisha kabisa jinsi tulivyofanya biashara. Mabadiliko mapya katika jinsi tulivyoendesha operesheni zetu yalifanyika. Ukweli ni kwamba mabadiliko makubwa yaliyotokea ni katika mawazo yetu na usimamiaji wetu wa kila siku. Bila shaka, hakuna chochote kati ya haya ambacho kingewezekana bila kuelewa kanuni ya mkakati. Nilihitaji sana kusikia hekima na mawazo ya ubunifu kutoka kwa Roho Mtakatifu ili kufikia malengo yetu. Roho Mtakatifu ndiye aliyesema kwamba tulikuwa tukifanya kazi chini ya uwezo wetu na akatuonyesha kile tulichohitaji kubadilisha ili kuchukua maeneo mapya.

> *Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote **mkiri Yeye**, naye atayanyosha mapito yako.*
>
> — Mithali 3:5-6

Tafakari kundi kubwa katika mkutano. Mwenyekiti wa mkutano anasema, "Ningependa kumtambua yule bwana pale nyuma ambaye amevaa sweta jekundu." Anamaanisha nini? "Nakualika uzungumze. Ninauona mkono wako ulioinuliwa." Ndivyo ilivyo kuhusu Roho

Mtakatifu. Usitegemee ufahamu wako mwenyewe.

**MRUHUSU ANENE!**

Wauzaji ni wazuri na maneno, na mikutano ya mauzo hufurahisha, lakini sivyo katika kuwa na uharaka. Uharaka kamwe si jambo la kustarehesha. Daima ni jambo la makusudi. Hii ndiyo sababu niliuliza, "Je, unataka kuvua samaki au kukata chambo?" Hakika, kuna wakati ambapo chambo kinahitaji kukatwa na kutayarishwa—lakini kamwe si wakati samaki wanakiuma. Huo ndio wakati wa kuwa na uharaka. Uharaka hudai lengo na mpango wazi wa utekelezaji. Ni rahisi kuvutwa na mielekeo tofauti unapokuwa na shughuli nyingi. Hilo ndilo lililokuwa kosa letu. Tulihitaji kukaa makini badala ya kuwa na shughuli nyingi. Haya yote yalidai tuangalie taratibu zetu; na tulipofanya hivyo, tuliona kwamba uwezo wetu ulikuwa umekamilika katika maeneo mengi. Wauzaji wetu walikuwa wakifanya kazi nyingi kwa makaratasi, vipande vingi vya makaratasi vilikuwa vikibandikwa kila mahali na kwenye madawati yao. Wengi wao walikuwa wakilazimika kushughulikia upande wa usimamizi wa biashara zao, na ilitubidi kufanya mabadiliko ambayo yangewaweka huru kuwa na wateja wao.

Labda umehusika katika kazi ya kukusanya na kupakia nyasi katika majira ya joto. Nyasi zinapaswa kuwekwa ghalani ili zisinyeshewe na mvua, kwa sababu nyasi zikilowa huwa na ukungu na huharibika. Kulikuwa na nyakati nyingi ningepigiwa simu ya haraka na mjomba wangu, ambaye baada ya kupakia nyasi nyingi, alihitaji msaada wangu kuingiza nyasi ghalani kabla ya mvua kuanza. Ikiwa mvua ilikuwa inakaribia, kila mtu alihitajika kufanya kazi kwa bidii. Kila mtu aliacha alichokuwa akifanya na kupakia nyasi, na hatukukoma hadi nyasi yote ilipoingizwa ghalani.

Kwa hivyo hapa kuna swali unalohitaji kujibu. Je, unafuatilia jambo lolote kwa uharaka hivi sasa, au unakata chambo? Utajuaje?

Je, huwa unatumia muda kiasi gani kutazama televisheni, kutafuta mambo kwenye simu yako au kupoteza muda? Pili, unafuatilia vitu sahihi, vitu ambavyo vitaleta athari kubwa ndani maisha yako? Uhusiano wako na Mungu, ndoa yako, watoto wako ukoje? Na unaposhughulika katika mavuno ya kazi zako, je, unajishughulisha kwa uharaka, ukimsikiliza Roho Mtakatifu akupe hekima, na kuwa mwepesi wa kwenda mbele na kutoahirisha mambo? Je, unazingatia kanuni ya umiliki ambapo unapata taarifa kutoka kwa wasimamizi, ukizingatia kwa makini maelezo ili uweze kuchukua hatua kwa kusababisha mabadiliko na sio tu kutaka kuhusika wakati mambo yashatokea?

**JE, UNAFUATILIA JAMBO LOLOTE KWA UHARAKA HIVI SASA, AU UNAKATA CHAMBO?**

Nilikuwa na mkutano wa jioni huko Pennsylvania kwenye kituo cha televisheni cha Kikristo. Mkutano huo uliratibiwa kuisha mwendo wa saa nne jioni hiyo. Sasa, kulikuwa na nyumba iliyopakana na mali yangu ambayo ilitakikana kuuzwa na sherifu saa 10:00 asubuhi iliyofuata. Ilikuwa ni mali ambayo nilikuwa nimetazama kwa muda mrefu na maana ilikuwa imepakana na kwangu, nilitaka kuinunua. Nilifikiria ningeweza kuikodisha au kumpa mmoja wa watoto wangu ambaye angehitaji makazi ya muda mfupi wakati fulani. Niliendesha gari usiku kucha kurudi Ohio na nilifika nyumbani dakika 30 kabla ya mauzo ya sheriff kuanza. Niliweza kuinunua. Lakini haya ndiyo mawazo unayopaswa kuwa nayo; mavuno yanadai uharaka! Bila shaka, hatuishi katika hali ya dharura, lakini samaki anapouma chambo, kila mtu anahitaji kufanya kazi kwa bidii.

**HAYA NDIYO MAWAZO UNAYOPASWA KUWA NAYO; MAVUNO YANADAI UHARAKA!**

Maneno haya mawili yameniletea mamia ya maelfu ya dola katika miaka sita iliyopita.

**Nyakua Fursa!**

Maneno mawili tu rahisi, lakini nilipoyatumia, yalibadilisha ulimwengu wangu; na nina hakika yatabadilisha wako pia.

Kanuni ya uharaka.

## SURA YA 11

# KANUNI YA UMUHIMU

Kanuni ya umuhimu ni kanuni muhimu ambayo ina uwezo wa kubadilisha kabisa maisha yako. Nina furaha ya kuishiriki nawe. Ikiwa ningeupa jina mjadala wetu hapa, ningeuita:

**Kufuatilia mambo makubwa na kukosa umuhimu wake.**

Nilipokuwa katika shule ya upili, nilipenda sana uwindaji. Kwa kawaida, nilipenda kuwinda sungura na chindi. Nilianza kuwinda kulungu katika miaka ya baadaye ya shule ya upili, lakini katika miaka ya awali, mara tu baada ya kupewa bunduki nzee nilipokuwa katika shule ya sekondari, niliwinda sungura na chindi. Siku moja nilipokuwa nikiwinda kwenye msitu wa rafiki yangu, kundi la bata lilijitokeza. Walizunguka, kisha nikawaona wakiruka hadi kwenye bwawa lililopakana na mali yake. Sikuwa nimewahi kufikiria kuwinda bata hapo awali, lakini nilipoona kundi hilo likiruka kwenda humo, nilikuwa na hamu ya ghafla ya kufanya hivyo. Nilienda nyumbani na kutoa majarida yangu machache ya uwindaji na kusoma hadithi chache kuhusu uwindaji wa bata, na kufuata vidokezo tu maana sikuwa nimewahi kufanya hivyo hapo awali.

Nilijua nilipaswa kupata kibali cha kuwinda katika bwawa hilo, na ingawa rafiki yangu aliishi karibu na bwawa hilo, hakujua ni nani aliyeishi katika shamba hilo. Kulikuwa na nyumba ndogo nyeupe pale karibu na barabara, kwa hiyo jioni moja, mimi na binamu yangu tulipitia huko kuzungumza na watu tuliowaona pale. Walisema hawakuwa wamiliki

wa ardhi hiyo bali walikuwa watunzaji tu, na wakasema hawakujali ikiwa tulitaka kuwinda huko.

Kulikuwa na jambo moja ambalo hadithi zote nilizokuwa nimesoma kuhusu uwindaji wa bata zilikuwa nayo, na hiyo ilikuwa kutumia midoli ya bata. Kwa hiyo, nilienda kwenye duka la bidhaa za michezo na kununua midoli sita ya bata ya plastiki. Mpango ulikuwa wa kwenda kuwinda siku iliyofuata baada ya kutoka shuleni. Kulingana na mpango wetu, mimi na rafiki yangu tulienda kwenye bwawa ili kuweka midoli yetu karibu na bwawa na kujiandaa kuwinda jioni. Tulirusha midoli yetu hapa na pale kisha tukajificha kwenye nyasi zilizopakana na bwawa na kungoja. Baada ya saa moja au zaidi, hakuna kitu kilichotokea. Lakini karibu na kidimbwi hicho, umbali wa takriban yadi 200, kulikuwa na kijito kilichopita katikati ya eneo hilo. Nilikuwa nimeona bata kadhaa wakiruka kando ya kijito hicho siku ambayo niliona kundi la bata wakiruka huku nikiwinda chindi. Kwa kuwa hakukuwa na shughuli nyingi kwenye bwawa, mimi na rafiki yangu tuliamua kutembea hadi kwenye kijito ili kuona kama bata walikuwa wameketi hapo. Tuliacha ile midoli yetu na kuelekea kwenye kijito, ambacho kilikuwa na sehemu chache kubwa zilizokuwa wazi ambazo nilifikiri zingefaa kwa bata, lakini hakukuwa na kitu. Kwa hiyo, tuliamua kurudi kwenye bwawa ili kusubiri hadi jioni.

Tulipokuwa tukirudi kwenye bwawa, tulisisimka kuona kundi la bata wakubwa wakizunguka bwawa na kisha kutua juu yake. Hili lilikuwa jambo zuri. Kulikuwa na bwawa lenye udongo lililozunguka bwawa lenyewe ambalo lingetuficha tulipokaribia na kujiweka mahali palipofaa. Nilipokaribia bwawa na kuanza kutambaa ili kupiga risasi, niliona maji yalikuwa yamefunikwa na bata. Kwa hiyo, niliona nipige bata moja risasi walipokuwa juu ya maji kisha nipige risasi bata wa pili wakati kundi lililosalia lilikuwa likijinyanyua kutoka kwa maji.

Naam, nilipoinua bunduki yangu kupiga risasi, bata hawakuwa

wameniona. Nilikuwa karibu kufyatua risasi kumuua bata mkubwa ambaye nilikuwa nimemwona kisha nikamwona mwingine mkubwa zaidi ambaye alikuwa nje ya maji kidogo. Alikuwa mkubwa karibu mara mbili ya wale bata wengine. Kwa hiyo, niliamua kumlenga huyo na kumuua. Kundi liliposikia mlio wa bunduki, lilinyanyuka kwa kishindo cha mbawa na makelele mengi. Lakini nilichanganyikiwa, kwa sababu bata mkubwa niliyempiga risasi hakuondoka. Badala yake, aligeuka na kuanza kuzama. Ghafla, nilitambua kilichotokea. Nilikuwa nimempiga mdoli wangu mwenyewe! Niliketi pale kwa hofu huku yule mdoli akizama taratibu asionekane. Nilikasirika zaidi kwa kukosa kumpiga bata kuliko nilivyokuwa nimekasirika kuhusu kumpiga mdoli wangu mwenyewe, lakini hakika nilijiona mjinga. Rafiki yangu alikuja na kuniuliza ikiwa nilikuwa nimefaulu. Kwa aibu, ilinibidi kukiri nilichokuwa nimefanya. Kwa hivyo hapa kuna somo. Nilipiga risasi nzuri, lakini haikuwa risasi muhimu. Huwezi kula plastiki!

Kabla sijaingia kwenye mada hii, hebu tufafanue masharti yetu kwanza. Kulingana na mtandao wa definitions.net, neno *nzuri* linamaanisha **kitu kisicho cha kawaida** kinapolinganishwa na vitu vingine.

Neno *muhimu*, kulingana na kamusi ya Kimombo iitwayo *Collins Dictionary*, linamaanisha **kuwa na athari kubwa**.

Na neno *athari*, kulingana na Kamusi ya Merriam-Webster, linamaanisha: **nguvu au uwezo wa kuleta matokeo: nguvu au ushawishi.**

Unaweza kuonekana kuwa mkuu au mzuri unapolinganishwa na wengine, lakini je, una athari kubwa na unaleta matokeo? Kwa mfano, nilipiga risasi nzuri lakini haikuwa muhimu kwa sababu haikuleta matokeo niliyohitaji.

Hebu nieleze hivi. Tuseme ninataka kukarabati saa. Ikiwa ninahitaji bisibisi, nitachagua bisibisi saizi gani? Nikichagua bisibisi

yenye kichwa bapa kirefu cha futi mbili, ninaweza kuiinua na kusema, "Lo!, sasa hii ndiyo bisibisi nzuri." Lakini haitafaa katika ukarabati mzuri wa saa hiyo. Bisibisi hiyo kubwa si muhimu katika hali yangu kwa sababu haina uwezo wa kuleta matokeo au ushawishi ninaohitaji. Ninahitaji mojawapo ya vibisibisi vidogo ili kukarabati saa. Bisibisi hiyo, ingawa si kubwa ina umuhimu mkuu kwa sababu ina uwezo wa kuleta matokeo ninayohitaji.

Kwa hivyo hapa kuna maswali machache kwako kutafakari:

- **Je, una maisha mazuri au muhimu?**
- **Je, una wafanyakazi wazuri au muhimu?**
- **Je! una taaluma nzuri au muhimu?**

Usichague mdoli!!! Tafuta umuhimu. Inashangaza kwamba watoto wengi wanataka kuwa waigizaji, waimbaji, au kuwa maarufu. Lakini tusichanganye umuhimu na ukuu.

Nafikiri sote tunaweza kukubaliana kwamba Yesu alikuwa kiongozi mkuu na aliishi maisha ya umuhimu. Kwa hivyo, hebu tuangalie kwa haraka masomo machache tunayopaswa kuzingatia kutoka kwa maisha Yake.

> *Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake,* ***akaweka mikono yake juu ya kila mmoja*** *akawaponya. Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema, "Wewe u Mwana wa Mungu." Akawakemea, asiwaache kunena, kwa sababu walimjua kuwa ndiye Kristo.*
>
> *Hata kulipokucha alitoka akaenda mahali pasipokuwa na*

> *watu; makutano wakawa wakimtafuta-tafuta, wakafika Kwake, wakataka kumzuia asiondoke kwao. Akawaambia, "Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia;* ***maana kwa sababu hiyo nalitumwa****."*
>
> —Luka 4:40-43

Mambo yote yalikuwa shwari katika huduma ya Yesu. Alikuwa na mikutano **mikuu**, pepo walikuwa wakipiga kelele, na watu walikuwa wakiponywa. Hakuna chochote kingine bora kushinda hicho. Si ajabu watu hawakutaka aondoke. Lakini Yesu alijua umuhimu ni bora kuliko ukuu. Angeweza kukaa huko na kuendelea kuwa na mikutano mikuu, lakini hakutumwa kufanya hilo. Alijua kwamba hakuja kufanya kazi ya kuwawekea mikono wagonjwa wote duniani. La, alikuwa hapa kwa kazi kubwa zaidi—kulipa gharama ya kisheria kwa ajili ya dhambi ya wanadamu wote na kisha kutuma jeshi ambalo lingeweka mikono **yao** juu ya wagonjwa na kuwaponya.

Kwa hiyo, ni hatua gani katika hali hiyo ambayo ingetokeza umuhimu mkubwa zaidi kwa Yesu? Tunajua kukaa huko kungeleta matokeo mazuri, ambayo bila shaka yenyewe yangekuwa muhimu, lakini ni mpango gani ungeleta umuhimu mkubwa zaidi? Ni mpango gani ungetokeza matokeo ambayo Mungu alikuwa anayafikiria? Sawa, tuangalie hili kwa kina zaidi. Ni nini kilimpa Yesu umuhimu? Ni jambo lile lile lililoipa ile bisibisi ndogo ya saa umuhimu. Uwezo wa kuleta matokeo na kutimiza kusudi.

**Kusudi!!!**

Bila kusudi, hakuna umuhimu. Watu wanaweza kuona yaliyo dhahiri, yale yanayometameta, lakini bila kusudi na matokeo, hakuna umuhimu hata kama kuna ukuu. Kusudi hutu-angazia na kutusaidia kuchuja umuhimu wa kweli katika maisha yetu. Kusudi huelekeza maamuzi yetu. Kila mtu anapaswa kujibu maswali haya, "Kwa nini

nilitumwa? Kusudi langu ni nini?"

**BILA KUSUDI, HAKUNA UMUHIMU.**

Ninataka kukupa kile ninachokiita viashiria tisa vya umuhimu ambavyo vitakusaidia kuchuja udanganyifu wa ukuu na kukufanya uendelee kutafuta umuhimu.

**#1 Unapaswa kuweka mikono yako juu ya nini?**

Kama nilivyoonyesha katika Maandiko, yanasema kwamba Yesu binafsi aliweka mikono Yake juu ya kila mgonjwa katika mkutano huo. Sote tuna mipaka na wakati tulio nao na tunahitaji kutambua kwamba hatuwezi kuweka mikono yetu juu ya kila kitu. Hatuwezi kumiliki kila kitu, na hatuwezi kufana kila kitu. Kuna mawazo na sababu nyingi nzuri zilizopo, ambayo yote ni ya kifahari na nia nzuri. Lakini je, umeitwa kuweka mikono yako hapo? Hatuhitaji mawazo mengine mazuri. Tunahitaji kupata wazo la Mungu la maisha yetu wenyewe. Yesu hakujiruhusu kukengeushwa na utume Wake wa msingi. Alijua kwa nini alitumwa na mahali alipohitaji kuweka mikono Yake. Alielewa nguvu ya umuhimu na kwa hekima alitumia wakati Wake kuzidisha juhudi Zake kwa kujizalisha Mwenyewe tena na tena. Aliwatuma wale 12 katika Marko 6:12, wale 72 katika Luka 10, naye akalituma kanisa katika Marko 16. Sasa, kuna mamilioni ya watu wanaoweka mikono yao juu ya wengine.

**HATUHITAJI MAWAZO MENGINE MAZURI. TUNAHITAJI KUPATA WAZO LA MUNGU LA MAISHA YETU WENYEWE.**

Kwa hivyo unahitaji kujibu swali lifuatalo:

**Je, unaweka mikono yako juu ya nani au nini ambacho kitazidisha umuhimu wako?**

Mimi na Drenda tumehama mara kadhaa katika maisha yetu pamoja. Hivi karibuni, tulienda kwenye orofa yetu ya chini na tulikuwa tukiangalia masanduku fulani na tukapata masanduku kadhaa ambayo yalikuwa yamepakiwa huko Tulsa miaka 25 iliyopita na hayakuwa yamewahi kupakuliwa tangu wakati huo. Wakati huo tulikuwa maskini, na yaliyokuwa kwenye masanduku tuliyofungua yalikuwa onyesho la kusikitisha la vitu visivyofaa ambavyo tulifikiri vilikuwa vya thamani wakati huo. Ingawa vitu vingi tulivyofungua havikuwa vya maana, kulikuwa na vitu vichache ambavyo vilikuwa muhimu kama kumbukumbu. Lakini jambo la kichaa ni kwamba tumehama mara mbili tangu tuhamie hapa kutoka Tulsa. Hiyo ina maana kwamba tulihamisha masanduku hayo hayo mara mbili bila kuyafungua na kuona kile tulichokuwa tukihamisha au ikiwa tulikihitaji. Kwa hivyo masanduku hayo yalikuwa na umuhimu kiasi gani? Mdogo sana maana tuliyahamisha mara mbili bila kuchukua wakati kuyafungua!

**Umebeba nini ambacho unahitaji kuacha nyuma?**

Je, ni mara ngapi umeweka mikono yako kwenye kitu kile kile tena na tena? Ondoa taka na kusafisha maisha yako. Nina kazi hapa kwako. Jiulize yafuatayo unapozingatia kazi ya kitu fulani katika maisha yako ya baadaye.

Hii ________, ni nzuri, lakini je, inaongeza umuhimu (inanisaidia kuwa na matokeo na ushawishi kuhusiana na kusudi la kazi yangu)? Je, inatimiza kusudi langu, na JE, NINAIHITAJI?

Si vibaya kuwa na vitu vichache vizuri ambavyo havina maana yoyote ila kukufurahisha, lakini uwiano unaofaa unahitajika katika hayo yote. Labda umewahi kwenda katika nyumba ambayo ina vitu vingi, rafu hadi rafi zimejaa midoli ya wanyama iliyojazwa manyoya, midoli ya wanyama iliyotengenezwa na kaure inayong'aa, au chochote kile. Je, unahisije unapoingia katika nyumba kama hiyo? Linganisha

hilo na hisia unazopata unaposafiri wakati wa likizo kwenda kwa hoteli ya kifahari na kuingia katika chumba chako cha mapumziko. Unapoingia katika chumba hicho, kwa sababu hakina vitu vingi, ni kama unavuta hewa safi. Kinakufanya uhisi kwamba umekaribishwa na uko huru. Kuna ubunifu katika mpangilio huo. Unahisi amani moyoni kuwa hapo. Fanya ofisi na nyumba yako kuwa vivyo hivyo!

Nilikuwa na wanandoa waliokuja kanisani kwetu tulipozindua huduma yetu. Walikuwa wameoana kwa muda mfupi. Mke alilelewa kwenye shamba la kuku, na familia yake ilikuwa na taratibu zao baada ya kila mlo. Walikuwa wakiweka mabaki ya chakula kwenye bakuli ambalo waliweka kwenye dirisha ili kuwapelekea kuku. Mume wake aliniambia kwamba walikuwa katika mwezi wao wa kwanza wa ndoa, na hakuweza kuelewa ni kwa nini mke wake mpya aliendelea kuweka mabaki ya chakula cha jioni kwenye bakuli juu ya dirisha. Kwa hiyo, siku moja alimuuliza kuhusu jambo hilo. Kisha akampa maelezo ambayo nilikuambia hivi punde. Baada ya maelezo yake mumewe alimwambia, “Lakini, Mpenzi, hatuna kuku wowote!” Je, umebeba mizigo aina gani? Kila unachokimiliki kinakumiliki wewe. Kila kitu unachokimiliki kinahitaji umakini. Kinahitaji kutiwa mafuta, kuoshwa, kupakwa nta au kuhifadhiwa.

**Maono yako ni madogo sana ikiwa huwezi kuondoa yale usiyohitaji!**

**#2 Wewe ni nani? Yesu alijua alikuwa nani.**

**...NI UPEKEE WAKO UNAOKUFANYA UWE WA THAMANI KWA KUSUDI LAKO.**

Upekee wako ni upi? Watu wengi hawajui wao ni akina nani. Nilikuwa Paris miaka michache iliyopita mwishoni mwa vuli ambapo unahitaji sana kuvaa koti ukiwa nje. Mimi na

Drenda tulikuwa tukitembea kwenye barabara yenye maduka ya rejareja ya hali ya juu sana. Tulikuwa tukiangalia mitindo yote ya kisasa kwenye madirisha ya duka na tukagundua kuwa rangi nyeusi ndiyo ilikuwa rangi ya mtindo mpya. Kila kitu kilikuwa cheusi. Mtaa ulikuwa na watu wengi siku hiyo, na nilipotazama mamia ya watu waliokuwa wakitembea barabarani, nilichoona ni weusi tu. Kati ya mamia ya watu, hakuna hata mmoja aliyekuwa amevaa vazi lenye chembe ya rangi nyingine. Kila mtu alikuwa amevaa mavazi ya rangi nyeusi na kijivu. Kila mtu anataka kuwa kama mtu mwingine, lakini ni upekee wako unaokufanya uwe wa thamani kwa kusudi lako. Hakikisha umeweka hilo akilini.

**#3 Fahamu unahitaji kusikia kutoka kwa Mungu.**

*Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda Zake mahali* ***pasipokuwa na watu****, akaomba huko.*

—Marko 1:35

Yesu alijua alihitaji kutumia wakati pamoja na Mungu na kuzingatia kazi Yake. Katikati ya mafanikio makubwa, Yesu alijua kwamba alimhitaji Mungu. Ni kosa kubwa sana kuamini ushindi na mikakati ya jana. Kuna sababu nyingi, lakini hebu nikupe moja kubwa sana. Una adui ambaye anataka kuharibu maisha yako, au hata vibaya zaidi, kukuua. Hili ni jambo ambalo unapaswa kufahamu kila wakati katika safari yako.

*Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika; bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele,*

> *kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangaliijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.*
>
> —1 Wakorintho 2:6-8

Tazama Maandiko yanasema kwamba kama Shetani angejua mpango wa Mungu, angelibadilisha mipango yake. Mpango uliofanya kazi jana unaweza kukosa kufanya kazi leo kwa sababu Shetani anaweza kuwa ameujua na yuko tayari kwa ajili yake. Daima unahitaji ufunuo mpya kutoka kwa Mungu ili kupigana vita vyako.

Nilipokea barua pepe kutoka kwa mmoja wa washirika wetu kitambo kidogo. Alisema kwamba alipoanza kutumia kanuni ya Ufalme kwa mara ya kwanza katika biashara yake ya kuuza mali, alianza kupata mafanikio makubwa. Lakini baada ya takriban miezi sita, alisema alianza kukumbana na kila aina ya matatizo. Matatizo na wafanyakazi wake, matatizo ya kumaliza mikataba iliyohitaji kumalizwa, na kadhalika. Alichanganyikiwa. Nilimjibu na kusema, "Utafanya nini kuhusu hilo?" Najua lilikuwa jibu la kushangaza kwa barua pepe iliyoomba usaidizi. Lakini nilitaka atafute suluhu. Alihitaji kuelewa kwamba sasa alikuwa anakabiliwa na mkakati mpya wa adui lakini alikuwa na mamlaka ya kukabiliana nao. Sikumuacha na jibu hilo butu. Niliendelea kumweleza kwamba sasa alikuwa kwenye mpango wa adui. Mafanikio yake na ushuhuda wake kuhusu Ufalme wa Mungu ulikuwa umesambaratisha ufalme wa giza, na shetani alikuwa amebadili mbinu. Nilimtia moyo kwa Maandiko haya.

> *Baadhi ya Wayahudi wenye kutanga-tanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu, wakisema, "Nawaapisha kwa Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo." Walikuwako wana saba wa*

> *mtu mmoja Skewa, Myahudi, kuhani mkuu, waliofanya hivyo. Yule pepo mchafu akawajibu, akawaambia,* ***"Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani?"*** *Na yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda, hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa.*
>
> —Matendo 19:13-16

Nikamwambia nilifurahi jina lake lilijulikana kuzimu; inapaswa kuwa hivyo. *"Lakini wewe ni nani?"* Nilitaka kuhakikisha tena kwamba alijua kwamba alikuwa na mamlaka ya kukabiliana na mbinu za adui za kukatisha tamaa.

Silaha kuu tuliyo nayo ni ile tuliyozungumzia tayari katika sura kuhusu kanuni ya mkakati, ambayo ni Roho Mtakatifu. Hebu tuende kwenye hadithi ya Biblia inayojulikana sana, nami nitaeleza.

> *Ikawa, hapo Mfilisti alipojiinua, akaenda akamkaribia Daudi, ndipo Daudi naye akapiga mbio, akalikimbilia jeshi ili akutane na yule Mfilisti. Daudi akatia mkono wake mfukoni, akatwaa humo jiwe moja, akalitupa kwa kombeo lake, akampiga Mfilisti katika kipaji cha uso; jiwe hilo likamwingilia kipajini, akaanguka chini kifudifudi.*
>
> *Hivyo Daudi akamshinda yule Mfilisti kwa kombeo na jiwe, akampiga Mfilisti, akamwua; walakini Daudi hakuwa na upanga mkononi mwake.*
>
> —1 Samweli 17:48-50

Katika simulizi hili la Biblia linalojulikana sana, Daudi alikabiliana na Goliathi, jitu la mwanamume na shujaa aliyezoezwa tangu ujana wake. Kusema kweli, Daudi hakuwa na uwezo wa kumshinda,

au alikuwa nao? Daudi alijaribu kuvaa silaha za Mfalme Sauli, na hazikumfaa. Pia Daudi hangeweza kumshinda Goliathi kwa kutumia mbinu ambayo Goliathi alikuwa akitarajia. Badala yake, Daudi aliegemea mbinu tofauti kabisa, ambayo hakuna mtu aliyeitarajia na ambayo ilimshtua kabisa Goliathi.

> *Mfilisti akamwambia Daudi, "Je! Mimi ni mbwa hata umenijia kwa fimbo?"*
>
> —1 Samweli 17:43a

Daudi alishika fimbo yake kwa mkono mmoja na kombeo katika mkono mwingine. Nina hakika kwamba Daudi alificha kombeo lake alipomkaribia Goliathi na alikuwa akitumia fimbo yake kwa njia ya hila. Goliathi alichanganyikiwa. Kijana Daudi angewezaje kumwendea Goliathi akiwa na fimbo tu, bila upanga? Lakini Daudi alikuwa na mpango wake. Badala ya kutembea kwenda vitani, Biblia inasema kwamba Daudi alipiga mbio kukutana na Goliathi. Nina hakika hiyo ilikuwa sehemu ya mshangao ambayo Daudi alikuwa akitegemea. Kupigia mbio kukutana na Goliathi kungefanya iwe vigumu zaidi kwa Goliathi kuwa na wakati wa kutambua hatari halisi, ambayo ilikuwa kombeo. Kwa hiyo, ni silaha halisi ya Daudi ilikuwa ipi? Mkakati usio wa kawaida wa Roho Mtakatifu.

**MRUHUSU MUNGU AKUONYESHE KILE UNACHOHITAJI KUFANYA. USIFANYE PEKE YAKO; DAIMA HAKIKISHA UNATENGA MUDA WA KUMSIKILIZA.**

Hii ndiyo sababu ninakuambia kwamba unahitaji kutumia muda na Mungu. Hata katikati ya mafanikio, adui daima hujaribu kuingilia mipango ya Mungu. Hakuna hofu katika hilo, na usiruhusu adui ajaribu

kukutia hofu. Ameshindwa na hana nguvu wala mamlaka juu yako.

Mwenzangu niliyekuambia kuhusu alirekebisha mambo machache katika ofisi yake na muundo wa kampuni yake, na leo anafanikiwa kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko hapo awali. Mruhusu Mungu akuonyeshe kile unachohitaji kufanya. Usifanye peke yako; daima hakikisha unatenga muda wa kumsikiliza.

**#4 Je, uhusiano huu unaleta umuhimu kwa maisha yangu?**

Mungu huwatumia watu, na Shetani hufanya vivyo hivo. Kuwa mwangalifu katika mahusiano yako. Jifunze kusema la, na jifunze kulinda wakati wako. Usijiruhusu kuwa jibu la mtu. Daima waelekeze kwa Yesu. Sisemi kwamba hupaswi kusaidia watu, lakini unahitaji kutazama watu ambao hawataki kuwa sehemu ya suluhu wanalohitaji bali wanataka uwe jibu lao kila wakati. Adui anapenda kutumia watu kukuchosha.

Tulipokuwa wachungaji wapya, tulihisi tulihitaji kuwepo wakati wowote na popote watu walipohitaji msaada. Tulivumilia masaa mengi katika mikutano na watu binafsi. Tulichukua jukumu la uwongo la kuwalipia bili zao. Mioyo yetu ilikuwa sawa, lakini bila kujua, adui alikuwa akiwatumia watu hao kutuchosha hadi tukakata tamaa hata ya kufanya kazi ya huduma. Tulikuwa tukipigiwa simu na watu wale wale tena na tena ambazo zilimaliza nguvu zetu. Katika kutokomaa kwetu, tulifikiri kwamba tulipaswa kusuluhisha matatizo ya kila mtu. Lakini hatimaye, Bwana alituambia tukomeshe hilo—si kwamba hatukuweza kuwasaidia watu, lakini ilitubidi tuwape jukumu la kutafuta suluhu lao wenyewe.

Kasisi mmoja mwenye busara alituambia kwamba hatukuwa na deni la wakati au pesa kwa watu wetu. Lakini tulikuwa na deni la mafundisho mazuri na yanayofaa kwa maisha yao. Alitukumbusha

kwamba hatukuwepo ili kuwa marafiki wao wa karibu bali wachungaji wao. Alisema kwamba deni lao tulilokuwa nalo ni kuwa mfano, kuwafundisha kuhusu Ufalme, na kuwa na furaha kufanya hivyo. Alisema ikiwa hatukuwa na furaha, basi hakuna yeyote ambaye angetaka kumtumikia Mungu? Ilibidi tukubaliane naye, na tulifanya mabadiliko katika jinsi tulivyosimamia wakati wetu na jinsi tulivyowajibisha watu.

**#5Unafanya nini?**

Lazima ni ____________. Walijaribu kumzuia Yesu asiondoke katika mji wao, *"Akawaambia, 'Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa.'"* (Luka 4:43).

Kufanya mambo makubwa sio mbadala wa kufanya mambo muhimu. Je, unapaswa kuwa ukifanya nini leo ambacho hufanyi, au unafanya nini leo ambacho hupaswi kufanya?

**Unaweza kusema la wakati unajua ndio yako!**

**#6 Unapaswa kufanyia wapi kile unachopaswa kufanya? Eneo lako, ujuzi wako, au kazi yako ni ipi?.**

Tazama kwamba Yesu alifahamu kwamba alipaswa kwenda katika miji mingine na hiyo ndiyo sababu alitumwa. Yesu angeweza kutathmini maendeleo Yake kwa sababu alijua alikokuwa akienda.

Hebu nirudie tena. Unaweza tu kutathmini maendeleo yako wakati unajua unakoenda. Hili linaturudisha katika kanuni zetu nne za kwanza, lakini ikiwa hujui unapoenda, utajuaje ukifika huko au ikiwa utawahi kufika huko?

**#7 Ndiyo sababu nilitumwa.**

Sababu yako na mwito wako ni upi, na unapigania nini? Kupata pesa ni sababu mbovu. Mara tu utakapozipata utakoma. Hapana, lazima uwe na kusudi wazi ambalo ni kubwa kuliko pesa! Kuwa na kile unachopigania binafsi tu ndicho kitakachokuamsha asubuhi. Hakuna mtu anapaswa kuniambia mimi na Drenda tujitokeze kanisani, tuhubiri, au tumweleze mtu fulani kuhusu Ufalme. Hii sio kazi yetu. Hiki ndicho tulicho. Unapofurahia kile unachofanya, basi uko katika njia sahihi.

**#8 Unataka kumwambia nani? Na unataka kumwambia nini?**

Neno muhimu hapa ni kutaka. Unavutiwa na nani? Je, ni kazi gani au misheni gani inayokufurahisha? Umuhimu wako unapaswa kujibiwa na swali hilo. Unapotamani kufanya jambo wala si kulazimika, basi unaelekea mahali sahihi. Bila shaka, kila kazi ina mambo ambayo huenda hatuyafurahii. Lakini jambo muhimu kwa ujumla ni kwamba umevutiwa na kazi unayoifanya, na una shauku nayo. Kutekeleza kazi ya mwito wako kunatia nguvu, na kunakufanya uchangamkie maisha yako ya usoni.

**Siku zako za usoni lazima ziwe kubwa kuliko leo yako** au unaweza kukoma wakati kuna shinikizo.

**#9 Ishi kama unavyofanya wiki moja kabla ya likizo**.

Unajua jinsi unavyotengeneza ile orodha kubwa ya mambo ya kufanya kabla ya kwenda likizo? Jinsi unavyoamka mapema na kulala usiku wa manane? Unatia bidii na kuwa makini. Inashangaza kiasi cha mambo unayokamilisha wiki hiyo. Tuzo iliyo mbele, yaani likizo

yako, inakuhimiza kufanya kazi kwa kiwango kingine. Tafuta kusudi maishani linalokufanya uishi hivyo kila siku.

**#10 Usikome!**

Nafikiri hili linajieleza. Kukoma si chaguo. Ikiwa unahisi kabisa kukoma, acha kazi na uende likizo. Daima ni rahisi kuona kwa udhahiri wakati umepumzika.

Mwishowe, kumbuka uko hapa sio kuwa mzuri bali muhimu. Katika kuwa muhimu, utafanyika mzuri!

## SURA YA 12

# KANUNI YA UKARIMU

Jioni moja tulikuwa tukila chakula cha jioni pamoja kama familia katika mkahawa fulani tunaopenda mtaani mwetu. Mhudumu alikuwa mwanadada ambaye alikuwa mjamzito sana. Nilipokuwa karibu kulipa bili yetu, ghafla nilihisi kumpa bakshishi kubwa kuliko ile ambayo mimi hutoa kwa kawaida, kwa hivyo niliongeza $100. Alichukua risiti niliyokuwa nimetia saini bila kuitazama na kurudi kuelekea jikoni. Ndani ya dakika moja, alirudi huku machozi yakimtoka. Alirudi kutushukuru. Alituambia jinsi alivyokuwa katika hali ngumu ya kifedha na alikuwa akishangaa angeishije. Tulipata fursa ya kushiriki Kristo pamoja naye na kumwombea kabla ya kuondoka. Hatukufanya lolote ila kuwa wakarimu na hilo lilifungua mlango wa huduma kwa moyo wake.

> *Au waudharau wingi wa wema Wake na ustahimili Wake na uvumilivu Wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate* ***kutubu****?*
>
> —Warumi 2:4

Tafsiri ya Kimombo ya King James inasema kwamba wema wa Mungu hutufanya tutubu.

**Kuwa mkarimu ni kutenda kama Mungu atendavyo.**

> *Ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana Yeye huwaangazia jua Lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.*
>
> —Mathayo 5:45

Mungu ni mwema, na ni mkarimu! Sisi ni watoto Wake, na asili yetu mpya katika Kristo ni kuwa wakarimu pia. Kama katika hadithi niliyosimulia hapo juu, kuwa mkarimu ni kushiriki moyo wa Mungu kuhusu watu. Kama vile kunywa maji baridi wakati wa joto jingi kunavyoleta kitulizo na tumaini, ndivyo kuwa mkarimu kunavyofanya ulimwenguni palipo na majangwa ya umaskini. Athari ya ukarimu inaonekana wazi katika maagizo ya Paulo aliyoyaandikia kanisa la Korintho.

> *Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*
>
> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu; kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.*
>
> —2 Wakorintho 9:10-15

Ukarimu huwafanya watu wamsifu na kumshukuru Mungu!!! Tazama kwamba Paulo alisema kuwa mkarimu ni utumishi wako kwa Mungu. Ufafanuzi wa neno huduma ni: Kutenda kazi au jukumu kwa mkuu au kama mtumishi. Ni sehemu ya wajibu wako kwa niaba ya Mungu, hapa duniani, kushiriki moyo Wake na kuwajali watu. Matokeo ni wazi—hilo hugusa mioyo ya watu na kuwafungua ili wampokea Kristo. Nafikiri sote tunaweza kukumbuka wakati mtu fulani alikuja kutusaidia na jinsi tulivyohisi.

**Ukarimu huonyesha watu moyo wako na moyo wa Mungu juu yao!**

Ukarimu una nguvu sana. Unapita maneno na kwenda moja kwa moja hadi moyoni. Inashangaza jinsi tulivyo na uwezo wa kukumbuka pongezi au zawadi ambayo mtu fulani alitupa. Kuna nyakati ambazo Mungu hutumia watu tusiowajua kututia moyo na kutufikia.

**UKARIMU UNA NGUVU SANA. UNAPITA MANENO NA KWENDA MOJA KWA MOJA HADI MOYONI.**

Wakati mmoja kama huo ninaokumbuka vyema ni wakati ambao mimi na Drenda tulikuwa tumeenda kuwinda ndege na marafiki wengine. Mimi na Drenda tulikuwa wanandoa wapya na tulikuwa tunaishi Tulsa. Tuliendesha gari kwa masaa matano hadi Kansas, tukawa na siku nzuri sana ya kuwinda, na kupata ndege waliotutosha. Lakini tulipokuwa tukirudi Tulsa, injini ya gari ya rafiki yetu iliharibika. Tulikuwa katikati ya mahali pasipokuwa na watu kwenye barabara ya ardhi na masaa mengi kutoka nyumbani. Ikiwa umewahi kwenda Kansas, basi unajua jinsi eneo hilo lililo na ukame. Sasa giza lilikuwa limeingia, na tuliona taa moja tu kwa mbali. Tulitembea hadi nyumbani kwa mkulima huyo na kumweleza hali yetu. Nilishtuka sana aliposema, "Vema, nitawapeleka nyumbani usiku wa leo. Nitaweka gari lenu juu ya

trela yangu, kisha nitawarudisha nyumbani kwenu ili mweze kwenda kazini Jumatatu." (Drenda alikuwa aanze kufanya kazi mpya ya muda asubuhi ya Jumatatu katika mkahawa fulani, na alikatishwa tamaa sana kwamba angehitaji kuwapigia simu kusema kwamba hangeweza kuwa hapo.)

Cha kushangaza ni kwamba, mtu huyo, ambaye hatukumjua hapo awali, alitupeleka nyumbani Tulsa kwa masaa tano kisha akageuka na kuendesha gari hadi Kansas kabla ya asubuhi kufika. Aliendesha gari usiku kucha! Sitasahau kamwe tendo hilo la fadhili lisilo na ubinafsi. Hakutaka hata senti moja ya petroli. Nitamshukuru mtu huyo milele. Kila ninapomkumbuka, huwa nafikiria ukarimu wake kwa shukrani.

Watu wanapokukumbuka, watamshukuru Mungu kwa ukarimu wako.

Mojawapo ya kanuni zenye nguvu zaidi nilizojifunza inapatikana katika kifungu kifuatacho ambapo Paulo anaendelea na maagizo yake juu ya kutoa.

> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu. Kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya <u>neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu.</u> Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*
>
> —2 Wakorintho 9:12-15

Kuzidi sana kunamaanisha: ya kiasi kikubwa au shahada ya juu; kuzidi, bora, au isiyo ya kawaida: *<u>miundo ya utukufu kupita kiasi</u>*.

Ni nini kitakuwa chako kwa kiasi kikubwa? Nini kitakuwa cha ajabu na kuzidi ukuu katika maisha yako? Neema ya Mungu!!!!! Hebu tuangalie ufafanuzi wa neema.

Neema: kibali cha Mungu kisichostahiliwa.

Hii ndiyo fasili ya kawaida ya neema, lakini hebu nikupe ufafanuzi bora zaidi.

“Mafundisho ya kawaida ya Kikristo ni kwamba neema ni rehema isiyostahiliwa (neema) ambayo Mungu alitoa kwa wanadamu kwa kutuma mwanawe kufa msalabani, na hivyo kutoa wokovu wa milele.

Hata hivyo, ufafanuzi huu pekee haushughulikii matumizi yote ya neno hili katika maandiko. Kwa kielelezo, Luka 2:40 (Tasfiri ya Biblia ya *‘UNION’*), *“Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake.”* Katika mfano huu unapotumia ufafanuzi wa neema kumaanisha kibali kisichostahiliwa haileti maana kwamba Kristo asiye na dhambi angehitaji hili.

James Ryle anapendekeza “Neema ni Uwepo wa Mungu utiao nguvu za kukuwezesha kuwa yule uliyeumbwa kuwa, na kufanya yale aliyokuita kufanya.” Kwingine, Bill Gothard anapendekeza “Neema hutupatia hamu na nguvu ya Mungu inayohitajika katika kutimiza mapenzi Yake.” Fasili hizi zote mbili zinaleta maana nzuri ya neno neema katika Biblia nzima.

Kwa hiyo, tunaona kwamba kile Paulo alichozungumzia katika kifungu hiki ni neema, au kutiwa nguvu, ili kufanikiwa. Karama hii ya neema, ilisifiwa kwa sababu iliwawezesha watu kufanikiwa! Karama hii, karama ya neema, iliadhimishwa kwa sababu ilikidhi hitaji la watu. Paulo alimalizia mjadala wake (katika 2 Wakorintho hapo juu) kwa kusema, ***“Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!”***

Hii ni nguvu inayoweza kukuweka huru kutoka kwa utumwa wa kifedha—Neema ya Mungu. Nguvu hii ya neema ya Mungu,

inapatikana kwa kila mwamini. Lakini hapa kuna suala. Tunaweza kutumia muda mwingi kuzungumza kuhusu kile ambacho Paulo alisema tufanye—yaani kutoa. Lakini ikiwa hatuelewi neema, ambayo ni uwezeshaji wa kufanikiwa kwa uwezo wa Mungu, tunakosa mavuno aliyoyakusudia Mungu kwa ajili yetu. Ni kama kupanda bustani yako msituni chini ya kivuli cha mti mkubwa—hakuna mwanga wa jua, hakuna nguvu za kuleta matokeo unayotamani

Mimi na Drenda tulisoma hadithi katika Biblia ambapo nguvu za Mungu zilidhihirika na kubadili kabisa hali kuwa nzuri. Itabidi nikiri kwamba tulisikia hadithi chache sana kama hizo zikitokea katika kanisa letu tulipokuwa tukikua. Nje ya wokovu, hakuna mtu aliyewahi kuzungumza kuhusu jinsi ya kuleta neema ya Mungu katika hali fulani. Ninaelewa kwamba wokovu wetu ndilo jambo muhimu zaidi. Lakini kama nilivyotaja, nilihitaji neema hiyo hiyo kufanya kazi katika kila eneo la maisha yangu, lakini sikujua jinsi ya kusababisha hilo. Na kwa sababu ya ujinga wangu, tulikosa pesa, tulikuwa wagonjwa, na wenye huzuni. Tulijua kuhusu wokovu—suala la wokovu wetu wa milele lilikuwa limeshughulikiwa kikamilifu—lakini hatukujua au kuelewa jinsi ya kuleta mbingu maishani mwetu na kudhihirisha nguvu za Mungu.

Haya ndiyo Bwana alikuwa ananiambia siku ile aliponena nami kuhusu Ufalme: “Uko katika hali hii mbaya kwa sababu hujawahi kujifunza jinsi Ufalme Wangu unavyofanya kazi!” Kwa maneno mengine, alikuwa akisema kwamba sikujua jinsi ya kuachilia mamlaka ya Mfalme hapa duniani. Sikuwa nimewahi kujifunza jinsi ya kufanya hivyo wala kufahamu kwamba hilo lingewezekana. Sikujua hata kidogo jinsi ya kupata neema, yaani nguvu ya Mungu. Hebu nitoe hoja hii hapa: Hebu nitoe hoja hapa: Hutawahi kuwa huru hadi utakapokuwa huru kifedha.

Na kama vile mimi na Drenda tumesema kwa miaka 30, hutawahi

kugundua wewe ni nani na kutimiza kusudi la kiroho la maisha yako hadi utakaposuluhisha suala la pesa. Na hebu niseme kwa uwazi pia: UNAWEZA KUWA HURU! Ni lazima upate uhuru wa kifedha si kwa ajili yako mwenyewe na familia yako tu bali pia ili watu waweze kuona Ufalme wa Mungu ukitenda kazi maishani mwako, na, kama mti wa matunda uliosheheni matunda yaliyoiva, utavutia watu kwenye Ufalme. Watu wanatafuta majibu. Wanatafuta mpango halisi. Wanahitaji sana kuona Ufalme wala si dini.

Mwanamke mmoja alinipigia simu nimtembelee, kwa kuwa alihitaji msaada kuhusu deni lake. Mimi na mmoja wa washirika wangu tulienda kukutana naye, na niliketi pale nikiwa nimepigwa na butwaa alipokuwa akieleza hali yake. Alikuwa na kadi 32 tofauti za mikopo, zote zikiwa zimetumika hadi mwisho. Alikuwa amefaulu katika kujenga gereza lake mwenyewe, na alikuwa akiniomba ufunguo wa kutoka. Akilini mwangu, jibu lilikuwa rahisi: *Koma kutumia kadi za mikopo. Huo ungekuwa mwanzo mzuri*. Kwa hiyo, nilimwambia akatekate kadi hizo na kusisitiza kwamba aishi kulingana na mapato yake. Pia nilipendekeza aanze kutumia kadi ya benki. Papo hapo alitokwa na machozi na kutoa kauli hii ya kushtua. "Nitawezaje kununua viatu?" Je, nilisikia vyema? Hakuwa na pesa za kutosha kununua chakula, lakini alikuwa akiuliza kuhusu viatu?

Unaweza kufikiri kwamba mwanamke huyo hakuwa mtu wa kawaida. Katika idadi ya kadi za mikopo alizokuwa nazo, haikuwa kawaida. Lakini inapohusu kuwa katika jela kifedha, ni kawaida. Angalia takwimu za hivi punde nchini Marekani:

- 57% ya watu hawana $1,000 katika benki.
- 44% hawawezi kulipa bili isiyotarajiwa ya $400.

Rafiki, Waamerika ni kama vile Mungu alivyoniambia—ni

watumwa. Tafakari kuhusu kile ambacho mtumwa hufanya. Hafanyi kazi kwa manufaa yake mwenyewe. Ingawa anafanya kazi na anazalisha faida, faida hiyo hutumwa kwa wakopeshaji kila mwezi, na kuacha pesa za kutosha tu ili familia iweze kuendelea kuishi kwa mwezi mwingine. Mtumwa huishi katika nyumba asiyoimiliki (maana yake ana rehani), na anaendesha gari asilolimiliki kwenda kazini ili kulipia nyumba asiyoimiliki. Mavazi yake ya kwenda kazini aliyanunua na kadi za mikopo, ili kulipia gari na nyumba asiyoimiliki, pamoja na mkopo wa shule ambao bado analipia. Unaelewa.

> *Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.*
>
> —Mithali 22:7

Kama nilivyotaja hapo awali, zaidi ya 80% ya watu hawapendi kazi zao, na 33% wanachukia kazi zao. Kwa nini basi wanafanya kazi mahali wanapofanya kazi? Kwa sababu wao ni watumwa, na watumwa hawana chaguzi! Kwa hiyo, je, kuna njia ya kutoka katika utumwa? Ndio! Huniamini? Ngoja nikuonyeshe.

> *Maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu. Kwa kuwa mkijaribiwa kwa utumishi huo, wanamtukuza Mungu kwa ajili ya utii wenu katika kuikiri Injili ya Kristo, na kwa ajili ya ukarimu wenu mliowashirikisha wao na watu wote. Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*
>
> — 2 Wakorintho 9:12-15

Hebu tuzingatie jibu hilo—neema ya Mungu, yaani uwezeshaji wa kufanikiwa!

Tambua pia kwamba adui anataka uishi maisha ya madeni na usijifunze njia ya kuwa huru. Ndiyo maana kuna bilioni 1.1 za kadi za mikopo zinazotumika Marekani. Pia ndiyo sababu ofa za kadi za mikopo bilioni saba hadi nane hutumwa kwa watu kila mwaka. Kuna yule anayetaka uishi katika madeni, na sio benki au wauzaji tu wanaokuomba ujaribu kadi zao. Shetani anajua kama anaweza kukuweka katika madeni, kamwe hutaweza kutimiza hatima yako ya kiroho, jambo ambalo anajua linaweza kuleta matatizo katika ufalme wake.

Kwa hivyo, hebu nikukumbushe kidogo. Kitabu hiki kinahusu kuwa mkarimu, sivyo? Jibu ni ndio na la. Ndio, tutazungumza juu ya faida zote za kutoa na kuwa mkarimu baada ya muda mfupi. Lakini kutoa peke yake sio jibu. Inakupasa kuwa na maarifa ya jinsi ya kupata neema, yaani uweza wa Mungu. Kwa hivyo, hebu niseme tena: Mfumo wa kutoa peke yake, kama fomula, sio ufunguo. Ni sehemu yake, bila shaka, lakini ili kufanikiwa, wewe na mimi tunahitaji ule uwezo usio wa kawaida, wa ajabu uitwao neema.

Dustin na Kendall waligundua ninachosema. Walikuwa wanandoa wachanga ambao hawakuelewa kabisa kwamba walihitaji neema ya Mungu katika fedha zao hadi walipojikuta katika hali mbaya. Walikuwa wamepata wazo jipya la biashara na kuamua kuendelea nalo. Gharama? $150,000, na yote kupitia kwa madeni. Mwezi huo huo walipoanza biashara hiyo, walikaguliwa na shirika la ushuru na walitozwa $53,000 kulipia kodi za awali. Dustin alisema walijikuta katika deni la zaidi ya $200,000 bila njia ya kutoka, haswa kwa vile mambo tayari yalikuwa magumu kifedha kabla ya kuanzisha biashara hiyo. Hapo awali walikuwa wamekopa pesa za kulipa bili ya hospitali ya mtoto wao wa mwisho na walikuwa wakilipia hilo. Ukaguzi

uliwasukuma kupita kiwango cha fedha walizokuwa nazo, na Dustin alihangaika kutafuta suluhisho.

Baada ya kutafuta, hatimaye alipata ofa ya mkopo wa $30,000, ambao uliidhinishwa, na akapeleka wazo hilo kwa mke wake ili kusikia maoni yake. Hakujua kwamba Kendall alikuwa akisoma na kutafakari kuhusu kitabu changu, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kupumzika*, ambacho pia kinashughulikia jinsi ya kupata neema ya Mungu. Kwa hiyo Dustin alipomwendea na wazo hilo la mkopo, Kendall hakufurahia hilo, alitumaini kwamba angemgeukia Mungu badala ya madeni. Aliamua kuzungumza naye kuhusu uamuzi wao na kumtia moyo amtumaini Mungu. Kwa neema, Dustin alipokea hekima ya mke wake. Walipokuwa wakiomba, walimsikia Roho Mtakatifu akisema watoe matoleo kama mbegu. Bila shaka, wakati huo hawakuwa na kiasi cha pesa ambacho Mungu alikuwa akiwaonyesha watoe, kwa hiyo walifanya kazi kwa siku 28 zilizofuata ili kupata pesa za kutosha kupanda. Matokeo? Biashara yao ilistawi.

Katika mwaka uliofuata, waliweza kulipa deni la $175,000, na Dustin alisema alipata pesa mara 12 zaidi mwaka huo kuliko pesa zozote alizowahi kupata maisha yake yote! Kendall na Dustin walipata kujua kwamba Ufalme unafanya kazi kila wakati!

**Jibu: Neema**

Tumekuwa tukizungumza kuhusu jinsi ukarimu unavyoathiri watu kiroho, jinsi unavyofanya mioyo yao kuwa miororo na kujawa na shukrani kwako na kwa Mungu. Pia tumeweka wazi kile Paulo alichosema, kwamba uwezo huu wa kuwa mkarimu ni matokeo ya neema ya Mungu katika maisha yetu.

*Nao wenyewe, wakiomba dua kwa ajili yenu, wawaonea shauku kwa sababu ya neema ya Mungu iliyozidi sana ndani*

*yenu. Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa Chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!*

— 2 Wakorintho 9:14-15

Tulizungumzia msisitizo Paulo alioweka juu ya neno iliyozidi wakati anaeleza kuhusu neema ya kufanikisha ambayo Mungu ametupa. Tuligundua kwamba neema ni uwezeshaji wa ajabu wa kukamilisha jambo fulani. Paulo anauita uwezeshaji huu wa neema ya Mungu kipawa kisichoweza kusifiwa kama ipasavyo! Nafikiri kila mtu anaweza kukubali kwamba ikiwa Mungu, Mwenyewe atawasaidia kufanikiwa maishani, hiyo ni faida kubwa sana. Ili kukusaidia kufahamu ukubwa wa kile ambacho Mungu anataka kufanya katika maisha yako na uwezo mkubwa uliopo kwa ajili yako, hebu turudi nyuma kidogo na tusome kuanzia mstari wa sita.

*Hili ndilo ninalomaanisha: Apandaye haba atavuna haba. Apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mmoja na atoe kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa kusita au kwa mkazo, kwa maana Mungu humpenda mtoaji mkunjufu.*

*Mungu aweza kuwajaza neema yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kujawa na matendo mema. Kama ilivyoandikwa: Alitawanya, akawapa maskini. Haki yake inadumu milele.*

*Naye ampaye mbegu mpandaji, na mkate kwa chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye ataongeza mavuno ya haki. Mtatajirishwa kwa kila namna ili mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo, jambo linaloleta shukrani kwa Mungu kupitia kwetu.*

— 2 Wakorintho 9:6-11 (Tafsiri ya '*EHV*')

Sasa, hapa ndipo mambo yanasisimua sana! Tunaona neno lile lile *neema* limetumika hapa, isipokuwa katika kifungu hiki Paulo anaongeza kivumishi yote. Paulo anazungumza waziwazi kuhusu kutoa na kupokea hapa na anatoa hoja kwamba mara tu unapotoa, neema yote ya Mungu inapatikana kwako ili kuleta mavuno. Neema yote ya Mungu inamaanisha kwamba nguvu zote, hekima, kibali, na ufahamu Wake sasa vinapatikana kwako ili kunyakua mavuno kutoka kwa mbegu hiyo. Sijui kukuhusu, lakini hilo hunipa msisimko! Lakini hiyo bado haimaanishi kwamba mavuno yatatokea peke yake.

Ikiwa mkulima tajiri sana angekuambia kwamba atakukopesha vifaa vyake vyote vya kilimo, vyenye thamani ya mamilioni ya dola, ili uweze kupanda na kuvuna mazao, lakini hujui chochote kuhusu kilimo, haitakufaidi chochote. Mungu amefanya nguvu Zake zote zipatikane kwetu, lakini bado tuna sehemu ya kufanya, kama jinsi mkulima anavyojua kuna mengi zaidi katika kilimo kuliko kupanda mbegu ardhini tu. Kwa sasa, ninachotaka uelewe ni kwamba uwezo wote wa Mungu unasimama karibu sio tu kukusaidia kuvuna baada ya kupanda lakini pia hata kukusaidia kujua wakati na mahali pa kupanda. Na kwa sababu hiyo, una mustakabali usio na kikomo wa kifedha!!!!!!!!

**...UWEZO WOTE WA MUNGU UNASIMAMA KARIBU SIO TU KUKUSAIDIA KUVUNA BAADA YA KUPANDA LAKINI PIA HATA KUKUSAIDIA KUJUA WAKATI NA MAHALI PA KUPANDA. NA KWA SABABU HIYO UNA MUSTAKABALI USIO NA KIKOMO WA KIFEDHA!!!!!!!!**

Sasa, tunahitaji kwenda hatua nyingine mbele na kuzungumzia ufunuo ulio wazi katika kifungu hiki kuhusu madhumuni ya kuwa na pesa kwanza.

> *Mungu aweza kuwajaza neema yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kujawa na matendo mema.*

Tunaona jambo la kwanza alilotaja Mungu ni kuwa na riziki za kila namna. Tazama, haihusu pesa tu. Anasema katika mambo yote na siku zote! Daima nasema hivi, "Wewe shughulikia kazi ya Mungu, Naye ataishughulikia yako." Kwa hiyo, "katika mambo yote na siku zote" inamaanisha kwangu kwamba hutawahi kuwa na ukosefu, haijalishi hali ya uchumi. Mungu anaposema mahitaji yako yatatimizwa, Yeye hamaanishi kuwa na riziki ya kutosha tu.

> *Nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya.*
>
> — Kumbukumbu la Torati 28:12b-13

Mungu anapozungumza kuhusu mahitaji yako yote kutimizwa, anamaanisha kuishi huru kikamilifu kifedha bila madeni, kutekeleza kazi yako kwa shauku, na kula mema ya nchi. Pia ni kuwa na afya na amani kamili.

Pili, baada ya mahitaji yako kutimizwa, unaanza kustawi sio kuishi tu,

> *Mtatajirishwa kwa kila namna ili mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo, jambo linaloleta shukrani kwa Mungu kupitia kwetu.*

Matokeo ya mwisho ni kuivuta mioyo ya watu kwa Mungu. Hilo linaweza kumaanisha kutoa na kuwa msaada kwa watu na kwa kazi ya Mungu duniani. Mifano hii yote miwili ni ya kuisukuma mioyo ya watu Kwake. Kwa kuzingatia hilo, hebu nishughulikie dhana ya uwongo ambayo mimi huisikia mara kwa mara. Mtu fulani aliniambia kwamba hawakuhitaji pesa zaidi, kwamba alikuwa nazo tele. Kweli, hakuelewa sababu ya kuwa na pesa. Ikiwa tutazingatia tu kwamba pesa zinatupa starehe na kutupa kila kitu tunachohitaji, basi nafikiri kuna mahali ambapo msukumo wa kupata pesa zaidi unaweza kupungua. Lakini hapa kuna sehemu ambayo unahitaji kunyakua. Mungu anahitaji pesa zaidi!!!! Wacha niseme hivyo tena:

**MUNGU ANAHITAJI PESA ZAIDI!**
Bado kuna kazi nyingi ya kufanywa.

> *Mungu aweza kuwajaza neema yote, ili katika mambo yote, siku zote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kujawa na matendo mema.*

Una matendo mema ya kushughulikia. Matendo mema ni kazi unayofanya kwa niaba ya Mfalme. Hakika, una kazi maalum sana ya kufanya, kulingana na Waefeso 4.

> *Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa Chake Kristo.*
>
> — Waefeso 4:7

> *Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha*

> *watakatifu, hata <u>kazi ya huduma</u> itendeke.*
>
> — Waefeso 4:11-12a

Watu wengi huwa na lengo la kuwa huru kifedha kwa sababu wamechoshwa na mbio za panya. Wanatafuta amani. Na kwa kuwa wengi hufanya kazi wasizopenda, wanatafuta uhuru unaoletwa na kuwa na pesa. Wanatafuta uhuru wa kufanya wanachotaka kufanya badala ya kile wanachopaswa kufanya Hapa kuna kauli inayowatia wazimu watu wa dini:

> *Mtatajirishwa kwa kila namna.*
>
> — 2 Wakorintho 9:11 (Tafsiri ya '*EHV*')

Ndio, neno linasema hivyo—utatajirishwa! Sasa neno utajiri bila shaka ni la kibinafsi, na mara nyingi halieleweki vyema katika tamaduni zetu. Kwa kweli hatuwezi kusema kwamba mtu ambaye ana dola bilioni moja ana furaha zaidi kuliko mtu aliye na $100,000.

La, kuwa "tajiri" kunamaanisha vitu tofauti kwa watu tofauti. Lakini, bila shaka, kunadokeza kwamba mahitaji yetu yote yametimizwa, kwamba tunaishi bila madeni, na kufurahia mema ya nchi. Lakini kuwa tajiri sio pesa tu. Pia kunahusu kucheza na wajukuu wangu, kushikana mikono na mke wangu, na mengine mengi ya ajabu maishani. Mimi na Drenda tuna watoto watano wazuri, wote wanampenda Mungu na kwa njia moja au nyingine wanahusika katika huduma. Sote tunaishi karibu kila mmoja, na, kwa kweli kabisa, tunapenda kubarizi pamoja. Naita huo utajiri!

**LAKINI HUWEZI KUWA NA PESA NYINGI KUPITA KIASI IKIWA UKO KATIKA BIASHARA YA WATU NA MUNGU.**

Watu wa dini hufikiri kwamba kuwa na pesa nyingi ni ulafi. Lakini huwezi kuwa na pesa nyingi kupita kiasi ikiwa uko katika biashara ya watu na Mungu. Daima kuna kazi mpya na maeneo mapya ya kuchukua.

Kwa hivyo tena, Mungu anataka uwe na riziki nyingi ili kuendeleza kazi Yake ulimwenguni. Mungu anataka uwe mkarimu kwa niaba Yake, kuwasaidia watu, na kufadhili kazi Zake. Lazima uwe na pesa ikiwa unatakiwa kuwa mkarimu kila wakati. Kila wakati inaweza kuwa kila siku au mara kadhaa kwa siku. Hebu tuseme ukweli. Ili kuweza kufanya hivyo, hupaswi kuishi mwezi hadi mwezi; unapaswa kuwa na pesa zaidi ya zile zinazohitajika kulipa bili zako, nyingi zaidi! Nafikiri kila mtu atakubaliana na hilo. Lakini hebu tutambue ukweli ni upi.

Kuna hofu gani katika kutoa? Kwamba hatutakuwa na pesa za kututosha sisi wenyewe, sivyo? *Ninahitaji pesa hizo*, unaweza kufikiria, na bila shaka unazihitaji. Lakini Mungu anazihitaji pia. Kwa hiyo Mungu atapata wapi pesa anazohitaji ili kufadhili ajenda yake? Pesa hizo zitakuja kutoka kwako na mimi na waumini wenzetu, bila shaka. Watu wa Shetani hawawezi kufadhili kazi ya Mungu. Mungu hatakuomba umpatie pesa zako ili azitumie bila ahadi ya kukurudishia, marejesho ya uwekezaji wako, sivyo? Naam, inategemea unauliza nani.

Waumini wengi husema ni makosa kumwamini Mungu kuwarudishia wanapotoa. Wanaamini kumtolea Mungu na kutarajia kurudishiwa chochote kuna msingi wa ulafi na kunadhoofisha tendo safi la kumwabudu Mungu. Je, unaamini mkulima hukosea anapoamini kwamba kutoa kwake kutaleta faida kwake na familia yake? Yeye hutumia tu sheria alizopewa na Mungu? Bila shaka hapana. Yeye hutumia tu sheria alizopewa na Mungu. Mungu hufurahi anapoona tukisitawi. Alitupa sheria ya kupanda na kuvuna kwa faida yetu. Yesu alitoa mfano uliozungumzia jambo hilo. Ni mfano mmoja

maarufu wa Yesu kuhusu suala hili hili, ambao umesimuliwa katika mafundisho ya Jumapili Asubuhi tangu zamani. Lakini kwa sababu moja au nyingine waalimu huwa wanasahau kutaja sehemu muhimu kila mara. Hebu tusome kuhusu mfano wa Msamaria Mwema katika Luka 10.

> *Na tazama, mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?"*
>
> *Akamwambia, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?"*
>
> *Akajibu akasema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako."*
>
> *Akamwambia, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi."*
>
> *Naye akitaka kujidai haki, alimwuliza Yesu, "Na jirani yangu ni nani?"*
>
> *Yesu akajibu akasema, "Mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwacha karibu ya kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando.*
>
> *Lakini, Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, 'Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa.'"*
>
> *Waonaje wewe, katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?*

*Akasema, "Ni huyo aliyemwonea huruma."*

*Yesu akamwambia, "Enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo."*

— Luka 10:25-37

Nafikiri sisi sote tumesikia hadithi hii somo likiwa: Mungu angefanya nini kama angekuwa anatembea barabarani na kumwona mtu huyo? Tunajua Bwana asingemwacha afe kando ya barabara. Somo ambalo makanisa mengi katika mafundisho ya Jumapili asubuhi hufunza kuhusu hili ni kwamba tuwe majirani wema. Tutunze wengine. Kutunza wengine ni moyo wa Mungu, na naweza kusema nakubaliana asilimia mia moja na tathmini hiyo. Ili kuelewa kweli karipio la Yesu kwa mtaalamu huyu wa sheria, unahitaji kuelewa kwamba Wayahudi waliwadharau Wasamaria na kuwaona kuwa wachafu. Kwa hiyo, Wayahudi walijiona kuwa watakatifu na waadilifu zaidi machoni pa Mungu kuliko Wasamaria. Kwa hiyo hadithi ya Yesu kimsingi ilimkemea huyu mwalimu wa kanuni kwa tabia yake ya uchaji Mungu. Lakini sehemu ambayo sijawahi kusikia hata kidogo ikifundishwa katika mafundisho yoyote ya Jumapili asubuhi, ni sehemu kuhusu hadithi ya sarafu mbili za fedha.

*Akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema, "Mtunze huyu, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."*

— Luka 10:34b-35

Katika hadithi hii tunaona jinsi wanadamu wanavyopigwa na kupondwa na Shetani, mwizi. Tunaelewa mafuta na divai vinawakilisha kinabii Roho Mtakatifu na agano la damu ambalo Yesu huwapa wote

wanaokuja Kwake. Pia tunaona kwamba, baada ya kumpaka mafuta na divai, Msamaria alifanya zaidi kwa kumpeleka mtu huyo aliyejeruhiwa kwenye nyumba ya wageni ili apone. Msamaria huyo alifahamu kwamba mtu huyo alihitaji wakati ili apone, na akampeleka mahali salama, yote kwa gharama yake. Nyumba ya wageni inawakilisha kanisa la mtaa. Hapa ndipo Yesu huwaleta watu waliopigwa na kuachwa kufa katika safari hii ya maisha. Wanazaliwa mara ya pili, wanatakaswa kutoka kwa dhambi kwa agano la damu na kufanywa hai na Roho Mtakatifu, lakini bado wana madoa na maumivu ya mfumo wa laana ya dunia. Wanahitaji muda wa kupona na kujifunza njia mpya kabisa ya kuishi. Yesu anawaweka katika kanisa la mtaa na chini ya mlinzi wa nyumba ya wageni, mchungaji wa mahali hapo, ili kusimamia maendeleo yao.

Lakini cha kusikitisha ni kwamba, tunapata mtazamo huuhuu wa mwalimu wa sheria katika kanisa. Watu hawataki kutoa ili kusaidia kazi iliyo katika nyumba ya wageni. Wachungaji hutumia muda wao mwingi kuwasihi watu wasaidie kwenye kitalu au kusaidia kuongoza kikundi kidogo. Lakini inaonekana watu tayari wana shughuli za kufanya mambo yao wenyewe na wanaona ni vigumu kujitolea kusaidia. Kwa kuwa watu hawatendi kwa hiari, dini hujaribu kuwatia hatiani kwa kusema, “Una deni kwa Mungu kutunza hili au lile. Tazama yale Mungu amekufanyia.” Na ninakubali, tunapaswa kuwa na mioyo iliyo tayari na inayotoa shukrani kwa Mungu, na kuwa na hamu ya kusaidia wengine, lakini kamwe Mungu hatumii mfumo wa “kudai.”

Alisema, “Ninakuachia sarafu mbili za kulipia gharama na nitakulipa gharama YOYOTE nyingine nitakaporudi.” Sasa, anaposema, “Nitakaporudi,” hasemi juu ya wakati Yesu atakaporudi bali, wakati mfanyabiashara anaporudi kwenye nyumba ya wageni. Hili linaenda sambamba na unabii uliopo tayari. Taarifa hii ilikusudiwa

kuashiria usaidizi wa kifedha wa wakati halisi kwa mlinzi huyo wa nyumba ya wageni.

Sasa, tunaweza kusema, "Vema. Mungu atalipia gharama za nyumba ya wageni;" lakini hilo bado haliwatii moyo watu wengi, na hii ndiyo sababu. Iwapo ningekuomba ulishe watu 200 kwa niaba yangu na nikakuambia kuwa nitagharamia chakula hicho, unaweza kuwa na msisimko au usifurahie kufanya hivyo. Ndio, unaweza kufanya hivyo kwa sababu ya uaminifu wako kwangu na upendo na wajibu wako kwa Mungu, na hayo yanahitajika wakati mwingine. Lakini ikiwa ningekuomba ufanya hivyo kama mtindo wa maisha, labda hungefurahishwa sana na hilo.

Ninaamini sababu ya wachungaji wengi kuhisi kwamba wanapaswa kuwasihi watu wao wajihusishe ni kwa sababu hawajawafundisha kwamba Mungu hutoa malipo ya ukarimu wetu. Anataka ujue hii ni biashara ya familia na una haki ya kuvuna kutoka kwayo. Paulo anazungumza kuhusu hili katika barua yake kwa kanisa la Korintho.

> *Ni askari gani aendaye vitani wakati wowote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi? Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo? Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, "Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka." Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe? Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake.*
>
> — 1 Wakorintho 9:7-10

Itabidi ukubali kwamba ikiwa unafanya kazi katika biashara yako mwenyewe, ukijua kuwa una haki ya kuvuna kutoka kwa juhudi zako, ungekuwa na motisha zaidi na kujawa na shauku. Hivi ndivyo Mungu anataka uelewe: Ni biashara ya familia. Mungu hataki umtumikie kwa hofu. Ukifanya hivyo utakuwa mtu mwenye nia ya wajibu. Anataka umtumikie kutoka moyoni mwako kwa ajili Yake na furaha ya malipo.

Yesu alichagua kutumia mfano wa mtunza nyumba wa wageni katika hadithi hiyo kwa sababu muhimu sana. Tunaelewa kwamba mwenye nyumba ya wageni ni mfanyi-biashara. Ameingiza katika bei ya kila siku malipo ya wafanyikazi. Lakini juu ya gharama zote za kuendesha nyumba ya wageni, yeye huongeza faida. Hiyo ni kweli, faida. Kwa sababu hiyo, mlinzi wa nyumba ya wageni ana mtazamo tofauti sana kuhusu mtu yeyote mwenye majeraha anayeletwa kwake. Haimgharimu chochote kumtunza. Mlinzi wa nyumba ya wageni anaelewa kwamba kila usiku mtu huyo anakaa huko, atapata faida, na maana mfanyabiashara amemruhusu kuwa huru kumtunza yule aliyejeruhiwa, basi ana furaha. Naweza kuwazia tu mazungumzo ya mwenye nyumba ya wageni pamoja na mfanyabiashara msafiri anapoondoka katika safari yake: "Haya, ukiona mtu mwingine yeyote anayehitaji msaada kando ya barabara, hakikisha umemleta hapa. Nitachukua wote unaoweza kuniletea, na nikikosa mahali, nitapanua nafasi!"

Kama unavyoona katika hadithi hii, kuna mengi zaidi kuliko tu hadithi inayojulikana kuhusu kile ambacho Yesu angefanya. Yesu alikuwa anasahihisha mtazamo wa kidini ambao yule mtaalamu wa sheria alikuwa nao kumhusu Mungu na pia alikuwa akisisitiza kwamba haigharimu kuwajali watu. Hakika kuna malipo kwa kufanya hivyo.

Kila wakati mimi huhuzunika ninaposikia watu wakisema kwamba Mungu huwafanyia watu wema mambo mabaya, au

ninapoona watu wakimtumikia Mungu kwa sababu ya wajibu wao wa kidini badala ya kuwa na maisha ya furaha ambayo wangeweza kuwa nayo. Shetani amejaribu kuficha wema wa Mungu kutoka kwa watu wa Mungu ili wasimtumikie kwa hiari na mioyo yao yote. Kwa watu wengi, kanisa ni jambo lingine tu kwenye kalenda zao wala hawaelewi kwamba wao ndio kanisa, yaani nyumba ya wageni ambapo Mungu huwatuma watu kuwa wakamilifu. Cha kuhuzunisha ni kwamba hawauelewi moyo wa Mungu, kwamba yuko tayari kulipa gharama yoyote ili kuwafikia watu, na Yeye wakati wote hutupatia zaidi ya kile tunachowekeza. Kila mara.

**SHETANI AMEJARIBU KUFICHA WEMA WA MUNGU KUTOKA KWA WATU WA MUNGU ILI WASIMTUMIKIE KWA HIARI NA MIOYO YAO YOTE.**

Ninakumbuka tulizungumza kuhusu jambo hili hili pamoja na kaka ya Drenda miaka mingi iliyopita—kwamba Mungu ni mwema na ni mtuzaji, na ametupa Ufalme unaotosheleza mahitaji yetu yote. Ukweli huu kuhusu Ufalme ulikuwa jambo geni kwa Johnny na mke wake, Candi, kwa kuwa walikuwa wametoka katika kanisa la kitamaduni ambako hawakufundishwa ukweli wote. Johnny na Candi walikuwa waalimu kule Georgia.

Wakati huo huo Johnny alikuwa akifanya kazi ya muda kwa kampuni yangu ya kifedha, Forward Financial Group. Katika mwaka wake wa kwanza katika kampuni, alipata mapato zaidi kwa mwaka kuliko yale aliyoyapata alipokuwa mwalimu, kwa hivyo aliamua kuacha kufundisha na kuanza kufanya biashara ya fedha pekee.

Mwanzoni, Johnny alifanya biashara vizuri sana. Lakini baadaye katika mwaka huo, niliona kwamba shughuli yake ilianza kupungua, na nilijua kwamba hangeweza kuendelea kwa mwendo huo kwa muda mrefu. Mimi na Drenda tulikuwa tumepanga safari ya kwenda

Georgia katika msimu wa Krismasi, na ilikuwa nia yangu kabisa kuwa na wakati pamoja na Johnny ili kuona kama ningeweza kutambua baadhi ya sababu za kutozalisha pesa ambazo angehitaji ili kuweza kuendelea na biashara. Kabla ya kumpigia simu, Johnny alinipigia na kuniuliza ikiwa ningepitia kumwona ili tuzungumzie biashara. Bila shaka, nilikuwa tayari kufanya hivyo. Niliweza kuona kwamba Johnny na Candi walikuwa na hofu. Tayari walikuwa na bili za mwezi huo za thamani ya $5,000, na hawakutarajia $5,000 katika mwezi uliokuwa ukifuata.

Nilipoketi na Johnny, maneno yake ya kwanza yalikuwa, "Haifanyi kazi." Nilijua kwamba ufahamu kuhusu Ufalme ulikuwa jambo jipya kwa Johnny na Candi, na nilihisi kwamba nilihitaji kuwazoeza jinsi ya kushughulikia hilo kiroho. Kwa sababu nilifahamu kwamba Ufalme hufanya kazi kila wakati! Kwa hiyo nilitumia karibu masaa mawili pamoja nao nikiwafundisha sheria za Ufalme na jinsi ya kuachilia imani yao. Nilipokuwa nikizungumza, nilihisi hofu ikififia na imani ikianza kuongezeka.

Nilijua Johnny alikuwa tayari kuchukua hatua iliyofuata. "Johnny," nikasema, "Unahitaji kutoa matoleo kama mbegu na kumwamini Mungu kupata pesa unazohitaji." Johnny na Candi walikubali, lakini hawakuwa na pesa. Ilifanyika tu kwamba nilikuwa nimekuja na malipo ya Johnny ya $160 kutoka ofisi yetu kuu. Nilijua walihitaji pesa hizo, lakini niliwahimiza badala ya kuzitumia wazitoe kama mbegu maana sote wawili tulijua kwamba dola 160, peke yake, hazingeweza kulipa bili za $5,000 walizokuwa nazo au bili za $5,000 zilizokuwa zikija. Walikubali.

Tulipokuwa karibu kuomba na kuachilia imani yetu pamoja, nilimuuliza Johnny, "Unaamini kupokea nini unapopanda pesa hizi?" Maneno yale yalipotoka kinywani mwangu, Roho Mtakatifu aliniambia nimzuie asiniambie, na nilijua kwa nini. Johnny angesema

aliamini kupata $5,000, kwa sababu ni wazi, hapo ndipo shinikizo lilikuwa. Badala yake, Roho Mtakatifu aliniambia, “Muulize ikiwa $12,000 kwa siku 30 zitatosha.” Kwa hiyo, nilifanya hivyo tu. Nilimzuia asijibu na kumuuliza ikiwa $12,000 kwa siku 30 zitatosha. Niliona macho yake yamefunguliwa wazi nilipotamka kiasi ambacho Bwana aliniambia nimuulize. Nilijua kwamba Johnny hakuwa amewahi kupata $12,000 ndani ya siku 30 katika maisha yake yote. Alikaa pale kwa dakika moja kisha akasema, ndio, angeweza kuamini hivyo pamoja na mimi. Nilimuuliza Candi swali lile lile, naye akajibu ndio pia. Tuliunganisha mikono, tukaiweka kwenye hundi hiyo, na kuachilia imani yetu kwa dola 12,000 ndani ya siku 30.

Baada ya majuma matatu, nilipokea simu kutoka kwa Johnny. Jamani, alikuwa na furaha. Alikuwa amefanya biashara ya kutosha katika wiki hizo tatu ambayo ingemlipa sio tu $12,000 bali $17,000. Alisema sasa alikuwa amefanyika muumini wa kweli.

Kwa bahati mbaya, baada ya miezi miwili, Johnny alipokuwa akielekea nyumbani usiku mmoja katika mvua nyingi, baada ya kukutana na mteja, alikuwa na ajali ya gari. Gari liliharibika kabisa, lakini Johnny alinusurika, jambo ambalo lilikuwa muujiza wa Mungu. Hata hivyo, kutokana na ajali hiyo, Johnny hakuweza kufanya kazi kwa sababu bado alikuwa anapata nafuu. Katika kipindi hicho, nyumba yake ilikuwa karibu kuuzwa na Afisa Mkuu Mtendaji wa Utekelezaji wa Sheria wa kaunti yao. Alihitaji $10,000 ili kuokoa nyumba isiuzwe.

Hata hivyo, wakati huo Johnny na Candi walikuwa wameamua kuhamia Ohio ili kupata mafundisho zaidi kuhusu Ufalme ambayo yalikuwa yakibadili maisha yao. Kwa hiyo, waliweka nyumba yao kwenye orodha ya nyumba zilizokuwa zikiuzwa, ingawa walijua walikuwa na mwezi mmoja tu kabla ya yule Afisa Mkuu kuja kuiuza. Kadiri tarehe ilivyokuwa inakaribia, hakuna wanunuzi halisi waliokuja hadi siku chache tu kabla ya Afisa Mkuu kuiuza wakati mtu mmoja

alipitia kwao na kujitolea kununua nyumba hiyo. Lakini alikuwa na ombi. Alitaka kujua kama angempa Johnny $10,000 saa hiyo, ili asiuze nyumba hiyo kwa siku 30 hadi amalize biashara nyingine ambayo ingefadhili ununuzi huo. Johnny alishtuka. Alijua kwamba ikiwa angeitoa nyumba hiyo kutoka kwa orodha ya mauzo ya Afisa Mkuu, ilibidi awe na mnunuzi ambaye angempa pesa taslimu maana siku ya mauzo ilikuwa inakaribia. Mnunuzi huyo alitaka kumwandikia Johnny hundi ya $10,000 papo hapo kisha amalize baadaye. Hiki ndicho kiasi halisi cha pesa ambazo Johnny alihitaji. Johnny alijua ni Mungu, alichukua hundi hiyo ya $10,000, na kulipa malipo yaliyohitajika hadi wakati huo. Ajabu! Na hizo $10,000 hazikuwa sehemu ya malipo ya nyumba bali juu ya bei waliyoinukuu.

Kwa hiyo Johnny na Candi walihamia Ohio na kuishi katika nyumba ya kukodisha. Walijihusisha na Kanisa la Faith Life, na Johnny akarudi kwenye biashara ya fedha kwa nguvu mpya. Lakini sasa walikuwa na tatizo jipya. Walikuwa na gari moja tu, na Johnny alilihitaji ili kugharamia miadi mingi aliyokuwa nayo wakati wa juma alipokutana na wateja. Naam, walijua la kufanya. Walipanda mbegu kwa ajili ya gari jipya na wakaamini walilipokea walipoomba, kulingana na Marko 11:24. Kisha jambo lisilo la kawaida likatokea.

Rafiki wa utotoni wa Johnny alimpigia simu. "Johnny, niliwahi kukulipa wakati ulinipa ile baiskeli tulipokuwa katika darasa la sita?" Akauliza. "La," Johnny akasema. Kisha rafiki yake akasema, "Sawa, nitakulipa sasa. Nitakununulia gari aina ya BMW." Walipokuwa watoto, walizungumza kila mara kuhusu magari, na alijua kwamba Johnny alikuwa akitaka BMW. Rafiki huyo alikuwa mwaminifu kwa neno lake na alimtumia Johnny pesa za kujinunulia BMW. Lakini mara tu Johnny alipopata pesa hizo, alitambua kwamba kwa sababu familia yake ilikuwa ikikua, hakuhitaji gari aina ya BMW. Yeye na Candi waliamua kumnunulia Candi gari kubwa la familia na dogo la

Johnny la kuendesha biashara maana gari dogo la Candi walilokuwa nalo lilikuwa kuukuu na lilikuwa na matatizo. Hivyo ndivyo ilivyotokea. Nakumbuka usiku ambao Johnny alinipigia simu. Alikuwa amekaa ndani ya gari lake jipya aina ya SUV katika kibarabara cha nyumbani kwake kando ya gari lake lingine jipya huku akitokwa na machozi na kuniambia alikuwa ameshtuka kwa sababu hii ilikuwa mara yake ya kwanza maishani kuwa na magari mawili bila madeni. Johnny alikuwa amefanyika mtu mpya. Alijua basi kwamba Mungu anaweza kufanya lolote.

Siku moja alikuja ofisini kwangu na kusema alikuwa amechoka kukodisha nyumba, kwamba yeye na Candi walitaka mali yenye shamba na walikuwa wakitafuta. Kweli nilijua kwamba mkopo kwa Johnny haukuwa sawa kwa sababu ya ile ajali aliyokuwa nayo na nikamtia moyo akodishe kwa muda zaidi ili aweze kujenga akiba yake ya pesa, na pia kuwa na muda wa kutosha wa kuongeza alama zake za mkopo. Lakini Johnny hakuonekana kutilia maanani sana nilichosema. Kisha akaniambia kwamba alikuwa ameona shamba mbele kidogo kutoka kwangu ambalo lilikuwa linauzwa, na alikuwa anaenda kuliangalia ili kulinunua. Bila shaka, kwa kuwa nilikuwa na kampuni ya rehani wakati huo, nilijua hangeweza kumudu shamba hilo. Nilijua pia hakuwa na malipo ya kwanza yanayolipwa mtu anaponunua shamba.

Nilishtuka aliporudi ofisini mwangu baada ya juma moja akiwa na tabasamu na kusema kwamba shamba ni lake. Aliponiambia hivyo, nilijua lazima nisikie hadithi hiyo. Bila shaka, yeye na Candi walikuwa wamepanda mbegu ya kifedha katika kazi ya Mungu kama walivyofundishwa kuamini kwamba walikuwa wamepokea walipoomba. Kisha Johnny akanieleza kilichotokea. Alikwenda kwa benki yake kuhusu ununuzi huo, na meneja akatoa ripoti yake ya mkopo na kuketi naye na kumwambia, "Johnny, ulikuwa sahihi kuhusu

mkopo wako. Huna uwezo wa kununua chochote." Lakini meneja alisema jambo la kushangaza. Alisukuma faili ya mkopo pembeni na kusema, "Lakini nakupenda. Ngoja nione ninachoweza kufanya."

Ili kufipisha hadithi ndefu, benki ilifadhili 100% ya ununuzi, ikampa miezi minne hadi upangishaji aliokuwa nao wakati huo uishe, walilipia gesi ya kupikia, wakalipa ushuru wa mali hiyo uliosalia, na baada ya kila kitu wakampa Johnny hundi ya $5,000 ili kurekebisha ufa katika saruji ya ukumbi wa mbele. Niliketi pale nikiwa nimeduwaa huku Johnny akiendelea na kuendelea kuhusu Ufalme. "Ajabu!" ndicho tu ningechoweza kusema.

Baada ya mwezi mmoja, Johnny aliniambia alikuwa amepanda mbegu ya trekta aina ya Ford. Aliniambia alihitaji trekta kwenye shamba lake jipya na alikuwa amepanda mbegu maalum kwa ajili ya trekta ya dizeli aina ya Ford, yenye rangi ya samawati. Tena, kwa vile alikuwa mfanyikazi wangu, na nilijua bei ya matrekta, nilifahamu kwamba bado hakuwa na kiasi hicho cha pesa. Lakini kwa hakika, baada ya majuma machache nilipotazama kuelekea barabarani, nilimwona Johnny akiendesha trekta ya dizeli aina ya Ford ya bluu kuelekea nyumbani kwake. Nilipomuuliza aliipata wapi na kwa jinsi gani, alisema mwanamke mmoja alimfuata kanisani na kumuuliza ikiwa alijua mtu yeyote ambaye angehitaji trekta. Walikuwa wakifilisi shamba la wazazi wake, na kulikuwa na trekta waliyokuwa wakitaka kuondoa. Johnny alimwambia alikuwa na haja nayo. Alimwambia asiwe na wasiwasi juu ya kumlipa, kwamba alipe alipoweza; hakuwa na haraka. Hivyo basi alipata trekta yake.

Mafanikio yake yaliendelea. Mwezi uliofuata, mapato ya biashara yake yalikuwa dola 72,000 kwa mwezi mmoja tu. Unapomuuliza Johnny jinsi hilo lilivyotukia, yeye husema lilitukia kwa kuwa mkarimu kwa Mungu na kuelewa sheria za Ufalme.

Ningali ninakumbuka nilipoketi pamoja na Johnny na Candi

katika nyumba yao kule Georgia usiku ule tuliposhiriki nao kuhusu Ufalme. Walikuwa wamelemewa na bili ya $5,000 na msimu wa Krismasi ulikuwa unakaribia, na bili nyingine ya $5,000 ya mwezi uliofuata ilikuwa ikija wala hawakuwa na chochote. Ili kuwasaidia, ilinipasa kuwasaidia kumwona Mungu katika giza la hali zilizowakabili. Niliwaonyesha kile ambacho tumekuwa tukizungumza, 2 Wakorintho 9:10-11.

> *Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*
>
> — 2 Wakorintho 9:10-11

Paulo alisema kwamba Mungu hatakupa kile unachohitaji tu ili uwe mkarimu, lakini pia atatoa mkate unaohitaji kwa mahitaji yako mwenyewe. Mkate unarejelea kila kitu unachohitaji kibinafsi katika maisha yako. Kutokana na hilo, ataongeza uwezo wako wa kutoa hata zaidi. Hiyo ina maana kwamba utazidisha. Tena, hofu katika kutoa ni nini? Kwamba hutakuwa na pesa za kutosha kulipia mahitaji yako mwenyewe. Lakini hapa Mungu anasema anampa mpanzi mbegu na mkate kuwa chakula.

Sasa hapa kuna swali muhimu sana. Je, ulicho nacho mkononi mwako ni mbegu au ni chakula? Ni chaguo lako; mbegu yako.

Baba ya mamangu, babu yangu, alikuwa mkulima maisha yake yote. Nakumbuka nilipokuwa mvulana mdogo nilikuwa nikicheza kwenye gari lake la mbegu. Huenda hujawahi kusikia kuhusu gari la mbegu. Labda hata kwa kawaida hakuna kitu kama hicho lakini kwa babu yetu kilikuwepo. Kila mwaka wakati wa mavuno, Babu

alihifadhi mbegu za kutosha kujaza gari alilokuwa nalo ghalani. Gari hilo lilikuwa limejaa mbegu alizokuwa akihifadhi ili kupanda katika majira ya kuchipua kwa ajili ya mazao ya mwaka uliofuata. Wakati wa miezi ya majira ya baridi kali, ilimbidi Babu alitazame lile gari kubwa lililojaa maharagwe ya soya, akijua kwamba alikuwa na chaguo la kuyauza ili kulipia mahitaji au kuyahifadhi ili kuyapanda katika majira ya kuchipua ambako alijua angepata mavuno mengi. Alikuwa na chaguo, lakini alisadiki sheria za wakati wa mbegu na mavuno, na aliziamini kabisa.

Iliwabidi Johnny na Candi wakabiliane na uamuzi huu huu nilipowapa ile hundi ya $160. Bila shaka wangeitumia kulipia hitaji kubwa, lakini badala yake, walifahamu kwamba ukarimu kwa Mungu huleta mavuno makubwa zaidi mwishowe. Na walikuwa sahihi.

> *Kuna atawanyaye, lakini huongezewa zaidi; kuna azuiaye isivyo haki, lakini huelekea uhitaji.*
>
> — Mithali 11:24

Kuna mfano mwingine ambao Yesu aliwapa na ninafikiri tunapaswa kuutazama tukiwa tungali katika sura hii, Mathayo 25.

> *Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaificha fedha ya bwana wake.*
>
> *Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale,*

*akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema, "Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama, talanta nyingine tano nilizopata faida."*

*Bwana wake akamwambia, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako." Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema, "Bwana, uliweka kwangu talanta mbili; tazama, talanta nyingine mbili nilizopata faida."*

*Bwana wake akamwambia, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako." Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, "Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako."*

*Bwana wake akajibu, akamwambia, "Wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoao riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake.*

*Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."*

—Mathayo 25:14-30

Hadithi hii inajulikana. Bwana aliondoka mjini na kuwaacha watumishi wake watatu wawe wasimamizi. Alimpa mmoja mifuko mitano ya dhahabu, mwingine mifuko miwili ya dhahabu, na mwingine mfuko mmoja wa dhahabu. Wawili wa kwanza walienda

kufanya kazi mara moja na wakazidisha mifuko ya dhahabu mara mbili. Bwana aliwapongeza kwa kazi yao. Lakini nataka tutazame mtumishi wa tatu. Hebu tuangalie kwa makini kile mtumishi huyo alichomwambia bwana wake alipotoa hesabu ya kile alichofanyia dhahabu ya bwana wake.

> *Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema, "Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa, nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako."*

Sikiliza kwa makini sentensi ya kwanza: *"Bwana, nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya."* Alikuwa akisema nini? Nitakwambia kile alichosema hasa. Alisema, "Kwa nini nijihusishe? Ikiwa unavuna mahali ambapo hukupanda, basi ni nani aliyelipia mbegu na ni nani aliyeitawanya na kufanya kazi yote ya kuikuza?" Sasa, hivyo sivyo bwana huyo alikuwa akimwomba afanye alipokuwa akimpa pesa za kununua mbegu. Lakini hivyo ndivyo mtumishi alivyomwona bwana wake, kama msimamizi mgumu sana. Kimsingi, mtazamo wake ulikuwa, "Hakuna faida yoyote kwangu katika hilo, kwa hivyo sina haja nalo."

Kwa sababu ya taswira yake kuhusu bwana wake, kwamba alikuwa mgumu, kimsingi alikataa kujihusisha. Alijaribu kuficha ukweli kwamba alimdharau bwana wake kwa kusema nia yake ya kuficha pesa ni kwa sababu aliogopa kuzipoteza, na hivyo kuficha dhahabu ili kuilinda. Lakini bwana huyo alitambua uwongo wake na kusema kwamba ikiwa kweli alimjali, angeweka pesa hizo kwenye amana kwenye benki, na hapo, zingepata faida. La, mtumishi huyo hakuogopa kupoteza dhahabu; alihofia gharama ya kujihusisha.

Alikuwa na taswira potovu na mbaya kumhusu bwana wake, potovu

kwa sababu kinyume chake ndicho kilichokuwa ukweli. Yule bwana hakuwa mgumu. Wale watumishi wengine wawili walithawabishwa kwa kupandishwa vyeo na kualikwa kufurahia mali ya bwana baada ya kufanya kazi kwa mafanikio na pesa za bwana. Mtumishi huyu, kwa sababu ya taswira yake mbaya kumhusu bwana wake, alichagua kutoshiriki.

Na hivi ndivyo hasa dini inavyotufundisha—kwamba Mungu ni mgumu na hakuna faida katika kufanya kazi Naye, kwa hivyo kwa nini kujihusisha? Lakini taswira hiyo kumhusu Mungu ni potovu kabisa na si kweli. Kusema Mungu hana haki ni uovu. Mungu ni kinyume kabisa na taswira hiyo. Yeye ni mwema na ni mtuzaji.

Lakini sasa nataka kusisitiza jambo muhimu sana ambalo limetolewa katika hadithi hii. Sikiliza kwa makini kile bwana alichofanyia dhahabu aliyoichukua kutoka kwa mtumishi mwovu.

> *Basi, mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."*

Je, nilisoma hilo vyema? Bwana alichukua mfuko wa dhahabu kutoka kwa mtumishi asiyefaa na kumpa yule aliyekuwa na kumi wala si yule aliyekuwa na nne? Sina hakika kwamba kufanya hivyo ni sahihi kisiasa, lakini ndivyo alivyofanya. SIKILIZA KWA MAKINI!!!!

Mungu hutoa mawazo na kazi Zake kuu kwa watoto Wake ambao wana faida Yake akilini na wale waliojithibitisha kuwa waaminifu katika kazi ndogo kwanza. Mungu si mjinga. Yeye huweka pesa Zake mahali ambapo zitapata faida kubwa zaidi.

Tafadhali tafakari kile ambacho nimesema—"Mungu huweka

pesa Zake mahali ambapo zitapata faida kubwa zaidi!"

Sasa, bila shaka, Mungu hafanyi biashara ya pesa, bali anafanya biashara ya watu. Na tunapokuwa waaminifu kufanya kazi Naye kwa bidii, atatukuza na kutupa kibali katika mambo Yake mema. Ndio, Mungu ana wale anaopendelea inapohusu wale anaowaamini kutekeleza kazi mbalimbali. Wale ambao wamethibitika kuwa waaminifu huaminiwa na Mungu kushughulikia kazi Zake kubwa na zenye thawabu kubwa zaidi.

**MUNGU HUTOA MAWAZO NA KAZI ZAKE KUU KWA WATOTO WAKE AMBAO WANA FAIDA YAKE AKILINI NA WALE WALIOJITHIBITISHA KUWA WAAMINIFU KATIKA KAZI NDOGO KWANZA.**

Angalia mtazamo wa wale watumishi wawili waliofaulu—walienda mara moja na kutumia pesa za bwana wao! Kwa nini mara moja? Kwa sababu walijua hii ilikuwa fursa, si uzito wa utumwa. Watu wengi wa Mungu huona kumtumikia Mungu kama jambo la kuchosha, wajibu unaopaswa kutimizwa wala si ukweli kwamba ni fursa.

Mimi na Drenda tulipokuwa tukijenga jengo letu la kanisa, The Now Center, ilitubidi tufanye uamuzi. Tulikuwa na washirika 300 pekee tulipoamua kujenga jumba la kudumu na kubwa zaidi kwa ajili ya kundi letu lilokuwa likikua. Tuliazimia kuchangisha pesa nyingi kadri tuwezavyo ili kutekeleza mradi huo ambao ungegharimu $6 milioni. Hiki kilikuwa kiasi kikubwa cha pesa kwetu wakati huo. Mpango ulikuwa kujenga miundombinu ya msingi kwa takriban dola milioni 4.2 na kisha kuongeza vifaa vilivyobaki vya dola milioni 2, na kujenga kadiri tulivyopata pesa.

Hii haikuwa mara yetu ya kwanza ya kuwa wakarimu kwa miradi ya Mungu, lakini ilikuwa mara yetu ya kwanza kuhusika katika mradi

mkubwa kiasi hicho. Hata hivyo, kama wale watumishi wawili katika hadithi ambao walifahamu wema wa Mungu, mara moja tulitaka kuhusika katika kuchanga fedha, na tulitaka kutoa kwa kiwango ambacho kingehitaji imani na utiifu kwa kile tulichoamini Mungu alikuwa akituambia. Siku ambayo kanisa nzima lilitangaza kile walichokubaliana kutoa kwa mradi huo, mimi na Drenda tulisema tungetoa $200,000. Wakati huo, hatukuwa na dola 200,000, lakini tulikuwa na mbegu ya takriban dola 20,000 ambazo tungepanda kama mbegu kusudi tupate pesa zilizosalia.

Ili kuweka msingi wa jinsi Mungu alivyoleta pesa hizi, nahitaji kukuambia kwamba tumemiliki kampuni ya kifedha kwa miaka 30 iliyopita. Kampuni hiyo inafanya kazi na wachuuzi na wataalamu mbalimbali, kama nilivyokueleza hapo awali. Wachuuzi wengi wakubwa tunaofanya kazi nao wana makongamano ya kila mwaka na mikusanyiko kwa ajili ya wateja wao.

Kulikuwa na mwaka fulani ambapo mmoja wa wachuuzi wetu alitualika mimi na Drenda twende London, kule Uingereza, kuhudhuria mkusanyiko wao. Tulikaa kwenye hoteli nzuri sana katikati ya jiji la London, na ilikuwa ya kupendeza tu, kama wanavyosema huko London. Basi, hafla yao ilikuwa upande mwingine wa jiji la London, na makamu wa rais alinialika mimi na Drenda tusafiri pamoja naye kwenye teksi hadi huko, jambo ambalo tulikubali kwa furaha. Tulipokuwa njiani makamu wa rais alitushukuru kwa biashara yote tuliyowafanyia kisha akaanza kutueleza kuhusu programu mpya yenye bonasi waliyokuwa wakianzisha mwaka huo. Aliendelea kueleza kuhusu muundo wa bonasi hiyo ambapo wangelipa washirika waliopendekeza bidhaa zao.

Nilifurahi sana maana nilijua tuliwafanyia biashara ya kutosha kuweza kuhitimu kupata bonasi aliyokuwa akizungumzia. Kisha, nilipouliza maelezo zaidi, ghafla alisema kwamba kampuni yetu

haingefuzu kupata bonasi kulingana na muundo wa uhusiano wetu na kampuni yake. Sikuamini. Kwa nini alinipa maelezo hayo yote kuhusu mpango huo mzuri kisha akaniondoa kwa dakika ya mwisho? Pia sikuelewa jinsi uhusiano wangu na kampuni yake ulivyoundwa ili nishindwe kuhitimu kupata bonasi. Ingawa nilimuuliza maswali zaidi, hakunipa jibu lililoeleweka. Jambo pekee nililojua kwa uhakika ni kwamba singeweza kufuzu kupata bonasi; hilo lilikuwa wazi.

Mwaka ulipita na uzalishaji wetu ulikuwa mzuri kwa mwaka huo, kwa hivyo nilipata wazo la kumpigia simu na kuuliza tena juu ya bonasi. Hata hivyo, safari hii nilipompigia simu sikuweza kumpata, hivyo niliacha ujumbe kwa msaidizi wake kuhusu swali langu. Siku iliyofuata, msaidizi wake alinipigia simu, na kwa sauti ya ukali, akasema kwamba makamu wa rais alikuwa tayari ameniambia mwaka mmoja awali kwamba sikuhitimu, na hakuna kitu ambacho angeweza kufanya kuhusu hilo. *Naam, sawa*, nikawaza, *angalau nilijaribu*.

Sasa, nilipokuwa nikiomba kuhusu mahali pa kupata zile $180,000 zilizokuwa zimesalia, nilimsikia Roho Mtakatifu akiniambia nimpigie simu makamu wa rais na niombe hiyo bonasi tena. Nakuambia sikufurahi kusikia hilo. Baada ya majibu aliyonipa nilipomuuliza kwa miaka miwili, nilijua msimamo wake. Alikuwa ameliweka hilo wazi kabisa. Kwa hivyo, niliamua kumtumia barua pepe ili kujaribu kutathmini hisia zake. Baada ya takriban siku saba nilipokea jibu lake, ambapo alisema kwamba alikuwa ametafakari jambo hilo na kuamua kuipa kampuni yangu bonasi. Ajabu ni kwamba bonasi ilikuwa $200,000! Sasa, hii ndiyo sehemu bora zaidi. Mabadiliko hayo katika mkataba wetu yamedumu sasa kwa MIAKA 14, na tumepokea bonasi hiyo ya $200,000 kila mwaka tangu wakati huo. Wajua, Mungu ni mtuzaji! Na kuna faida katika kuwa mkarimu kwa kazi Yake.

Takriban miaka mitano ilipita, na tukaamua kwamba kama kanisa tulihitaji kutafuta pesa zaidi ili kukamilisha mambo machache

**WEWE SHUGHULIKIA MAMBO YA MUNGU, NAYE ATAYASHUGHULIKIA YAKO!**

kanisani na kununua vifaa. Tena, ilibidi mimi na Drenda tuamue ni kiasi gani tulitaka kupanda kwa miradi hiyo, na tukaamua kutoa $500,000. Lo, hizo zilikuwa pesa nyingi sana. Lakini tulihisi tungeweza kumwamini Mungu baada ya kuona alichofanya na zile $200,000. Tena, tulipanda tulichoweza, ambacho nafikiri kilikuwa dola 50,000, na tulikuwa tukimwamini Roho Mtakatifu atuonyesha mahali na jinsi ya kupata dola 450,000 zilizosalia. Nafikiri wiki sita zilipita, na nikapokea taarifa kwamba kungekuwa na mabadiliko machache ya kimkataba kuhusu jinsi kampuni yetu ingekuwa inalipwa. Baada ya kufanya hesabu ya mabadiliko hayo, tuliona kwamba katika miaka mitatu iliyokuwa ikija tungepata takriban $630,000 juu ya zile tulizokuwa tukipata. Vyema kabisa, sivyo? Naam, unajua nini? Mabadiliko hayo ya kimkataba yamedumu sasa kwa miaka 11, na tungali tunapata kiwango hicho cha fedha kila mwaka. Mungu ni Mungu wa faida. Yeye ni mwema na ni mtuzaji.

Tena, wacha niseme kwa mara nyingine. Wewe shughulikia mambo ya Mungu, naye atayashughulikia yako!

SURA YA 13

# KANUNI YA MAADHIMISHO

Inaonekana watu wengi siku hizi hawana mengi ya kusherehekea kwani inaonekana kuwa ni jambo lile lile siku baada ya siku. Na hivyo si vizuri hata kidogo, kwa sababu maisha yanapaswa kuwa sherehe ya kusherehekea wema wa Mungu kila siku. Lakini ninaelewa. Ikiwa unajitahidi kuishi maisha ya unusuru, ni vigumu kusherehekea. Lakini kusherehekea ni sehemu ya jibu lako, ufunguo wa kutoka kwa jela yako. Hebu nianze mazungumzo yetu kwa kukuuliza swali.

**Unaadhimisha nini?**

Maadhimisho yanapaswa kuwa sehemu ya kila kitu unachofanya na kupanga kufanya.

Hebu turejee kwenye mjadala tuliokuwa nao hapo awali ambapo nilikuwa nikikuambia kuhusu safari na bonasi ambazo wachuuzi katika kampuni yangu ya kifedha walitoa. Safari walizotoa zilikuwa za kustaajabisha sana huku kukiwa na malazi ya kifahari yaliyolipiwa gharama zote katika baadhi ya maeneo ya kigeni na maridadi zaidi duniani. Unajua kwamba safari hizo ziligharimu kampuni mamia ya maelfu ya dola kutoa, hivyo kwa nini wao hufanya hivyo? Kweli, bila shaka wana bidhaa zao wanazotaka kutangaza kwa umma, lakini wanaweza tu kufanya bidhaa zipatikane kupitia kwa tovuti ya mtandaoni au matangazo ya runinga. Lakini kwa uzoefu wao, waligundua kuwa watu wanahitaji kusaidiwa kuelewa jinsi bidhaa zao zinavyofanya kazi na ni kwa manufaa ya kampuni kutoa maelezo hayo.

Katika utafiti wao, waligundua kuwa mazungumzo na mtu halisi yalithibitika kuwa njia bora zaidi ya kuwasilisha habari hii kwa watumiaji. Kwa hivyo, kampuni hizi huajiri wauzaji kufanya hivyo. Lakini kuna mamia ya bidhaa za kifedha zilizopo, kwa hivyo kampuni za kifedha zitawahimizaje mawakala wa mauzo kutoa bidhaa zao maalum? Kuna njia nyingi za kufanya hivyo.

Kuwa na bidhaa shindani zaidi au bidhaa ambayo hufanya kazi bora zaidi katika kukidhi mahitaji ya watumiaji kuliko ile ya mshindani hakika ni njia mojawapo ya kufanya hivyo. Kulipa mawakala wa mauzo kamisheni kubwa kuliko ile ya washindani pia ni njia nzuri ya kuhamasisha watu kuuza bidhaa. Lakini ushindani ni mkali kati ya makampuni, na kuna makampuni mengi makubwa yenye bidhaa bora, yote ambayo ni mazuri kwa mteja. Kwa hivyo utawahimizaje mawakala wa mauzo kuchagua bidhaa ya kampuni yako ili kuwauzia wateja wao? Hapa ndipo safari za kutia motisha hutumika.

Wawakilishi wa mauzo ambao wanauza bidhaa hizi za kifedha kwa kawaida hawafungwi na mkataba wa mauzo, kumaanisha kwamba wauzaji hawa wako huru kuchagua kampuni na bidhaa yoyote wanayotaka wanapotoa bidhaa kwa wateja wao.

Kwa hivyo, hebu tuseme kwamba kuna bidhaa kadhaa bora ambazo zina ubora sawa na faida kwa mteja wako kwa takriban bei sawa. Tuseme kwamba kampuni nyingi hazina mpango wa safari ya kutia motisha lakini kampuni moja hufanya hivyo. Na tuseme kwamba kampuni moja ambayo ina programu ya kutia motisha inatoa safari ya kwenda Bora Bora kwa wawakilishi wao wa mauzo wanaozalisha kiasi fulani cha pesa kila mwaka. Ikiwa kila kitu kingine ni sawa, thamani sawa na bei sawa kwa mteja, ni kampuni gani utakayomchagulia mteja wako? Nafikiri si vigumu kupata jibu hilo. Kwa hivyo, ingawa kampuni zingine zina bidhaa nzuri, kwa gharama sawa na ile ambayo umechagua, hawatapata biashara yako. Kwa nini?

Hebu tuchambue jinsi kampuni hii yenye programu ya motisha ilivyopata biashara. Kampuni hii inaelewa asili ya binadamu. Wanaweka lengo na pia kuweka tuzo. Tafadhali andika hili.

**Weka lengo, na weka tuzo.**

Sasa hebu tubadilishe neno tuzo na neno sherehe. Kwa nini? Kwa sababu neno sherehe lina taswira ya kusisimua na ya kina zaidi kuhusu kile ninajaribu kukueleza.

**Weka lengo, na weka sherehe.**

Ni ukweli kwamba wawakilishi wengi wa mauzo hujisukuma kupita kasi chao cha kawaida ili kufikia lengo linalowafaa kupata tuzo. Nimekuwa nikiuza bima maisha yangu yote na kila wakati ninapenda kufikia kiwango cha uzalishaji kitakachonipa fursa ya kwenda katika mojawapo ya safari hizi nzuri au kupokea bonasi. Nilipokuwa nikifanya kazi mwaka mzima, kila mara nilikuwa nikiwaza kuwa katika eneo la safari ya mwaka huo. Niliwaza jinsi ingekuwa vizuri kwenda huko. Lengo hilo lingenisukuma kupita kasi yangu ya kawaida ya starehe hadi katika kiwango kipya cha shughuli. Hatimaye nilipowasili kwenye mkusanyiko wa kampuni na kuheshimiwa kupokea safari hiyo na hundi ya bonasi, hiyo ilikuwa hisia nzuri sana. Sio tu kwamba nilikuwa nimehitimu kupata safari, lakini pia kuridhika sana kwa kile nilichoweza kutimiza katika mwaka huo wa biashara.

Kampuni iliyotoa safari ya kutia motisha ilikuwa bora. Hawakungoja hadi nilipohitimu kupata safari kabla ya kunieleza kuihusu. "Habari, ulifanya kazi nzuri mwaka huu. Tutakuzawadia kwa safari ya kwenda Bora Bora." La, sivyo. Walikuambia miezi mitatu au minne kabla ya mwaka wa kufuzu kuanza, pamoja na maelezo ya jinsi ya kufuzu. Kwa nini? Ili uweze kurekebisha mikakati na michakato yako, ikiwa inabidi, ili kukuwezesha kufikia lengo hilo.

Nilikuambia hadithi yangu kuhusu jinsi Mungu alivyonielekeza katika nyanja ya mauzo baada ya chuo kikuu na jinsi ilivyokuwa

vigumu kwangu. Nilikuwa mwenye haya. Kulazimika kupiga simu na kuzungumza na watu ili kupata riziki kulikuwa nje ya eneo langu la faraja. Ingawa nilichukia kupiga simu, nilipenda biashara ya kifedha. Nilipenda kujifunza yote kuhusu bidhaa za kifedha, uchumi, na kuwa sehemu ya kampeni ya kusaidia watu. Lakini ilikuwa vigumu; nilitaka kuiacha kila siku. Najua unafikiri, *Vema, ikiwa uliichukia, basi ulijihusishaje nayo?*

Nilipokuwa katika chuo kikuu na baada ya kumaliza masomo, nilikuwa nikifanya kazi katika duka la rejareja ambalo liliuza vifuniko vya madirisha, kama vile mapazia na neti ndogo, na aina mbalimbali ya vifuniko vya sakafu. Nilikuwa msakinishi wa madirisha katika kazi hiyo. Siku moja nilipokuwa nikitayarisha oda ya usakinishi, wakala wa bima ya mwenye nyumba alikuja kuzungumza naye kuhusu mambo fulani ya bima. Sikuweza kujizuia kusikia mazungumzo hayo, na cha ajabu, nilivutiwa.

Muda mfupi baada ya hapo, mwanamume ambaye sikumjua alinipigia simu na kusema kwamba alikuwa akitafuta kuajiri wawakilishi wa kampuni mpya ya kifedha. Alipewa jina langu na mtu ambaye alijua kwamba nilikuwa ninatafuta kazi mpya. Aliniambia kwamba alikuwa na mkutano kwenye anwani fulani na fulani katika tarehe fulani, na ikiwa ningetaka kujua zaidi, niende huko. Kweli, nilipendezwa na hilo, kwa hiyo nilihudhuria mkutano huo. Nilichojifunza kwenye mkutano huo kilikuwa cha kupendeza, na jambo lililochochewa ndani yangu lilisema, *Ndio, nataka kufanya hivi.* Lakini kumbuka, niliitwa na Mungu kuhubiri Neno Lake. Vipi kuhusu hilo?

Naam, wakati hayo yalikuwa yakitokea, ulikuwa muda mfupi tu baada ya kumwambia Drenda kwamba nilitaka kumuoa; na tulikuwa tumefunga safari ya kwenda hadi Georgia, nyumbani kwao. Tayari nilikuwa nimekutana na familia yake—maana walikuja Tulsa mara

moja—lakini hii ingekuwa mara yangu ya kwanza kwenda Georgia, na nilitaka kumwomba babake Drenda mkono wake katika ndoa.

Nikiwa huko, ningetembelea kanisa lake la mtaani pamoja naye. Nitakubali nilichanganyikiwa kidogo nifanye nini kuhusu ofa hii ya kufanya kazi katika biashara hii ya fedha. Kulikuwa na kitu ndani yangu ambacho kilitaka kuifanya ingawa ilionekana kama kazi nisingelipenda kufanya. Baada ya ibada ya Jumapili asubuhi, mwanamke ambaye sikumfahamu, lakini Drenda alimfahamu, alinijia na kusema alikuwa na neno kutoka kwa Mungu kunihusu. Alisema, "Unatafakari kuhusu ofa ya kazi fulani. Bwana alinionyesha mambo kumi kuhusu kazi hiyo," na akataja kila kitu ambacho ningefanya katika kazi hiyo mpya. Alisema, "Unapaswa kuchukua kazi hiyo, na Bwana yu ndani yake.

Kwa hivyo, nilichukua kazi hiyo na kuanza kuhudhuria mafundisho. Lilikuwa jambo la kichaa sana. Nilikuwa na hamu kubwa ya kujifunza jinsi ya kufanya kazi na wateja, lakini wakati huo huo, nilikuwa na woga wa kuzungumza na watu. Ilikuwa vita kweli kwangu kuingia katika nyanja hii. Lakini neno hilo la kinabii nililopokea katika kanisa hilo lilinithibitishia kwamba Mungu alikuwa katika jambo hilo, na nilijua huo ndio mwelekeo niliopaswa kufuata, ingawa haukuwa na maana akilini mwangu.

Kwa hiyo mimi na Drenda tulifunga ndoa, na tulitegemea malipo ya kamisheni pekee. Lo, hilo lilikuwa pambano kubwa. Katika mwaka huo wa kwanza, kampuni niliyokuwa nikiiuzia bima ilikuwa na safari ya kutia motisha katika Hoteli ya Boca Raton huko Florida. Mkusanyiko wao haukuvutia umakini wangu hata kidogo. Sikuwa nimewahi kusafiri au kwenda likizoni hapo awali. Na maana nilikuwa mpya katika biashara, nilifikiri haingewezekana kwangu kufuzu hata kidogo. Mafunzo yangu ya kusema la kabla ya kusema ndio yalitupilia mbali jambo hilo kama kitu kisichowezekana. Mbali na hilo, nilikuwa

na shida na shinikizo la kutosha katika kujitahidi kupata pesa za kutosha kulipa bili.

Lakini Drenda alikuwa na mtazamo tofauti kabisa wa maisha. Alipokuwa shuleni alikuwa rais wa darasa lao la wanafunzi 500 miaka yote minne ya shule ya upili. Alikuwa na wastani wa alama nne na alikuwa mhitimu katika kidato chake cha mwisho. Pia alikuwa mhariri wa kila mwaka wa jarida la shule yao la kila mwaka. Wakati huo tulikuwa tofauti kabisa lilipokuja suala la bidii na shauku.

Drenda alipoona video hiyo ikitangaza safari hiyo, alisisimka na kusema, "Tunaenda!" Sikukubaliana maana kiwango cha uzalishaji kilichohitajika kilikuwa cha juu sana. Lakini hakutaka kutulia. Alinifanya nitazame video ya matangazo ya kampuni hiyo kila siku, na aliweka brosha kuhusu safari hiyo kwenye dawati langu pia. Mwanzoni, video hiyo haikunivutia. Lakini ni shauku yake ambayo hatimaye ilinifanya nifikirie juu yake. Kwa hivyo nilifanya hesabu ya kiasi cha biashara tulichopaswa kufanya katika kipindi kilichobaki cha shindano ili kufuzu, na bado nilifikiria haingewezekana, lakini singejua ikiwa tungefua dafu au la.

Miezi miwili ilipokuwa imebaki, bado hatukuwa na kiasi cha biashara kilichohitajika, lakini cha kushangaza ni kwamba, hatukuwa na upungufu mwingi jinsi nilivyofikiria ingekuwa. Tulipokuwa tukijadili hali hiyo, Drenda aliniambia alitaka kupata leseni yake ili kunisaidia. Kufikia wakati alipopita mtihani wake wa leseni, mwezi wa mwisho wa kipindi cha shindano. Alitembelea familia kadhaa tulizozijua na kuwauzia baadhi yao, na pamoja na kile nilichokuwa nikifanya kilitusaidia kuwa karibu zaidi.

Ilifika usiku wa mwisho wa shindano, na tulikuwa na upungufu wa wateja wawili. Nilikuwa na mpango wa kukutana na mteja usiku huo, na yeye pia. Tulikuwa tukutane katika ofisi ya Federal Express kutayarisha taarifa yetu kwa usiku mmoja kwani ilibidi ifike katika

ofisi yao kuu siku iliyofuata ili kuhesabiwa katika shindano hilo. Ofisi ya Federal Express huwa inafungwa saa tano usiku, na nilifika hapo dakika chache kabla ya saa ya kufunga nikitumaini kwamba Drenda tayari alikuwa amefika, lakini hakuwepo. Sasa, hii ilikuwa kabla ya simu za rununu, kwa hivyo sikuwa na njia ya kupiga simu ili kujua mahali alikuwa. Nilijua kwamba miadi yake ilikuwa saa moja jioni, na alipaswa kuwa ameimaliza muda mrefu kabla ya wakati huo.

Ilipokaribia wakati wa kufunga, nilihangaika, si tu kuhusu taarifa yetu bali pia kumhusu. Wakala kwenye dawati alisema iliwabidi kufunga saa tano usiku ili kufikisha vifurushi vyao vyote kwenye uwanja wa ndege kwa wakati uliofaa. Dakika mbili kabla ya tano ya usiku, Drenda alikuja akipiga mbio kwenye maegesho ya gari na kuingia ndani kabla ya milango kufungwa. Tulijaza fomu zote kwa haraka na kumpa wakala na tukafurahi sana kiasi kwamba tulienda kwenye mgahawa usiku wa manane na kila mmoja akanywa soda. Kwa nini soda mbili tu? Kwa sababu hizo tu ndizo pesa tulizokuwa nazo. Lakini TULIFAULU! Tulihitimu kwenda katika safari hiyo ambayo gharama zote zilikuwa zimelipiwa, na kupata mapumziko hayo ya ajabu. Hiyo ndiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza kati ya mara nyingi ya kwenda mapumzikoni au kuketi mezani kula chakula cha jioni kwenye meza iliyokuwa na vitambaa vyeupe.

Maisha yangu yalibadilika kihalisi, na maono yangu kwa maisha yetu hayakuwa jinsi yalivyokuwa awali tena kwa sababu ya safari hiyo.

**KWA HIVYO KUMBUKA, WEKA LENGO, NA WEKA MAADHIMISHO.**

Ndio maana nikasema nabadilisha neno tuzo kuwa sherehe katika maelezo yangu hapo juu.

Hakika ilikuwa sherehe tofauti na kitu chochote nilichowahi kuona hapo awali. Lakini tuliwezaje kuhitimu hilo? Bila shaka, Mungu alikuwa akifanya kazi nasi, lakini tuzo—sherehe iliyoahidiwa, ndiyo

iliyotuchochea kusukuma na kufanya zaidi ya kile ambacho yeyote kati yetu alikuwa amewahi kufanya hapo awali.

Lo, ninatamani tu kwamba ungehisi furaha ya sherehe ambayo nilikuwa nayo wiki hiyo. Na unajua nini? Naamini unaweza! Kwa hivyo kumbuka, weka lengo, na weka sherehe.

Walakini, hivi sivyo jinsi kampuni nyingi zinavyofanya kazi. Wanatoa bonasi kulingana na miaka ya huduma. Je, hiyo inatoa motisha gani? Unataka kusherehekea kwamba mfanyakazi wako amedumu kwa muda fulani? Je, hiyo ndiyo sababu ulimwajiri, ili kujaza wakati? Au ulimwajiri kufanya mambo? Kumbuka, unahitaji kusherehekea lengo wazi ambalo litathibitisha kwa nini ulimwajiri mtu huyo. Je, kujaza wakati kutalipa bili? Nina hakika tayari umegundua kwamba hilo hufanya kinyume.

Kampuni zingine hutoa nyongeza kulingana na jinsi mfanyakazi anavyofanya kazi mwaka mzima, jambo ambalo linasikika kuwa nzuri. Kosa lao ni kutoweka tuzo inayotegemea wanaohitimu kupimika na pia kutokuwa na sherehe iliyofafanuliwa wazi ikiwa watafikia kiwango kinachohitajika kwa muda uliowekwa. Bila shaka, hili linapaswa kushirikishwa kwa mfanyakazi kabla ya muda halisi kuanza, si mwishoni au katikati.

Kisha huwa naona kampuni zingine zikitoa nyongeza za moja kwa moja kulingana na uchumi wa nchi ya Amerika. Hiyo ni sawa katika kudumisha au kutunza wafanyakazi wako lakini si kwa madhumuni ya motisha. Huwezi kamwe kuhamasisha mfanyakazi kwa kumpa njia ya kulipa bili zake tu. Weka malengo ya timu zako, kisha ufuatilie kwa sherehe nzuri.

Katika siku za mwanzo za kanisa letu, nafikiri tulikuwa na washirika 500, tuliwaambia wafanyakazi wetu kwamba mara tu tukifika washirika 1,600 kwa wikendi, tungewachukua wote hadi Hawaii. Tuliweka lengo hilo mbele yao, na ndivyo tulivyofanya.

Tulipofika washirika 1,600, tulipeleka wafanyakazi wetu wote kule Hawaii kwa juma moja. Ilikuwa safari ya ajabu.

Lakini ninapotazama nyuma, ningejiwekea angalau malengo na sherehe ndogo. Pengo kutoka 500 hadi 1,600 lilikuwa pengo kubwa sana kushughulikia katika kipindi cha wakati nilichotarajia, na wengi walikata tamaa ya kufuzu. Kuna usanii wa kuweka malengo—kwa njia inayohamasisha vya kutosha lakini sio mbali sana kiasi cha kufanya timu yako ifikiri hilo haliwezekani. Kumbuka, malengo madogo huongezeka hadi kufikia ushindi mkubwa.

**...MALENGO MADOGO HUONGEZEKA HADI KUFIKIA USHINDI MKUBWA.**

Nilipoanza kufanya biashara ya mauzo, ofisi yetu ilikuwa na kibao kikubwa ambacho kilikuwa na wawakilishi wote wa mauzo na uzalishaji wao wa kila wiki. Mikutano yetu ya mauzo daima ilikuwa ya kutia moyo, na tulikuwa tukitoa fulana ili kutambua viongozi kila mwezi. Huwezi kuamini jinsi wawakilishi hao walivyopigania fulana hizo! Nilijifunza kwamba kutambuliwa kulikuwa na maana zaidi kuliko pesa kwa wengi wao.

Niligundua kwamba watu wanataka kushindana; wanataka kushinda. Wanataka njia iliyo wazi ya kufanya hivyo. LAZIMA KUWE NA TUZO! Watu lazima wajue kwamba ikiwa watapambana, kutakuwa na tuzo, sherehe iko karibu.

Ingawa ninaelewa ni kwa nini kampuni nyingi hutumia mfumo wa mishahara kulipa wafanyikazi wao, ninapendekeza kwa dhati kwamba utathmini upya jinsi mpango wako wa malipo unavyofanya kazi. Mungu alituumba ili tuunde vitu, na alitupa mawazo. Tunafanya kazi vyema tunapojua kwamba tuna nyakati za usoni zisizo na vizuizi. Kwa kuwashirikisha watu wako katika kufanyia kazi malengo, unaingia katika mawazo na ubunifu wao. Utagundua kuwa majibu ambayo umekuwa ukitafuta kwa muda wote yapo kwa watu wako,

lakini lazima uchochee pampu ili yajitokeze. Je, mtu anayelipwa mshahara ana motisha gani ya kuwa na matokeo zaidi? Je, unafaa kuwa mpango wa motisha unaosababisha hofu? Kwamba usipozalisha unaweza kuondolewa kesho? Au inapaswa kuwa, “Ukifanya hivi, sisi tutakutuza na hili?”

Mishahara yenyewe haihamasishi. Litafakari jambo hili; mfanyakazi wako anajua atalipwa malipo yake ya kawaida iwe amehusika au la. Hatimaye, anajiuliza kwa nini aendelee kujisukuma sana; haibadilishi mshahara wake. Iwe anapunguza kasi au anafanya haraka, hakuna tofauti. Mfumo huu hautafanya kazi! Kwa hiyo, mwajiri anafikiri, *Sawa, nitaongeza malipo ya mtu huyu. Hii itampa motisha ya kufanya kazi kwa bidii na kuchukua kazi zaidi*. Si jambo sahihi. Bado hutumii mfumo unaotia motisha. Mara watu wanapokuwa na cheo fulani, wao huamua kasi yao katika ngazi ya usimamizi, kwa kusimamia kazi zao kwa mawazo ya kufuata taratibu fulani. Mtazamo wa kufuata taratibu fulani husababisha mawazo ya kufanya kile wanachoambiwa, kile wanacholazimika kufanya.

**HUTAKI WATU WAKO WAWE NA MTAZAMO WA KUFUATA TARATIBU FULANI TU!**

Unataka watu wafanye kazi kwa mawazo ya mjasiriamali. Hakuna mjasiriamali mwenye ndoto ya kuanzisha biashara ili tu kupata kazi. La, yeye huanza biashara yake ili awe na mustakabali usio na vizuizi. Anatumia wakati katika kuanzisha biashara yake kwa sababu anahamasishwa na tuzo ya uhuru na ustawi. Pili, mtu anayeanzisha biashara yake mwenyewe hatafuti maisha rahisi. Najua, mimi kama mjasiriamali, hufanya kazi kwa masaa mengi zaidi kuliko mshahara wowote ambao mtu yeyote angeweza kunilipa. Kwa nini? Kwa sababu nina maono na shauku ya kile ninachofanya. Mustakabali wangu sio kujaza wakati wangu; bali kazi ninayoifanya ndiyo ninataka kufanya.

Hivi ndivyo nilivyo, na ninapenda kuwa hivyo.

Waajiri ninaowajua husema jinsi ilivyo vigumu kupata watu wanaomiliki vyeo vyao kama wamiliki. Wanasema kwamba kila mtu anaonekana kuwa na tabia ya mwajiriwa. Nakubali, na wana tabia hiyo kwa sababu wanalipwa kama waajiriwa. Sizungumzii kiasi cha pesa wanazolipwa. Nimesema jinsi wanavyolipwa. Kwa kawaida huwa wanalipwa mshahara bila umiliki au faida inayotoka kwa kile wanachojenga. Hilo linakatisha tamaa kama nini?

Hapa kuna sehemu ya kusikitisha: Kwa sababu hawapati kushiriki katika faida ya kile wanachojenga pamoja na wewe, wote wako nyuma ya pazia, nyuma ya mgongo wako, wakipanga kutoroka ili kuwa huru. Ubunifu wanaotamani kutumia unatumiwa baada ya masaa kufikiria jinsi ya kujenga biashara zao wenyewe, sio zako. Hatimaye, wataondoka. Jambo la kusikitisha ni kwamba waliondoka kiakili muda mrefu kabla ya kuacha kazi yako. Kwa hiyo, ikiwa unataka kujenga kitu ambacho kitadumu, lazima uwaruhusu watu wako kushiriki katika furaha na sherehe ya kujenga kitu. Kitu ambacho kinawanufaisha na kuwathawabisha kwa kazi na maono yao. Usipofanya hivyo, unafundisha washindani wako tu. Kwa hiyo, tukumbuke tulichosema hapo mwanzo.

Weka lengo, na weka sherehe, yaani tuzo.

Jambo la mwisho: Huwezi kujaza hewa kwa puto iliyo na mashimo, haijalishi bidii utakayoitumia kufanya hivyo. Acha nikuonyeshe mojawapo ya Maandiko ninayopenda zaidi, kisha nitaeleza ninachomaanisha.

> *Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina Lake takatifu. Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili Zake zote. Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote,*

*aukomboa uhai wako na kaburi, akutia taji ya fadhili na rehema, aushibisha mema uzee wako, ujana wako ukarejezwa kama tai.*

—Zaburi 103:1-5

Angalia inasema unaposhibishwa na mema, hilo linarejesha ujana wako! Si wewe tu katika timu yako ambaye ana matamanio. Kuanzisha mfumo wa fidia unaowatuza wafanyakazi wako kwa kile wanachofanya—badala ya kuandika majina yao kwenye lahajedwali ya shirika—kutatia nguvu timu yako na maisha yako ya baadaye. Si vibaya kumlipa mtu mshahara ilimradi utumie mfumo unaolipa bonasi, au kugawa faida, au mfumo wa malipo unaowatuza watu kwa sababu ya kile walichofanya kwa hiari, sio kile walichopaswa kufanya. Mfumo wako lazima uwe na lengo la kina na muundo wa malipo unaowasilishwa kwa wale wanaohusika. Kuwa na nyakati za sherehe kutaongeza nguvu zako na zao! Yanakufanya wewe na timu yako kutaka kutimiza malengo yenu tena. Yanaonyesha kwamba tuzo inastahili gharama iliyotumika. Kazi bila tuzo, hata hivyo, ni kinyume chake, kama ilivyo wazi katika mataifa ambayo yamejaribu ujamaa.

Angalia Venezuela, taifa ambalo wakati mmoja lilikuwa taifa tajiri zaidi katika Amerika ya Kusini. Cha ajabu ni kwamba Venezuela inajulikana kote ulimwenguni kama taifa lenye akiba kubwa zaidi ya mafuta, kuliko Saudi Arabia, lakini kimsingi ni taifa lililofilisika. Acha ninukuu sehemu ya makala niliyosoma hivi majuzi ambayo inaonyesha wazi kile kinachotokea unapoondoa tuzo yote ya kazi ngumu kutoka kwa nchi.

*Wakati Hugo Chavez alipochaguliwa kuwa Rais, moja ya hatua zake za kwanza ilikuwa kuanza kutaifisha sekta ya kilimo, eti kupunguza umaskini na ukosefu wa usawa kwa*

*kuchukua kutoka kwa wamiliki wa ardhi matajiri kuwapa wafanyakazi maskini. Kuanzia 1999 hadi 2016, serikali yake iliiba zaidi ya hekta milioni 6 za ardhi kutoka kwa wamiliki wake halali.*

*Utaifishaji uliharibu uzalishaji katika sekta zilizoathiriwa kwa sababu hakuna serikali iliyo na uwezo wa kuendesha maelfu ya biashara au kuwa na nia ya faida kwa kuziendesha kwa ufanisi. Badala yake, maafisa wa serikali wanakabiliwa na motisha ya kuwafurahisha wapiga kura kwa kuuza bidhaa kwa bei ya chini na kuajiri wafanyikazi zaidi kuliko inavyohitajika, hata wakati huo ni uamuzi mbaya kitasnia.*

*Kama nadharia ya kiuchumi ilivyotabiriwa, udhibiti wa serikali wa tasnia ya kilimo ulipoongezeka, uzalishaji wa chakula wa Venezuela ulipungua kwa 75% katika miongo miwili huku idadi ya watu nchini ikiongezeka kwa 33%. Hii ilisababisha uhaba na maafa ya kiuchumi. Baada ya kilimo, serikali ilitaifisha sekta za umeme, maji, mafuta, benki, maduka makubwa, ujenzi, na sekta nyinginezo muhimu. Na katika sekta zote hizi, serikali iliongeza malipo ya mishahara na kutoa bidhaa kwa gharama ya chini, na kusababisha kukatika kwa umeme kwa siku nyingi nchini kote, kukatizwa mara kwa mara kwa huduma ya maji, kushuka kwa uzalishaji wa mafuta, na biashara za serikali kufilisika.*

Kazi bila tuzo haichochei uzalishaji. Mungu anajua hili. Hivi ndivyo alivyotuumba—si kufanya kazi bali pia kufurahia matunda ya kazi yetu. Hata Yesu alielewa kanuni ya kuweka lengo na kisha kuweka sherehe.

> *Wapeni watu vitu nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa, na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika; ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*
>
> —Luka 6:38

Tazama muda unaotumiwa kueleza matokeo ya kutoa. Mungu angesema virahisi, “Mimi ni Mungu. TOA!” La, hilo halingefanya kazi. Wanadamu wangemchukia Mungu, maana Yeye hangekuwa tofauti na serikali za kijamaa tunazoziona duniani. Mungu angekuwa msimamizi mgumu.

Paulo alielewa kanuni hii hii.

> *Hili ndilo ninalomaanisha: Apandaye haba atavuna haba. Apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mmoja na atoe kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa kusita au kwa mkazo, kwa maana Mungu humpenda mtoaji mwenye moyo mkunjufu.*
>
> *Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili katika mambo yote, sikuzote, mkiwa na riziki za kila namna, mpate kufurika katika kila tendo jema. Kama ilivyoandikwa: “Alitawanya; akawapa maskini. Haki Yake hudumu milele.”*
>
> *Naye ampaye mbegu mpandaji, na mkate kwa chakula, atawapa na kuzizidisha mbegu zenu za kupanda, naye ataongeza mavuno ya haki yenu. Mtatajirishwa kwa kila namna ili mpate kuwa wakarimu kwa kila jambo, jambo litakaloleta shukrani kwa Mungu kupitia sisi.*
>
> — 2 Wakorintho 9:6-11 (Tafsiri ya ‘*EHV*’)

Tena, tunaona kwamba masuala kuhusu lengo, tuzo au sherehe

yamewekwa wazi hapa. Tena, tunaona muda mwingi na maelezo zaidi yametumiwa kuzungumzia tuzo na sherehe kuliko maagizo ya kutoa. Ikiwa huo ndio mfumo ambao Mungu hutumia kwetu, nafikiri ni vyema zaidi kutumia mfumo huo huo kwa wale wote walio chini yetu katika jambo lolote tunalofanya.

Tena, kwanza weka lengo, na pili, weka sherehe—thawabu itakuwa nini lengo linapotimizwa katika wakati uliowekwa kama ilivyoagizwa. Waachie ubunifu wa jinsi ya kukamilisha kazi. Usijiruhusu kudhibiti michakato yao. Watakushangaza wewe na wao wenyewe.

Nilisema nitakuambia ninachomaanisha ninapozungumzia kujaribu kujaza hewa kwa puto lililo na mashimo. Haiwezekani. Nilisema haiwezekani, sivyo? Cha kusikitisha ni kwamba, hivi ndivyo viongozi wengi hufanya kazi. Badala ya kukarabati mashimo, wanafikiri wakijaribu zaidi kidogo, na kuwekeza pesa zaidi, kila kitu kitakuwa sawa. Lakini, bila shaka, wanagundua kwamba si kweli. Kwa hivyo koma na urekebishe mfumo. Kuajiri watu wapya au kuwekeza pesa zaidi kwenye puto hakutarekebisha kitu. Watu na pesa zitapotea tu kwa sababu ya shida zile zile zilizosababisha wale wa mwisho kuondoka. Unaweza kufanya marekebisho; Mungu atakusaidia.

Kanuni ya maadhimisho—kila mtu anapenda sherehe!

# HITIMISHO

Natumai umefurahia kitabu hiki, lakini muhimu zaidi, natumai kulikuwa na mambo machache ambayo yamezungumza nawe, yamekutia moyo, na kukusaidia kuongeza kasi katika maisha yako na kazi yako. Kama nilivyosema mwanzoni mwa kitabu hiki, kuna kanuni nyingine nyingi za kuongeza kasi ambazo zinaweza kuandikwa. Lakini haya ndiyo niliyoyaona katika ndoto yangu, yale ambayo Roho Mtakatifu aliniambia nifunze watu na kutekeleza ili kufikia malengo ambayo Bwana ameweka katika maisha yangu.

Kwa kumalizia, kuna kanuni mbili ambazo nataka kutaja ambazo ni za juu kuliko kanuni yoyote ambayo huenda nimeitaja katika kitabu hiki. Nazo ni:

> *Akamwambia, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii."*
>
> —Mathayo 22:37-40

# KIAMBATISHO KUHUSU IMANI

**Imani ni nini?**

Imani ni neno ambalo Wakristo hutumia kiholela. Na nina hakika kwamba wengi hawajui imani kwa kweli ni nini, kwa nini inahitajika, jinsi ya kujua kama wako katika imani, na jinsi ya kupata imani. Ikiwa imani ndiyo iliyomponya yule mwanamke katika Mathayo 9:20-22, kama Yesu alivyosema, basi tunahitaji kuchunguza neno hili kwa makini sana! Tunapata ufafanuzi wetu wa imani katika Warumi 4:18-21. Lo, najua unachofikiria, *La, Gary. Ufafanuzi wetu wa neno imani unapatikana katika Waebrania 11:1.*

*Imani ni kuwa na hakika juu ya yale tunayotumainia, kusadiki juu ya mambo tusiyoyaona.*
—Waebrania 11:1 (Tafsiri ya '*EHV*')

Ndio, hilo ndilo jibu tunalolijua, lakini ukiangalia Maandiko, Waebrania 11:1 inatuambia faida za imani, si imani hasa ni nini. Ninaamini Maandiko haya katika Warumi yatatupa picha wazi ya imani ni nini hasa.

*Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa,*

> *"Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu; huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*
>
> —Warumi 4:18-21

Hebu tuelewe mpangilio wa hadithi hii. Ibrahimu na Sara hawangeweza kupata watoto. Simaanishi walikuwa na shida kupata mtoto na walipaswa kuendelea kujaribu. Namaanisha walikuwa karibu miaka 100, na kamwe haingewezekana. Miili yao haingeweza kupata watoto; haingewezekana kabisa! Lakini Mungu alimwahidi Ibrahimu mtoto ingawa katika hali ya asili haingewezekana kabisa. Biblia inasema kwamba Ibrahimu alikuwa amesadiki kikamilifu kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyosema licha ya mambo ya asili yaliyodhihirisha ukweli tofauti.

***"IMANI NI KUWA NA HAKIKA JUU YA YALE TUNAYOTUMAINIA, KUSADIKI JUU YA MAMBO TUSIYOYAONA."***
**— WAEBRANIA 11:1 (TAFSIRI YA 'EHV')**

Huu hapa ndio ufafanuzi wetu wa neno imani: "kuwa na hakika kabisa kwamba Mungu ana uwezo wa kufanya yale ambayo ameahidi." Ninaliweka hivi: **"Moyo wako unapokubaliana na mbingu."** Si kukubaliana tu kiakili na kile anachosema Mungu bali kusadiki kikamilifu.

**Ufafanuzi wetu wa maana ya imani:**

Hebu nirudie mara moja tena ili kuwa na uhakika kwamba

umeelewa jambo hili. Imani ni kusadiki kikamilifu kile anachosema Mungu! Ni wakati mioyo na akili zetu zinakubaliana na mbingu, wakati ambapo mioyo yetu imeshawishika kikamilifu, ina ujasiri, na kuwa katika pumziko.

**Kwa nini imani inahitajika?**

Mbona Mungu huwa hamponyi kila mtu hospitalini anapotaka? Kwa nini huwa hakomeshi vita? Kwa nini huwa hatumi malaika kutuhubiria Injili? Nina hakika umesikia maswali haya yote hapo awali. Jibu ni kwamba hawezi kufanya hivyo. Si kwamba Mungu hana uwezo wa kufanya hivyo, lakini hana mamlaka ya kufanya hivyo. "Gary, unasema kwamba Mungu hawezi kufanya chochote anachotaka?" Najua hili linasikika geni kwako sasa hivi, lakini hebu tuangalie Biblia ili kupata jibu letu kwa hilo.

> *Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema: "Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake."*
>
> *Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*
>
> —Luka 4:5-7

Tunaweza kuona kutokana na Maandiko haya kwamba Mungu alimpa mwanadamu mamlaka kamili ya kisheria juu ya ulimwengu wote alipowekwa hapa. Hakuna kitu ambacho

hakikuwa chini ya mamlaka yake. Alitawala juu ya eneo hili kwa mamlaka kamili. Uwezo wake wa kutawala kwa mamlaka uliungwa mkono na serikali iliyomweka hapa. Kimsingi, alitawala akiwa na mamlaka aliyokabidhiwa na Ufalme wa Mungu. Alivaa taji ya serikali hiyo, ambayo iliwakilisha utukufu wa Mungu, upako, na cheo cha heshima au mamlaka aliyokuwa nayo.

Ili kupata picha nzuri ya jambo hili, tafakari kuhusu mfalme wa asili. Ingawa yeye ni mtu wa asili na hana nguvu halisi katika utu wake wa asili, yeye huvaa taji, ambayo inaashiria kwamba hajiwakilishi mwenyewe tu bali ufalme mzima na serikali. Maneno yake yanabeba mamlaka kwa sababu yanaungwa mkono na nguvu na maliasili zote za serikali na ufalme anaowakilisha.

Ukifikiria polisi anayeelekeza magari barabarani, yeye husimamisha lori kubwa na mamlaka yanayosema, "Simama kwa jina la sheria." Ndio, lori hilo ni kubwa zaidi kumliko—naye mwenyewe, hawezi kulinganishwa na lori—lakini lori hilo husimama, si kwa sababu ya mtu mwenyewe bali kwa sababu ya beji aliyo nayo, ambayo inawakilisha serikali. Katika hali hii, serikali ni kubwa zaidi kuliko mtu mwenyewe. Dereva wa lori huwa hamhofu mtu mwenyewe, lakini anaihofu serikali ambayo mtu huyo anawakilisha, na hilo humfanya dereva wa lori kusimama.

Vile vile ni kweli hapa. Adamu alitawala kila kitu kilichoumbwa katika ulimwengu. Nguvu na enzi ya Mungu, iliyowakilishwa na taji ya utukufu na heshima, ilimpa mwanadamu uhakikisho kwamba maneno yake yalitawala kwa niaba ya Ufalme wa Mungu.

Ni muhimu sana kutambua kwamba Adamu alipopoteza uwezo wake wa kutawala juu ya dunia kwa kufanya uhaini dhidi ya serikali ya Mungu, alipoteza taji yake. Dunia ulichafuka na kubadilika. Kifo kiliingia katika ulimwengu, kisha Shetani akawa

na dai la kisheria la mamlaka na ushawishi katika mambo ya wanadamu. Ni muhimu uelewe kwamba bado mwanadamu ndiye mtawala halali wa dunia, maana Mungu ndiye aliyempa cheo hicho, lakini sasa hana mamlaka ya kutawala kiroho kama ilivyokuwa hapo awali. Hata katika hali yake ya dhambi, bado ndiye msimamizi. Ndio, hana taji yake ya serikali ya Mungu ya kumtegemeza. Hana mamlaka ya kutawala kwa nguvu na utukufu wa Mungu, na amepoteza cheo chake cha heshima. Lakini bado yeye ndiye mlango pekee wa kisheria wa kuingia ulimwenguni. Hii ndiyo sababu inambidi Mungu kutumia watu waliojazwa na Roho ili kutimiza mapenzi Yake katika maisha ya wanadamu.

**HII NDIYO SABABU INAMBIDI MUNGU KUTUMIA WATU WALIOJAZWA NA ROHO ILI KUTIMIZA MAPENZI YAKE KATIKA MAISHA YA WANADAMU.**

Vivyo hivyo, Shetani hutumia watu waliovuviwa na roho waovu kuathiri ulimwengu kutekeleza mpango wake kwa mwanadamu. Kanuni hii ya mamlaka ya mwanadamu juu ya dunia ni muhimu kwa uelewaji wako wa sheria ya Ufalme, na mara tu utakapoielewa, itajibu maswali mengi unayoweza kuwa nayo wakati ujao kuhusu kwa nini mambo fulani hutokea au kutotokea kiroho.

Unaweza kusema, "Lakini nilifikiri Mungu ndiye anayemiliki dunia na yote yaliyomo?" Ni kweli, ndivyo ilivyo. Natumai mfano huu utakusaidia kuelewa ninachosema. Nikikodisha nyumba ninayoimiliki kwako, ingawa ninaimiliki kihalali, huwa sina haki kisheria ya kuja wakati wowote ninapotaka. Kuna kifungu katika ukodishaji wa nyumba kinachobainisha wakati wenye nyumba wanaweza kuingia kihalali katika majengo yao—kwa mfano, kushughulikia jambo la dharura au kufanya matengenezo—

na kiasi cha notisi kinachohitajika. Nikijaribu kuingia katika jengo langu nje ya mkataba huu, itakuwa ni kama nimevunja na kuingia, hata kama mimi ni mmiliki. Iwapo nitakiuka sheria kama ilivyobainishwa katika ukodishaji, basi ninaweza kulazimishwa kisheria kuondoka katika jengo hilo ingawa mimi ndiye mmiliki. Hiyo inaonyesha kwa nini ilimbidi Shetani kupitia kwa Adamu ili kuupata ulimwengu. Adamu pekee ndiye aliyekuwa na ufunguo! Ilimbidi Shetani apitie mlangoni na ilibidi awe amepewa ufunguo kutoka kwa yule aliyeumiliki kihalali au angelazimika kutoka kisheria.

> *Akampandisha [Yesu] juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, "Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako."*
>
> — Luka 4: 5-7

Unaweza kuona katika mstari huu kwamba Shetani anadai kwamba mamlaka na fahari (mali) ya falme za wanadamu amepewa yeye. Anadai mamlaka kamili juu ya dunia inapohusu wanadamu. Kwa hivyo ni nani aliyempa mamlaka haya? Ni yule aliyekuwa nayo, ambaye ni Adamu! Hivyo Mungu hawezi kuingilia mambo ya wanadamu bila mlango wa kisheria, au itakuwa ni kinyume cha sheria. Shetani atadai kutofanyiwa haki. La, Mungu hana budi kupitia mlango uleule ambao Shetani alitumia, ili kuleta serikali na mamlaka Yake duniani kupitia kwa mtu aliye duniani. Lakini kulikuwa na mtu kama huyo?

> *Bwana akamwambia Abramu, "Toka wewe katika*

*nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; Nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."*

— Mwanzo 12:1-3

Ibrahimu anaitwa baba wa imani yetu kwa sababu yeye ndiye mtu aliyemfungulia Mungu mlango wa ulimwengu ambao kupitia kwake mataifa yote duniani yangebarikiwa. Bila shaka, mstari huu unapozungumza juu ya mataifa kubarikiwa, unazungumzia Yesu Kristo, ambaye baadaye angefungulia serikali ya Mungu njia ya kisheria ya kuingia ulimwenguni kupitia kwa imani ya Ibrahimu.

***BASI IMANI, CHANZO CHAKE NI KUSIKIA; NA KUSIKIA HUJA KWA NENO LA KRISTO. — WARUMI 10:17***

Imani ya Ibrahimu ilifungulia Mungu mlango wa kudumu kisheria kwa kufanya mapatano ya kisheria kati yake, uzao au warithi wake, na Mungu Mwenyewe.

Hebu nifafanue kile ninasema. Serikali ya mbinguni inaweza kuingia ulimwenguni kupitia kwa mwanadamu tu kwa sababu ana mamlaka ya kisheria hapa. Uhalali huo unaweza kutimizwa tu ikiwa mwanadamu atashawishika kabisa katika moyo wake kuhusu kile ambacho Mungu amesema (imani).

Njia nyingine ya kusema hili ni kwamba mbingu zinaweza tu kuathiri kisheria mwanadamu aliye duniani ambaye anatamani na kuchagua kuwa chini ya utawala na mamlaka ya Mungu. Hii ndiyo kanuni ileile ambayo Shetani alitumia kuingia duniani,

akimtumia Adamu kufanya hivyo. Alimsadikisha Adamu kwamba Mungu hangeweza kutegemewa na kuutoa moyo wa Adamu kutoka katika mapatano na Mungu. Kwa hiyo, Adamu alichagua kumwamini Shetani na kukataa mamlaka ya Mungu.

Mungu basi alitumia kanuni hiihii kurudisha serikali na mamlaka yake duniani kupitia kwa Ibrahimu. Ibrahimu alimwamini Mungu, na mapatano yake yakahesabiwa na Mungu kuwa haki, jambo ambalo lilimaanisha kwamba mapatano ya kisheria yaliyohitajika yalikuwepo. Makubaliano haya ya pande zote mbili, Mungu na Ibrahimu, yalimruhusu Mungu kufanya mkataba wa kisheria (agano) uliohakikisha ufikiaji wa mbinguni katika dunia, LAKINI ni muhimu kutambua kwamba mapatano haya yaliathiri Ibrahimu na warithi wake tu. Ishara ya agano hili ilitolewa kwa warithi wote wa Ibrahimu, ambayo ilikuwa tohara. Tohara ilikuwa ni kukatwa kwa govi kutoka kwa uume wa kiume. Mwanamume alipopanda mbegu yake ndani ya mwanamke, ilibidi uzao wake upite katika uume ule uliotahiriwa, ambao ulitangaza kwa Shetani na baba na mama wenyewe kwamba mtoto huyo alisimama mbele ya mbingu kama mrithi wa agano hilo la kisheria ambalo Mungu na Ibrahimu walikuwa wameimarisha.

Hata hivyo, kama tulivyosoma hapo awali, ingawa kila mtu alikuwa chini ya mapatano hayo ya kisheria, bado alipaswa kutimiza matakwa ya kisheria ya moyo wake mwenyewe akiwa amesadikishwa kikamili kuhusu yale ambayo Mungu alisema ili kufurahia faida za kibinafsi za mapatano hayo kati ya Mungu na Ibrahimu. Kimsingi, agano lilipeleka waya hadi nyumbani kwao, lakini bado walilazimika kuwasha swichi kwa kuamini na kutenda kulingana na Neno la Mungu kibinafsi.

Sasa tunajua imani ni nini na kwa nini imani inahitajika kisheria, lakini bado tunahitaji kujua jinsi ya kupata imani na jinsi

ya kujua ikiwa tunayo.

**Tunapataje imani?**

Hapa kuna dokezo: Huwezi kuomba kupokea imani. Umeshangaa? Nilidhani hivyo.

> *Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*
>
> —Warumi 10:17

Imani hujaje kwa kusikia Neno la Mungu? Mchakato ni upi? Je, kusikia tu Neno ndilo jambo pekee linalohitajika ili imani isitawishwe katika roho ya mwanadamu? Ili kuelewa jinsi imani inavyokuja na kile ambacho Warumi 10:17 inazungumzia, tunaweza kutazama Marko sura ya 4. Sikuzote mimi husema ukirusha Biblia yako hewani, inapaswa kutua kwenye Marko sura ya 4; andiko hili ni muhimu hivyo! Yesu alisema katika Marko 4:13 kwamba usipoelewa kile alichokuwa akifundisha katika sura hiyo, huwezi kuelewa mfano mwingine wowote katika Biblia. Hili ni jambo muhimu sana!

Kwa nini sura hii ni muhimu sana? Kwa sababu inatuambia jinsi mbingu inavyoingiana na ulimwengu, jinsi inavyopata mamlaka, na mahali hilo hutukia. Hakuna kitu muhimu zaidi katika maisha yako kuliko kujua sura hii yote inazungumzia nini. Unaweza kuuliza, "Ufalme wa Mungu unatendaje kazi?" Soma Marko sura ya 4! Katika sura hii, Yesu anatuambia mifano mitatu kuhusu jinsi imani inavyokuja katika roho ya mwanadamu, ambayo ni, kama unavyojua sasa, hitaji la mbingu kuivamia Dunia kihalali.

Hadithi tatu katika sura hii ni mfano wa mpanzi, mfano wa mtu anayetawanya mbegu, na hadithi ya mbegu ya haradali.

Hebu tuanze kwa kutazama hadithi ya pili ambayo Yesu

anasimulia katika Marko sura ya 4, hadithi ya mtu aliyetawanya mbegu.

> *Akasema, "Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."*
>
> —Marko 4:26-29

Kabla hatujaingia katika kifungu hiki, hebu kwanza tufafanue masharti yetu. Je, ni mbegu gani ambayo Yesu anazungumzia na ardhi ni nini? Yesu anafafanua maneno hayo mawili katika mfano uliotangulia wa mpanzi katika sura hiyohiyo. Mbegu ni Neno la Mungu, na ardhi ni moyo wa mwanadamu au roho ya mwanadamu. Kwa hiyo katika mfano huu, Yesu anasema mtu hutawanya Neno la Mungu moyoni mwake. Kisha peke yake, udongo, au moyo wa mwanadamu, huanza kutokeza imani (makubaliano na mbinguni) duniani.

Kabla sijaendelea, ni muhimu kukumbuka maana ya imani ni nini: ni wakati moyo wa mwanamume au mwanamke unashawishika kwa uthabiti kuhusu kile mbingu inasema. Kifungu hiki kinasema kwamba ingawa mwanadamu hajui jinsi mchakato huo unavyofanya kazi, Neno lililopandwa moyoni mwake huanza kukua na kutoa mapatano peke yake. Hii hutokea ikiwa amelala au yuko macho; haijalishi, mchakato unaendelea. Mwanadamu anapoweka Neno moyoni mwake, polepole moyo wake unapatana na yale ambayo mbingu amesema, na imani inazalishwa.

Rejeo letu la Maandiko katika Marko sura ya 4 linatuambia

kwamba moyo hutokeza mapatano kupitia mchakato fulani. Hadithi inatuambia kwamba mwanzoni wakati moyo wetu unapokea Neno, imani huanza kukua. Yesu alilinganisha hilo na chipukizi. Kisha chipukizi huendelea na kukuwa bua. Hatimaye, kichwa hujitokeza kwenye bua, lakini hata katika awamu hii, hakuna matunda, hakuna makubaliano, na hakuna mabadiliko katika ulimwengu wa asili. Kisha Yesu alisema mchakato huo huendelea huku kichwa kinapokomaa na kutoa nafaka iliyokomaa. Mbegu iliyokomaa inapojitokeza kichwani, panakuwa na mapatano na imani inaingia, na kumpa mwanadamu fursa ya kuvuna ulimwenguni kile mbingu ilikuwa imepanda ndani ya moyo wake.

Sasa kuwa makini sana. Hebu tupitie kile kinachotokea. Mbingu hupanda Neno la Mungu ndani ya moyo wa mwanadamu aliye duniani ambapo makubaliano yanahitajika. Wakati huo, moyo wa mtu huyo hauna mapatano na mbingu, lakini mchakato huanza kutokea ndani ya moyo ambao unafanya moyo, peke yake, kupatana na kile kilichopandwa. Yesu alitumia mfano mzuri kutuonyesha mchakato huu. Akilinganisha mchakato huu na mkulima anayepanda mbegu na jinsi mmea unavyokomaa, Yesu alitupa picha ya mwonekano wa imani. Katika ulimwengu wa asili, wakati mbegu katika kichwa imekomaa, itaonekana **SAWASAWA** ile mbegu iliyopandwa ardhini. Hebu nirudie tena.

**Mbegu iliyo kwenye kichwa cha mmea inapokomaa, itaonekana SAWASAWA—na ile iliyopandwa ardhini.**

Panda mmea wa mahindi, na mbegu iliyokomaa kwenye sikio itafanana na ile uliyoipanda. Zinafanana. Zinafanana na zina ladha sawa; huwezi kuzitofautisha. Kwa hivyo hebu nifafanue kile Yesu alichosema. Tunaposikia Neno la Mungu (Warumi 10:17), tunalitawanya ndani ya utu wetu wa roho, yaani mioyo

yetu. Tukiliweka Neno hilo mioyoni mwetu, litakua na kukomaa; na litakapokomaa, mioyo yetu itasadikishwa kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu imesema.

Kwa maneno mengine unapopanda ahadi kutoka mbinguni ndani ya moyo wako, polepole itazalisha peke yake ujasiri wa kile ambacho Mungu alisema. Hatimaye, moyo wako utashawishika kikamilifu kuhusu kile ambacho mbingu inasema, na makubaliano yatakuwa pale. Kwa mfano, ikiwa unakabiliwa na ugonjwa, hali yako mwilini inazungumza nawe kwamba wewe ni mgonjwa. Unapopanda Neno la Mungu linalosema kwamba Mungu amelipa gharama ya uponyaji wako kupitia yale aliyoyafanya Yesu, moyo wako peke yake polepole unaanza kusadikishwa na kile ambacho Mungu amesema.

Neno hilo linapokomaa moyoni mwako, ujasiri ya kuwa umepona unakuwa kile **unachoamini** na kusema. Hunukuu tu kile ambacho mbingu inasema tena. Moyo wako sasa umesadikishwa kabisa. Unaposema, "Nimepona," hunukuu fomula fulani; bali hivi ndivyo unavyoamini na unajua ni ukweli. Kile ambacho mbingu inasema sasa kinakuwa mtazamo wako mwenyewe wa ukweli.

Ndiyo maana Waebrania 11:1 (EHV) inasema:

> *Imani ni kuwa na hakika juu ya yale tunayotumainia, kuwa na hakika juu ya mambo tusiyoyaona.*

Kuna uhakikisho usio wa kawaida wa kile mbingu inasema wakati imani iko, lakini bado kuna hatua nyingine katika mchakato huo.

Mtu sasa lazima atie mundu wake ili kuvuna, ili kuleta katika mazingira yake, kile alicho na uhakika kuhusu moyoni mwake.

> *Hata matunda yakiiva, mara **atapeleka mundu**, kwa kuwa mavuno yamefika.*
>
> —Marko 4:29

Tambua kwamba ingawa moyo unapatana na mbingu, na uhalisi wa mbinguni umekuwa uhalisi wa mtu, hakuna mabadiliko halisi katika ulimwengu wa kiasili. Kwa sababu mwanadamu ndiye ambaye kwa asili ana mamlaka hapa duniani, yeye ndiye anapaswa kuachilia mamlaka hayo ya mbinguni katika ulimwengu huu. Mungu hawezi kufanya hivyo bila mwanadamu. Ninaweza kukuonyesha hili katika Andiko tunalolijua sana ambalo tulizungumzia hapo awali.

> *Kwa maana kwa moyo mtu huamini na **kuhesabiwa haki,** na kwa kinywa mtu **hukiri** na kuokolewa.*
>
> —Warumi 10:10 (Tafsiri ya '*ESV*')

**HIVI NDIVYO MBINGU INAVYOPATA UHALALI KATIKA ULIMWENGU—MOYO NI KIOLESURA CHA MBINGU ULIMWENGUNI, KISHA SWICHI ZINAZOACHILIA NGUVU ZA MBINGUNI HAPA DUNIANI NI MANENO NA MATENDO YETU.**

Kwa moyo mtu huamini Neno, huzaa imani, na kuhesabiwa haki. Kuhesabiwa haki ni maneno ya kisheria na maana yake ni kutekeleza sheria. Kwa hiyo moyo wa mtu unapopatana na mbingu, na kusadikishwa kabisa na kile mbingu inachosema, anahesabiwa haki. Sasa ni halali kwa mbingu kutiririka katika maisha yake duniani. Lakini kuhesabiwa haki peke yake hakuachilii nguvu za Mungu. Kama vile nyumba ilivyo na

nguvu za umeme zinazotoka kwa kituo cha umeme, kuna hatua moja zaidi—kuwasha swichi ili kuachilia nguvu, kisha taa zinawaka. Kwa nini? Kwa sababu kama Warumi 10:10 inavyoonyesha, kuna hatua moja zaidi baada ya kuhesabiwa haki.

Mtu aliyehesabiwa haki duniani na mbinguni lazima basi akiri au achukue hatua kulingana na makubaliano aliyoyafanya ili kuachilia nguvu na upako wa Mungu katika ulimwengu. Tafadhali soma Maandiko hayo tena na tena mpaka uelewe kabisa ninachosema. Hivi ndivyo jambo hili linavyofanya kazi! Hivi ndivyo mbingu inavyopata uhalali katika ulimwengu—moyo ni kiolesura cha mbingu ulimwenguni, kisha swichi zinazoachilia nguvu za mbinguni hapa duniani ni maneno na matendo yetu. Tafadhali zingatia kwa makini sehemu ya pili ya mstari huo tena: Sisi ndio tunaopaswa kuachilia mamlaka ya mbinguni hapa.

Dhana ya mbingu kumngoja mtu, kwanza kabisa, atoe uhalali na, pili, mamlaka katika ulimwengu waweza kuonekana kupitia yale ambayo Yesu alifundisha katika Mathayo 16:19 na Mathayo 18:18.

> *Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*
>
> — Mathayo 16:19

> *Amin, nawaambia, lolote mtakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote mtakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*
>
> — Mathayo 18:18 (Tafsiri ya '*ESV*')

Yesu alisema katika Mathayo 16:19 kwamba atalipa kanisa funguo (mamlaka) za Ufalme wa mbinguni hapa duniani. Alisema chochote utakachofunga duniani, mbingu zitaunga mkono, na vivyo hivyo chochote utakachofungua duniani. Tena tafakari afisa wa polisi; yeye ana mamlaka, lakini serikali ina nguvu. Afisa wa polisi ndiye anayeshikilia ufunguo au mamlaka ya serikali, maana aliapishwa kuwa mwakilishi wa serikali hiyo. Serikali inaunga mkono anachosema. Kumbuka ni mwanadamu tu aliye na mamlaka ya kisheria hapa, na hivyo ndiye pekee anayeweza kuipa mbingu mamlaka ya kisheria hapa.

Kuna suala lingine muhimu zaidi unalohitaji kufahamu kuhusu imani. Hebu nirejelee andiko letu katika Marko sura ya 4 kwa muda mfupi.

> *Maana nchi* ***huzaa yenyewe;*** *kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke.*
>
> — Marko 4:28

Kumbuka, Yesu alifafanua udongo unaotajwa katika mfano huu kama moyo au roho ya mwanadamu, kama nilivyotaja hapo awali. Tazama mahali ambapo imani huzalishwa; hilo linakushangaza? Imani haitoki mbinguni, kama watu wengi wanavyoamini, bali ni zao la moyo wako hapa duniani. Huwezi kumwomba Mungu akupe. Imani haihitajiki mbinguni maana hatuhitaji makubaliano huko. La, inahitajika hapa ulimwenguni tu, na inapaswa kuzaliwa katika mioyo ya wanadamu duniani. Kama mfano katika Marko 4 unavyofundisha, kuna njia moja tu ya kuipata, kwa kuweka Neno la Mungu moyoni mwako na kuruhusu mchakato wa makubaliano ufanyike. Kwa hivyo ikiwa ninahitaji imani, ninapaswa kufanya nini? Kutawanya Neno la

Mungu moyoni mwangu na kuliacha likue mpaka imani ikiwepo. Hiyo ndiyo njia pekee imani huja.

Kabla sijatoka kwa Marko 4, nataka kuzungumzia tena mundu uliotajwa hapo.

> *Hata matunda yakiiva, mara* ***atapeleka mundu****, kwa kuwa mavuno yamefika*
>
> — Marko 4:29

Ninaamini waumini wengi duniani hawajafundishwa jinsi ya kutumia mundu, kumaanisha kwamba hawajafundishwa jinsi ya kuvuna kile wanachohitaji. Kanisa kwa ujumla limefundishwa jinsi ya kutoa matoleo lakini sio jinsi ya kupalilia na kuvuna kutoka kwa mbegu waliyoipanda. Yesu alisema wazi katika mstari huu kwamba mavuno ya imani yetu yanapopatikana, ni lazima tutumie mundu. Hata iwe tumefanya kazi nzuri ya kuachilia mbegu zetu kwa imani, tusipojua kutumia mundu, hakutakuwa na mavuno. Kusema kweli, sikujua lolote kuhusu hili hadi Bwana alipoanza kunifundisha jinsi Ufalme ulivyofanya kazi. Niruhusu nikupe mifano michache ya jambo hili.

Nilialikwa kuhubiri katika kanisa fulani huko Atlanta. Ilikuwa ibada ya Jumatano jioni na kanisa halikuwa kubwa vile, lakini hilo lilikuwa sawa kwangu. Nilipenda sana kufundisha watu kuhusu Ufalme. Nilipofika kanisani, nilistaajabu kwamba milango ilikuwa imefungwa na hakuna mtu aliyekuwepo. Ilikuwa dakika kumi kabla ya ibada kuanza. Kisha nikasikia mlio wa gari kubwa sana nyuma yangu; ilionekana kana kwamba haikuwa na kifaa cha kuzima sauti hata kidogo. Nilipotazama nyuma, niliona gari kuukuu, bovu, likiingia kwa kichochoro kilichoelekea kanisani. Sikufikiria chochote kuhusu hilo maana nilikuwa katika jiji la

Atlanta. Nilipokuwa nikingoja, mwanamume mmoja alikuja akitembea kutoka nyuma ya jengo na kujitambulisha kuwa yeye ndiye mchungaji. Aliomba radhi kwa kuchelewa kwa sababu gari lake kuukuu lilikataa kuwaka. Aliniambia ilimbidi aanzishe gari kwa mteremko kwa sababu kibonyezi cha kuwasha gari kilikuwa kimeharibika. Alisema mara nyingi gari lilikataa kuwaka kabisa, na ilimlazimu atembee maili tano hadi kanisani.

Alipoendelea kunieleza kuhusu kanisa lake, aliniambia kwamba ingawa alikuwa mchungaji wa kanisa hilo, kazi kuu ya kanisa ilikuwa kulisha maskini wa jiji. Walilisha zaidi ya watu 10,000 kwa mwezi mahali hapo.

Mchungaji alipokuwa akizungumza, nilijawa na fadhaha. Huyu ni mtu wa Mungu anayelisha watu 10,000 kwa mwezi, lakini hana hata gari la kutegemewa? Alikuwa picha pekee ya Mungu ambayo wengi wa watu hao aliowalisha wangewahi kuona. Ikiwa walimwona akisongwa na shida, huku akilazimika kutembea maili tano katika siku ya kiangazi yenye digrii 37 kwenda kanisani, wangekuwa na uhakika gani kwamba Mungu angeweza kuwasaidia? Niliamua kushughulikia hitaji hilo. Nilikuwa na gari mpya nyumbani iliyokuwa imesafiri maili 20,000 pekee ambayo ningempa. Nilimweleza kuhusu mpango wangu na kwamba ningemtuma mmoja wa wafanyakazi wangu Atlanta ili amletee gari. Yeye, bila shaka, alifurahia sana. Jioni hiyo nilimfundisha pamoja na kanisa lake dogo kuhusu Ufalme wa Mungu na jinsi unavyofanya kazi inapohusu fedha.

Niliporudi nyumbani, nilipanga gari liendeshwe hadi Atlanta. Wakati mfanyakazi wangu alikuja nyumbani kwangu kuchukua gari, nilifahamu nilikuwa ninafanya shughuli ya kiroho mbinguni. Nilijua kwamba nilipoachilia gari hilo katika Ufalme wa Mungu, ningeweza kumwamini Mungu kupata gari nililohitaji pia. Mimi

sio mtu wa magari, maana yake sipendi magari sana. Kuna watu wanaopenda magari sana, lakini si mimi. Gari ni chombo tu kwangu. Bila shaka napenda kuwa na gari zuri, lakini huwa ninaziendesha hadi zitakapohitaji kubadilishwa.

Mfanyikazi wangu alipopitia, nilienda kwenye karakana yangu, na kuwekelea gari hilo mikono yangu na kusema, "Baba, ninaachilia gari hili lifanye kazi ya huduma Yako, na ninapoliachilia, ninapokea gari…" Nilisita. Ninajua jinsi Ufalme wa Mungu ulivyo mahususi, na nilijua kusema neno "gari" tu haingefua dafu. Pia nilifahamu nilipaswa kuwa mahususi na kwamba mimi na Drenda tulihitaji kukubaliana kuhusu jibu hususa ambalo tungepokea. Nilipokuwa katikati ya mazungumzo yangu, niligundua pia kwamba sikujua ni aina gani ya gari nililotaka. Kwa hiyo nilianza tena, "Bwana, leo ninaachilia gari hili kwenye huduma Yako, na ninaamini nitapokea gari zuri sana ninapotoa hili, lakini itabidi nirudi kwako kuhusu aina ninayotaka nitakapojua hilo." Tosha gari; gari liliondoka. Kwa kweli sikuwa na aina yoyote ya gari akilini ambayo ningeweza kusema, "Naam, nataka gari FULANI."

Miezi michache ilipita. Drenda alikubaliana nami kuhusu kutoa gari na, kama mimi, hakujua ni aina gani ya gari alilotaka. Kwa kipindi cha miezi miwili iliyofuata tulizungumza kuhusu magari, na hatimaye siku moja alisema, "Wajua nini, nafikiri ningefurahia kuwa na gari ambalo linaweza kuendeshwa bila paa." Nilimwambia nilikubaliana na hilo, na nikasema nilifikiri hilo lilikuwa jambo la kufurahisha, lakini gari aina gani? Tena, hatukujua ni aina gani ya magari kama hayo yaliyokuwepo.

Lakini siku moja tulipokuwa tukienda kula chakula cha mchana, mke wangu alisema ghafula, "Ndio ile!" "Ni nini?" Nikasema. "Ndio ile," alisema huku akiashiria kwa kidole sehemu ya maegesho ya mkahawa ambao tulikuwa tumeingia. "Ni nini?" Nikasema. "Hilo

ndilo gari ninalotaka!" Kisha nikaona gari aina hiyo kwenye eneo la maegesho. "Twende tuone ni aina gani," nikasema. Kwa hiyo tuliendesha gari hadi kwenye gari hilo na kusimama nyuma yake. Naam, si ajabu tulilipenda. Lilikuwa gari aina ya BMW 645Ci, la kifahari, na bei kubwa sana. Kusema kweli, nilipoona lile gari, niliwaza, *"Sawa, Bwana, tuonyeshe cha kufanya."* Nilijua singelipa $115,000 ili kununua BMW mpya, lakini pia nilijua kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ya ajabu. Mimi na Drenda hatukumwambia mtu yeyote kuhusu gari hilo wala kumtajia mtu yeyote kuwa tunatafuta gari.

Baada ya karibu wiki mbili, kaka ya Drenda alitupigia simu na kusema, "Nimepata gari la Drenda!" "Unamaanisha nini umepata gari la Drenda?" Nikasema. "Niliona gari likiuzwa, na ghafla, nikahisi kwamba linapaswa kuwa gari la Drenda; na ilinibidi nikwambie kulihusu," Akasema. "Ni gari aina gani?" Nikauliza. "Ni BMW 645Ci, na liko katika hali nzuri kabisa. Lina umri wa miaka miwili, halijasafiri sana, wala halina mkwaruzo juu yake. Ni kamilifu kabisa. Zaidi ya hayo, unamjua mtu anayeliuza." "Kweli?" Nikasema. "Ndio," akajibu; "Na unapaswa kumpigia simu mtu huyo." Aliponiambia muundo na aina ya gari hilo, huku nikiwa na ufahamu kwamba hilo ndilo gari tulilolipenda mimi na Drenda wiki chache awali, nilijua kwamba Mungu alikuwa na kusudi fulani.

Nilimpigia simu mwenye gari. Ndio, nilimfahamu, na tulizungumza kidogo juu ya gari, na alikuwa akiniambia jinsi gari hilo lilivyokuwa katika hali nzuri. Kisha akaniambia maneno haya. "Wajua, tangu tuanze kuzungumza kwa simu kuhusu gari hili, nahisi kama linapaswa kuwa gari la Drenda." Sikuwa nimemtajia hata kidogo kwamba nilikuwa ninatafutia Drenda gari. Kisha mtu huyo akasema, "Nitakwambia nitakachofanya, nitakuuzia kwa dola 28,000." Masikio yangu hayakuamini kile nilichokuwa nimesikia.

Gari lilikuwa na thamani kubwa kuliko hiyo. Nilipomwambia Drenda kuhusu hilo, alifurahi sana. Tulilipia gari hilo pesa taslimu na bado tuko nalo hadi leo. Bado linaenda sawa na linaonekana vizuri. Bado halina mkwaruzo juu yake, na tumeliendesha mara nyingi bila paa, huku radio yake ikicheza muziki kwa sauti kubwa, na jua likiwaka juu yetu kuondoa uchovu wa siku.

Safari tuliyoipenda zaidi kwa gari hilo la kifahari ilikuwa katika milima ya Colorado, huku tukiwa na vifaa vyetu vya kupiga kambi kwenye lori. Binti yetu Kirsten alikuwa nasi katika safari hiyo, na ninakumbuka nikiendesha gari kupitia jimbo la Kansas kwenye barabara kuu ya I-70 usiku huku sehemu ya paa ya gari ikiwa imetolewa. Kirsten alikuwa amelala kwenye kiti cha nyuma huku nikiendesha gari. Nyota ziling'aa sana juu ya vichwa vyetu, na barabara ilikuwa wazi isipokuwa lori moja au mbili mara kwa mara. Ulikuwa mojawapo wa usiku mwema ambapo hewa ilikuwa safi na kila kitu ulimwenguni kilikuwa ajabu. Tulitumia wiki mbili zilizofuata kuendesha gari milimani, na nikatambua jinsi lilivyokuwa gari la ajabu. Ni maneno machache tu yanayoweza kueleza wakati wetu huko—Ajabu kupita fahamu!

Lakini swali muhimu ni hili. Gari hili lilikujaje kwetu? Kwa nini lilikuwa gari haswa ambalo Drenda alisema, "Ndilo hilo!?" Nilifahamu kwamba Ufalme wa Mungu ulileta gari hilo maishani mwetu. Nilijua kwamba nilipotoa gari langu kwa mchungaji yule, nilikuwa nimetumia sheria ya kiroho. Nakumbuka sikutaja muundo wa gari ambao ningependa kupokea bali nilisema ningepata gari kubwa na nzuri. Lakini ilitubidi mimi na Drenda tutumie mundu. Gari hili halingekuja ikiwa hatukusema, "Ndilo hilo!" Ingawa nilikuwa na imani nilipoachilia gari langu, hatukuwa tumetumia mundu hadi Drenda aliposema, "Ndilo hilo."

Tukio lingine lilitokea ambalo lilidhihirisha kanuni hii kwa njia

kubwa zaidi. Kama unavyojua, napenda kuwinda. Ninaishi katika eneo zuri sana la uwindaji, na nimebarikiwa kumiliki ardhi yangu ya kuwinda. Katika ekari zangu 60, nina takriban ekari 19 za msitu na 10 zenye kinamasi. Mimi huwa na mafanikio makubwa katika uwindaji wa kulungu na kindi kila mwaka. Kila wakati huwa kuna bata na bata bukini wanaorukaruka hapo, lakini kwa sababu moja au nyingine, sikuwa nimewahi kufikiria kuwawinda hata kidogo. Mara moja au mbili katika miaka mingi, mimi na vijana wangu tulienda kwenye bwawa na kupiga risasi bata bukini wachache ili kuwala jioni. Lakini hatukuwa tumewahi kuwinda bata kweli.

Naam, miaka michache iliyopita, nilipotazama bata kadhaa wakiruka kwenye kinamasi, nilifikiri kwamba ningejaribu kuwawinda. Lo, hilo lilisisimua sana! Nilipata uraibu wa kuwawinda. Katika msimu huo wa vuli wa kuwinda bata, nilitambua kwamba nilihitaji mazoezi mengi ya kuwapiga bata risasi. Nilifanikiwa kubeba kadhaa na kupata kwamba zilikuwa tamu sana kula. Niligundua kwamba mara nyingi sikuwa nawaua kwa sababu walikuwa mbali au bunduki yangu haikuweza kuwafikia. Nilikuwa nikitumia bunduki yangu ya kawaida aina ya Remington 11-87, ambayo nilitumia kuua kila kitu iwe sungura au kulungu. Usielewe vibaya, ninaipenda bunduki hiyo, na ni bunduki nzuri sana. Lakini nilikuwa nimesikia kulikuwa na aina mpya za bunduki zilizotengenezwa kwa ajili ya kuwinda bata pekee. Haikuwa rahisi kuziona na zilikuwa na nafasi ya kubeba risasi zenye urefu wa inchi tatu na nusu, jambo ambalo nilijua lingesaidia nilipohitaji kufyatua risasi mbali. Niliamua kutafuta moja ya hizo kabla ya msimu mwingine wa kuwinda bata kuanza.

Kweli, msimu wa bata ulikuwa umekwisha, sasa ilikuwa Januari, na nilikuwa nikipitia duka linaloitwa Cabela's ambalo linauza vifaa mbalimbali na nikafikiri kupitia sehemu yenye

bunduki ili kuona jinsi bunduki hizo zilivyoonekana. Nilipoingia kwenye sehemu yenye bunduki, niliona kwamba walikuwa na sehemu nzima iliyotengwa kwa ajili ya bunduki za kuwinda bata pekee. Nilichunguza chache na nikataka kununua ile niliyopenda, lakini ilikuwa $2,000 na msimu wa kuwinda bata ulikuwa umesalia miezi kadhaa. "*Nitasubiri*," nilijiwazia. Lakini nilifanya jambo lisilo la kawaida nilipokuwa karibu kuondoka. Kwa kweli sikutambua nilichokuwa nikifanya wakati nilipokifanya. Nilikifanya bila kufikiria. Nilielekeza kidole kwa bunduki niliyoitaka kisha nikasema kwa sauti. "Nitakuwa na bunduki hii, katika jina la Yesu." Sikufikiria jambo hilo sana; nilikuwa nikitangaza tu kwamba ningekuwa na bunduki hiyo. Moyo wangu ulikuwa na picha dhahiri ya bunduki ya bata niliyoitaka.

Nilialikwa kuhubiri katika kongamano la biashara, na jambo fulani lilitokea huko ambalo lilivutia umakini wangu. Baada ya kuhubiri, mwenye kampuni alinijia na kusema walitaka kunipa zawadi ili kunishukuru kwa kuja. Alisema, "Tulijua unapenda kuwinda, kwa hivyo tuli-kununulia bunduki hii." Nilipigwa na butwaa walipotoa bunduki mpya aina ya Benelli ya kuwinda bata, kama ile niliyoona pale dukani, na kuielekezea kidole! Je, unaona hii? Je, bunduki hiyo haswa ilikujaje? Nilikuwa nimetoa bunduki nyingi kwa miaka mingi lakini sikuwa nimewahi kutumia mundu. Kwa maneno mengine, nilikuwa nimetoa bunduki hizo kwa imani na ukarimu lakini sikuwahi kutumia mundu. Sikuwa nimewahi kusema, "Bwana, ndiyo hiyo! Hiyo ndiyo ninayoitaka." Lakini mara tu nilipofanya hivyo, mavuno yalitokea!

Nilikuwa nikimsimulia rafiki yangu mhudumu kuhusu hadithi hii ya bunduki. Alisema, "Naam, nafikiri Mungu hufanya hivyo wakati mwingine. Yeye hutubariki na zawadi ndogo maalum ya kutuambia anatupenda." Nilipotafakari kile alichosema, nilitambua,

"La, hilo halikuwa sahihi. Ndio, Mungu ananipenda, lakini hataki tu kunishangaza na zawadi ndogo." Mbwa, samaki, kulungu waliokuja kwa mpangilio huo, magari, na yote yaliyokuwa yamekuja haikuwa kwa sababu Mungu alitaka tu kunionyesha kwamba ananipenda. Alinionyesha ananipenda alipomtuma Yesu kwa ajili yangu na kunipa Ufalme!

Nimesema kwa miaka mingi kwamba kanisa limefanya kazi nzuri sana ya kufundisha juu ya kutoa lakini kazi mbovu kuhusu jinsi ya kuvuna. Kwa hiyo unaweza kutambua mundu ni nini kutoka kwa hadithi nilizosimulia awali? Natumaini ni dhahiri! Mundu ni maneno yetu!

**MUNGU ALITAKA TU KUNIONYESHA KWAMBA ANANIPENDA. ALINIONYESHA ANANIPENDA ALIPOMTUMA YESU KWA AJILI YANGU NA KUNIPA UFALME!**

*Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na wao waupendao watakula matunda yake.*

— Mithali 18:21

Kulikuwa na msimu ambao kanisa lilionekana kufundisha sana kuhusu matamshi yetu. Nimekuwa pamoja na watu, na labda wewe pia, ambao wanasema jambo fulani kisha wanafunika midomo yao na kusema, "Ninahitaji kuchunga maneno yangu." Hiyo inaonekana kama kazi nzuri, na ninakubali kwamba itasaidia kuweka Neno moyoni mwako. Walakini, kuchunga maneno yako kwa kweli hakuna uhusiano wowote na mundu. Eti nini? Lakini nilifikiri umesema mundu ni maneno yetu. Ndio, lakini kujua jinsi ya kutamka maneno sahihi pekee sio jambo muhimu.

> *Amin, nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, bali aamini kwamba hayo ayasemayo yametukia, yatafanyika kwake.*

Tena, mundu katika Marko sura ya 4 ni maneno yako! Kufikia wakati Marko sura ya 4 inazungumzia mundu, tayari imezungumzia mchakato wa imani na jinsi ya kuipata. Inasema mbegu inapokomaa unatumia mundu kwa kuwa mavuno yamekuja. Mavuno yamekuja kwa sababu uko na imani kwa kukubaliana na mbingu moyoni mwako. Aya hii ya Marko 11 inadhihirisha kanuni hiyo hiyo. Moyo wako unaamini Neno, kisha unatamka na kuachilia mamlaka ya mbinguni. Lakini tazama maneno haya, "aamini kwamba hayo asemayo yametukia." Kujaribiwa katika imani kunadhihirisha ikiwa unaamini unachosema. Kutamka au kukiri Neno la Mungu pekee sio imani. Moyo wako usipokubaliana na mbingu, unaweza kukiri mpaka uchoke wala hakuna kitakachotokea. Kwa hiyo je, tunapaswa kuchunga maneno yetu au mioyo yetu?

> *Mtu mwema hutoa lililo jema kutoka katika lile jema lililowekwa moyoni mwake, na mtu mwovu hutoa lililo ovu kutoka katika uovu ulio ndani. Kwa hakika, kile kinywa chake huzungumza hutoka moyoni.*
>
> — Luka 6:45 (Tafsiri ya '*EHV*')

> *Zaidi ya yote linda moyo wako, maana ndiko zitokako chemchemi za uzima. Ondoa upotovu kinywani mwako; weka mbali na midomo yako mazungumzo ya ufisadi.*
>
> —Mithali 4:23-24 (Tafsiri ya 'BSB')

Tunaweza kuona wazi kwamba yale tunayosema yanatoka moyoni mwetu na yale unayoamini. Kwa kufuata mchakato katika Marko sura ya 4, tutajua jinsi ya kubadili kile ambacho mioyo yetu inaamini na kukifanya kipatane na mbinguni katika imani. Kisha tutakaposhawishika kabisa, itatubidi tutumie mundu ya maneno na matendo yetu. Umeelewa? Vema, tuendelee.

Tunapoendelea na mjadala wetu juu ya imani, nataka kuuliza swali ambalo lazima uweze kujibu.

**Nitajuaje kama kweli Niko na imani?**

Hili ni swali zuri ambalo **unapaswa** kufahamu kwa sababu haiwezekani kuomba maombi ya imani bila kuwa na imani kwanza. Kuna njia nyingi za kujua ikiwa uko na imani au la, na dalili nyingi unazohitaji kujua na kutafuta. Wakati hauna imani unaweza kufanya maamuzi mengi yasiyofaa kwa sababu ya hofu. Maamuzi yanayotokana na hofu kila mara yatakufanya uwe mateka chini ya laana ya dunia na kukufanya ukose kile Mungu anachokutakia.

Kwa hivyo ishara ya kuwa na imani ni nini? Ya kwanza ni rahisi; unaweza kutazama nyuma katika ufafanuzi wetu wa imani na kuelewa kwamba kusadiki kikamilifu moyoni mwako ni jambo muhimu. Lakini mara nyingi huwa tunafikiri kwamba tumeshawishika lakini tunakubaliana tu katika akili zetu na Neno wala sio mioyo yetu. Unahitaji kuwa na uwezo wa kutofautisha. Unaposadiki kikamilifu, bila shaka kuna mapatano ya kiakili na yale ambayo Neno linasema lakini pia ufahamu wa hakika, na ujasiri unaoleta amani na matarajio.

*Imani ni kuwa na hakika juu ya yale tunayotumainia, kusadiki juu ya mambo tusiyoyaona.*

— Waebrania 11:1 (Tafsiri ya '*EHV*')

Ikiwa una ushahidi kwamba una kitu fulani, je, bado unahitaji kuhakikishiwa kwamba unacho? La hasha. Ukiwa na imani, kuna ufahamu, amani, na ujasiri kwamba una kile ambacho Neno la Mungu linasema, hata ingawa hujakiona. Watu wengi husema hivi: "Ninajua kwamba ninajua kwamba ninajua ninacho." Ufahamu huu unatoka ndani yetu na sio kutoka kwa jinsi hali zilivyo. Uko rohoni au moyoni mwako. Hofu inatoweka, hakuna tena mawazo sumbufu ya wasiwasi yanayoshambulia akili yako; unajua yote yamekamilika.

Kipengele kingine cha kuwa na imani ni furaha na matarajio. Jibu lako limekuja. Unalo! Imani ni zaidi ya hisia ya amani au ujasiri, ingawa utakuwa na yote mawili. Unapaswa pia kuwa na uwezo wa kutetea msimamo wako kiroho. Ninaposema hivyo, tafakari mahakama ambapo wewe ni wakili anayemhoji shahidi. Kwa nini unaamini kile unachokiamini kuhusu hali yako? Ungeteteaje msimamo wako? Kuna jibu moja tu, nalo ni Neno la Mungu.

Kwa mfano, mtu akija nyumbani kwako na kusema, "Ondoka nyumbani kwangu," je, utasema, "Samahani; tupe siku moja, nasi tutaondoka?" La, hutafanya hivyo; labda utacheka. Mtu huyo akisema, "La, hii ni nyumba yangu; toka la sivyo tutaonana mahakamani," jibu lako litakuwa, "nitafurahi kukuona mahakamani!" Wakati wa kusikilizwa kwa kesi yako, utamwonyesha hakimu hati ya umiliki wako kwa utulivu. Ataiangalia mara moja na kumkamata yule mwingine kwa kukunyanyasa na kumfanya alipe gharama zote za mahakama. Ujasiri wako haukuegemea kwa jinsi ulivyohisi na hisia zako, bali juu ya sheria na ukweli kwamba wewe ni mmiliki halali wa nyumba hiyo.

Linapokuja suala la kuwa na imani, naona kwamba mara nyingi watu ambao hawaelewi imani ni nini huchanganyikiwa kwa urahisi kwa kuweka ujasiri wao katika matendo yao badala

ya chanzo chao pekee cha imani, ambacho ni Neno la Mungu. Ni rahisi kuchanganya kitendo au kanuni ya kutenda kulingana na Neno la Mungu na nguvu halisi ya Ufalme, ambayo hutoka kwa moyo uliosadiki kwa uhakika. Kwa mfano, ikiwa ulitoa matoleo ya kifedha katika Ufalme wa Mungu, na nikakuuliza kwa nini unaamini kwamba utapokea marejesho ya utoaji huo, jibu lako halipaswi kuwa, "Kwa sababu tarehe fulani nilitoa kiasi fulani cha pesa." Jibu hilo linazingatia kitendo chako tu wala halina nanga ya uhakikisho. Uhakikisho wako uko katika Neno la Mungu pekee.

Siwezi kuhesabu idadi ya watu ambao wamenitazama bila jibu nilipowauliza kwa nini waliamini wangepokea nilipowaombea. Ninapouliza, ninatafuta imani yao, yaani makubaliano yao na mbingu. Ninataka kuwasikia wakisema, "Najua nitapokea kwa sababu Mungu ameniahidi katika kitabu fulani na fulani na katika mstari fulani kwamba kitu hiki ni changu." Ikiwa hawanipi andiko kuna uwezekano kwamba hawana nanga na hawajui hakika mashua yao inaelekea wapi.

**IMANI NI KUWA NA HAKIKA JUU YA YALE TUNAYOTUMAINIA, KUSADIKI JUU YA MAMBO TUSIYOYAONA. — WAEBRANIA 11:1 (TAFSIRI YA 'EHV')**

Kumbuka, imani inaweza kuwepo tu unapojua mapenzi ya Mungu. Kwa nini? Kwa sababu imani inaweza kuwepo tu wakati moyo wako unakubaliana na mapenzi ya Mungu. Ninaamini kwamba watu wengi hufikiri wana imani wakati sivyo. Tena, akili zao zinaweza kukubaliana kwamba Neno la Mungu ni kweli na ni jema, lakini imani huja wakati mioyo yao imesadiki kabisa. Kwa wengi, akili zao zinakubaliana na Neno la Mungu, lakini mioyo yao haina utulivu.

Hapa kuna kielelezo kizuri cha kile ninachokizungumzia,

ambacho ninaamini kitaonyesha kuwa wengi hawana imani wanapodhani wanayo. Je, kama ningekuambia niligundua hivi majuzi kwamba anga haikuwa ya rangi ya samawati, kama watu walivyosema, kwamba rangi ya samawati ilikuwa rangi ya njano? Kwa maneno mengine, nilikuambia kwamba maisha yetu yote tulifundishwa kimakosa kuhusu rangi na kwamba rangi ya samawati sio samawati, bali ni njano. Ungefanya nini? Je, ungeshtuka na kunyakua simu yako ya mkononi haraka na kumpigia mwalimu wako wa darasa la kwanza na kumzomea, huku ukimshutumu kwa kuharibu maisha yako, kwa kukufundisha vibaya kuhusu rangi zote? Sidhani. Hautaitikia kwa hofu wala kufanya mambo mengi. Utajua tu kwamba mimi ni mjinga, na useme kwamba maneno yangu hayana maana, kisha uendelee na shughuli zako. Kwa nini? Kwa sababu una hakika kabisa kwamba rangi ya samawati ni rangi ya samawati!

Sasa, hebu tulinganishe mfano wangu na mjadala wetu kuhusu imani. Je, ikiwa umesadiki kabisa yale anayosema Mungu kuhusu uponyaji, lakini daktari akuambie kwamba utakufa kwa sababu ya ugonjwa wa saratani. Je, utamtazama daktari na kusema yeye ni mjinga maana unafahamu hilo kamwe haliwezi kutokea? Kwa nini? Kwa sababu unasadiki kikamilifu kuhusu uponyaji alioulipia Yesu. Unaona jambo hili? Bila shaka, watu wengi huomba, lakini ninapochunguza, napata maombi yao sio maombi ya imani bali ya tumaini, wala hawana uhakika wa matokeo. Rafiki yangu, hii ndiyo sababu ni muhimu sana tujijenge wenyewe katika Neno la Mungu. Tunahitaji kujua mapenzi ya Mungu ni nini ili tuwe na uhakika katika kile anachosema, na pia tuweze kukataa kile ambacho si mapenzi Yake. Hebu nikupe mfano kutoka kwa maisha yangu binafsi kuhusu jinsi ilivyo muhimu kujilisha na kile Mungu anachosema juu ya maisha.

Nilikuwa na uchovu, kwa sababu ya kuwa na ugumu katika biashara yangu kwa majuma kadhaa (hii ilikuwa kabla ya kuanzisha kanisa). Ratiba yangu ilikuwa imejaa simu za wateja wangu, na bila shaka, shinikizo la kifedha la kuishi kwa kulipwa kamisheni. Nilikuwa nimeenda kwa daktari wangu wa meno kwa matibabu ya mara kwa mara. Kila kitu kilikuwa kawaida hadi daktari alipodunga dawa ya kupunguza maumivu. Alipoingiza ile sindano, nilishtuka kisha taya yangu ikakufa ganzi mara moja, badala ya kufa ganzi polepole. Nilishangaa na nikamwambia daktari kilichokuwa kimetokea. Akasema, "Doh! nafikiri niligusa neva." Nilimuuliza haraka, "Je, hiyo ni kawaida?" Alisema maneno haya, "Kwa kawaida huwa inapona." Eti nini? Je, nilimsikia kwa usahihi? "Daktari, unamaanisha nini unaposema hivyo?" Akasema, "Huwa inapona kabisa asilimia 80 hadi 85 bila athari mbaya inayodumu."

Eti nini? Ghafla hofu iliniingia. Sasa nini? Je, itapona? Akili yangu ilianza kuingiwa na mawazo ya woga. Baada ya kutibiwa na daktari, uso wangu uliendelea kukufa ganzi, jambo lisilo la kawaida maana ganzi huisha polepole. Nilikuwa ninaelekea kukutana na mteja takriban saa moja kutoka kwa daktari wa meno, kwa hivyo nilikuwa na wakati mwingi wa kufikiria juu ya kile ambacho kilikuwa kimetokea. Lakini safari hiyo yote nilikuwa na uchungu, si kwa maumivu yoyote, bali kwa kukosa amani na kuingiwa na hofu akilini mwangu.

Njiani kwenda nyumbani mchana baada ya kukutana na mteja wangu, nilipitia kwa nyumba ya rafiki. Uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi, na nilikuwa nikitafuta uhakikisho fulani kutoka kwa mtu kwamba ningepona. Tazama kosa langu: Sikulitumaini Neno la Mungu bali mtu ambaye hakuwa mwamini mwenye nguvu ili kunipa ujasiri. Nilimwambia rafiki huyo wangu kilichotokea na nilikuwa nikingojea aseme, "Hilo si jambo kubwa, Gary; utapona!"

Badala yake, nilisikia yafuatayo. "Doh! Hapana! Nilikuwa na rafiki ambaye jambo hilohilo lilimfanyikia, na uso wake kamwe haukupona bali ulipooza tangu wakati huo." Sikuamini nilichokisikia! Akili yangu sasa iliingiwa na hofu nyingi kupita kiasi. Nilijifanya kana kwamba nilifahamu ingekuwa sawa na nikamshukuru kwa kunipa wakati wake. Kwa moyo ulioukata tamaa, nilipitia kwa nyumba ya rafiki yangu mwigine kuuliza swali lile lile, na kwa mshtuko, nilisikia jibu lile lile, "Doh! Hapana," akasema, "Nilikuwa na rafiki ambaye alipita jambo hilo hilo, na uso wake haukupona kamwe; uso wake bado umepooza leo." Sikuamini nilichokisikia! Akili yangu ilijawa hofu kupita kiasi. Nilijifanya nilijua kila kitu kingekuwa sawa na kumshukuru kwa wakati wake.

Kwa kukata tamaa, nilipitia nyumbani mwa rafiki mwingine na kuuliza swali lilelile, na kwa mshtuko, nikasikia jibu lile lile, "Loo, la," akasema, "Nilikuwa na rafiki ambaye alipatwa na jambo hili, na uso wao haukupona kamwe. Uso wao bado umepooza hadi leo."

Baada ya ziara hiyo, nilivunjwa moyo kabisa. Nilifahamu kwamba Mungu huponya (katika mawazo yangu), lakini sikuweza kuondoa woga huo. Moyo wangu kweli haukuwa umeshawishika. Usiku huo, nilikuwa na uchungu mwingi! Akili yangu ilijawa na hofu, na uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi kama ilivyokuwa kwenye ofisi ya daktari wa meno. Nilipokuwa nikijaribu kupata usingizi, nilianza kusikia maumivu kidogo chini ya sikio langu la kulia. Je, ulikuwa ugonjwa wa babangu wa kupooza? Alipambana nao kwa mwaka mmoja au miwili awali, na aliniambia kwamba ulianza kwa maumivu chini ya sikio lake. Ugonjwa huu hutokea wakati neva inayodhibiti misuli ya uso na inayopitia tundu dogo la mfupa chini ya sikio, inapobanwa na maambukizi au kuvimba.

Nilipolala pale huku nikijaribu kupata usingizi, nilichoweza kusikia tu ni maneno haya kupitia kwa mawazo yangu, "Utakuwa na

ugonjwa wa kupooza kama babako." Nilipoamka asubuhi, nilikuwa na ugonjwa wa kupooza! Sasa, si tu kwamba taya yangu ilikuwa imekufa ganzi, bali pia uso wangu wote wa upande wa kulia, na sikuweza kufunga macho yangu au mdomo wangu. Nilikuwa katika hali mbaya.

Nilienda kwa daktari aliyekuwa karibu ili kuthibitisha tuhuma zangu. Baada ya uchunguzi, alinitazama na kusema kwamba kwa hakika nilikuwa na ugonjwa wa kupooza. Kisha nikauliza, "Ni nini kitatokea baada ya hili?" Akasema, "Takriban asilimia 80 hadi 85 ya wagonjwa hupona kabisa bila kupooza kudumu." "Je, alisema kile nilichofikiri alikuwa amesema?"

Papo nilijua kwamba nilikuwa nimeingia shidani. Nilijua kwamba shetani hangemalizia hapo, na sikutaka kuona kile ambacho kingefuata. Nilifahamu vya kutosha kuhusu vita vya kiroho kutambua kwamba nilikuwa nikielekea katika njia potovu. Kumbuka, hii ilikuwa miaka mingi kabla ya kupata ufahamu wa mengi ya mambo haya. Lakini nilijua vya kutosha kutambua kwamba nilipaswa kukabiliana na jambo hili kwa kiroho ikiwa ningefanikiwa kwa njia yoyote kulishinda. Pia niligundua kwamba huu ulikuwa mpango wa kishetani wa kunitega wakati nina uchovu na kutotazamia matatizo yoyote.

Papo hapo nilitambua kwamba tumaini langu pekee lilikuwa Neno la Mungu. Ndani yangu sikuwa na uwezo kabisa wa kuizuia hofu iliyokuwa inaishambulia akili yangu. Kwa hivyo niliandika maandiko ya uponyaji kwa kadi ndogo ambazo nilibandika kote nyumbani kwangu. Nilitubu mbele za Bwana na kuanza mchakato wa kukuza imani moyoni

**PAPO HAPO NILITAMBUA KWAMBA TUMAINI LANGU PEKEE LILIKUWA NENO LA MUNGU.**

mwangu. Nilijua kwamba nilipaswa kupanda Neno moyoni mwangu ili imani ikue, kwa hivyo nilitafakari Neno la Mungu siku nzima.

Mwanzoni hakuna kitu kilichobadilika. Uso wangu ulikufa ganzi, na mara kwa mara nilipambana na roho ya woga. Baada ya wiki moja, nikiwa katika hali hiyo ya kutokuwa na mabadiliko yoyote, ghafula jambo lilitokea!

Kama ule mchakato ambao andiko letu katika Marko 4:26-28 linavyofundisha, nilipotawanya Neno moyoni mwangu, imani ilianza kukuzwa, kwanza jani, suke, kisha ngano pevu kwenye suke.

Katika mchakato huu wote, hakuna makubaliano na hivyo hakuna imani—bado. Walakini, ingawa hatuoni mabadiliko au kufahamu jinsi mchakato huu unavyofanya kazi, kulingana na andiko letu katika Marko 4, mambo yanabadilika kweli.

Mabadiliko ninayozungumzia bado hayajadhihirishwa katika ulimwengu wa asili, bali yanatokea mioyoni mwetu. Tukilishikilia Neno, linabadilisha polepole mfumo wa imani ya mioyo yetu kutoka kwa kutokuamini hadi kukubaliana na mbingu.

Kwa hiyo nilishikilia Neno, huku nikijua kwamba hilo ndilo lililokuwa jibu langu pekee. Ghafla, siku moja, nilipokuwa nikitembea nyumbani mwangu nikiwa na kadi hizo zote zenye maandiko ya uponyaji zikiwa zimebandikwa kila mahali, nilitazama moja ambayo nilikuwa nimeiona mara mia moja. Lakini safari hii nilipoitazama, ghafla, upako ulinijia, hofu ikaondoka mara moja, NIKAJUA kuwa nimepona. Ndio, uso wangu ulikuwa bado umekufa ganzi. Hakukuwa na mabadiliko, lakini nilijua nilikuwa mzima. Baada ya masaa kadhaa, uso wangu ulikuwa kawaida kabisa, na ganzi yote ilikuwa imekwisha. Bwana asifiwe! Jamani neno linafanya kazi!

Ingawa nilikuwa nimeruhusu maisha yangu ya kiroho

kudhoofika kwa sababu ya shughuli nyingi na kupuuza kwangu, hatimaye nilitambua kosa langu na kutubu kutokana na upumbavu wangu. Huu ni wakati nilikuwa nikijifunza kwa mara ya kwanza jinsi imani inavyofanya kazi, na sikuwa na uzoefu mwingi kuihusu. Ilikuwa upumbavu kwangu kuuliza watu kuhusu siku zangu za usoni wakati wa shida badala ya kwenda moja kwa moja kwenye Neno la Mungu. Mara nilipoelewa kilichokuwa kikiendelea, niligeukia Neno la Mungu kwa ujasiri. Cha kusikitisha ni kwamba, watu wengi hawana ujasiri katika mchakato huu kwa sababu hawajawahi kufundishwa kuhusu imani na jinsi inavyokuja. Kwa sababu hawajui mchakato huu, wanapokuwa chini ya shinikizo, huwa wanaacha Neno, wakidhani kuwa halifanyi kazi.

**Elewa mashambulizi ya Shetani.**

Christine alipokuja kanisani mwetu hakujua mengi kumhusu Mungu. Aliokoka katika mojawapo ya ibada zetu za Jumapili asubuhi na maisha yake yalibadilika sana. Katika kanisa letu tuna mafundisho ya kuwajulisha waumini wapya kuhusu Ufalme. Moja ya maeneo tunayozungumzia na kufundisha ni haki ya kisheria ya kupokea uponyaji. Christine alikuwa na shida na masikio yake kwa miaka mingi. Alikuwa ametumia kifaa cha kumsaidia kusikia kwa miaka 40 na tayari alikuwa amepoteza zaidi ya asilimia 50 ya uwezo wake wa kusikia. Mamake alikuwa kiziwi, na kakake pia alikuwa na shida hiyohiyo ya kupoteza uwezo wa kusikia. Christine aliposikia kwamba, yeye kama muumini, alikuwa na haki ya kisheria ya kuponywa, alisisimka sana!

Darasani, mke wangu alimwekelea mikono na kuomba kwamba masikio yake yafunguliwe, na papo hapo, aliweza kusikia kikamilifu. Christine alianza kupiga kelele na kulia na kumsifu Mungu. Mke wangu, Drenda, na Christine walipokuja na kuniambia habari njema,

nilihisi msukumo wa kumwonya kuhusu mashambulizi ya kulipiza kisasi ya Shetani. Nilimwambia Drenda amwelekeze Christine kwamba dalili zikianza kumrudia anenee suala hilo kwa ujasiri na atangaze kuwa amepona na kwamba Shetani aondoke. Asubuhi iliyofuata jaribu lilikuja. Kusikia kwake kulikuwa kumedhoofika na hakuweza kusikia vyema. Kwa hivyo alifanya jinsi tulivyosema, "LA! Shetani, ninakataa hili. Niliponywa na nimepona, kwa jina la Yesu!" Mara moja! Masikio yake yalifunguka na yamekaa wazi tangu wakati huo.

Kumbuka kwamba Shetani hushambulia ili kujaribu kutwaa eneo hilo tena. Usimruhusu afanye hivyo. Simama kwa Neno la Mungu!

Katika kiambatisho hiki, nimechukua muda kukupa ufahamu wa kimsingi kuhusu maana ya imani, jinsi inavyofanya kazi, jinsi ya kujua kama uko na imani, na mahali pa kupata imani. Ili Ufalme wa Mungu ufanye kazi maishani mwako, unapaswa kujua hili. Kumbuka, Yesu alimwambia yule mwanamke katika Mathayo 9:20-22, *"Imani yako imekuponya."* Na ndivyo itakavyokuwa kwako: Imani yako, moyo wako ulio na hakika kabisa kuhusu kile mbingu inachosema, na kutumia mundu ndiyo suluhisho lako kwa shida au hitaji lolote utakalokabili maishani.

Nyenzo zangu zote zinapatikana kwenye garykeesee.com.

Nenda kwa FLNFree.com
ili kupakua mafundisho zaidi
ya bure katika lugha yako!

Je, ungependa nyenzo zaidi za mafundisho
BILA MALIPO katika lugha yako?
Nenda kwa **FLNFree.com**

## TAZAMA FURSA

## USIACHE NDOTO ZAKO KWENYE MEZA.

**Jiandae kugundua jinsi ya kuharakisha mafanikio yako na kutimiza ndoto zako!**

Je, unajua kwamba zaidi ya 80% ya Wamarekani hawapendi kazi zao? Kwa hivyo, kwa nini wanaendelea kuamka kila asubuhi kwenda kufanya kazi wanayoichukia? Kwa sababu kulipa bili kumechukua nafasi ya maono yao. Madeni yameteka uhuru wao na kuwafanya wakate tamaa na ndoto zao.

*Kazi Ambayo Haijakamilika: Sheria Tisa za Kuongeza Kasi* kinaweka kila kitu wazi na kukusaidia kupiga hatua zitakazobadili mtazamo wako—fikra zako—na kuzifanya kuwa zenye kuona **fursa** na **kuongeza kasi**, ili usiache ndoto zako zozote, athari yako, au kutotimiza hatma yako iliyoundwa na Mungu.

Pamoja na mseto wake wa maarifa ya vitendo, hadithi na Maandiko, Gary Keesee atakusaidia kuchukua hatua rahisi kutoka kwenye hali ya unusuru hadi hali ya ustawi.

Gary na mkewe, Drenda, walikuwa mfano halisi wa watu wenye madeni na majanga. Hofu ilitawala maisha ya Gary hadi akawa anatumia dawa za kupunguza huzuni na kujitahidi kutoka kitandani asubuhi. Kisha, alipoanza kutumia hatua zilizofunuliwa katika kitabu hiki, aliweza kutoka katika hali ya kujitahidi na kupata ushindi.

Akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 30, Gary amesaidia watu wengi kutimiza ndoto na makusudi yao waliyopewa na Mungu. Anataka kukusaidia kupata ushindi maishani, kuchukua maeneo, na kuhakikisha kwamba hauachi nyuma kazi ambayo haijakamilika.

**Jitayarishe kupata uzoefu wa *kuongeza kasi!***



Gary Keesee ni mwandishi, mmnenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni—*Fixing the Money Thing* na *Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.

FaithLifeNow.com | 1-(888)-391-LIFE
P.O: Box 779, New Albany, OH 43054